SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR



## RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA NA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023





SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

## AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

# RIPOTI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

# KUHUSU UKAGUZI WA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA NA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023

**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR**
2 Mtaa wa Tume, 71125 Kilimani Zanzibar, S.L.P 258
Simu/Nukushi: +255 24 223 400, Barua Pepe: info@ocagz.go.tz
Tovuti: www.ocagz.go.tz

**MAREJEO NAM: CAC.132/385/01/4** **TAREHE: 26 MACHI, 2024**

**MHE. DKT HUSSEIN ALI MWINYI,**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI,**
**AFISI YA RAIS IKULU,**
**S.L.P. 437,**
**ZANZIBAR, TANZANIA.**

**KUH: KUWASILISHA RIPOTI YA MWAKA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KUHUSU UKAGUZI WA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA NA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023**

---

Ninayo furaha kuwasilisha kwako Ripoti ya Mwaka inayohusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mashirika ya Umma na Taasisi Zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 kwa mujibu wa kifungu nambari 112(5) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 pamoja na kifungu nambari 46(1) cha Sheria nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023.

Naomba kuwasilisha.

Ahsante.

.............................................
**DKT. OTHMAN ABBAS ALI**
**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU**
**WA HESABU ZA SERIKALI**
**ZANZIBAR.**

# AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI ZANZIBAR

## Mamlaka

Kwa mujibu wa kifungu nambari 112 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 pamoja na kifungu nambari 46(1) cha Sheria nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kikatiba kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa za ukaguzi huo angalau mara moja kila mwaka.

## Dira

Kuwa na Taasisi ya ukaguzi iliyo huru na inayoongoza katika kusimamia uwajibikaji na uwazi.

## Dhamira

Kusimamia uwajibikaji wa Taasisi za umma kwa kufanya ukaguzi wa hesabu wenye kuleta tija na kulihakikishia Taifa kwamba rasilimali za Umma zitatumika kama ilivyokusudiwa.

## MISINGI YA MAADILI YA UKAGUZI

1. **Uaminifu** – Kuhakikisha Afisi ina kiwango cha juu cha uaminifu na kuzingatia utawala bora unaozingatia Sheria.
2. **Uadilifu** – Kuwa ni Afisi inayozingatia misingi ya uadilifu kwa kutoa huduma bila ya upendeleo.
3. **Kuwa Huru** – Kuwa ni Afisi iliyo huru na inayotekeleza majukumu yake bila ya kuingiliwa kwa mujibu wa Sheria.
4. **Uwezo na Taaluma ya Ukaguzi** – Kuwa ni Afisi yenye kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora wa kiwango cha juu.
5. **Kutunza Siri** – Kuwa ni Afisi yenye kutunza siri katika utekelezaji wa kazi zake.
6. **Uwazi na Uwajibikaji** – Kutoa taarifa sahihi na muhimu kwa wadau ili kuweza kupima uwajibikaji katika matumizi bora ya rasilimali za Umma

# YALIYOMO

YALIYOMO....V
ORODHA YA MAJADWELI....VIII
VIFUPISHO....XIV
SHUKURANI....XVI
DIBAJI....XVII
MUHTASARI....XIX
**SURA YA KWANZA**....1
1.0 UTANGULIZI....1
1.1 MAJUKUMU YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI....1
1.2 UPEO NA MADHUMUNI YA RIPOTI YA UKAGUZI....2
1.3 NJIA ZILIZOTUMIKA KATIKA UKAGUZI....2
1.4 UMUHIMU WA UKAGUZI KATIKA KUIMARISHA UTAWALA BORA....3
1.5 KAMATI ZA BARAZA LA WAWAKILISHI....3
**SURA YA PILI**....5
2.0 MUHTASARI WA MAMBO YALIYOBAINIKA PAMOJA NA UFAFANUZI WA HATI ZA UKAGUZI....5
2.1 MUHTASARI WA MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023....5
2.1.1 DOSARI ZA KIUTENDAJI ZILIZOBAINIKA KATIKA UKAGUZI....5
2.2 UWASILISHAJI WA HESABU ZA MWISHO WA MWAKA KWA MASHIRIKA NA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA....7
2.3 HATI ZA UKAGUZI....9
2.3.1 AINA YA HATI ZA UKAGUZI....9
2.3.2 AYA YENYE MASUALA YA MSISITIZO KWENYE RIPOTI ZA MKAGUZI....10
2.3.3 MASUALA MUHIMU YA UKAGUZI....10
2.3.4 MSINGI WA HATI ZA UKAGUZI....10
2.3.5 HATI ZA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023....11
2.4 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA HOJA ZA UKAGUZI KWA MWAKA ULIOPITA....14

**SURA YA TATU** ........ 16
3.0 TATHMINI YA MIFUMO YA UDHIBITI WA NDANI ........ 16
3.1 MATOKEO YA TATHMINI YA MFUMO WA UDHIBITI WA NDANI ........ 16
3.1.1 DOSARI ZA UJUMLA ZILIZOBAINIKA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023. 16
**SURA YA NNE** ........ 32
4.0 MASHIRIKA YA UMMA YA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR ........ 32
4.1 TATHMINI YA UENDESHAJI WA FAIDA KWA MASHIRIKA YA UMMA NA KAMPUNI ZA SERIKALI........ 33
4.1.1 SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR........ 33
4.1.2 SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR (ZPC)........ 38
4.1.3 SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC) ........ 45
4.1.4 KAMPUNI YA MWANI ZANZIBAR ........ 49
4.1.5 SHIRIKA LA MELI NA UWAKALA ZANZIBAR........ 51
4.1.6 SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR (ZBC)........ 53
4.1.7 SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR (ZHC) ........ 61
4.1.8 SHIRIKA LA MAGAZETI YA SERIKALI ZANZIBAR ........ 68
**SURA YA TANO**........ 74
5.0 MAMLAKA ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR........ 74
5.1 TAARIFA ZA UKAGUZI WA MAMLAKA ZA SERIKALI........ 74
5.1.1 MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR (ZURA)........74
5.1.2 MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI ZANZIBAR (ZMA) ........ 76
5.1.3 MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR (ZAA) ........ 82
5.1.4 MAMLAKA YA MAJI ZANZIBAR ........ 86
5.1.5 MAMLAKA YA KUKUZA UWEKEZAJI ZANZIBAR (ZIPA)........ 96
5.1.6 MAMLAKA YA UNUNUZI NA UONDOAJI WA MALI ZA UMMA ZANZIBAR (ZPPDA)........101
5.1.7 MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI (VTA) ........ 102
5.1.8 MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI........ 111
5.1.9 MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA........ 113
**SURA YA SITA**........ 122
6.0 UKAGUZI WA WAKALA ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR........ 122
6.1 TAARIFA ZA WAKALA WA SERIKALI KWA MWAKA 2022/2023 ........ 122

6.1.1 WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR (ZAGPA) ........ 124
6.1.2 WAKALA WA MIUNDOMBINU YA TEHAMA ZANZIBAR (ZICTIA) ........ 128
6.1.3 WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII ........ 145
6.1.4 WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO. 149
6.1.5 WAKALA WA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI ZANZIBAR (ZFDA) ........ 151
6.1.6 WAKALA WA MAJENGO ZANZIBAR ........ 154
6.1.7 WAKALA WA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI ........ 160
6.1.8 WAKALA WA KARAKANA KUU YA MAGARI ZANZIBAR ........ 161
6.1.9 WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA MALI ZANZIBAR ........ 165
6.1.10 WAKALA WA SERIKALI MTANDAO ZANZIBAR (eGAZ) ........ 169
6.1.11 WAKALA WA ULINZI – JKU ........ 172
6.1.12 WAKALA WA BARABARA ZANZIBAR ........ 174
6.1.13 WAKALA WA MAENDELEO YA VIWANDA VIDOGO VIDOGO, VIDOGO NA VYA KATI (SMIDA) ........ 175
6.1.14 WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ........ 177

**SURA YA SABA** ........ 181

7.0 UKAGUZI WA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR ........ 181

7.1 TAARIFA ZA HESABU ZA TAASISI MBALIMBALI ZINAZOJITEGEMEA ZA SERIKALI KWA MWAKA 2022/2023 ........ 181

7.1.1 BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ) ........ 181
7.1.2 MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR (ZRA) ........ 191
7.1.3 MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (ZSSF) ........ 198
7.1.4 MFUKO WA BARABARA (ZRF) ........ 206
7.1.5 KAMPUNI YA UJENZI ........ 210
7.1.6 KAMPUNI YA UVUVI ZANZIBAR (ZAFICO) ........ 211
7.1.7 KAMPUNI YA UUNGANISHAJI WA MAUDHUI (ZMUX) ........ 213
7.1.8 CHUO CHA UTAWALA WA UMMA ........ 214
7.1.9 CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (SUZA) ........ 215

**SURA YA NANE** ........ 220

8.0 UKAGUZI WA AWALI WA MAFAO YA WASTAAFU NA MALIPO YA FIDIA KWA WATUMISHI WA UMMA ........ 220

**9.0 HITIMISHO** ........ 227

**VIAMBATISHO** ........ 228

# ORODHA YA MAJADWELI

Jadweli Nambari 1: Mashirika na Taasisi zinazojitegemea zilizowasilisha Hesabu za Mwisho wa Mwaka ........ 7

Jadweli Nambari 2: Hati za ukaguzi zilizotolewa kwa Mashirika na Taasisi zinazojitegemea katika kipindi cha miaka Minne ........ 11

Jadweli Nambari 3: Mwenendo wa hati za ukaguzi ........ 13

Jadweli Nambari 4: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi kwa Asilimia ........ 13

Jadweli Nambari 5: Dosari za kiutendaji zilizobainika kwa vitengo vya usimamizi na udhibiti wa ndani ........ 17

Jadweli Nambari 6: Taasisi zilizochelewa kuwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka........ 18

Jadweli Nambari 7: Taasisi zilizobainika kuwa na mapungufu katika daftari la Kuhifadhia Mali za Kudumu ........ 18

Jadweli Nambari 8: Taasisi zilizokuwa hazikufuata muongozo wa ufungaji wa hesabu (Vote book)........ 19

Jadweli Nambari 9: Taasisi zilizoshindwa kuandaa "Segment Report"........ 20

Jadweli Nambari 10: Taasisi zisizokuwa na bajeti ya mapato na matumizi ........ 21

Jadweli Nambari 11: Taasisi ambazo hazikutenganisha masjala ya siri na masjala bayana 21

Jadweli Nambari 12: Watumishi wa kutwa walioajiriwa bila ya Kibali ........ 22

Jadweli Nambari 13: Vyombo vya Usafiri Ambavyo Havijakatiwa Bima ........ 25

Jadweli Nambari 14: Taasisi ambazo hazijaanza kutumia Mfumo wa e-Office ........ 26

Jadweli Nambari 15: Taasisi ambazo hazina vifaa vya huduma ya kwanza........ 26

Jadweli Nambari 16: Taasisi ambazo hazikufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ........ 27

Jadweli Nambari 17: Taasisi ambazo hazijatayarisha daftari la kumbukumbu za mikataba "Contract Registers"........ 28

Jadweli Nambari 18: Taasisi ambazo hazijatekeleza utaratibu wa Mahudhurio wa Kidijitali. 28

Jadweli Nambari 19: Taasisi za Serikali zilizoshindwa kuwandaa Mpango Mkakati ........ 29

Jadweli Nambari 20: Taasisi zisizokuwa na Kitengo cha Usimamizi wa Mali pamoja na Mpango wa matengenezo wa Mali ........ 30

Jadweli Nambari 21: Taasisi Ambazo Hazijawasilisha Mpango wa Manunuzi kwa ZPPDA.... 30

Jadweli Nambari 22: Ufanisi wa Utendaji wa Mashirika kwa mwaka wa fedha 2022/2023.. 32

Jadweli Nambari 23: Madeni ya muda mrefu yanayodaiwa kwa wateja wa ZECO........ 35

Jadweli Nambari 24: Manunuzi ya Shirika la Umeme yaliyokosa ushindani ........ 37

Jadweli Nambari 25: Manunuzi yaliyofanywa kwa njia iliyozidi kizingiti kilichowekwa........ 38

Jadweli Nambari 26: Miradi ya Ujenzi iliyoanza kutekelezwa bila ya kuwepo Mshauri Elekezi ........ 39
Jadweli Nambari 27: Wadaiwa wa Shirika la Bandari Zanzibar ........ 41
Jadweli Nambari 28: Wadaiwa wa muda mrefu ........ 42
Jadweli Nambari 29: Orodha ya waombaji wa misamaha ya tozo ........ 43
Jadweli Nambari 30: Orodha ya madeni yaliyoshindwa kulipwa ........ 44
Jadweli Nambari 31: Malimbikizo ya madeni ya mapato ya muda mrefu ........ 45
Jadweli Nambari 32: Madeni ya muda mrefu yatokanayo na majengo ya uwekezaji ........ 46
Jadweli Nambari 33: Mapato na Matumizi ya Tawi la ZSTC Dar es Salaam kwa mwaka 2022/2023 ........ 47
Jadweli Nambari 34: Majengo ya ZSTC ambayo hayana Hatimiliki ........ 48
Jadweli Nambari 35: Hasara inayotokana na kupungua kwa uzito wa karafuu ........ 49
Jadweli Nambari 36: Vifaa vya ukulima wa mwani vilivyochelewa kugaiwa kwa wakulima . 50
Jadweli Nambari 37: Hasara itokanayo na mwani ulioharibika ........ 51
Jadweli Nambari 38: Matumizi ya Shirika la Meli yaliyozidi bajeti iliyoidhinishwa ........ 53
Jadweli Nambari 39: Watumishi waliokaimu nafasi kinyume na utaratibu ........ 56
Jadweli Nambari 40: Madeni yanayodaiwa na Shirika la Utangazaji Zanzibar ........ 57
Jadweli Nambari 41: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu ........ 59
Jadweli Nambari 42: Mikataba ya ukodishwaji Minara ambayo haikupatikana kwa ukaguzi ........ 60
Jadweli Nambari 43: Malipo kwa watoa huduma ambao hawajasajiliwa na ZPPDA ........ 61
Jadweli Nambari 44: Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu kwa wapangaji wa nyumba za Serikali ........ 62
Jadweli Nambari 45: Manunuzi yaliyofanyika bila ya kutumia mfumo wa kielektroniki (e- Proz) ........ 66
Jadweli Nambari 46: Kutonunua vifaa kutoka kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji ........ 66
Jadweli Nambari 47: Nyumba za fidia zilizofanyiwa matengenezo ........ 68
Jadweli Nambari 48: Mapato ya ndani ya Shirika katika kipindi cha miaka miwili iliyopita .. 69
Jadweli Nambari 49: Mapato na matumizi ya Shirika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ..... 69
Jadweli Nambari 50: Takwimu za mgawanyo wa Magazeti ........ 70
Jadweli Nambari 51: Madeni ya mapato ya muda mrefu ........ 71
Jadweli Nambari 52: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu ........ 75
Jadweli Nambari 53: Ununuzi wa Mapazia ambao hauendani na uhalisia ........ 76
Jadweli Nambari 54: Kutokufuatwa kwa Mfumo wa Manunuzi Ipaswavyo ........ 76

Jadweli Nambari 55: Sifa za Waombaji wa nafasi za kazi katika ZMA ............................... 78
Jadweli Nambari 56: Waombaji walioshinda na kukataliwa katika Mchakato wa Ajira ........ 78
Jadweli Nambari 57 : Manunuzi yaliyofanyika nje ya Mfumo wa e-Proz ........................... 79
Jadweli Nambari 58: Upungufu wa Watumishi ................................................................ 81
Jadweli Nambari 59: Bajeti na Makusanyo halisi ya tozo ya Usalama wa Abiria ya ZAA ..... 82
Jadweli Nambari 60: Madeni wadaiwa wa Mamlaka ya ZAA ............................................ 85
Jadweli Nambari 61: Shehia ambazo zina changamoto za mtandao wa maji kwa upande wa Wilaya za Mjini Unguja ................................................................ 87
Jadweli Nambari 62: Malimbikizo ya Madeni ya Muda Mrefu........................................... 90
Jadweli Nambari 63: Wastani wa Uzalishaji Maji kwa Robo ya Nne ya 22/23 .................... 92
Jadweli Nambari 64: Deni la Kodi ya Mapato (PAYE) Ambalo Halijawasilishwa TRA ........... 93
Jadweli Nambari 65: Malipo Yaliyofanyika kwa Njia ya Fedha Taslimu ............................. 94
Jadweli Nambari 66: Malimbikizo ya Madeni ya Muda Mrefu........................................... 95
Jadweli Nambari 67: Mafuta yaliyonunuliwa bila ya Mkataba........................................ 101
Jadweli Nambari 68: Matumizi yaliyofanyika zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa katika vifungu husika................................................................................ 106
Jadweli Nambari 69: Malipo ya fedha kwenda Mfuko Mkuu wa Hazina ........................... 107
Jadweli Nambari 70: Manunuzi yaliofanyika nje ya Mfumo wa Manunuzi ........................ 108
Jadweli Nambari 71: Malipo yaliyolipwa kinyume na utaratibu....................................... 126
Jadweli Nambari 72: Manunuzi yaliyofanywa nje ya mfumo wa manunuzi ...................... 112
Jadweli Nambari 73: Upungufu wa Watumishi ............................................................. 113
Jadweli Nambari 74: Mapato yaliokusanywa nje ya Mfumo wa IFMIS ............................ 114
Jadweli Nambari 75: Idadi ya Tuhuma katika hatua ya upelelezi hadi Oktoba, 2023........ 118
Jadweli Nambari 76: Idadi ya majalada ya kesi zilizofikishwa Mahkamani hadi Oktoba 2023 .............................................................................. 118
Jadweli Nambari 77: Hatua za kesi zilizofikishwa Mahkamani hadi Oktoba, 2023 ............ 119
Jadweli Nambari 78: Malipo kwa ajili ya shughuli mbali mbali yenye vielelezo pungufu ... 123
Jadweli Nambari 79: Manunuzi yaliofanywa kwa njia ya kuvunjwavunjwa ...................... 124
Jadweli Nambari 80: Hati za malipo kwa ajili ya ukodishaji wa gari na ufungaji wa Faiba. 126
Jadweli Nambari 81: Upungufu wa Watumishi ............................................................. 126
Jadweli Nambari 82: Orodha ya bili zilizolipwa kwa mujibu wa daftari la mapato ........... 129
Jadweli Nambari 83: Orodha ya Deni kwa mujibu wa Ankara ....................................... 135

Jadweli Nambari 84: Mchanganuo wa deni pamoja na asilimia kumi ilioshindwa kujumuishwa katika deni ..... 138

Jadweli Nambari 85: Kiasi kilichoshindwa kudaiwa (Unbilled Amount)..... 139

Jadweli Nambari 86: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu ..... 140

Jadweli Nambari 87: Malipo yaliofanywa kwa fedha Taslim ..... 143

Jadweli Nambari 88: Mlinganisho wa matumizi na bajeti iliyoidhinishwa ..... 144

Jadweli Nambari 89: Tofauti ya Taarifa za mapato baina ya taarifa za benki na taarifa za makusanyo ya Vituo..... 146

Jadweli Nambari 90: Manunuzi yaliyofanyika nje ya Mpango wa Manunuzi..... 147

Jadweli Nambari 91: Watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi ... 148

Jadweli Nambari 92: Upungufu wa Watumishi ..... 148

Jadweli Nambari 93: Upungufu wa Watumishi ..... 150

Jadweli Nambari 94: Upungufu wa Watumishi ..... 152

Jadweli Nambari 95: Bidhaa ambazo zimekosa Vibali vya Ukaguzi ..... 153

Jadweli Nambari 96: Vifaa ambavyo havijanunuliwa na havikutumika katika ujenzi..... 155

Jadweli Nambari 97: Malimbikizo ya Madeni ya Muda Mrefu..... 156

Jadweli Nambari 98: Majengo ya Wakala yanayokaliwa bila ya Malipo ..... 157

Jadweli Nambari 99: Malimbikizo ya Deni la Ukodishaji wa Nyumba ..... 158

Jadweli Nambari 100: Vyombo vya usafiri ambavyo havijapasishwa..... 160

Jadweli Nambari 101: Deni Ambalo Halijakusanywa kwa Kipindi Kirefu ..... 161

Jadweli Nambari 102: Mafundi wa Karakana pamoja na taaluma zao..... 163

Jadweli Nambari 103: Upungufu wa Watumishi ..... 163

Jadweli Nambari 104: Mchanganuo wa fedha za Tirka..... 167

Jadweli Nambari 105: Tofauti ya fedha za Tirka baina ya hesabu za benki na Taarifa ya Ufungaji wa Hesabu ..... 167

Jadweli Nambari 106: Upungufu wa Watumishi ..... 168

Jadweli Nambari 107: Mafuta yaliyonunuliwa bila ya Mkataba..... 170

Jadweli Nambari 108: Upungufu wa Watumishi ..... 171

Jadweli Nambari 109: Manunuzi yaliyofanywa Nje ya Mfumo wa Manunuzi (e-Proz) ..... 173

Jadweli Nambari 126: Malimbikizo ya Madeni ya Muda Mrefu..... 173

Jadweli Nambari 111: Watumishi waliokaimu nafasi kinyume na utaratibu ..... 175

Jadweli Nambari 112: Miradi ilioshindwa kukamilika kwa muda uliopangwa ..... 175

Jadweli Nambari 113: Orodha ya Wajasiriamali walioshindwa kurudisha fedha walizokopeshwa

kwa muda uliopangwa ........................................................ 176
Jadweli Nambari 114: Tofauti ya Makusanyo ya mapato kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenda Wakala wa Uwezeshaji ................................................ 178
Jadweli Nambari 115: Ripoti za tathmini zilizopitwa na wakati kwa mujibu wa Sera ya Benki ........................................................................ 182
Jadweli Nambari 116: Mthamini ambae hajaidhinishwa na benki ................................. 182
Jadweli Nambari 117: Mthamini ambae hajaidhinishwa na benki ................................. 183
Jadweli Nambari 118: Taarifa za akaunti za dharura ................................................. 185
Jadweli Nambari 119: Malipo ya posho la usumbufu yaliyolipwa bila ya kuzingatia taratibu za kiutumishi ........................................................................ 187
Jadweli Nambari 120: Mikopo iliyotolewa kwa watumishi walio katika kipindi cha majaribio........................................................................... 187
Jadweli Nambari 121: Mikopo iliyotolewa kwa watumishi walio katika kipindi cha majaribio........................................................................... 188
Jadweli Nambari 122: Mikopo iliyoidhinishwa kinyume na sera ya mikopo ya Benki ........ 189
Jadweli Nambari 123: Cases Noted to Illustrate delay in execution of Annual Procurement Plan caused by user department in furnishing of user requirements/TOR/Specifications ............................................... 193
Jadweli Nambari 124: Procurement Performance Vs Budget Performance ...................... 194
Jadweli Nambari 125: Tozo zinazotozwa Bandarini kwa wasafiri wa Kigeni na Wazawa.... 198
Jadweli Nambari 126: Upungufu wa thamani ya vifaa vya Makumbusho katika Mnara wa Mapinduzi ........................................................................ 198
Jadweli Nambari 127: Tathmini ya Ufanisi wa Miradi ya Uwekezaji ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii........................................................................... 200
Jadweli Nambari 128: Mwenendo wa uendeshaji wa Hoteli Kihasara ............................ 200
Jadweli Nambari 129: Riba ya Mikopo ambayo haijalipwa ........................................... 201
Jadweli Nambari 130: Mwenendo wa ukuaji wa madeni ............................................. 203
Jadweli Nambari 131: Kodi ya zuio ambayo haijawasilishwa TRA................................. 211
Jadweli Nambari 132: Walinzi wasiokuwa na mikataba ya ajira ................................... 214
Jadweli Nambari 133: Mafuta ambayo hayakurikodiwa katika daftari la kurikodia bidhaa za ghalani........................................................................... 215
Jadweli Nambari 134: Vifaa vya kuandikia vilivyonunuliwa nje ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar ................................................................ 216
Jadweli Nambari 135: Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha Taslimu .......................... 217
Jadweli Nambari 136: Mafao ya Kiinua Mgongo ......................................................... 220
Jadweli Nambari 137: Mafao ya Pencheni.................................................................. 220
Jadweli Nambari 138: Majalada yaliyorejeshwa kwa ajili ya kufanyiwa masahihisho........ 221

Jadweli Nambari 139: Dosari za Ukokotoaji wa Mafao ya Wastaafu ............................... 223
Jadweli Nambari 140: Mlinganisho wa dosari za ukokotoaji wa mafao ya wastaafu......... 223
Jadweli Nambari 141: Ziada ya wastaafu ambao hawakuhakikiwa................................ 224
Jadweli Nambari 142: Malipo ya Wastaafu ambao hawakufanyiwa Uhakiki.................... 224
Jadweli Nambari 143: Tofauti ya Idadi ya wastaafu kati ya mwezi wa Januari na Februari 2022/2023 ........................................................................ 225
Jadweli Nambari 144: Tofauti baina ya Ripoti ya Uhakiki na Idadi halisi ya Wastaafu kwa mwezi wa Januari na Februari.................................................. 225
Jadweli Nambari 145: Kukosekana kwa ufafanuzi wa Malipo ya Wastaafu waliofariki ..... 226

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AR | Account Receivables |
| ARMFA | African Road Maintenance Funds Association |
| BLM | Baraza la Mapinduzi |
| BoQ | Makisio ya gharama za ujenzi. |
| BoT | Benki Kuu ya Tanzania |
| BPRA | Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar |
| BTS | Base Transceiver Station |
| CA | Current Asset |
| CAG | Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar |
| CIMIS | Mfumo Mkuu wa Usimamizi wa Biashara ya Bima |
| CL | Current Liability |
| CMS | Central Medical Store |
| CRDB | Cooperative and Rural Development Bank |
| DRPC | Idara ya Uchakataji na Ukusanyaji wa Marejesho |
| EY | Ernst & Young |
| GAAP | General Accepted Accounting Principles |
| HQ | Makao Makuu |
| IAS | International Accounting Standards |
| ICT | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| IFRS | International Financial Reporting Standards |
| INTOSAI | Shirika la Kimataifa la Taasisi za Juu za Ukaguzi |
| IPSAS | International Public Sectors Accounting Standards |
| JKU | Jeshi la Kujenga Uchumi |
| KIST | Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknologia |
| MOFP | Wizara ya Fedha na Mipango |
| MoICT | Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi |
| NAOT | Afisi ya Taifa ya Ukaguzi |
| NBAA | National Board of Accountants and Auditors |
| NMB | National Microfinance Bank |
| NTR | Mapato yasiyo ya kodi |
| PAARM | Public Audit Act and Related Matters No.7/ 2023 |
| PAC | Public Account Committee |
| PBZ | Benki ya Watu wa Zanzibar |
| PDMU | Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi na Uondoaji |
| PMU | Kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi |
| PPDA | Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 |
| PPE | Property Plant and Equipments |
| PPR | Kanuni ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2020 |
| PWC | Price Waterhouse Coopers |
| SAIs | Supreme Audit Institutions |

| | |
|---|---|
| SMIDA | Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo vidogo, Vidogo, na vya Kati |
| TAC | Tanzania Audit Corporation |
| TANESCO | Shirika la Umeme Tanzania |
| TAPA | Sheria ya Usimamizi na Taratibu za Ushuru Na.7 ya 2009 |
| TCB | Tanzania Commercial Bank |
| TOR | Masharti ya Marejeleo |
| TPB | Tanzania Postal Bank |
| TRA | Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| TRAI | Idara ya Ukaguzi, Usajili na Upelelezi kwa Walipakodi |
| Tsh./Tshs/TZS/Shs | Shilingi ya Kitanzania |
| TWDV | Thamani ya Salio la Kodi |
| USD | Dola ya Marekani |
| VAT | Kodi ya Ongezeko la Thamani |
| ZAA | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar |
| ZAFICO | Zanzibar Fishing Corporation |
| ZAGPA | Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar |
| ZAG-TAC | Zanzibar Agency Tally |
| ZANROAD | Wakala wa Barabara Zanzibar |
| ZASCO | Zanzibar Seaweed Company |
| ZAT | Huduma ya Usafiri wa Anga na Biashara ya Usafiri Zanzibar |
| ZBA | Wakala wa Majengo Zanzibar |
| ZBC | Zanzibar Broadcasting Corporation |
| ZECO | Shirika la Umeme Zanzibar |
| ZFDA | Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi |
| ZFDA | Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar |
| ZHC | Zanzibar Housing Corporation |
| ZIFA | Chuo cha Usimamizi wa Fedha |
| ZIPA | Zanzibar Investment Promotion Authority |
| ZITAS | Mfumo wa Usimamizi wa Mapato ya Kodi Zanzibar |
| ZMA | Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar |
| ZMUX | Zanzibar Multiplex |
| ZPC | Zanzibar Port Corporation |
| ZPDC | Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi |
| ZPPDA | Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar |
| ZPRA | Mamlaka ya Udhibiti, Utafiti na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar |
| ZRA | Mamlaka ya Mapato Zanzibar |
| ZRFB | Bodi ya Mfuko wa Barabara Zanzibar |
| ZSSF | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar |
| ZSTC | Zanzibar State Trading Corporation |
| ZSTDA | Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe |
| ZURA | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar |

# SHUKURANI

Napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa jitihada zake za mara kwa mara anazoendelea kuzichukuwa ikiwa ni pamoja na kuweka msisitizo na kutoa maelekezo katika kufanya maboresho juu ya dosari mbalimbali zinazobainishwa katika Ripoti za Ukaguzi wa Hesabu za Serikali pamoja na hatua anazoendelea kuzichukua kutokana na hoja za ukaguzi zinazoibuliwa kuhusu matumizi ya fedha pamoja na usimamizi wa rasilimali za Umma.

Vile vile napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Viongozi Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar akiwemo Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Othman Masoud Othman, Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Hemed Suleiman Abdulla, pamoja na watendaji mbali mbali wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mashirikiano yao wanayokupatia katika utekelezaji wa majukumu yako ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa lengo la kuwaletea maendeleo endelevu ya nchi yao.

Shukurani zangu za dhati ziende kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Zubeir Ali Maulid, Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa kujitolea kwa dhati kujadili na kutoa mapendekezo pamoja na kufuatilia hatua zinazochukuliwa na Serikali kutokana na dosari zilizojitokeza na kuibuliwa katika Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kusimamia uwajibikaji na utekelezaji wa majukumu ya watendaji katika sekta mbalimbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Aidha, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Katiba Sheria, Utumishi na Utawala Bora Mhe. Mwalimu Haroun Ali Suleiman kwa kuniunga mkono na kunipa nguvu katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kikatiba pamoja na jitihada zake anazozichukuwa katika kusimamia misingi ya utawala bora na kupelekea kuimarika kwa nidhamu na uwajibikaji.

Vile vile nitoe shukurani zangu za dhati kwa Bodi ya Utumishi ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kusimamia maadili na nidhamu ya wafanyakazi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kupelekea kuimarika kwa nidhamu na uwajibikaji katika utekelezaji wa majukumu ya kazi za ukaguzi.

Kwa namna ya kipekee niwashukuru wafanyakazi wote wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Afisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT), Tanzania Audit Corporation (TAC Associates), Price Waterhouse Coopers (PWC), pamoja na Ernst & Young (EY) kwa kufanya kazi za ukaguzi kwa mashirikiano na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na juhudi zao mbalimbali walizozichukuwa hadi kukamilika kwa ripoti hii.

Mwisho, niwashukuru wale wote waliochangia kwa namna moja au nyengine kuanzia kazi za ukaguzi, ufuatiliaji wa maeneo mbalimbali yaliyokaguliwa hadi kukamilika kwa ripoti hii ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Aidha, nitakuwa mchache wa shukurani kama sitatambua jukumu la vyombo mbali mbali vya habari kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuutambulisha Umma juu ya kazi zinazofanywa na Afisi ya Mdhibiti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambapo matokeo na mapendekezo ya kazi hizo huwasilishwa kwa jamii kupitia vyombo mbali mbali vya habari.

Natumia fursa hii, kuwasihi wafanyakazi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuendelea kuwa na moyo wa dhati katika kufanya kazi kwa bidii na kuongeza mashirikiano kwa ajili ya siku zijazo ili kuendelea kudumisha nidhamu ya Afisi ya Mdhibiti katika kutoa huduma za ukaguzi zenye ubora.

# DIBAJI



Ninafuraha kubwa ya kuwasilisha Ripoti ya Ukaguzi inayohusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Mashirika ya Umma na Taasisi zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023. Wasilisho hilo ni kwa mujibu wa Kifungu cha 112(5) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 pamoja na kifungu nambari 46(1) cha Sheria Nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023, ambapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kikatiba kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa zake za ukaguzi huo angalau mara moja kwa kila mwaka.

Taarifa hizo zitaelezea hali halisi za mapato na matumizi ya fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na utekelezaji wa Sheria mbali mbali zikiwemo Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016, Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 pamoja na sheria mbali mbali zilizopitishwa na Baraza la Wawakilishi na kutumiwa ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa Mujibu wa Mamlaka niliyonayo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ni jukumu langu la kutoa taarifa huru, zilizosahihi na zilizojitosheleza kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuhusiana na usimamizi wa fedha pamoja na matumizi sahihi ya rasilimali za Umma na hatimae taarifa hizo kuwasilishwa Baraza la Wawakilishi kwa hatua za utekelezaji.

Ripoti hii inajumuisha mambo muhimu yaliyobainika wakati wa ukaguzi wa taasisi za Serikali kwenye tathmini na ukaguzi wa taarifa za fedha pamoja na nyaraka husika, mifumo ya udhibiti wa ndani, taratibu na mchakato wa manunuzi na uzingatiaji wa Sheria na Kanuni mbali mbali. Kufuatia kukamilika kwa ukaguzi huo nimetoa hati za ukaguzi kwa kila taasisi kuhusiana na taarifa za fedha zilizoandaliwa kama zinaonesha hali halisi ya shughuli zilizofanywa kulingana na mfumo wa uandaaji wa taarifa za fedha.

Nilifanya ukaguzi huo kwa kuangalia mifumo ya udhibiti wa ndani, taratibu za ununuzi, utayarishaji wa taarifa za fedha na nyaraka zilizoambatishwa, kwa kuzingatia Sheria na Kanuni zilizowekwa pamoja na kuzingatia Viwango kubalifu vya Kitaifa na Kimataifa vya Taasisi za Juu za Hesabu za Serikali (ISSAIs) vinavyotolewa na Shirika la Kimataifa la Taasisi za Juu za Ukaguzi (INTOSAI) ambazo zinahusu ukaguzi wa Sekta za Umma.

Nimetoa Hati za Ukaguzi kwa kuzingatia Taarifa za Fedha nilizozikagua na kuzitolea ripoti ya ukaguzi kwa kila taasisi ambayo ilikaguliwa. Aidha, nilitoa barua za ukaguzi "Management Letters" zinazoonesha dosari zilizobainika kwa kila Shirika na Taasisi inayojitegemea iliyokaguliwa na mapendekezo ya kutekeleza ili kuboresha na kuondoa dosari zilizobainika kwa lengo la kutokujirejea kwa mara nyengine.

Ni matumaini yangu kwamba Baraza la Wawakilishi litaona taarifa zilizomo katika ripoti hii ni za umuhimu katika kuisimamia Serikali na kuongeza uwajibikaji katika matumizi ya fedha na usimamizi wa rasilimali za umma ili kuhakikisha kunakuwa na utoaji bora wa huduma kwa umma wa Wazanzibari ambao inawahudumia. Katika suala hili nitashukuru kama nitapokea maoni kutoka kwa watumiaji wa ripoti hii juu ya jinsi ya kuiboresha zaidi katika siku zijazo.

Kwa mara nyengine tena nichukue fursa hii kumshukuru na kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa jitihada zake anazoendelea kuzichukuwa katika kufuatilia Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa lengo la kusimamia na kuimarisha uwajibikaji katika matumizi ya fedha na usimamizi wa rasilimali za Umma hali inayopelekea kuimarika kwa utawala bora.



...............................................

**DKT. OTHMAN ABBAS ALI**

**MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI**

**ZANZIBAR**

# MUHTASARI

Ripoti hii imekusanya jumla ya sura nane (8) zenye kuelezea mambo mbalimbali yaliyobainika katika ukaguzi uliofanyika kwenye Mashirika ya Umma, Mamlaka, Wakala na Taasisi Zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Ukaguzi uliofanyika umebaini uwepo wa dosari mbalimbali ambapo dosari hizo zimewasilishwa kwenye uongozi wa Taasisi zilizokaguliwa kwa njia ya hoja za ukaguzi na kutolewa mapendekezo kwa lengo la kuimarisha dosari hizo, baadhi ya dosari ziliweza kufanyiwa kazi na Maafisa Masuuli wakati wa kipindi cha ukaguzi na kutolewa majibu kwa wakaguzi ili kuweza kujiridhisha juu ya uhalali wa dosari hizo. Aidha baadhi ya dosari zilizobainika hazikuweza kupatiwa majibu wakati wa ukaguzi na kupelekea kuingizwa katika Ripoti hii. Mambo yaliyobainika yamefafanuliwa katika sura tofauti zilizomo katika ripoti hii kama ifuatavyo:-

**Sura ya Kwanza:** Sura hii imekusanya taarifa za Utangulizi wa ripoti ikiwemo majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, upeo na madhumuni ya ukaguzi, njia zilizotumika katika ukaguzi. Vile vile imeeleza umuhimu wa kufanya ukaguzi pamoja na taarifa za Kamati za Baraza la Wawakilishi.

**Sura ya Pili:** Sura hii inaeleza kwa muhtasari mambo yaliyobainika katika ukaguzi wa hesabu pamoja na ufafanuzi wa Hati za Ukaguzi zilizotolewa kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ambapo miongoni mwa mambo yaliyobainika ni utoaji wa hati za ukaguzi, pamoja na utekelezaji wa mapendekeo ya hoja za ukaguzi kwa mwaka uliopita.

**Sura ya Tatu:** Sura hii inaeleza tathmini ya Mifumo wa udhibiti wa ndani pamoja na dosari za ujumla zilizobainika katika ukaguzi uliofanyika ambazo zimesababishwa na mapungufu ya mfumo wa udhibiti wa ndani.

**Sura ya Nne:** Sura hii inaeleza kwa kina kuhusiana na tathmini ya utendaji wa Mashirika 8 ya Umma kifaida au kihasara, pamoja na dosari za kiutendaji zilizobainika katika ukaguzi wa mwaka 2022/2023 ambapo matokeo na mapendekezo ya ukaguzi na ushauri yalibainishwa.

**Sura ya Tano:** Sura hii inaeleza kwa kina kuhusiana na taarifa za Mamlaka 12 za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kufanya uchambuzi unaohusiana na michango ya vyanzo vya mapato vya Mamlaka, utendaji wa mwaka kwa kila chanzo cha mapato pamoja na kubainisha dosari za kiutendaji zilizojitokeza wakati wa ukaguzi na kushauri njia za utatuzi wa dosari hizo.

**Sura ya Sita:** Sura hii imeeleza kwa kina kuhusu matokeo na mapendekezo ya ukaguzi uliofanyika kwa Taasisi 15 Wakala za za Serikali za Mitaa ambapo dosari mbalimbali za kiutendaji zimebainishwa pamoja na athari zake na kutolewa ushauri kwa uongozi wa Taasisi hizo.

**Sura ya Saba:** Sura hii imeeleza kwa kina kuhusu matokeo na mapendekezo ya ukaguzi uliofanyika kwa Taasisi 10 Zinazojitegemea za SMZ ambapo dosari mbali mbali za kiutendaji zimebainishwa pamoja na athari zake na kutolewa ushauri kwa uongozi wa Taasisi hizo.

**Sura ya Nane:** Sura hii imeeleza kwa kina kuhusu ukaguzi wa awali kwa Mafao ya Pencheni, Kiinua Mgongo na Malipo ya Fidia kwa watumishi wanaopata ajali kazini kutoka katika Taasisi mbalimbali za Serikali na Sekta binafsi ambapo dosari mbali mbali za kiutendaji zimebainishwa pamoja na athari zake na kutolewa ushauri kwa uongozi wa Taasisi hizo.

## Tathmini ya Mifumo ya Udhibiti wa Ndani

Ukaguzi ulitathmini mifumo ya udhibiti wa ndani ikiwemo udhibiti katika kitengo cha ukaguzi wa ndani, kamati ya ukaguzi pamoja na Bodi ya Zabuni. Kwa ujumla tathmini iliyofanyika imebainika kujitokeza kwa maboresho makubwa katika vitengo vya ukaguzi wa ndani, Kamati za Ukaguzi pamoja na Bodi za Zabuni kwa baadhi ya Taasisi kupiga hatua za mafanikio ingawa zipo baadhi ya Taasisi zimebainika kuwepo kwa dosari mbali mbali katika mfumo wa udhibiti wa ndani ambapo miongoni mwa dosari kubwa zilizobainika ni kwamba baadhi ya Taasisi zimeshindwa kushirikisha vitengo vya ukaguzi wa ndani na Kamati za Ukaguzi kupitia taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka za Taasisi hizo jambo ambalo lilipelekea hesabu zilizowasilishwa kuwa na dosari za kiutendaji na hatimae kurejeshwa ili ziweze kufanyiwa marekebisho katika hatua za awali za ukaguzi jambo ambalo lilipelekea kutokukamilika kwa kazi za ukaguzi kwa wakati uliopangwa.

## Tathmini katika ukusanyaji wa Mapato

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023, ukaguzi ulibaini hali ya ukusanyaji wa mapato katika Taasisi mbalimbali umeimarika ukilinganisha na ukusanyaji wa mapato kwa mwaka uliopita. Hata hivyo baadhi ya taasisi zimebainika kuwa na dosari za kiutendaji ambazo zinahitaji marekebisho ya haraka ili kunusuru kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma unaotokana na baadhi ya taasisi kukusanya mapato nje ya mfumo, mapato kutumika kabla ya kuwasilishwa benki, ucheleweshwaji wa mapato kuwasilishwa sehemu husika, upotevu wa vitabu vya kukusanyia mapato, kutokulingana kwa mapato halisi yanayokusanywa na yale yanayowasilishwa benki pamoja na kutokuoneshwa kwa mapato halisi yaliyokusanywa katika hesabu za mwisho wa mwaka.

Kutokana na dosari zilizobainishwa hapo juu zimepelekea baadhi ya Taasisi kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kulikosababishwa na baadhi ya watendaji kushikilia fedha za mapato mikononi pasi na kuziwasilisha sehemu husika na hatimae hesabu za taasisi hizo kutokuonesha sura halisi na sahihi.

### Tathmini ya Uendeshaji wa Mashirika

Ukaguzi umefanya tathmini ya uendeshaji wa Mashirika ya Umma ili kuweza kubaini dhana nzima ya uanzishwaji wa Mashirika hayo ikiwemo kugawa gawio kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Katika tathmini hiyo imebainika uwepo wa baadhi ya Mashirika kushindwa kujiendesha na kutegemea kwa kiwango kikubwa upokeaji wa ruzuku kutoka Serikalini ili yaweze kumudu gharama za uendeshaji wa shughuli walizojipangia. Mfano wa Mashirika hayo ni Shirika la Magazeti, Shirika la Utangazaji, Kampuni ya Uvuvi, na nyenginezo. Hata hivyo yapo baadhi ya Mashirika yamekuwa yakijiendesha kwa mtaji hasi na hatimae dhana ya uanzishwaji wa mashirika hayo kutokuonekana.

Pamoja na dosari hiyo yapo baadhi ya mashirika yalibainika kuimarika siku hadi siku na kupelekea kuongezeka kwa gawio wanalolichangia kutokana na faida kubwa inayopatikana kwa mwaka. Miongoni mwa Mashirika na Taasisi zinazojitegemea ambazo zinajiendesha kifaida ni kama PBZ, ZSSF, ZECO, ZRA na mengineyo.

### Tathmini ya Usimamizi wa Matumizi

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023 ukaguzi umebaini kuimarika kwa nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa taasisi mbalimbali na kupelekea kuongezeka kwa hati zinazoridhisha na kuleta faraja na nidhamu juu ya usimamizi wa matumizi ya fedha za umma.

Hata hivyo zipo baadhi ya taasisi zimebainika kuwa na mapungufu mbalimbali katika nidhamu ya usimamizi wa matumizi na kupelekea kutokuzingatia matakwa ya Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016. Miongoni mwa dosari kubwa zilizobainika katika nidhamu ya matumizi ni kufanyika kwa malipo kwa fedha taslim, dosari katika uzuwiaji wa kodi, ucheleweshwaji wa mapato ya Serikali kuwasilishwa benki kwa wakati pamoja na kutokuzingatia maelekezo ya Serikali kuhusiana na kudai stakabadhi za kielektroniki wakati wa ufanyaji wa malipo.

### Tathmini ya Usimamizi wa Manunuzi

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni 2023, ukaguzi ulibaini uwepo wa maboresho katika Mashirika na Taasisi mbali mbali zilizofanya manunuzi kwa kufanya manunuzi kupitia mfumo wa manunuzi pamoja na kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zinazohusiana na manunuzi hayo, ingawa zipo baadhi ya Taasisi zilibainika kutokuzingatia Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya 2016 pamoja na Kanuni zake wakati wa kufanya manunuzi.

Aidha, baadhi ya taasisi zimebainika kufanya manunuzi bila ya kuzingatia ushindani wa bei, kufanya manunuzi kwa kutumia rasimu za mikataba, kufanya manunuzi bila ya kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu kupitia rasimu za mkataba walizoziwasilisha, kutokuambatishwa kwa nyaraka muhimu za manunuzi katika hati za malipo, kufanya manunuzi kinyume na mpango wa manunuzi, kutokuwasilishwa kwa mpango wa manunuzi kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali jambo ambalo limepelekea baadhi ya Taasisi kufanya manunuzi nje ya Mfumo wa manunuzi au kufanya manunuzi yaliyo na gharama kubwa zaidi kuliko uhalisia wa bajeti iliyowekwa kwenye mpango wa manunuzi.

### Tathmini katika Usimamizi wa Mikataba

Katika mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023 ukaguzi ulibaini mapungufu mbali mbali yanayotokana na ukiukwaji wa Sheria na taratibu za manunuzi unaotokana na baadhi ya Taasisi kushindwa kuwasilisha rasimu za mikataba yao Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa lengo la kufanyiwa mapitio na kupatiwa ushauri wa kisheria juu ya namna bora ya kufanya maboresho ya dosari zilizobainika katika rasimu za mikataba hiyo.

Hata hivyo zipo baadhi ya taasisi zimebainika kutokutekeleza maagizo na mashauri yanayotolewa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuhusiana na maboresho ya rasimu za mikataba na hatimae kufanya manunuzi na kuingia katika makubaliano ya kimkataba bila ya uwepo wa mikataba yenye tija na maslahi kwa Serikali na hatimae kupelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma kunakotokana na kutokutekelezwa kwa maagizo ya mikataba inayopitiwa na Mwanasheria Mkuu.

### Tathmini ya Hati za Ukaguzi

Kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023, ukaguzi ulifanyika kwa taasisi mbali mbali kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa. Kutokana na kuzingatiwa kwa vigezo vya ufungaji wa hesabu kwa taasisi za umma kumepelekea kuimarika kwa Hati za ukaguzi zinazoridhisha kwa taasisi mbali mbali zilizokaguliwa. Hata hivyo zipo baadhi ya Taasisi ziliendelea kuwa na dosari kubwa za ufungaji wa hesabu zao na kupelekea kulazimika kufanyiwa marekebisho kwa hesabu hizo

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, nilikamilisha ukaguzi wa Taasisi **45**. Kati ya Taasisi hizo jumla ya Mashirika **8**, Mamlaka **12 ,** Wakala **15** na Taasisi zinazojitegemea **10** za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kutoa hati za ukaguzi kwa Taasisi **45**. Kati ya hati hizo zilizotolewa hati **39** ni hati zinazoridhisha sawa na asilimia **86.67** ya hati zilizotolewa, na hati **6** ni hati zenye shaka sawa na asilimia **13.33** ya hati zilizotolewa na sikuwa na hati ya kushindwa kutoa maoni.

Nichukuwe fursa hii kuwapongeza Maafisa Masuuli kutokana na jitihada walizozichukuwa katika kusimamia ufungaji wa hesabu uliozingatia vigezo vilivyowekwa kitaifa na kimataifa pamoja na kuwajengea uwezo watendaji wao katika utekelezaji wa majukumu yao.

## Tathmini ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi kwa mwaka uliopita

Tathmini iliyofanyika kwenye hali ya utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi ya Mwaka Uliopita nimebaini jumla ya mapendekezo 760 yalitolewa kwa taasisi 44 zilizokaguliwa na kuwasilishiwa ripoti za ukaguzi. Kati ya mapendekezo hayo jumla ya mapendekezo 552 yaliweza kutekelezwa na kuondolewa ambayo ni sawa na asilimia 72.63, mapendekezo 87 yapo katika hatua ya utekelezaji sawa na asilimia 11.45 Hata hivyo, mapendekezo 56 bado hayajatekelezwa ambayo ni sawa na asilimia 7.37 na mapendekezo 41 yamejirudia sawa na asilimia 5.39, vile vile mapendekezo 24 yamepitwa na wakati sawa na asilimia 3.16.

Ili kusimamia vyema rasilimali za umma, napendekeza kuimarishwe udhibiti wa ndani kwa kuhakikisha Sheria na taratibu zilizowekwa zinafuatwa kikamilifu. Pia, kuhakikisha kuwa mifumo ya utawala inakuwepo na inafanya kazi ipasavyo.

# SURA YA KWANZA



# 1.0 UTANGULIZI

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibu wa kukagua hesabu zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ukaguzi huo unafanyika kwa mujibu wa Kifungu nambari 112 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984. Ukaguzi wa Hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar unajumuisha hesabu zote za Serikali kuu, Mashirika ya Umma na Taasisi zinazojitegemea, Serikali za Mitaa, Mamlaka na Taasisi mbali mbali pamoja na Miradi mbali mbali ya maendeleo na baadae kutoa taarifa ya ukaguzi wa hesabu hizo kwa mujibu wa masharti ya Katiba ya Zanzibar.

Kutokana na mamlaka ya kikatiba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibu wa kuhakikisha kwamba fedha zote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar matumizi yake yameidhinishwa kisheria ambapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibu wa kuidhinisha matumizi kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kufanya Ukaguzi wa hesabu hizo.

## 1.1 Majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

Kwa mujibu wa kifungu nambari 112 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kukagua hesabu za Taasisi za Serikali na baadae kutoa taarifa zake za ukaguzi huo angalau mara moja kila mwaka. Taarifa hizo zitaelezea hali halisi za mapato na matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na utekelezaji wa Sheria mbali mbali zikiwemo Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016, Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 pamoja na Sheria mbalimbali zilizopitishwa na Baraza la Wawakilishi na kutumiwa ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Kwa mujibu wa Kifungu nambari 112 (3) cha Katiba ya Zanzibar ya 1984, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu anawajibika kufanya yafuatayo:-

a) Kuhakikisha kwamba fedha zote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, matumizi yake yameidhinishwa kisheria na iwapo atatosheka kwamba masharti hayo yatatekelezwa ipasavyo basi ataidhinisha fedha hizo zitolewe.

b) Kuhakikisha kwamba fedha zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa yanatokana na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au fedha ambazo matumizi yake yameidhinishwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi, na ambazo zimetumika kwa ajili ya shughuli zilizohusika na matumizi ya fedha hizo na kwamba matumzi hayo yamefanywa kwa kufuata idhini iliyotolewa kuhusu matumizi hayo; na

c) Angalau mara moja kwa kila mwaka kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu zinazosimamiwa na watumishi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, hesabu za Mahkama zote za Zanzibar, hesabu za Tume au vyombo vyengine vilivyoanzishwa na Katiba hii na hesabu zozote zinazohusika na Baraza la Wawakilishi.

Ukaguzi wa hesabu umefanywa kwa kuzingatia miongozo na vigezo mbali mbali vya ukaguzi ili kukidhi matarajio ya wadau wetu na wananchi kwa ujumla. Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaendelea kufanya uchambuzi wa njia bora zaidi kwa kufanya ukaguzi utakaoleta tija na kuongeza wigo na maeneo yanayokaguliwa kwa lengo la kuimarisha utendaji na uwajibikaji katika sekta za Umma.

## 1.2 Upeo na Madhumuni ya Ripoti ya Ukaguzi

Ripoti hii imekusanya taarifa za ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yakiwemo Mashirika na Taasisi zinazojitegemea kwa kuzingatia taarifa za mapato na matumizi ya kawaida, matumizi ya maendeleo pamoja na michango mbali mbali kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2023.

Ukaguzi ulifanyika kwa mujibu wa viwango vya kitaifa na kimataifa vya ukaguzi na kujiridhisha kwamba taarifa zitakazotolewa zitaonyesha sura halisi ili kutoa uhakika kwamba taarifa za mapato na matumizi zimefuata Sheria, Kanuni na taratibu zilizopo. Taarifa za hesabu zilizokaguliwa zilijumuisha hesabu za mwisho wa mwaka pamoja na taarifa mbalimbali zinazohusiana na hesabu hizo.

Mabadiliko ya mifumo ya ukaguzi na uhasibu yanayotokea kwa mujibu wa viwango vya kitaifa na kimataifa yamepelekea kuwepo na mafanikio makubwa katika utendaji na uwajibikaji kwenye sekta za Umma katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya rasilimali za umma. Mafanikio hayo yametokana na kuimarika kwa mfumo wa fedha pamoja na utekelezaji wa sheria mbalimbali zikiwemo Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016, Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 pamoja na sheria mbalimbali zilizopitishwa na Baraza la Wawakilishi na kutumiwa ndani ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kupelekea kuimarika kwa uwazi na uwajibikaji katika taasisi za Umma pamoja na utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo na kuleta tija kwa wananchi na kufanikisha lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha dhana nzima ya utawala bora.

## 1.3 Njia zilizotumika Katika Ukaguzi

Katika kufanya ukaguzi wa hesabu za Serikali mbinu na njia mbalimbali za ukaguzi zilitumika ikiwemo taratibu za ukaguzi zifuatazo: -

i. Kutoa barua za awali za maandalizi ya ukaguzi (Engagement Letter) kwa Taasisi inayokaguliwa.

ii. Kuangalia viashiria vya maeneo hatarishi katika taasisi zinazokaguliwa kwa lengo la kupata uelewa wa mazingira ya taasisi hiyo ikiwemo mfumo wa udhibiti wa ndani na kubaini viashiria vitakavyoathiri udhibiti wa ndani pamoja na utendaji wa taasisi.

iii. Kuandaa mikakati ya ukaguzi kuanzia mpango wa awali hadi mpango mkuu wa ukaguzi (Pre Planning, Strategic Planing and detailed Planning) itakayozingatia muelekeo na upeo wa ukaguzi ambapo utaonyesha dira na dhamira nzima ya ukaguzi huo.

iv. Kufanya kikao cha kuanza kazi za ukaguzi (Entrance Meeting) pamoja na uongozi wa Taasisi zinazokaguliwa.

v. Kupitia na kuhakiki nyaraka mbalimbali pamoja na kupata taarifa kutoka kwa wahusika ili kupata uelewa wa kazi za Taasisi zinazokaguliwa.

vi. Kutumia njia na mbinu mbalimbali za ukaguzi kama ilivyoainishwa kwenye muongozo wa ukaguzi (Compliance Audit Manual & Financial Audit Manual).

vii. Kufanya kikao cha kumaliza ukaguzi (Exit Meeting) na uongozi wa Taasisi inayokaguliwa baada ya kumaliza ukaguzi ambapo katika kikao hicho wakaguzi na uongozi wa taasisi hupitia kwa pamoja hoja zilizojitokeza wakati wa ukaguzi.

viii. Kutoa ripoti ya ukaguzi ya awali (Management letter) kwa uongozi wa taasisi inayokaguliwa itakayoainisha hoja za ukaguzi pamoja na mambo mbalimbali yaliyobainika wakati wa ukaguzi na kutoa nafasi kwa uongozi kutoa majibu na vielelezo kuhusiana na ripoti hiyo kwa muda unaotakiwa kwa mujibu wa sheria.

ix. Kufuatilia majibu ya hoja za ukaguzi yaliyotolewa katika ripoti ya ukaguzi ya awali ili kuweza kujiridhisha na majibu ya hoja hizo.

x. Kutoa Ripoti Kuu ya Mwaka kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

## 1.4 Umuhimu wa ukaguzi katika kuimarisha Utawala Bora

Lengo kuu la kufanya ukaguzi ni kuhakikisha kwamba fedha inayoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa sheria inatumika ipasavyo na kwa malengo yaliyokusudiwa kwa kuleta ufanisi na tija kwa maslahi ya wananchi na taifa kwa ujumla. Aidha, ukaguzi wa hesabu unalenga kuimarisha uwajibikaji wa matumizi ya rasilimali za umma na kupelekea kuimarika kwa dhana nzima ya Utawala Bora.

Kuimarika kwa utendaji wa kazi za ukaguzi kunapelekea kuongezeka na kuimarika kwa uwazi na uwajibikaji katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha na rasilimali za umma na kuleta tija na ufanisi na kufanikisha kutekeleza malengo yaliyopangwa na Serikali kwa wakati uliopangwa. Aidha kuimarika kwa utendaji wa kazi za ukaguzi kunapelekea kuimarika kwa hali ya uchumi wa nchi na kufanikiwa kuimarika kwa hali za wananchi kwa jumla.

Katika kufanikisha malengo ya Serikali ya kuimarisha utawala bora nchini, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imejipanga kutekeleza majukumu yake ya kikatiba kwa kuongeza ufanisi wa kazi pamoja na kuendelea na jitihada zake za kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kuwapatia mafunzo na mbinu mbali mbali za ukaguzi ili kwenda sambamba na mabadiliko ya mifumo ya uhasibu na ukaguzi pamoja na mabadiliko ya kasi ya teknolojia duniani katika masuala ya udhibiti na ukaguzi wa hesabu za Serikali.

## 1.5 Kamati za Baraza la Wawakilishi

Katika kuleta ufanisi na kufikia malengo ya Serikali iliyojipangia, Baraza la Wawakilishi ni nguzo imara katika kuimarisha uwajibikaji na kusimamia rasilimali za umma kuweza kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa na kuleta tija kwa jamii. Aidha, Kamati za Baraza la Wawakilishi zinatoa mchango mkubwa katika kujenga na kusimamia misingi ya utawala bora na uwajibikaji wa matumizi ya fedha na rasilimali za Umma.

Kwa kuzingatia majukumu na umuhimu wa Kamati za Baraza la Wawakilishi, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imekuwa ikishirikiana na Kamati hizo katika kufuatilia utekelezaji wa bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na kuhakikisha kwamba taasisi za Serikali zinatekeleza malengo waliyojipangia kama yalivyoainishwa katika Bajeti zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi.

Hata hivyo upeo wa mahusiano wa Taasisi za ukaguzi duniani (SAIs) na Mabunge (Baraza la Wawakilishi) unatofautiana baina ya nchi na nchi duniani ambapo kuna baadhi ya nchi taasisi za ukaguzi huwa ni sehemu ya Bunge (Legislative) na baadhi huwa chini ya utawala (Executive) na baadhi ya nchi nyengine Taaisisi za ukaguzi huwa haziko kokote yaani (si legislative wala Executive). Kwa hivyo taasisi za ukaguzi zina jukumu la kuzijengea uwezo Kamati za Ukaguzi za Bunge (Baraza la Wawakilishi) kwa lengo la kuzisimamia ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kutoa ushauri na mapendekezo yao kwa taasisi za umma pamoja na Serikali.

Kutokana na utendaji kazi wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi (PAC) matokeo ya ukaguzi yanayotolewa pamoja na suala zima la kuidhinishwa bajeti ya taasisi za ukaguzi yamewekwa chini ya mamlaka ya Kamati hizo kwa mujibu wa kifungu nambari 35(1)(2) cha Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kwa lengo la kuimarisha ufanisi, uwazi na uwajibikaji.

# SURA YA PILI



# 2.0 MUHTASARI WA MAMBO YALIYOBAINIKA PAMOJA NA UFAFANUZI WA HATI ZA UKAGUZI

Sura hii inaelezea muhtasari wa mambo yaliyobainika katika ukaguzi wa hesabu pamoja na ufafanuzi wa Hati za Ukaguzi zilizotolewa kwa Mashirika na Taasisi zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

## 2.1 Muhtasari wa mambo yaliyobainika katika ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilibainika uwepo wa dosari mbali mbali za kiutendaji ambazo hadi ukaguzi unakamilika hazikupatiwa majibu au majibu yake hayakuridhisha hali iliyopelekea kujitokeza kwa hoja za ukaguzi.

### 2.1.1 Dosari za kiutendaji zilizobainika katika Ukaguzi

Katika ukaguzi wa hesabu wa mwaka wa fedha 2022/2023 kulijitokeza dosari za kiutendaji ambazo zimepelekea kuathiri utendaji wa taasisi zilizokaguliwa pamoja na utekelezaji wa sheria mbalimbali. Dosari hizo ni kama zifuatazo:-

a) Mfumo wa udhibiti wa Ndani.

b) Utekelezaji wa Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 na Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016.

c) Usimamizi wa matumizi.

d) Mifumo ya ukusanyaji wa mapato.

e) Usimamizi wa mikataba.

**a) Mfumo wa udhibiti wa ndani**

Mfumo wa udhibiti wa ndani ni taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria za usimamizi wa fedha ambazo zinahitajika kuwa imara ili kuweza kusaidia taasisi za umma kuweza kufanya kazi zake kwa weledi na kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria.

Ukaguzi ulibaini udhaifu katika mfumo wa udhibiti wa ndani kwa Taasisi tano (5) kati ya Taasisi arubaini na tano (45) zilizokaguliwa miongoni mwa Taasisi arubaini na tisa (49) zilizowasilisha taarifa za hesabu. Vile vile jumla ya Taasisi mbili (2) zilibainika kuwa na madhaifu katika Kamati zao za Ukaguzi (Audit Committee) na Taasisi tatu (3) zilibainika kuwa na mapungufu katika Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani (Internal Audit Unit).

Hata hivyo ukaguzi unapongeza jitihada zilizochukuliwa na Maafisa Masuuli kuweza kuimarisha vitengo vya ndani kwa kuvijengea uwezo wa kutekeleza majukumu yao ikiwemo kufanya ukaguzi wa awali pamoja na mapitio ya hoja zinazotolewa na Mkaguzi wa Ndani pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali jambo ambalo limepelekea kuimarika kwa hati za ukaguzi ukilinganisha na mwaka uliopita wa ukaguzi.

### b) Utekelezaji wa Sheria Nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 pamoja na Sheria Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016

Katika tathmini iliyofanywa ya utekelezaji wa sheria mbali mbali kwa Taasisi za umma imebainika Maafisa Masuuli wamechukuwa jitihada za kusimamia utekelezaji wa sheria, kanuni na miongozo mbali mbali iliyotolewa katika usimamizi wa fedha na rasilimali za umma pamoja na kuwapatia mafunzo watendaji katika utekelezaji wa majukumu yao jambo ambalo limepelekea kuimarika kwa hati za ukaguzi zilizotolewa.

Aidha, pamoja na uwepo wa mafanikio makubwa zipo baadhi ya Taasisi zilibainika kukengeuka kutekeleza na kusimamia kwa sheria, kanuni na miongozo mbali mbali iliyotolewa katika usimamizi wa fedha na rasilimali za uma na kupelekea baadhi ya Taasisi kuwa na dosari kubwa za kiutendaji.

### c) Usimamizi wa Matumizi

Kutokana na tathmini iliyofanyika juu ya usimamizi wa matumizi imebainika uwepo wa marekebisho makubwa yaliyofanyika kutokana na mapendekezo yaliyotolewa katika Ripoti ya Ukaguzi ya mwaka wa fedha 2022/2023 na hatimae dosari mbali mbali zilizobainishwa ziliweza kufanyiwa kazi ingawa zipo baadhi ya dosari hazikuweza kufanyiwa kazi kikamilifu kutokana na baadhi ya Taasisi kutokuwa na mfumo mzuri wa matumizi.

Kutokuwepo kwa mfumo mzuri wa usimamizi wa matumizi kunaweza kupelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma, ukaguzi unachukuwa fursa ya kuzinasihi baadhi ya Taasisi zilizobainishwa katika ripoti hii kuwa na usimamizi usioridhisha wa matumizi kuchukuwa jitihada za makusudi za kuhakikisha wanayafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa katika barua ya dosari za ukaguzi zilizowasilishwa katika uongozi wakati wa kikao cha kukamilika kazi za kaguzi (exit meeting).

### d) Mifumo ya ukusanyaji wa Mapato

Kutokana na tathmini iliyofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika Mifumo ya Ukusanyaji wa Mapato imeimarishwa na kusimamiwa vizuri jambo ambalo limepelekea kuongezeka kwa ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ukilinganisha na mwaka wa fedha 2022/2023.

Aidha, imebainika uwepo wa baadhi ya Taasisi kuendelea kukusanya mapato nje ya mfumo na kupelekea baadhi ya mapato kutokuwasilishwa kwa wakati, kutokujuulikana mapato sahihi yaliyokusanywa au kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa mapato ya umma unaosababishwa na ukiukwaji wa Sheria, taratibu na miongozo iliyowekwa.

### e) Usimamizi wa Mikataba

Ukaguzi umebaini dosari katika usimamizi wa mikataba kwa baadhi ya Taasisi za Serikali ikiwemo kukiuka vipengele muhimu vilivyoainishwa katika mikataba hali iliyopelekea kutokufikiwa kwa malengo yaliyopangwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kuwepo kwa ukiukwaji wa vipengele hivyo kumepelekea kwa baadhi ya miradi kutokamilika kwa wakati na kutofikia malengo yaliyokusudiwa.

Aidha, kujitokeza kwa baadhi ya Taasisi kutelekeza miradi ya maendeleo kwa kutumia rasimu ya Mkataba jambo ambalo limepelekea kuitia hasara Serikali kwa kufanya malipo ya ziada kutokana na kutokuzingatia masharti ya jumla ya mikataba au kushindwa kutoza tozo ya fidia kulikosababishwa na baadhi ya wazabuni kushindwa kukamilisha kazi kwa wakati, kutokuwasilishwa kwa hati ya dhamana ya utendaji kazi pamoja na baadhi ya Taasisi kushindwa kutekeleza ushauri wa kitaalamu uliotolewa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu uliowataka kufanya marekebisho ya rasimu za mikataba kabla ya utekelezaji.

## 2.2 Uwasilishaji wa Hesabu za mwisho wa mwaka kwa Mashirika na Taasisi zinazojitegemea

Kwa mujibu wa kifungu nambari 119(1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016, Mashirika na Taasisi zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinatakiwa zitayarishe na ziwasilishe kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu za mwisho wa mwaka ndani ya miezi mitatu baada ya kumalizika mwaka wa fedha ambapo hesabu hizo zitajumuisha taarifa za mapato na matumizi ya Taasisi hizo.

Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kwamba uwasilishaji wa taarifa za hesabu za Serikali kwa baadhi ya Taasisi umeimarika na kupelekea hesabu hizo kuwasilishwa kwa wakati na kwa mujibu wa Sheria. Hali ya uwasilishaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka ni kama inavyoonekana hapo chini:-

**Jadweli Nambari 1: Mashirika na Taasisi zinazojitegemea zilizowasilisha Hesabu za Mwisho wa Mwaka**

| Nam. | Fungu | Shirika/Taasisi | Tarehe iliyowasilishwa kwa ukaguzi | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 | 2022/2023 |
| | | **Mashirika ya Serikali** | | | | |
| 1. | Linajitegemea | Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) | 30/09/2020 | 29/09/2021 | 27/09/2022 | 29/09/2023 |
| 2. | Linajitegemea | Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC) | 29/09/2020 | 30/09/2021 | 29/09/2022 | 29/09/2023 |
| 3. | Linajitegemea | Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) | 30/09/2020 | 30/09/2021 | 28/09/2022 | 29/09/2023 |
| 4. | Ruzuku | Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar | 30/09/2020 | 01/10/2021 | 28/09/2022 | 29/09/2023 |
| 5. | Ruzuku | Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) | 30/09/2020 | 29/09/2021 | 29/09/2022 | 29/09/2023 |
| 6. | Linajitegemea | Shirika la Nyumba Zanzibar (ZHC) | 28/09/2020 | 30/09/2021 | 29/09/2022 | 29/09/2023 |
| 7. | Ruzuku | Shirika la Huduma za Maktaba | 30/09/2020 | 30/09/2021 | 30/09/2022 | 22/09/2023 |
| 8. | Ruzuku | Shirika la Magazeti | 30/09/2020 | 02/10/2021 | 29/09/2022 | 29/09/2023 |
| | | **Mamlaka za Serikali** | | | | |
| 9. | Inajitegemea | Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) | 30/09/2020 | 24/09/2021 | 29/09/2022 | 29/09/2023 |
| 10. | Inajitegemea | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) | 30/09/2020 | 30/09/2021 | 30/09/2022 | 29/09/2023 |
| 11. | Inajitegemea | Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA) | 30/09/2020 | 29/09/2021 | 28/09/2022 | 29/09/2023 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mamlaka za Serikali** | | | | | | |
| 12. | Inajitegemea | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA) | 17/09/2020 | 27/09/2021 | 28/09/2022 | 29/09/2023 |
| 13. | Ruzuku | Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) | 30/09/2020 | 30/09/2021 | 30/09/2022 | 29/09/2023 |
| 14. | Ruzuku | Mamlaka ya Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA) | 28/09/2020 | 27/09/2021 | 28/09/2022 | 29/09/2023 |
| 15. | Ruzuku | Mamlaka ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar (ZPPDA) | 29/09/2020 | 29/09/2021 | 29/09/2022 | 29/09/2023 |
| 16. | Ruzuku | Mamlaka ya Udhibiti Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asili Zanzibar (ZPRA) | 22/09/2020 | 27/09/2021 | 21/10/2022 | 29/09/2023 |
| 17. | Ruzuku | Mamlaka ya Mafunzo ya Vyuo ya Amali | 30/09/2020 | 29/09/2021 | 27/09/2022 | 22/09/2023 |
| 18. | Ruzuku | Mamlaka ya Kusimamia Mazingira | - | - | - | 26/09/2023 |
| 19. | Ruzuku | Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe | 26/08/2020 | 30/09/2021 | 30/09/2022 | 25/09/2023 |
| 20. | Ruzuku | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar | 27/09/2020 | 29/09/2021 | 29/09/2022 | 27/09/2023 |
| 21. | Ruzuku | Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani | - | 03/09/2021 | 26/09/2022 | 26/09/2023 |
| 22. | Ruzuku | Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya | - | - | - | 29/09/2023 |
| **Wakala za Serikali** | | | | | | |
| 23. | Ruzuku | Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar (ZAGPA) | - | - | 29/09/2022 | 27/09/2023 |
| 24. | Ruzuku | Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA | - | 27/09/2022 | 30/09/2022 | 29/09/2023 |
| 25. | Ruzuku | Wakala wa Serikali Mtandao | - | - | - | 27/09/2023 |
| 26. | Ruzuku | Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii | 26/09/2020 | 30/09/2021 | 30/09/2022 | 29/09/2023 |
| 27. | Ruzuku | Wakala wa Serikali wa huduma za Matrekta na Zana za Kilimo | - | 07/09/2021 | 30/09/2022 | 27/09/2023 |
| 28. | Ruzuku | Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi (ZFDA) | - | 29/09/2021 | 30/09/2022 | 26/09/2023 |
| 29. | Ruzuku | Wakala wa Majengo Zanzibar | - | 08/09/2021 | 28/09/2022 | 29/09/2023 |
| 30. | Ruzuku | Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu | - | 17/09/2021 | 28/09/2022 | 27/09/2023 |
| 31. | Ruzuku | Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar | - | 24/09/2021 | 29/09/2022 | 29/09/2023 |
| 32. | Ruzuku | Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar | - | 24/09/2021 | 07/09/2022 | 07/09/2023 |
| 33. | Ruzuku | Wakala wa Vipimo | - | - | - | 29/09/2023 |
| 34. | Ruzuku | Wakala wa Ulinzi JKU | - | - | - | **02/10/2023** |
| 35. | Ruzuku | Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na Vya Kati (SMIDA) | - | - | - | 26/08/2023 |
| 36. | Ruzuku | Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | - | - | 14/11/2022 | 29/09/2023 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 37. | Ruzuku | Wakala wa Barabara Zanzibar | - | - | - | **06/10/2023** |
| | | **Taasisi Zinazojitegemea** | | | | |
| 38. | Inajitegemea | Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) | 06/01/2020 | 08/12/2021 | - | 16/01/2023 |
| 39. | PBZ Hisa | Mufindi Commercial Bank (MuCoBa) | - | - | - | 16/01/2023 |
| 40. | Unajitegemea | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) | 30/09/2020 | 28/09/2021 | 28/09/2022 | 22/09/2023 |
| 41. | Ruzuku | Mfuko wa Barabara Zanzibar | 29/09/2020 | 03/09/2021 | 27/09/2022 | 29/09/2023 |
| 42. | Inajitegemea | Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) | 30/09/2020 | 30/09/2021 | 30/09/2022 | 29/09/2023 |
| 43. | Ruzuku | Kampuni ya Ujenzi | - | 30/09/2021 | 30/09/2022 | **20/12/2023** |
| 44. | Ruzuku | Kampuni ya Uunganishaji wa Maudhui (ZMUX) | - | 29/09/2021 | 30/09/2022 | 29/09/2023 |
| 45. | Ruzuku | Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi (ZPDC) | - | 29/09/2021 | 30/09/2022 | 29/09/2023 |
| 46. | Ruzuku | Chuo cha Utawala wa Umma (IPA) | 30/09/2020 | 29/09/2021 | 30/09/2022 | 29/09/2023 |
| 47. | Ruzuku | Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia (KIST) | 30/09/2020 | 30/09/2021 | 30/09/2022 | 29/09/2023 |
| 48. | Ruzuku | Chuo cha Kiislamu Zanzibar | - | 29/09/2021 | 30/09/2022 | 29/09/2023 |
| 49. | Ruzuku | Skuli ya Sheria Zanzibar | - | - | - | 26/09/2023 |

## 2.3 Hati za Ukaguzi

Hati ya ukaguzi hutolewa kwa kuzingatia tathmini ya hitimisho inayotokana na ushahidi wa ukaguzi uliopatikana kuhusiana na iwapo taarifa za fedha kwa ujumla wake zimetayarishwa kwa njia zote muhimu na kwa mujibu wa mfumo unaotumika wa kuripoti taarifa za fedha, kama vile Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu (IFRS) au Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu Katika Taasisi za Umma (IPSAS). Hati ya ukaguzi hutolewa kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi namba 1200. Hili linafanikiwa kwa kuandaa ukaguzi kwa njia ambayo itamuwezesha mkaguzi kupata uhakika wa kuridhisha kulingana na tathmini ya matokeo dhidi ya kipimo kilichowekwa. Pia, maoni ya ukaguzi yanajumuisha mahitimisho juu ya uzingatiaji wa Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma na Kanuni zake, na Sheria ya bajeti na Kanuni zake.

### 2.3.1 Aina ya Hati za Ukaguzi

Kuna aina nne za hati za ukaguzi ambazo ni:-

**Hati Inayoridhisha:** Hati hii hutolewa wakati Mkaguzi anaporidhika kuwa hesabu zimetayarishwa kwa usahihi na kwa kuzingatia Viwango na mfumo unaokubalika wa utoaji wa taarifa za fedha.

**Hati Yenye Shaka**: Hati hii hutolewa pale hesabu zinapoonekana zimeandaliwa kwa usahihi isipokuwa baada ya kupata vielelezo vya kutosha, mkaguzi anahitimisha kuwa makosa kwenye hesabu ama likiwa moja au yakiwekwa pamoja yana atahari, lakini hayaathiri maeneo yote katika taarifa za fedha. Mkaguzi anaposhindwa kupata uthibitisho wa kutosha kumwezesha kuhitimisha ukaguzi lakini athari zinazotokana na kukosa uthibitisho huo kwa ujumla wake haziathiri maeneo yote ya taarifa za fedha.

**Hati Mbaya**: Hati hii hutolewa pale Mkaguzi anapokuwa amepata vielelezo vya kutosha kuonesha kuwa taarifa za fedha kwa kiasi kikubwa zinamakosa; na zikiangaliwa kwa ujumla wake zinakuwa hazikufuata Viwango vinavyokubalika vya uandaaji wa taarifa za fedha.

**Kushindwa kutoa Hati**: Hati hii hutolewa pale Mkaguzi anaposhindwa kupata uthibitisho wa kutosha kuhusu taarifa za fedha ambazo ni msingi wa kutoa hati, hivyo Mkaguzi huhitimisha kuwa athari za makosa yanayoweza kuwa kwenye hesabu ambayo hayakubainika yanaweza kuwa makubwa na yenye athari kwa sehemu zote za hesabu hizo. Mkaguzi huwa anashindwa kutoa hati katika mazingira ya nadra sana yaliyohusisha mashaka; hivyo huhitimisha kuwa, licha ya kupata ushahidi wa kutosha wa ukaguzi katika maeneo yenye shaka kwenye taarifa za fedha, haitawezekana kutoa hati kuhusu taarifa za fedha kwa kuwa kuna viashiria vya mashaka vyenye madhara kwenye taarifa za fedha.

### 2.3.2 Aya yenye masuala ya Msisitizo kwenye ripoti za Mkaguzi

Kama nitaona kuna umuhimu wa kuwaarifu watumiaji wa taarifa za fedha kuhusu suala ambalo limeoneshwa au kuainishwa kwenye taarifa za fedha,kwa mtazamo wangu suala hilo ni muhimu na lamsingi kwa ajili ya kuleta uwelewa wa taarifa hizo, nitaiweka aya hii kwenye taarifa za ukaguzi. Aya hii itawekwa pale tu ambapo nimepata vielelezo vya kutosha kuwa taarifa za fedha hazijakosewa; na inapaswa itokane na suala ambalo limeoneshwa au kuainishwa kwenye taarifa za fedha.

### 2.3.3 Masuala Muhimu ya Ukaguzi

Aya ya masuala muhimu ya ukaguzi hutoa taarifa za ziada kwa watumiaji wa taarifa za fedha ili kuwasaidia kuelewa masuala ya kitaalamu ya ukaguzi ambayo yalikuwa na umuhimu mkubwa katika ukaguzi wa taarifa za fedha za taasisi husika. Uwasilishaji wa masuala muhimu ya ukaguzi huongeza thamani na uwazi kwenye taarifa za ukaguzi.

### 2.3.4 Msingi wa Hati za Ukaguzi

Ili kufikia kwenye hati zilizotolewa, ukaguzi ulizingatia hali halisi ya matokeo ya ukaguzi kwa kila taasisi iliyokaguliwa. Ukaguzi huo ulifanyika kulingana na matakwa ya Viwango vya Kimataifa vya Taasisi Kuu za Ukaguzi kwenye Sekta za Umma (ISSAIs). Viwango hivyo vinanitaka kuandaa mpango wa ukaguzi, kufanya ukaguzi, na kutoa ripoti ya matokeo ya ukaguzi huo. Pia, vinanitaka kufuata maadili ya ukaguzi ili kuhakikisha kuwa ukaguzi uliofanyika una ubora unaokubalika kwa hali ya juu. Ukaguzi ulijumuisha uchunguzi wa nyaraka mbalimbali zinazohusiana na kiasi cha fedha kilichoripotiwa kwenye taarifa za fedha. Pia, ulijumuisha tathmini ya makadirio na maamuzi yaliyofanywa na uongozi wa Mashirika na Taasisi zinazojitegemea wakati wa uandaaji wa taarifa za fedha, utoshelezi wa mambo yaliyoripotiwa kwenye taarifa za fedha, iwapo sera za uhasibu zinazotumika zinaendana na mazingira halisi ya utekelezaji wa majukumu ya taasisi inayokaguliwa na kwa mujibu wa Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta za Umma, na kama sera hizo zinajitosheleza na zimekuwa zikitumika mwaka hadi mwaka.

Ukaguzi uliofanyika ulipangwa na kutekelezwa kwa namna ambayo iliwezesha ukusanyaji wa taarifa zote muhimu na maelezo ya uongozi yaliyokuwa yanahitajika ili kuhakikisha upatikanaji wa kutosha wa nyaraka kwa ajili ya kutoa uhakika iwapo taarifa za fedha zilizokaguliwa hazina mapungufu makubwa yaliyosababishwa na ubadhirifu au kwa bahati mbaya.

Nilifanya ukaguzi wangu kwa uhuru na sikuwa na mgongano wa maslahi na taasisi yoyote niliyoikaguwa kwa mujibu wa kanuni za maadili zilizotolewa na Bodi ya Kimataifa ya Viwango vya Maadili kwa Wahasibu pamoja na Kanuni za Maadili zilizotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA) na nilitekeleza wajibu wangu wa kimaadili kwa mujibu wa matakwa hayo.

Ni imani yangu kuwa ushahidi nilioupata ulikuwa sahihi na ulijitosheleza katika kutoa hati za ukaguzi na pale ambapo nilishindwa kupata ushahidi wa kutosha sikutoa hati za ukaguzi.

### 2.3.5 Hati za Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, nilikamilisha ukaguzi wa Taasisi **45.** Kati ya Taasisi hizo jumla ya Mashirika **8**, Mamlaka **12 ,** Wakala **15** na Taasisi zinazojitegemea **10** za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kutoa hati za ukaguzi kwa Taasisi **45.** Kati ya hati hizo zilizotolewa hati **39** ni hati zinazoridhisha sawa na asilimia **86.67** ya hati zilizotolewa, na hati **6** ni hati zenye shaka sawa na asilimia **13.33** ya hati zilizotolewa na sikuwa na hati ya kushindwa kutoa maoni. Orodha ya Taasisi nilizozikaguwa pamoja na hati za ukaguzi nilizozitoa ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 2: Hati za ukaguzi zilizotolewa kwa Mashirika na Taasisi zinazojitegemea katika kipindi cha miaka Minne**

| Nam. | Fungu | Shirika/Taasisi | Hati zilizotolewa | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Aina ya Hati iliyotolewa 2019/2020 | Aina ya Hati iliyotolewa 2020/2021 | Aina ya Hati iliyotolewa 2021/2022 | Aina ya Hati iliyotolewa 2022/2023 |
| **Mashirika ya Serikali** | | | | | | |
| 1. | Linajitegemea | Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | **Hati Yenye Shaka** | Hati Inayoridhisha |
| 2. | Linajitegemea | Shirika la Bandari Zanzibar (ZPC) | Hati Isiyoridhisha | Hati Inayoridhisha | **Hati Yenye Shaka** | Hati Inayoridhisha |
| 3. | Linajitegemea | Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) | **Hati yenye shaka** | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 4. | Ruzuku | Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 5. | Ruzuku | Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 6. | Linajitegemea | Shirika la Nyumba Zanzibar (ZHC) | **Hati yenye shaka** | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 7. | Ruzuku | Shirika la Huduma za Maktaba | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 8. | Ruzuku | Shirika la Magazeti | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | **Hati Inayoridhisha yenye aya ya Msisitizo** |
| **Mamlaka za Serikali** | | | | | | |
| 9. | Inajitegemea | Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) | Hati Isiyoridhisha | Hati Isiyoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 10. | Inajitegemea | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 11. | Inajitegemea | Mamlaka ya Usafiri Baharini (ZMA) | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | **Kushindwa Kutoa Maoni** | **Hati Yenye Shaka** |
| 12. | Inajitegemea | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar (ZAA) | Hati Isiyoridhisha | Hati Isiyoridhisha | **Hati Yenye Shaka** | Hati Inayoridhisha |
| 13. | Ruzuku | Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) | **Hati yenye shaka** | Hati Isiyoridhisha | **Hati Inayoridhisha yenye aya ya Msisitizo** | **Hati Inayoridhisha yenye aya ya Msisitizo** |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 14. | Ruzuku | Mamlaka ya Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA) | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | **Hati Inayoridhisha yenye aya ya Msisitizo** | **Hati Inayoridhisha yenye aya ya Msisitizo** |
| 15. | Ruzuku | Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar (ZPPDA) | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 16. | Ruzuku | Mamlaka ya Mafunzo ya Vyuo ya Amali | **Hati yenye shaka** | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 17. | Ruzuku | Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 18. | Ruzuku | Mamlaka ya Kuzuiza Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | **Hati Inayoridhisha yenye aya ya Msisitizo** |
| 19. | Ruzuku | Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani | - | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 20. | Ruzuku | Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya | - | - | - | Hati Inayoridhisha |
| **Wakala za Serikali** | | | | | | |
| 23. | Ruzuku | Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar (ZAGPA) | Hati Isiyoridhisha | Haijakaguliwa | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 24. | Ruzuku | Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA | - | Hati Isiyoridhisha | Hati Inayoridhisha | **Hati Yenye Shaka** |
| 25. | Ruzuku | Wakala wa Serikali Mtandao | - | - | - | Hati Inayoridhisha |
| 26. | Ruzuku | Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii | Hati Inayoridhisha | Hati Isiyoridhisha | **Hati Yenye Shaka** | Hati Inayoridhisha |
| 27. | Ruzuku | Wakala wa Serikali wa huduma za Matrekta na Zana za Kilimo | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 28. | Ruzuku | Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi (ZFDA) | Hati Inayoridhisha | Hati Isiyoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 29. | Ruzuku | Wakala wa Majengo Zanzibar | Hati Inayoridhisha | Hati Isiyoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 30. | Ruzuku | Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 31. | Ruzuku | Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | **Hati Yenye Shaka** |
| 32. | Ruzuku | Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | **Hati Yenye Shaka** |
| 33. | Ruzuku | Wakala wa Vipimo | - | - | - | Hati Inayoridhisha |
| 34. | Ruzuku | Wakala wa Ulinzi JKU | - | - | - | Hati Inayoridhisha |
| 35. | Ruzuku | Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na Vya Kati (SMIDA). | - | - | - | Hati Inayoridhisha |
| 21. | Ruzuku | Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi | - | - | - | Hati Inayoridhisha |
| 22. | Ruzuku | Wakala wa Barabara Zanzibar | - | - | - | Hati Inayoridhisha |

| Taasisi zinazojitegemea | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 23. | Inajitegemea | Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 24. | PBZ Hisa | Mufindi Community Bank LTD (MuCoBa) | - | - | **Hati Yenye shaka** | **Hati Yenye shaka** |
| 25. | Unajitegemea | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF) | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 26. | Ruzuku | Mfuko wa Barabara Zanzibar | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | **Hati Yenye shaka** |
| 27. | Inajitegemea | Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 28. | Ruzuku | Kampuni ya Ujenzi | - | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 29. | Ruzuku | Kampuni ya Uunganishaji wa Maudhui (ZMUX) | - | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 30. | Ruzuku | Chuo cha Utawala wa Umma (IPA) | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 31. | Ruzuku | Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia (KIST) | Hati Inayoridhisha | Hati Isiyoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |
| 32. | Ruzuku | Chuo cha Kiislamu Zanzibar | - | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha | Hati Inayoridhisha |

**Mwenendo wa Hati za Ukaguzi**

Mwenendo wa hati za ukaguzi kwa miaka minne mfululizo kwa Mashirika ya Umma pamoja na Taasisi zinazojitegemea kutoka 2019/2020 hadi 2022/2023 umeoneshwa kwenye jadweli zifuatazo hapo chini:-

### Jadweli Nambari 3: Mwenendo wa hati za ukaguzi

| Aina ya hati ya ukaguzi | Mwaka wa fedha | | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 | 2022/2023 |
| Hati Inayoridhisha | 26 | 30 | 35 | 39 |
| Hati yenye shaka | 8 | 9 | 5 | 6 |
| Hati mbaya | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kushindwa kutoa maoni | 0 | 0 | 1 | 0 |
| **Jumla** | **34** | **39** | **41** | **45** |

### Jadweli Nambari 4: Mwenendo wa Hati za Ukaguzi kwa Asilimia

| Aina ya hati ya ukaguzi | Mwaka wa fedha | | | |
|---|---|---|---|---|
| | 2019/2020 | 2020/2021 | 2021/2022 | 2022/2023 |
| Hati Inayoridhisha | 76. 50 | 77 | 85.36 | 86.67 |
| Hati Yenye Shaka | 23.50 | 23 | 12.19 | 13.33 |
| Hati Mbaya | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kushindwa Kutoa Maoni | 0 | 0 | 2.45 | 0 |
| **Jumla** | **100** | **100** | **100** | **100** |

## 2.4 Taarifa ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Hoja za Ukaguzi kwa Mwaka Uliopita

Taarifa ya utekelezaji wa Mapendekezo ya Hoja za Ukaguzi kwa mwaka uliopita inaeleza kwa muhtasari hali ya utekelezaji wa hoja na hatua zilizochukuliwa na Maafisa Masuuli katika kusimamia na kufuatilia mapendekezo ya ukaguzi yaliyotolewa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 kwa Mashirika, Mamlaka, Wakala na Taasisi zinazojitegemea.

Kiujumla hali ya utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi imeimarika ambapo baadhi ya Taasisi zimeonekana kupiga hatua katika kufanya marekebisho ya dosari zilizobainika ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 dosari hizo hazikuweza kujirejea na kwa baadhi ya Taasisi zimeweza kupunguza idadi ya hoja zilizobainishwa ukilinganisha na mwaka uliopita.

Tathmini niliyofanya kwenye hali ya utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi ya Mwaka Uliopita nimebaini jumla ya mapendekezo 760 yalitolewa kwa taasisi 44 zilizokaguliwa na kuwasilishiwa ripoti za ukaguzi. Kati ya mapendekezo hayo jumla ya mapendekezo 552 yaliweza kutekelezwa na kuondolewa ambayo ni sawa na asilimia 72.63, mapendekezo 87 yapo katika hatua ya utekelezaji sawa na asilimia 11.45 Hata hivyo, mapendekezo 56 bado hayajatekelezwa ambayo ni sawa na asilimia 7.37 na mapendekezo 41 yamejirudia sawa na asilimia 5.39, vile vile mapendekezo 24 yamepitwa na wakati sawa na asilimia 3.16.

# SURA YA TATU


INTERNAL CONTROLS
STANDARDS
COMPLIANCE
POLICIES
REGULATIONS
RULES

# 3.0 TATHMINI YA MIFUMO YA UDHIBITI WA NDANI

Sura hii inaelezea tathmini ya mifumo ya udhibiti wa ndani inayoendeshwa ndani ya Mashirika na Taasisi zinazojitegemea kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Vile vile inaelezea mapungufu yaliyojitokeza katika tathmini ya mifumo ya udhibiti wa ndani, pamoja na masuala ya utawala bora, Kamati za Ukaguzi na Kazi za Ukaguzi wa Ndani.

## 3.1 Matokeo ya Tathmini ya Mfumo wa Udhibiti wa Ndani

Ripoti hii inaeleza matokeo ya tathmini ya mfumo wa udhibiti wa ndani na mapendekezo pamoja na njia ambazo zinaweza kutumika katika kudhibiti na kusimamia ambapo mfumo huo unaweza kuboreshwa ili kuongeza ufanisi kwa lengo la kudhibiti vihatarishi vinavyoweza kujitokeza.

Ukaguzi wa udhibiti wa ndani ulikuwa na malengo ya kutambua mapungufu yatokanayo na utekelezaji wa matakwa ya sheria ya Uanzishwaji wa vitengo vya ukaguzi wa ndani, kamati za ukaguzi pamoja na ufanyaji kazi wa vitengo hivyo. Mambo yaliyojitokeza katika taarifa hii ni yale tu yanayotokana na ukaguzi, na ambayo tunaamini kuwa yanatakiwa kuletwa mbele ya umma. Hatuwezi kuwajibika na kuripoti vitu vyote vya vihatarishi vinavyohusiana na udhaifu wa udhibiti wa ndani.

Maafisa Masuuli pamoja na viongozi wa Serikali wanawajibika kwa masuala ya usimamizi na uendeshaji ambapo watalazimika kubainisha viashiria vya upotevu wa fedha za umma pamoja na kuvichukulia hatua za kiutendaji ili visiweze kujitokeza kwa mara nyengine, hata hivyo watakuwa na jukumu la kuhakikisha kunakuwa na udhibiti wa matumizi bora ya fedha za umma katika Taasisi zao.

### 3.1.1 Dosari za ujumla zilizobainika kwa mwaka wa fedha 2022/2023

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika uwepo wa dosari mbalimbali zinazotokana na makosa ya kiutendaji pamoja na ukiukwaji wa sheria ambapo imepelekea uwepo wa dosari hizo kujitokeza mara kwa mara kwa baadhi ya Mashirika na Taasisi zinazojitegemea. Kuwepo kwa dosari hizo kunaweza kukapelekea kuharibu mtazamo wa hati za ukaguzi na hatimae Shirika au taasisi kuweza kupata hati yenye shaka.

Baadhi ya dosari za ujumla zilizobainika kutoka katika hesabu za Mashirika na Taasisi zinazojitegemea ni kama inavyobainishwa hapo chini:-

#### 3.1.1.1 Mapungufu katika Mfumo wa Udhibiti wa Ndani

Mifumo ya udhibiti wa ndani ni namna ambavyo rasilimali za umma zinavyopangiliwa, zinavyosimamiwa na kupimwa. Udhibiti wa ndani unatumika kama chombo muhimu katika kudhibiti ubadhirifu na matumizi mabaya ya mali za umma zinazoshikika na zisizoshikika.

Katika Taasisi yoyote lengo la mfumo wa udhibiti wa ndani ni kuhakikisha shughuli za Shirika au Taasisi husika zinafanywa kwa kuzingatia miongozo na taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria na kanuni.

Ukaguzi umebaini baadhi ya Mashirika na Taasisi zinazojitegemea bado hazina usimamizi mzuri wa udhibiti wa ndani kwa kutokuanzisha vitengo au kwa kutokufanya kazi kwa vitengo hivyo kwa mujibu wa utaratibu, au kujitokeza dosari mbali mbali za kiutendaji ambazo zinakwaza kamati hizo kufanya kazi zake kwa mujibu wa sheria jambo ambalo linapelekea kamati za ukaguzi (Audit Committee) pamoja na kitengo cha ukaguzi wa ndani (Internal Audit Unit) kutokupitia ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hesabu za mwisho wa mwaka pamoja na kushindwa kutoa maoni ya marekebisho ya dosari na kasoro mbali mbali zilizobainishwa katika ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Ukaguzi unawashauri viongozi wa Mashirika ya Umma na Taasisi zinazojitegemea kuhakikisha wanaweka udhibiti mzuri wa ndani ikiwemo kuvijengea uwezo vitengo vya ukaguzi wa ndani pamoja na Kamati za ukaguzi kwa kuvipatia mafunzo ya muda mfupi juu ya namna bora ya kutekeleza kazi zao. Taasisi zilizobainika kuwa na dosari hizo ni kama zifuatazo:-

**Jadweli Nambari 5: Dosari za kiutendaji zilizobainika kwa vitengo vya usimamizi na udhibiti wa ndani**

| Namba | Jina la Taasisi | Dosari zilizobainika | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Kamati ya Ukaguzi | Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani | Bodi ya Zabuni |
| 1. | Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Pemba | -- | Hakijaanzishwa | -- |
| 2. | Shirika la Magazeti ya Serikali Pemba | -- | Hakijaanzishwa | -- |
| 3. | Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar | Kutokufanya kazi ipaswavyo | -- | -- |
| 4. | Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma | Kutokufanya kazi ipaswavyo | Uwepo wa uhaba wa Watumishi | -- |

### 3.1.1.2 Ucheleweshaji wa uwasilishaji wa Taarifa za Hesabu za Mwisho wa Mwaka

Kwa mujibu wa kifungu nambari 119(1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinawataka Wakuu wa Taasisi kutayarisha taarifa za mapato na matumizi na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ndani ya kipindi cha miezi mitatu baada ya kukamilika kwa mwaka wa fedha.

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya Mashirika na Taasisi zinazojitegemea zimechelewa kuwasilisha hesabu za mapato na matumizi yanayosimamiwa na taasisi hizo kwa ajili ya ukaguzi ambapo ni kinyume na kifungu nambari 119(1) cha sheria niliyoitaja hapo juu. Kuchelewa kuwasilisha taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka kunapelekea kujitokeza ugumu wa kuzifanyia kazi taarifa hizo ikiwemo kuzitolea maoni ya kitaalamu kutokana na kujitokeza kwa uharaka wa kuwahi kuwasilisha taarifa zilizokaguliwa kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mujibu wa matakwa ya Kifungu nambari 112(5) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Ukaguzi unawashauri maafisa masuuli kuhakikisha wanawasilisha taarifa zao za hesabu za mwisho wa mwaka kwa wakati ili ziweze kutolewa maoni ya kitaalamu na kupelekea kuziwasilisha taarifa hizo kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mujibu wa sheria.

Baadhi ya Taasisi zilizobainika kuchelewesha kuwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 6: Taasisi zilizochelewa kuwasilisha hesabu za mwisho wa mwaka**

| Namba | Jina la Taasisi | Tarehe ya Uwasilishaji | |
|---|---|---|---|
| | | Mwaka wa fedha 2021/2022 | Mwaka wa fedha 2022/2023 |
| 1. | Wakala wa Ulinzi JKU | -- | 02/10/2023 |
| 2. | Wakala wa Barabara Zanzibar | -- | 06/10/2023 |

#### 3.1.1.3 Dosari katika Daftari la Kuhifadhia Mali za Kudumu (Fixed Assets Register)

Kwa mujibu wa kifungu nambari 29(1)(a) (2) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kwamba "Afisa Mhasibu wa Taasisi za Umma atahusika na kusimamia mali za Taasisi ya Umma na katika kutimiza majukumu yanayohusina na usimamizi wa mali, Afisa Mhasibu atatunza daftari la mali zote zilizopo chini ya udhibiti wa Taasisi ya Umma".

Aidha, kifungu nambari 58(c) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba "Afisa Masuuli wa taasisi ya Umma atakuwa na jukumu la kuhifadhi na kuimarisha kila muda daftari la mali za umma kwa kujumuisha mali mpya za umma zinazopatikana na kuondosha vifaa vilivyoondolewa"

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika baadhi ya taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hazina daftari la kuhifadhia mali za kudumu, au kutokufanyiwa maboresho kwa daftari hilo kwa kuwekwa mali mpya na kuondolewa zilizochakaa jambo ambalo linaweza kupelekea kutokujua umiliki wake na hatimaye kupelekea kupotea kwa mali hizo.

Kukosekana daftari la kuhifadhia mali za kudumu au kutokufanyiwa maboresho kunaweza kupelekea mali zilizonunuliwa, zilizochakaa, zilizouzwa pamoja na zilizohamishwa kutokutambuliwa na kusababisha upotevu wa mali hizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuhakikisha unatekeleza matakwa ya Sheria nilizozinakili hapo juu ili kuepusha kujitokeza kwa vitendo vya upotevu wa mali za umma bila ya kuzibaini. Mchanganuo wa taasisi zilizobainika na dosari hizo ni kama zifuatazo:-

**Jadweli Nambari 7: Taasisi zilizobainika kuwa na mapungufu katika daftari la Kuhifadhia Mali za Kudumu**

| Namba | Jina la Taasisi | Hali Halisi ya Daftari Iliyobainika |
|---|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Maji Pemba | Haina |
| 2. | Wakala wa Karakana Kuu ya Magari ya Serikali Pemba | Haina |
| 3. | Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Zanzibar | Haina |
| 4. | Wakala wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo Zanzibar | Haina |
| 5. | Wakala wa Miundombinu ya Tehama Zanzibar | Haina |
| 6. | Wakala wa Barabara Zanzibar | Haina |
| 7. | Shirika la Nyumba Pemba | Halina |
| 8. | Shirika la Magazeti ya Serikali Pemba | Halina |
| 9. | Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya | Haina |
| 10. | Benki ya Watu wa Zanzibar | Halijafanyiwa Maboresho |

#### 3.1.1.4 Kutokuwepo kwa Daftari la makadirio ya Vifungu vya Matumizi (Vote Book)

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya Mashirika na Taasisi zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hufanya matumizi mbali mbali bila kuwepo kwa daftari la makadirio ya vifungu vya matumizi (Vote Book).

Kutokuwepo kwa daftari la vifungu vya matumizi kunapelekea kushindwa kufanya tathmini ya uingizwaji wa fedha za matumizi kwa kila kifungu pamoja na matumizi ya kifungu hicho jambo ambalo ni kwenda kinyume na toleo lenye kumbukumbu namba AD.5/184/01/07/80 la tarehe 9/6/2021 linalowataka wahasibu kufunga hesabu zao kwa mujibu wa daftari la makadirio ya vifungu vya matumizi.

Ukaguzi unawashauri Maafisa Masuuli kuhakikisha wanasimamia watendaji wao kikamilifu ili kutekeleza maagizo ya muongozo huo kwa lengo la kuhakikisha wanafuata taratibu na misingi ya ufungaji wa hesabu kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa kitaifa na kimataifa ili kuepusha ukiukwaji wa Sheria ya Usimamizi wa fedha za Umma. Dosari hii imebainika kwa taasisi mbali mbali kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 8: Taasisi zilizokuwa hazikufuata muongozo wa ufungaji wa hesabu (Vote book)**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Pemba |
| 2. | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege – Pemba |
| 3. | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Pemba |
| 4. | Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya |
| 5. | Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar |

#### 3.1.1.5 Kutokufikiwa kwa malengo ya uandaaji wa Taarifa za Fedha "Segment Reports"

Kwa mujibu wa muongozo nambari 2 wa mwaka 2022/2023 wenye kumbukumbu nambari ACGEN/BC.195/393/01/01 wa tarehe 13/06/2023 kutoka Afisi ya Rais Fedha na Mipango unaohusiana na zoezi la kufunga hesabu la mwaka wa fedha 2022/2023 ikisisitiza ufungaji wa hesabu uzingatie muongozo uliotolewa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 wenye kumbukumbu nambari AD.5/184/01/08/90 uliotolewa na (OR) Fedha na Mipango Zanzibar tarehe 9/6/2022 unazitaka taasisi zote za Serikali kuandaa "Segment Reports" kwa kuzingatia mapato na matumzi ya mwaka wa fedha husika, taarifa za mapato, matumizi pamoja na bakaa katika segments kwa jumla zionekane sawa na "Consolidated financial statements, Statement of Receipt and Payment na Statement of Comparison of Budget and Actual".

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kutokufikiwa kwa lengo lililokusudiwa kwa mujibu wa muongozo uliotolewa kwa baadhi ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutokana na Taasisi hizo kutokupatiwa mafunzo ya kutosha ya namna ya uandaaji wa ripoti hizo pamoja na uchelewaji wa kutolewa kwa muongozo unaozitaka taasisi hizo kuandaa Taarifa za fedha "Segment Reports" jambo ambalo limepelekea ukaguzi kushindwa kujiridhisha na taarifa za fedha zilizoandaliwa kutokana na uwepo wa dosari nyingi za kiutendaji pamoja na baadhi ya Taasisi kushindwa kuandaa taarifa hizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha unatoa mafunzo endelevu kwa taasisi zote zilizokuwa na uelewa mdogo wa kuandaa taarifa za fedha ili ziweze kuendana na mabadiliko yanayotarajiwa kujitokeza ya kuhama kutoka katika Mfumo wa Fedha Taslim "Cash Basis" kwenda katika Mfumo wa Madeni "Accrual Basis". Taasisi zilizobainika kuwa na dosari hiyo ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 9: Taasisi zilizoshindwa kuandaa "Segment Report"**

| Namba | Taasisi zilizoshindwa kuandaa "Segment Report" |
|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Pemba |
| 2. | Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Pemba |
| 3. | Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi Pemba |
| 4. | Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Pemba |
| 5. | Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Pemba |
| 6. | Wakala wa Barabara Pemba |

### 3.1.1.6 Kutokuwepo kwa bajeti ya mapato na matumizi kwa baadhi ya Taasisi za Serikali Pemba

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika baadhi ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa upande wa Pemba zinatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa matakwa ya Sheria, Kanuni na Miongozo zinazosimamia Taasisi hizo.

Ukaguzi umebaini uwepo wa changamoto mbali mbali zinazozikabili taasisi hizo ambazo zinapelekea kutokuwa na ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yao na hatimae kutokufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa kutokana na kukosekana kwa bajeti halisi ya mapato na matumizi katika uendeshaji wa shughuli za taasisi hizo.

Miongoni mwa dosari zinazozikumba taasisi hizo ni kama zifuatazo:-

- Kutokuwepo kwa mpango wa utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kwa mujibu wa bajeti ya taasisi hizo.
- Kukosa muelekeo wa utekelezaji wa shughuli zilizopangwa kwa mwaka husika kutokana na kutokujuwa thamani halisi ya fedha inayoweza kupatikana katika kusimamia shughuli iliyopangwa.
- Kutumiwa fedha za matumizi ya kazi za kawaida kwa baadhi ya taasisi ikiwemo matumizi ya mafuta, umeme, vifaa vya kuandikia kwa njia ya miamala ya simu (Tigo Pesa, Ezy Pesa, Airtel Money) au kupitia hesabu za watumishi binafsi jambo ambalo ni kinyume na utaratibu wa miongozo ya fedha za umma.

Kuwepo kwa dosari hizo kunaweza kupelekea kutokufikiwa kwa lengo la utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa ufanisi uliokusudiwa.

Ukaguzi unawashauri Maafisa Masuuli wa Taasisi hizo kuwasiliana na Afisi ya Rais Fedha na Mipango kuchukuwa jitihada za kulitafutia ufumbuzi suala hilo ili kunusuru uwezekano wa kujitokeza kwa upotevu wa fedha za umma kutakakosababishwa na baadhi ya watumishi waliokosa uaminifu. Mchanganuo wa Taasisi zisizokuwa na bajeti ya mapato na matumizi ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 10: Taasisi zisizokuwa na bajeti ya mapato na matumizi**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Pemba |
| 2. | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Pemba |

### 3.1.1.7 Kutokutenganishwa kwa Afisi ya Masjala ya Siri na Bayana

Kanuni ya 52(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inaeleza kuwa "Kila taasisi ya umma itakuwa na masjala ya siri na bayana ambazo zitahifadhi kumbukumbu zote za Taasisi husika kwa utaratibu ufuatao:-

(i) Masjala ya siri itahusika na uhifadhi wa nyaraka zote za siri zinazoingia na kutoka ndani ya taasisi.

(ii) Masjala ya bayana itahusika na uhifadhi wa nyaraka zote za wazi zinazoingia na kutoka ndani ya taasisi.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa baadhi ya Taasisi hazina masjala ya siri na bayana kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu zinazoingia na kutoka katika taasisi hizo. Hali hii inaweza kupelekea kuchanganyika kwa majalada ya masjala ya siri na bayana hivyo kusababisha uwezekano wa kuvuja kwa taarifa za siri za Serikali. Kutokutenganishwa ofisi za masjala ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kuweka afisi za masjala ya siri na bayana ili kudhibiti uchanganyikaji wa majalada kunakoweza kupelekea uvujaji wa siri za Serikali. Mchanganuo wa Taasisi hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 11: Taasisi ambazo hazikutenganisha masjala ya siri na masjala bayana**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Pemba |
| 2. | Mamlaka ya Maji Pemba |
| 3. | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Pemba |
| 4. | Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Pemba |
| 5. | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Pemba |
| 6. | Wakala wa Serikali wa Uchapaji Pemba |
| 7. | Mamlaka ya Usafiri Baharini Pemba |
| 8. | Shirika la Magazeti ya Serikali Pemba |

### 3.1.1.8 Kutokukamilika kwa taratibu za kuwaombea ajira ya kudumu kwa watumishi wa kutwa

Kwa mujibu wa kanuni ya 135 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014, inaeleza kuwa hakutakiwi kuwepo kwa wafanyakazi wa kutwa katika Utumishi wa Umma na kama kuna ulazima wa kuwepo Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi atalazimika kuomba kibali kwa Tume ya Utumishi husika na kumjazisha mkataba, ambapo mtumishi wa kutwa hatozidi miezi sita.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 baadhi ya Taasisi za Umma zilikuwa na watumishi wa kutwa ambao walikuwa wakitumikia katika maeneo tofauti ya Taasisi hizo. Baadhi ya watumishi hao wameshatumikia kwa zaidi ya miaka mitano (5) na wamekuwa ni chachu katika kuzilinda na kuzitunza rasilimali za Taasisi zao.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni uwepo wa watumishi wa kutwa bila ya kupata ithibati ya kuwepo kwa kibali cha uajiri kutoka Tume ya Utumishi Serikalini kwa ajili ya kupata idhini. Hali hii inaweza ikapelekea kujitokeza kwa migogoro isiyo ya lazima pindipo mtumishi wa kutwa atakapokosa sifa za uajiri wa kudumu au kujitokeza kwa uajiri wa mtumishi asiyekuwa na maadili mema.

Kuwatumia watumishi wa ajira za kutwa kwa muda mrefu ni kwenda kinyume na Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 kama nilivyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kuendelea kufuatilia vibali vya ajira ili kuweza kuwaajiri katika ajira ya kudumu wale wote wanaoweza kuajirika kisheria. Mchanganuo wa watumishi wa kutwa walioajiriwa bila kibali ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 12: Watumishi wa kutwa walioajiriwa bila ya Kibali

| Namba | Jina la Mtumishi | Umri | Muda wa Utumishi (Miaka) | Elimu | Kitengo cha Kazi |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Pemba** | | | | | |
| 1. | Abdalla Rashid Said | 39 | 7 | Form II | Wahudumu Mazingira |
| 2. | Abeid Abdalla Rashid | 26 | 7 | Form IV | |
| 3. | Ali Abdalla Nassor | 31 | 4 | Form IV | |
| 4. | Ali Moh'd Ali | 43 | 7 | Form IV | |
| 5. | Ali Said Said | 49 | 11 | Form II | |
| 6. | Ali Salum Khamis | 30 | 7 | Form II | |
| 7. | Ashura Massoud Issa | 26 | 4 | Form IV | |
| 8. | Dhamir Abass Omar | 32 | 7 | Form II | |
| 9. | Fardat Salim Moh'd | 24 | 5 | Form IV | |
| 10. | Habiba Shaib Mbarouk | 28 | 5 | Form IV | |
| 11. | Hafidh Abdalla Seif | 40 | 7 | Form IV | |
| 12. | Hamad Mbarouk Hamad | 38 | 8 | Form II | |
| 13. | Is-haka Kombo Khamis | 31 | 5 | Form IV | |
| 14. | Juma Moh'd Ali | 48 | 11 | Form II | |
| 15. | Khamis Omar Kassim | 33 | 11 | Form II | |
| 16. | Khamis Juma Ali | 35 | 7 | Form IV | |
| 17. | Khamis Salum Khamis | 28 | 7 | Form II | |
| 18. | Khamis Thiney Abeid | 38 | 7 | Form II | |
| 19. | Mahmoud Omar Iddi | 47 | 11 | Form II | |
| 20. | Mbarouk Abass Hamad | 53 | 11 | Form II | |
| 21. | Omar Juma Shaibu | 40 | 7 | Form II | |
| 22. | Omar Said Omar | 36 | 5 | Form II | |
| 23. | Othman Abdalla Mjaka | 26 | 11 | Form IV | |
| 24. | Rashid Moh'd Rashid | 26 | 7 | Form II | |
| 25. | Ridhwan Abdalla Said | 33 | 7 | Form IV | |
| 26. | Said Hassan Shaame | 37 | 7 | Form IV | |
| 27. | Suleiman Ali Juma | 47 | 11 | Form II | |
| 28. | Yussuf Ali Kombo | 27 | 7 | Form II | |
| 29. | Massoud Said Khamis | 37 | 5 | Form IV | Walinzi |
| 30. | Moh'd Abdalla Massoud | 33 | 5 | Form IV | |
| 31. | Msellem Bakar Hamad | 24 | 4 | Form IV | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 32. | Raya Mbarouk Hamad | 37 | 5 | Form IV | Hospitality Inn |
| 33. | Sada Khamis Mwalim | 29 | 5 | Diploma | |
| 34. | Shuwena Ali Moh'd | 35 | 5 | Form IV | |
| 35. | Zainab Hafidh Abdalla | 23 | 5 | Form IV | Hospitality Inn |
| 36. | Zainab Salum Moh'd | 39 | 11 | Form II | Watunza Bustani |
| 37. | Salma Moh'd Saleh | 46 | 11 | Form II | |
| 38. | Samira Ali Yahya | 33 | 6 | Form IV | V.I.P |
| 39. | Najila Rashid Hemed | 38 | 4 | Form IV | |

**Mamlaka ya Maji Pemba**

| Namba | Jina | Umri | Muda wa Utumishi (Miaka) | Kiwango cha Elimu |
|---|---|---|---|---|
| 40. | Ali Moh'd Suleimani | 41 | 9 | Kidato cha IV |
| 41. | Moh'd Khamis Kassim | 29 | 6 | Kidato cha II |
| 42. | Muhamad Mabrouk Juma | 28 | 5 | Cheti cha ufundi bomba. |
| 43. | Ali Said Haji | 37 | 6 | Cheti cha ufundi bomba. |
| 44. | Hamad Omar Ali | 30 | 3 | Cheti cha ufundi umeme |
| 45. | Idd Zuli Faki | 33 | 3 | Kidato cha IV |
| 46. | Ali Abdalla Mohamed | 29 | 3 | Kidato cha I |
| 47. | Iki Khamis Omar | 31 | 6 | Kidato cha I |
| 48. | Ali Rashid Salim | 31 | 3 | Darasa la VII |
| 49. | Nassor Said Juma | 63 | 3 | Kidato cha III |
| 50. | Haji Mohamed Ali | 28 | 3 | Kidato cha IV |
| 51. | Faki Bakar Faki | 32 | 3 | Cheti cha Ufundi bomba. |
| 52. | Wahid Kassim Ali | 27 | 3 | Kidato cha IV |
| 53. | Moh'd Suleiman Moh'd | 33 | 2 | Kidato cha IV |
| 54. | Hafidh Mohamed Juma | 28 | 2 | Kidato cha II |
| 55. | Ibrahim Said Massoud | 25 | 2 | Kidato cha IV |
| 56. | Shadya Moh'd Shaffi | 39 | 2 | Cheti cha Bima |
| 57. | Seif Ramadhan Omar | 31 | 2 | Stashahada ya Rasilimali watu. |
| 58. | Bakari Ali Juma | 26 | 2 | Cheti cha ufundi bomba |
| 59. | Hemed Mohamed Kassim | 31 | 2 | Kidato cha IV |
| 60. | Fadhil Juma Ame | 35 | 2 | Cheti cha Ufundi bomba |
| 61. | Salum Hamed Ali | 32 | 2 | Cheti cha Fundi Bomba |
| 62. | Saleh Haji Machano | 32 | 2 | Cheti Cha Ufundi Bomba |
| 63. | Omar Malik Seif | 37 | 2 | Dereva |
| 64. | Khatib Kai Pandu | 36 | 2 | Kidato cha IV |
| 65. | Salum Rashid Haji | 25 | 2 | Cheti cha Ufundi Umeme |
| 66. | Ali Ameir Mwadini | 33 | 2 | Cheti cha Ufundi Bomba |
| 67. | Seif Mussa Hamad | 28 | 2 | Kidato cha IV |
| 68. | Mwanaate Machano Hamad | 32 | 2 | Kidato cha IV |
| 69. | Idrisa Shante Shaaban | 25 | 2 | Kidato cha IV |
| 70. | Seif Kassim Seif | 29 | 2 | Cheti cha Ufundi umeme |
| 71. | Khamis Ali Suleiman | 36 | 1 | Kidato cha II |
| 72. | Wahbi Massoud Khamis | 23 | 2 | Cheti cha udereva |
| 73. | Zahor Ali Hamad | 23 | 1 | Cheti cha Ufundi bomba |
| 74. | Raisat Mkubwa Moh'd | 25 | 1 | Kidato cha II |
| 75. | Salim Hamad Mussa | 24 | 1 | Shahada ya mazingira |
| 76. | Juma Omar Iddi | 25 | 1 | Dereva |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 77. | Saghir Ali Abdalla | 26 | 1 | Kidato cha II |
| 78. | Zaynab Ali Abeid | 25 | 1 | Cheti za Rikodi |
| 79. | Asya Juma Omar | 24 | 1 | Cheti cha Ufundi Bomba |

| Kampuni ya Uunganishaji wa Maudhui (ZMUX) | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Namba** | **Jina** | **Tarehe ya Kuanza Mkataba** | **Tarehe ya Kumaliza** | **Cheo** |
| 80. | Daulat Khalid Bakari | 01/08/2022 | 31/01/2023 | Muhudumu /Rahaleo |
| 81. | Arafa Suleiman Ali | 01/09/2022 | 31/08/2023 | Mtoa huduma kwa wateja |
| 82. | Juma Amiri Juma | 01/01/2022 | 31/12/2022 | Mhamasishaji wateja |
| 83. | Said Abdallah Said | 01/08/2022 | 31/07/2023 | Fundi |
| 84. | Ameir Kailu Ameir | 01/08/2022 | 31/07/2023 | Fundi |
| 85. | Abdulhakim Juma Saleh | 01/08/2022 | 31/07/2023 | Fundi |
| 86. | Ahmed Japhet Luzinga | 01/08/2022 | 31/07/2023 | Fundi |
| 87. | Bakari Moh'd Ame | 01/01/2017 | 31/12/2022 | Mlinzi /Pemba |
| 88. | Ali Kombo Khamis | 01/01/2017 | 31/12/2022 | Mlinzi /Muyuni |
| 89. | Shaaban R. Said | 01/01/2017 | 31/12/2022 | Mlinzi /Muyuni |
| 90. | Ame Haji Tubi | 01/01/2017 | 31/12/2022 | Mlinzi /Nungwi |
| 91. | Abdalla Mussa Koke | 01/01/2017 | 31/12/2022 | Mlinzi |
| 92. | Ali Hemed Mbarouk | 01/01/2017 | 31/12/2022 | Fundi |
| 93. | Mohammed A. Khamis | 01/01/2017 | 31/12/2022 | Mlinzi |
| 94. | Elias Simon Elias | 01/01/2017 | 31/12/2022 | Fundi |
| 95. | Abdulbasit H. Ali | 01/01/2017 | 31/12/2022 | Mhamasishaji wateja |

### 3.1.1.9 Kutokukatiwa Bima kwa Vyombo vya Usafiri

Kwa mujibu wa kanuni 124(5) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014, Mkuu wa Taasisi anatakiwa kuhakikisha kuwa vyombo vya usafiri vya Serikali vilivyo chini ya mamlaka yake vinapasishwa na kukatiwa bima.

Ukaguzi umebaini kuwa baadhi ya Taasisi zinamiliki vyombo mbalimbali vya usafiri ikiwemo gari, piki piki na vespa ambapo baadhi ya vyombo hivyo vinatumika bila ya kukatiwa bima. Hali hii imetokana na Taasisi hizo kutoweka kipaombele cha ukataji wa bima kwa vyombo vya usafiri. Kutokukatiwa bima kwa vyombo vya usafiri kunaweza kuisababishia Serikali kupata hasara ya utumiaji wa fedha kwa matengenezo pindipo vyombo hivyo vikipata ajali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kuhakikisha kwamba inaweka kipaombele cha ukataji wa bima kwa vyombo vya usafiri ili kunusuru kujitokeza kwa gharama zisizokuwa za lazima pale chombo kinapopata ajali. Mchanganuo wa vyombo hivyo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 13: Vyombo vya Usafiri Ambavyo Havijakatiwa Bima

| Namba | Nambari ya Chombo | Aina ya Chombo | Mahali Kilipo |
|---|---|---|---|
| **Mamlaka ya Maji Pemba** | | | |
| 1. | SLS 230 A | | |
| 2. | SLS 259 A | Gari | Chake Chake |
| 3. | SLS 150 B | | |
| 4. | SLS 212 B | | |
| 5. | SLS 227 B | | |
| 6. | SLS 226 B | | |
| 7. | SLS 263 B | | |
| 8. | SLS 288 B | | |
| 9. | SLS 289 B | | |
| 10. | DFP 39 | | |
| 11. | SLS 175 C | Pikipiki | |
| 12. | SLS 211 C | | |
| 13. | SLS 174 C | | Micheweni |
| 14. | SLS 159 | | Chake Chake |
| 15. | SLS 177 C | | Mkoani |
| 16. | SLS 176 C | | Wete |
| 17. | SLS 132 C | Vespa | Chake Chake |
| 18. | SLS 144 C | | Micheweni |
| **Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Pemba** | | | |
| 19. | SMZ 135A | Gari | ZAECA Kaskazini |
| 20. | SMZ 877C | Vespa | ZAECA Kaskazini |
| 21. | SMZ 491A | Gari | ZAECA Kusini |
| 22. | SMZ 779C | Vespa | ZAECA Kusini |

### 3.1.1.10 Kutokuunganishwa na Kutumika kwa Mfumo wa Afisi Mtandao

Kwa mujibu wa muongozo wenye kumbukumbu namba AB.168/233/01/1 wa tarehe 08/12/2022 kutoka Afisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora unaohusu utumiaji wa mfumo wa e-Office katika Taasisi zote za Serikali.

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya Taasisi za Umma hazijaunganisha na kutumia mfumo wa Afisi Mtandao (e-Office) katika Afisi zake wala hakuna mtumishi aliyepata mafunzo ya utumiaji wa mfumo huo. Hali hii inaweza kupelekea uzorotaji wa utoaji wa huduma za Taasisi kutokana na kuchelewa kushuka kwa maagizo kwa wanaohusika.

Kutokuunganishwa na kutumika kwa mfumo wa afisi mtandao ni kwenda kinyume na muongozo niliounakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao ili waweze kuunganishwa na kutumia huduma ya afisi mtandao kwa lengo la kurahisisha mawasiliano pamoja na kuongeza ufanisi wa kiutendaji na hatimae kupatikana kwa tija iliyokusudiwa.

Orodha ya Taasisi ambazo hazijaanza kutumia Mfumo wa Afisi Mtandao (e-Office) ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 14: Taasisi ambazo hazijaanza kutumia Mfumo wa e-Office**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi Pemba |
| 2. | Wakala wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo Pemba |
| 3. | Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Pemba |
| 4. | Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Pemba |
| 5. | Wakala wa Majengo Pemba |
| 6. | Wakala wa Serikali wa Uchapaji Pemba |

### 3.1.1.11 Kukosekana kwa vifaa vya huduma ya kwanza

Kanuni ya 125(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inaeleza kuwa Kila Mkuu wa Taasisi atalazimika kuhakikisha ndani ya Taasisi yake kunakuwa na upatikanaji wa huduma ya kwanza ya afya na vifaa vya huduma ya kwanza kwa watumishi. Aidha, kifungu nambari 85 cha Sheria nambari 8 ya Afya na Usalama Kazini ya 2005 kinazitaka Taasisi "Kuweka vifaa vya zima moto pindi janga litakapotokea".

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya Taasisi za Umma zimeshindwa kuandaa utaratibu wa upatikanaji wa vifaa vya huduma ya kwanza (First Aid) pamoja na vifaa vya kuzimia moto (Fire extinguisher) pindi inapotokea dharura kwa watumishi na mali za Afisi. Hali hii inaweza kusababisha kutokea kwa hasara kubwa pindipo pakitokea janga la moto au mtumishi kupata ajali akiwa kazini.

Kutokuweka vifaa vya huduma ya kuzimia moto na huduma ya kwanza ndani ya majengo ya Afisi ni kwenda kinyume na Sheria na kanuni zinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kufanya jitihada za kuandaa utaratibu wa upatikanaji wa vifaa vya huduma ya kwanza kwa lengo la kulinda usalama wa wafanyakazi kwa kufuata utarabibu wa Sheria na Kanuni zilizoekwa. Orodha ya Taasisi zilizokosa vifaa vya huduma ya kwanza ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 15: Taasisi ambazo hazina vifaa vya huduma ya kwanza**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Pemba |
| 2. | Wakala wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo Pemba |
| 3. | Wakala wa Karakana Kuu ya Magari ya Serikali Pemba |
| 4. | Wakala wa Serikali Mtandao Pemba |
| 5. | Wakala wa Barabara Pemba |
| 6. | Wakala wa Majengo Pemba |
| 7. | Wakala wa Serikali wa Uchapaji Pemba |

### 3.1.1.12 Kutokufikiwa kwa lengo la ukusanyaji wa mapato

Kifungu nambari 30(1-4) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinamtaka "Afisa Masuuli kuwajibika kwa uwezo wake wote katika suala la usimamizi katika ukusanyaji wa mapato".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba baadhi ya Taasisi za Umma hazikufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kwa mujibu wa makadirio ya vyanzo vyao vya ndani vya kibajeti jambo ambalo limepelekea kuathiri utekelezaji wa kazi walizojipangia.

Kutokufikiwa kwa lengo la ukusanyaji wa mapato kwa vyanzo vya ndani kumetokana na baadhi ya Taasisi kuwa na mifumo duni ya ukusanyaji wa mapato au kutokutoa kipaombele cha uhamasishaji wa malipo yatokanayo na vyanzo vyao vya mapato au kuwa na ubunifu duni wa uanzishwaji wa vyanzo vipya vya ukusanyaji wa mapato pamoja na kushindwa kuvisimamia vyanzo hivyo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi za umma kuongeza umakini katika ukusanyaji wa mapato ikiwemo kuwapatia elimu watumishi wanaoshughulikia ukusanyaji wa mapato pamoja na kuhamasisha wananchi njia bora ya kuchangia mapato ya Serikali ikiwemo kubuni njia bora zaidi zitakazohakikisha kuwa mapato yanakusavywa kikamilifu na kuibua vyanzo vipya vya mapato ili kuhakikisha zinafikia malengo yaliyowekwa. Miongozi mwa taasisi hizo ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 16: Taasisi ambazo hazikufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa fedha 2022/2023**

| Namba | Jina la Taasisi | Makadirio ya Makusanyo (Tsh.) | Makusanyo Halisi (Tsh.) | Asilimia ya Makusanyo (%) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar | 4,304,000,000 | 2,135,254,200 | 50 |
| 2. | Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar | 5,231,619,126 | 4,505,105,723 | 86 |
| 3. | Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo Pemba | 180,000,000 | 109,122,000 | 60.62 |
| 4. | Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Pemba | 866,500,000 | 440,668,300 | 50.9 |
| 5. | Mamlaka ya Maji Pemba | 3,764,207,666 | 751,379,410.66 | 19.96 |
| 6. | Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Pemba | 16,000,000 | 4,690,800 | 29.32 |
| 7. | Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Zanzibar | 2,327,900,000 | 1,712,882,195.73 | 75 |
| 8. | Wakala wa Majengo Pemba | 90,000,000 | 20,617,000 | 23 |
| 9. | Wakala wa Majengo Zanzibar | 300,000,000 | 127,057,750 | 42.4 |
| 10. | Wakala wa Barabara Zanzibar | 20,033,644,000 | 2,517,008,552.35 | 12.5 |
| 11. | Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati Zanzibar | 209,064,000 | 38,030,000 | 18.19 |
| 12. | Shirika la Nyumba Pemba | 525,024,000 | 267,640,000 | 50.98 |
| 13. | Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe | 250,000,000 | 81,325,000 | 32.53 |

### 3.1.1.13 Kutokuwepo kwa Daftari la Kuwekea KumbuKumbu za Mikataba (Contract Register)

Kanuni ya 47 ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaeleza kwamba "Afisa Mhasibu anatakiwa aweke daftari la mkataba lenye kufanyiwa marekebisho kwa mikataba yote walioingia kwa mwaka wa fedha husika".

Ukaguzi umebaini kwamba kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kuwepo kwa dosari kwa baadhi ya Taasisi kutokuwepo/kutokufanyiwa maboresho kwa daftari la kuwekea kumbukumbu za mikataba kwa ajili ya kutekeleza shughuli za miradi jambo ambalo linaweza kupelekea uwezekano wa kupotea kwa kumbu kumbu muhimu za miradi au shughuli za Afisi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kuhakikisha kwamba zinaanzisha daftari la kuwekea kumbu kumbu za mikataba kwa mujibu wa matakwa ya kisheria. Mchanganuo wa Taasisi hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 17: Taasisi ambazo hazijatayarisha daftari la kumbukumbu za mikataba "Contract Registers"**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar |
| 2. | Wakala wa Miundombinu ya Tehama Zanzibar |
| 3. | Wakala wa Matukio ya Kijamii |
| 4. | Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi |
| 5. | Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo |

### 3.1.1.14 Kutokuweka utaratibu wa kuchukuwa mahudhurio ya watumishi kwa njia ya kielektroniki

Kwa mujibu wa toleo nambari CAB.78/388/01/58 la tarehe 12 Oktoba, 2022 linaeleza ya kwamba "Kiujumla Taasisi zote za Umma zinatakiwa kuweka Daftari la Mahudhurio ya watumishi wakati wa kuingia na kutoka katika maeneo yao ya kazi, uwekaji wa daftari hilo linatokana na matakwa ya Kanuni ya 45(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inayofafanua kuwa "Kutakuwa na daftari la mahudhurio ambalo litatumika kuweka kumbukumbu ya muda wa mahudhurio kwa watumishi wa umma katika Wizara, Idara na vituo vyote vya kazi". Aidha, kutokana na mabadiliko ya teknolojia yaliyopo kwa sasa, kuzuia udanganyifu unaofanywa na watumishi wa Umma, kuongeza ufanisi na uwajibikaji imezilazimu Taasisi kuweka mfumo wa kuchukua mahudhurio ya watumishi kwa njia ya kielektroniki (biometric). Katika kuzingatia umuhimu wa suala hilo, Kanuni nambari 45(8) ya Kanuni za Utumishi wa Umma imeruhusu kutumia utaratibu wa kielektroniki wa kuchukua mahudhurio ya kuingia na kutoka kazini kwa watumishi wa umma ambapo imeeleza kuwa "Kunaweza kuwekwa utaratibu mwengine wa kushughulikia mahudhurio ya watumishi ya kutoka na kuingia kazini kwa njia ya elektroniki" .

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 ukaguzi umebaini uwepo wa baadhi ya Taasisi ambazo zimeshindwa kutekeleza agizo la toleo lililonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unawashauri Wakuu wa Taasisi kutekeleza matakwa ya agizo la toleo hilo kutokana na mabadiliko ya teknolojia yaliyopo kwa sasa ili kuweza kuzuia udanganyifu unaofanywa na watumishi wa Umma pamoja na kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika vituo vya kazi. Miongoni mwa Taasisi zilizoshindwa kutekeleza agizo hilo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 18: Taasisi ambazo hazijatekeleza utaratibu wa Mahudhurio wa Kidijitali**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar |
| 2. | Wakala wa Barabara Zanzibar |
| 3. | Wakala wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo Zanzibar |

### 3.1.1.15 Kutokuandaliwa kwa Mpango Mkakati (Strategic Planning)

Mpango Mkakati ni mfumo wa maandishi unaonyesha kazi zinazotakiwa kufanywa na hatua mbalimbali za kufikia malengo ya muda mrefu yaliyowekwa kwa muda wa kipindi cha miaka mitatu au miaka mitano kwa lengo la kuleta ufanisi katika taasisi husika. Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya Taasisi za Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 zimeshindwa kuwandaa Mpango Mkakati (strategic plan) unaohusiana na Taasisi zao.

Kufanya hivyo kunapelekea kutopatikana kwa udhibiti na ufatiliaji wa vipaombele vinavyohitajika kufanywa na Taasisi jambo ambalo linaweza likapelekea kutoenda sambamba na Mpango Mkuu wa Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Taasisi hizo kusimamia kwa karibu uandaaji wa mpango mkakati kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kazi kutokana na malengo yaliyokusudiwa. Mchanganuo wa Taasisi ambazo zimeshindwa kuandaa mpango mkakati ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 19: Taasisi za Serikali zilizoshindwa kuwandaa Mpango Mkakati**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Wakala wa Serikali Mtandao |
| 2. | Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe Zanzibar |
| 3. | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar |
| 4. | Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani |

### 3.1.1.16 Kutokuwepo kwa Kitengo cha usimamizi wa mali pamoja na Mpango wa matengenezo wa Mali za Taasisi za Umma

Kwa mujibu wa kifungu 59(1) cha Sheria nambari 6 ya ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba "Kutakua na kitengo cha usimamizi wa mali katika kila taasisi ya Umma".

Aidha, kwa mujibu wa kifungu nambari 66 cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba "Kutakuwa na mpango wa matengenezo wa mali utakaoandaliwa na Taasisi ya Umma unaohakikisha kwamba mali zinabaki katika ubora kwa matumizi yaliyokusudiwa.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kutokuwepo kwa kitengo cha Usimamizi wa Mali pamoja na mpango wa matengenezo wa mali ambao unaoonesha utaratibu mzima wa kuzifanyia matengenezo mali/vifaa vinavyomilikiwa na kutumika kwa shughuli za Taasisi jambo ambalo linaweza kupelekea kuwepo kwa uharibifu mkubwa wa mali na hatimae kupelekea kutumia gharama kubwa ya matengenezo au kuwepo kwa upotevu wa mali za Taasisi husika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Taasisi hizo kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kuanzisha Kitengo cha Usimamizi wa Mali pamoja na uandaaji wa mpango wa matengenezo wa mali hizo ili kuepusha uwezekano wa kutokea kwa uharibifu wa mali za Taasisi. Mchanganuo wa Taasisi zenye dosari hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 20: Taasisi zisizokuwa na Kitengo cha Usimamizi wa Mali pamoja na Mpango wa matengenezo wa Mali**

| Namba | Jina la Taasisi |
|---|---|
| 1. | Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar |
| 2. | Wakala wa Matukio ya Kijamii Zanzibar |
| 3. | Wakala wa Majengo Zanzibar |
| 4. | Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo Zanzibar |
| 5. | Shirika la Utangazaji Pemba |
| 6. | Shirika la Magazeti ya Serikali Pemba |
| 7. | Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar |
| 8. | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar |
| 9. | Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya |
| 10. | Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar |

### 3.1.1.17 Kutowasilishwa kwa utekelezaji wa Mpango wa Manunuzi kwa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar

Kanuni nambari 64(2)(c) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya 2020 kinazitaka taasisi za ununuzi na uondoshaji wa mali za umma kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa manunuzi ya robo mwaka kwa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar, ndani ya siku saba baada ya kumalizika mwezi husika au kumalizika kwa robo hiyo ya mwaka.

Aidha, kanuni nambari 64(2)(d) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya 2020 kinazitaka taasisi za ununuzi na uondoshaji wa mali za umma kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa manunuzi ya mwaka kwa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar, ndani ya siku thelathini baada ya kumalizika kwa mwaka wa fedha husika.

Ukaguzi umebaini kuwa Mashirika mengi pamoja na Taasisi Zinazojitegemea za Serikali hazikuwasilisha ripoti za utekelezaji wa Manunuzi ya robo mwaka na ya mwaka kwa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar na nyengine zimewasilisha nje ya muda uliotajwa katika Kanuni za Manunuzi ya Umma ya 2020.

Kutokuwasilisha ripoti za utekelezaji wa Manunuzi ya robo mwaka na ya mwaka kwa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar ni kwenda kinyume na kanuni za manunuzi ambapo pia kunaweza kupelekea Mamlaka ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kushindwa kupata taarifa za utekelezaji wa mipango ya manunuzi ya Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mashirika na Taasisi zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuandaa na kuwasilisha kwa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar taarifa za utekelezaji wa manunuzi kwa wakati kama Sheria na kanuni za manunuzi zinavyoelekeza.

Mashirika ya Umma na Taasisi zinazojitegemea za Serikali zilizobainika kuwa na changamoto ya uwasilishaji wa ripoti za utekelezaji wa Manunuzi ya robo mwaka na ya mwaka kwa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 21: Taasisi Ambazo Hazijawasilisha Mpango wa Manunuzi kwa ZPPDA**

| Namba | Jina la Taasisi | Maelezo |
|---|---|---|
| 1. | Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar | Limechelewa kuwasilisha |
| 2. | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar | Haikuandaa |

# SURA YA NNE









# 4.0 MASHIRIKA YA UMMA YA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

Sura hii inaelezea kwa kina hoja za ukaguzi ikiwemo matokeo na mapendekezo ya ukaguzi wa Ripoti za Mashirika ya Umma na Taasisi zinazojitegemea kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2022/2023.

## 4.1 TATHMINI YA UENDESHAJI WA FAIDA KWA MASHIRIKA YA UMMA NA KAMPUNI ZA SERIKALI

Ukaguzi umebaini kuwa Mashirika na Taasisi nyingi zinazojitegemea za Serikali zimeendelea kufanya vizuri katika kujiendesha kwa faida kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kufanya vizuri huku ni kwa taasisi zinazofunga hesabu kwa mujibu wa mwaka wa fedha wa Serikali na hata zile Taasisi zinazofunga hesabu kwa mujibu wa mwaka wa kalenda.

Hata hivyo ukaguzi umebaini kuwa baadhi ya Mashirika yamekuwa yakichelewesha kuwasilisha gawio la Serikali baada ya kupata faida kinyume na miongozo iliyotolewa na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango. Aidha, tathmini hii imejumuisha baadhi ya mashirika na kampuni ambazo zinajiendesha kwa faida na zile ambazo hazijiendeshi kwa faida kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 22: Ufanisi wa Utendaji wa Mashirika kwa mwaka wa fedha 2022/2023**

| Namba | Mashirika yanayojiendesha kwa Faida | Namba | Mashirika na Kampuni zinazojiendesha kwa hasara |
|---|---|---|---|
| 1. | Shirika la Bandari Zanzibar | 1. | Shirika la Magazeti ya Serikali |
| 2. | Shirika la Biashara la Taifa | 2. | Shirika la Utangazaji Zanzibar |
| 3. | Shirika la Nyumba Zanzibar | 3. | Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta |
| 4. | Benki ya Watu wa Zanzibar | 4. | Kampuni ya Uvuvi |
| 5. | Shirika la Umeme Zanzibar | 5. | Kampuni ya Ujenzi |
| 6. | Shirika la Meli na Uwakala | | |

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Msajili wa Hazina ifanye tathmini ya kina juu uwezo wa Mashirika ya Umma na Taasisi zinazojitegemea za Serikali kwa mujibu wa kiasi walichopangiwa na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ili kuja na mapendekezo ya kiasi halisi kinachoendana na uwezo na hali ya kifedha wa mashirika na Taasisi hizo na hatimae kuziwezesha kulipa gawio kwa wakati unaotakiwa bila ya kuathiri shughuli za uwekezaji na uboreshaji wa utoaji huduma. Hii inatakiwa kwenda sambamba na uharakishaji wa ukamilishaji wa sera ya gawio (dividend policy) ya Serikali.

Aidha, ukaguzi unaishauri Ofisi ya Msajili wa Hazina kufanya tathmini kwa Taasisi nyengine za Serikali ambazo zina uwezo wa kuingia katika kundi la Taasisi za Uwekezaji wa Umma na kuja na ushauri utakaomuwezesha Waziri wa Nchi Ofisi Rais, Fedha na Mipango kuziteua Taasisi hizo kuwa Taasisi za Uwekezaji wa Umma baada ya kupata idhini ya Baraza la Mapinduzi kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 77 cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021.

Hii itasaidia Ofisi ya Msajili wa Hazina kuweza kuzisimamia taasisi hizo pamoja na kuongeza kiwango cha gawio la Serikali.

Katika ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kwamba mfumo wa uwekaji wa kumbukumbu na taarifa mbali mbali za hesabu ikiwemo taarifa za fedha na rasilimali za umma pamoja na mfumo wa udhibiti wa ndani umekuwa ukiimarika ingawa kumejitokeza dosari mbali mbali za kiutendaji.

Katika ukaguzi huo kulijitokeza dosari za kiutendaji kwa baadhi ya Mashirika na Taasisi zinazojitegemea za Serikali ambapo baadhi ya dosari hizo ziliweza kurekebishwa na kupatiwa ufafanuzi wakati wa ukaguzi. Hata hivyo baadhi ya dosari zilizobainika hazikuweza kupatiwa ufafanuzi hadi ukaguzi unakamilika na kupelekea kujitokeza kwa hoja za ukaguzi ambapo matokeo ya ukaguzi huo yameainishwa kupitia taasisi mbalimbali zilizokaguliwa zikiwemo Mashirika, Mamlaka, Wakala na Taasisi nyengine zinazojitegemea za Serikali kama ifuatavyo:-

### 4.1.1 SHIRIKA LA UMEME ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.1.1.1 Ukosefu wa Mita inayotumika kupima Umeme unaoingia na kutoka katika vituo vidogo vya usambazaji umeme na Transfoma

Ukaguzi ulifanya mapitio ya ufanisi wa uendeshaji wa vituo vidogo (sub stations) vya usambazaji wa umeme pamoja na transfoma na kubaini kukosekana kwa mita ya kusoma umeme wa laini kuu unaoingia na kutoka katika vituo vidogo pamoja na Transfoma. Kupitia majadiliano na uongozi wa Shirika la Umeme, ukaguzi ulibaini sababu iliyopelekea dosari hiyo ni ukosefu wa fedha kwa ajili ya mita ya laini kuu na kuchelewa kuwekwa kwa mfumo wa kusoma mita moja kwa moja.

Aidha, ukaguzi ulibaini kuwa haikuwezekana kufuatilia usomaji wa mita kwa umeme ulioingia na kusambazwa (wakiwemo watumiaji wakubwa wa umeme) na vituo vidogo vya umeme kutokana na kukosekana kwa usomaji mita ya laini kuu au katika vituo vidogo vya usambazaji wa umeme.

Kukosekana mita ya laini kuu na vituo vidogo vya usambazaji umeme kwa ajili ya kusoma umeme unaoingia na kutoka kunaweza kusababisha Shirika kushindwa kuelewa umeme unaopotea kutokana na wizi katika eneo maalum na kwa wakati.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Umeme Zanzibar uwasiliane na Serikali Kuu ili kupata fedha za ziada kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya usambazaji wa umeme pamoja na kuhakikisha kuwa mita zote za laini kuu au vituo vidogo vya usambazaji umeme zinapatikana na zinawekwa katika vituo husika ili kuongeza ufanisi katika kubaini wizi au upotevu wa umeme.

#### 4.1.1.2 Ucheleweshaji mkubwa wa kushughulikia malalamiko ya wateja

Ukaguzi ulipitia ufanisi wa uwezo wa Shirika la Umeme Zanzibar katika kushughulikia malalamiko ya wateja kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na kubaini kuwa kati ya malalamiko 20,348 yaliyosajiliwa kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2023 malalamiko 6,163 ya wateja (sawa na asilimia 30) hayakuhudumiwa ndani ya kipindi cha kuanzia siku 1 hadi siku 363, malalamiko 6,794 (sawa na asilimia 33) yalihudumiwa kwa kuchelewa kwa kiasi kikubwa kuanzia muda wa siku 7 hadi siku 355.

Kuchelewa kushughulikia malalamiko ya wateja ni kinyume na aya ya 5.1, 5.2 na 5.3 ya Mkataba wa Wateja wa Shirika la Umeme. Ucheleweshaji wa utatuzi wa malalamiko kunaweza kusababisha kutoridhika kwa wateja na kuharibu hadhi ya Shirika pamoja na uaminifu wa wateja.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Umeme Zanzibar kufanya mapitio ya kina ya michakato ya ushughulikiaji wa malalamiko ya wateja na kufanya maboresho ili kuhakikisha ufanisi na kutathmini mahitaji ya rasilimali, ikiwa ni pamoja na wafanyakazi na teknolojia, ili kukidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye ya wingi wa malalamiko.

### 4.1.1.3 Kutokukusanywa kwa mwaka mzima madeni ya wateja wanaolipa baada ya kutumia umeme shilingi 7,596,399,436.42

Kifungu nambari 7.3(c) cha Muongozo wa Sera na Taratibu za Uhasibu na Fedha wa Shirika la Umeme wa mwaka 2004 unampa mamlaka Meneja Biashara kufuatilia kikamilifu ulipaji wa madeni ya wateja wenye madeni makubwa na kuanzisha taratibu za kukata huduma ya umeme kwa mujibu wa sera zilizowekwa.

Ukaguzi umebaini uwepo wa wateja 42 wanaofanya malipo baada ya matumizi ya umeme (postpaid) ambao hawakufanya malipo yoyote kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa madeni yao wanayodaiwa yenye thamani ya shilingi 7,596,399,436.42.

Ukaguzi ulifanya uchambuzi kwa kulinganisha baina ya bili zote zilizotolewa katika mwaka wa fedha 2022/2023 na muda ziliokaa bila ya kulipwa (age analysis). Uwepo wa wateja hawa kunaibua wasiwasi juu ya kufuata kifungu nilichokinakili hapo juu.

Aidha, ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ina deni kubwa lenye jumla ya shilingi 54,216,259,718. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 13 (shilingi 6,237,350,092.51) kutoka deni la mwaka jana la shilingi 47,978,909,625. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi wa mwaka jana kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022, ilielezwa wasiwasi juu ya madeni haya na kati ya mapendekezo tuliyoyatoa ni umuhimu wa Shirika la Umeme Zanzibar kushirikiana kikamilifu na Mamlaka ya Maji Zanzibar ili kutafuta hatma ya malimbikizo ya madeni yaliyopita na yajayo.

Ukaguzi unapendekeza kwa uongozi wa Shirika la Umeme Zanzibar kuimarisha utaratibu madhubuti wa ukusanyaji wa madeni na hatua za ukataji wa huduma ya umeme kama ilivyoelekeza kifungu 7.3 (c) cha mwongozo wa Shirika pamoja na kuanzisha vipimo vya utendajikazi na taratibu za uwajibikaji kwa ajili ya kufuatilia na kuboresha ufanisi wa ukusanyaji wa madeni.

Mchanganuo wa wateja 42 wanaofanya malipo baada ya matumizi ya umeme (postpaid) ambao hawakufanya malipo yoyote kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kwa madeni yao wanayodaiwa ni kama inavyoonekana hapo chini:-

### Jadweli Nambari 23: Madeni ya muda mrefu yanayodaiwa kwa wateja wa ZECO

| Namba | Nambari ya Hesabu | Jumla ya Deni (Tsh.) | Bakaa ya Deni hadi Tarehe 30/06/2023 (Tsh.) | Kiasi kilicholipwa ndani ya Mwaka 2022/2023 |
|---|---|---|---|---|
| 1. | D000039252 | 164,676,159.62 | 164,676,159.62 | 0 |
| 2. | D000021488 | 115,994,487.77 | 115,994,487.77 | 0 |
| 3. | D000039254 | 102,524,849.59 | 102,524,849.59 | 0 |
| 4. | D000037345 | 56,922,862.27 | 56,922,862.27 | 0 |
| 5. | D000037710 | 56,671,807.52 | 56,671,807.52 | 0 |
| 6. | 000000015N | 51,739,296.81 | 51,739,296.81 | 0 |
| 7. | 000000003K | 51,057,039.61 | 51,057,039.61 | 0 |
| 8. | D000039271 | 42,328,917.84 | 42,328,917.84 | 0 |
| 9. | 000001023N | 37,630,944.58 | 37,630,944.58 | 0 |
| 10. | D000037429 | 35,864,370.57 | 35,864,370.57 | 0 |
| 11. | D000039138 | 29,118,327.21 | 29,118,327.21 | 0 |
| 12. | D000039180 | 29,072,302.79 | 29,072,302.79 | 0 |
| 13. | D000039439 | 18,839,952.19 | 18,839,952.19 | 0 |
| 14. | D000008233 | 14,360,149.65 | 14,360,149.65 | 0 |
| 15. | D000038625 | 14,096,899.32 | 14,096,899.32 | 0 |
| 16. | D000039311 | 6,413,982.83 | 6,413,982.83 | 0 |
| 17. | D000014171 | 5,551,664.40 | 5,551,664.40 | 0 |
| 18. | D000038952 | 4,481,620.58 | 4,481,620.58 | 0 |
| 19. | D000039431 | 4,248,944.57 | 4,248,944.57 | 0 |
| 20. | D000039126 | 3,917,657.15 | 3,917,657.15 | 0 |
| 21. | D000039461 | 3,745,329.47 | 3,745,329.47 | 0 |
| 22. | D000021266 | 3,582,358.23 | 3,582,358.23 | 0 |
| 23. | D000039465 | 3,576,370.70 | 3,576,370.70 | 0 |
| 24. | D000039459 | 3,353,603.16 | 3,353,603.16 | 0 |
| 25. | D000039441 | 3,280,324.35 | 3,280,324.35 | 0 |
| 26. | D000039462 | 2,864,963.55 | 2,864,963.55 | 0 |
| 27. | D000039440 | 2,678,105.07 | 2,678,105.07 | 0 |
| 28. | D000013047 | 2,560,630.92 | 2,560,630.92 | 0 |
| 29. | D000039336 | 1,983,209.52 | 1,983,209.52 | 0 |
| 30. | 000030219W | 1,755,000.78 | 1,755,000.78 | 0 |
| 31. | D000039442 | 1,690,305.05 | 1,690,305.05 | 0 |
| 32. | D000039463 | 1,548,024.75 | 1,548,024.75 | 0 |
| 33. | 000000113M | 210,783,282.59 | 210,783,282.59 | 0 |
| 34. | D000039307 | 44,596,583.58 | 44,596,583.58 | 0 |
| 35. | D000039443 | 47,472,859.05 | 47,472,859.05 | 0 |
| 36. | D000039448 | 8,174,460.00 | 8,174,460.00 | 0 |
| 37. | D000039348 | 23,173,991.01 | 23,173,991.01 | 0 |
| 38. | D000021626 | 16,357,368.49 | 16,357,368.49 | 0 |
| 39. | D000039310 | 12,434,330.03 | 12,434,330.03 | 0 |
| 40. | 000000106O | 43,693,786.48 | 43,693,786.48 | 0 |
| 41. | D000039153 | 74,232,219.77 | 74,232,219.77 | 0 |
| 42. | ZAWA | 6,237,350,092.51 | 6,237,350,092.51 | 0 |
| | **Jumla** | **7,596,399,435.93** | **7,596,399,435.93** | **0** |

*Chanzo: Uchambuzi wa madeni ya wateja na muda wake*

#### 4.1.1.4 Kuchelewa kwa kiasi kikubwa kwa huduma ya uunganishaji umeme kwa wateja

Kifungu namba 2.1 cha Mkataba wa Huduma kwa wateja wa Shirika la Umeme Zanzibar (Customer Charter) wa mwaka 2015 kinaelezea muda unaotarajiwa kwa kila hatua ya mchakato wa uunganishaji huduma ya umeme kwa wateja wapya ili kuhakikisha utoaji wa huduma kwa wakati. Hatua za mchakato huo ni pamoja na usajili, upimaji, makisio ya gharama, malipo, ufungaji mita na uboreshaji wa mfumo.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, ukaguzi ulibaini kuwepo kwa ucheleweshaji mkubwa katika huduma ya uunganishaji umeme kwa wateja wapya kutoka siku 97 hadi siku 238. Muda huu ni kinyume na Mkataba wa Huduma kwa wateja kama ilivyoainishwa katika kifungu namba 2.1 kinachohusiana na ufanisi wa shughuli za uunganishaji umeme kwa wateja.

Baada ya kufanya mahojiano na Uongozi wa Shirika, ukaguzi umebaini kuwa changamoto ya kutofikia muda uliowekwa inatokana na uhaba wa vifaa vya kuunganisha umeme.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Umeme Zanzibar kuhakikisha unafuata muda wa Mkataba wa Huduma kwa wateja kwa kufanya tathmini ya mara kwa mara ya vifaa vinavyohitajika ili kuzuia uhaba wa baadaye katika kukidhi mahitaji ya wateja pamoja na kufanya tathmini na kuwasiliana na mamlaka husika kuhusu uhaba wa wafanyakazi.

#### 4.1.1.5 Ucheleweshaji mkubwa wa kutafuta ufumbuzi wa miamala isiyo ya kawaida iliyomo katika taarifa ya usuluhishi wa kibenki

Ukaguzi ulipitia taarifa za usuluhishi wa kibenki (bank reconciliation statements) na kubaini uwepo wa miamala isiyo ya kawaida ambayo imeshindwa kutafutiwa ufumbuzi kwa zaidi ya miezi miwili (2) ambapo ni kinyume na kifungu nambari 9.8 (c) cha Muongozo wa Sera na Taratibu za Uhasibu na Fedha wa Shirika la Umeme wa mwaka 2004. Miamala hiyo inajumuisha hundi zilizokwishafanyiwa malipo ambazo bado hazijalipwa benki, pamoja na fedha zilizopelekwa benki ambazo bado hazijaingizwa katika hesabu. Kiasi kinachohusika ni kikubwa na kinatia wasiwasi juu ya usahihi wa taarifa za kifedha za Shirika la Umeme.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Umeme Zanzibar kuboresha udhibiti wa ndani unaohusiana na mchakato wa usuluhishi wa kibenki ili kupunguza vihatarishi vya kupata tofauti pamoja na kuhimiza mapitio ya mara kwa mara ya taarifa za usuluhishi wa kibenki ili kugundua na kushughulikia tofauti zinazojitokeza kwa wakati.

#### 4.1.1.6 Mchakato wa ununuzi usio wa ushindani wenye thamani ya shilingi 3.24 bilioni na USD milioni 138.07

Ukaguzi ulipitia majalada 17 ya michakato ya manunuzi na nyaraka nyengine zinazohusiana na mikataba ya manunuzi hayo na kubaini uwepo wa mikataba sita iliyotolewa kwa wazabuni mbalimbali bila kufanya taratibu za ununuzi wa ushindani. Uongozi wa Shirika uliandaa na kutoa tu taarifa za kushinda zabuni (notification of award) au taarifa ya kukubalika kwa zabuni (letter of acceptance) kulikofuatiwa na uingiaji wa mkataba. Hakukuwa na mwaliko wa maombi ya ushindani wala nyaraka za zabuni zilizotumwa kwa wazabuni. Aidha, hakukuwa na michakato ya tathmini ya zabuni wala mazungumzo ya mapatano kabla ya kuingia mkataba. Hii ni kinyume na kifungu cha 66(1)(a)(b) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.

Kushindwa kufuata taratibu za manunuzi za ushindani kunapunguza uwezo wa Shirika kufaidika na bei ya ushindani na pia kukosa thamani halisi ya fedha (Value for Money) katika shughuli za manunuzi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Umeme Zanzibar kuzingatia taratibu zote za ununuzi wa bidhaa kwa kutumia taratibu husika kama zilivyoelezwa katika kifungu nilichokinakili hapo juu. Mchanganuo wa manunuzi yaliyobainika kutokuwa na ushindani ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 24: Manunuzi ya Shirika la Umeme yaliyokosa ushindani**

| No. | Namba ya Zabuni/ Mkataba | Maelezo | Jina la Mzabuni | Kiasi cha Fedha | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Shs. | USD |
| 1. | No. Contract prepared by ZECO | Provision of Software Assurance Agreement | LANDIS + Gyr (Pty) Ltd SA | - | 138,000,000 |
| 2. | ZECO/CW/01/2023/09 | Repair of House No S1 | Isadeco Construction Zanzibar | 35,697,438.00 | - |
| 3. | ZECO/GR/12/2022/26 | Supply of Wooden Poles | Poles (T) Limited | - | 70,924.61 |
| 4. | ZECO/GR/10/2022/17 | Supply of High Tension &Low Tension Materials | VOLEX Electrical & Decorators Co. LTD | 3,121,100,000 | - |
| 5. | ZECO/SR/01/2023/01 | Provide Support& Maintenance for call center System | Soft Net Technologies Limited | 31,049,112 | - |
| **Jumla** | | | | **3,238,096,950** | **138,070,925** |

*Chanzo: Daftari la Mikataba ya manunuzi la ZECO kwa mwaka 2022/23*

### 4.1.1.7 Kutumia njia ya ununuzi isiyosahihi shilingi bilioni 11.63

Jadweli la Tano la Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 linataja viwango vya ukomo vinavyopedekezwa kwa kila njia ya manunuzi vinavyotakiwa kufuatwa na Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji ya Mali za Umma wakati wa mchakato wa zabuni za bidhaa, kazi na huduma za Ushauri elekezi. Kwa upande wa njia ya manunuzi ya maombi ya ushindani, jadweli linaweka wazi kuwa kwa bidhaa, ukomo ni baina ya shilingi milioni 15 hadi shilingi milioni 50, kwa kazi ni baina ya shilingi milioni 20 hadi shilingi milioni 100 na kwa huduma za ushauri elekezi ukomo ni kutoka shilingi milioni 5 hadi shilingi milioni 75.

Kifungu nambari 72(1) – (3) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma inaweza kununua na kuuza kwa njia ya manunuzi ya maombi ya ushindani kwa bidhaa, kazi na huduma za ushauri elekezi zinazopatikana na zilizo tayari. Endapo thamani inayokadiriwa ya mkataba imezidi kizingiti cha zabuni Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma itapata uthibitisho wa awali wa Mamlaka kwa ajili ya kushiriki katika ununuzi na uondoshaji wa mali za umma kwa njia ya uanishaji.

Ukaguzi ulipitia majalada 17 ya mchakato wa manunuzi na nyaraka nyengine zinazohusiana na mikataba na kubaini kuwa uongozi wa Shirika ulinunuwa bidhaa kwa njia ya maombi ya ushindani (open quotation) zenye jumla ya shilingi 11,627,929,490 ambayo ni zaidi ya kizingiti cha juu kinachotakiwa kwa ajili ya kutumia njia hii. Kizingiti cha juu kwa njia hii ya ushindani wa wazi ni shilingi milioni 50. Aidha, ukaguzi haukupata ushahidi wa maombi ya Uongozi wa Shirika kuomba ruhusa kutoka kwa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar (ZPPDA) kwa ajili ya kutumia njia ya maombi ya ushindani.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 72(1)-(3) na jadweli la Tano la Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 na kunazuia ushindani mpana na uwazi na hatimae kukosekana kwa ufanisi wa bei.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Umeme Zanzibar kuhakikisha kuwa manunuzi yote ya Shirika yanafanywa kwa mujibu wa Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 na Kanuni zake za 2020. Mchanganuo wa manunuzi yaliyofanyika kwa njia iliyozidi kizingiti kilichowekwa ni kama yanavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 25: Manunuzi yaliyofanywa kwa njia iliyozidi kizingiti kilichowekwa**

| Namba | Namba ya Mkataba | Maelezo | Jina la Mzabuni | Kiasi (Shs.) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | ZECO/GR/09/2022/16/17 | Supply of Fuel | GAPCO Zanzibar Limited | 4,239,648,000 |
| 2. | ZECO/GR/45/2021/72 | Supply of Miters | BAOBAB Energy System Tanzania | 7,388,281,490 |
| | | **Jumla** | | **11,627,929,490** |

*Chanzo: Majadala ya michakato ya manunuzi na mikataba ya ZECO*

### 4.1.2 SHIRIKA LA BANDARI ZANZIBAR (ZPC)

Ukaguzi wa hesabu za Shirika la Bandari Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.1.2.1 Kukosekana kwa Mshauri elekezi katika miradi ya ujenzi ya Shirika la Bandari yenye thamani ya shilingi 12,500,530,762

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kuwa Shirika la Bandari Zanzibar limeingia mikataba ya kazi za ujenzi na wakandarasi mbali mbali yenye thamani ya shilingi 12,500,530,762 bila ya kuwepo au kuchelewa kuajiriwa kwa mshauri elekezi jambo ambalo linaweza kupelekea kutekelezwa kwa miradi chini ya kiwango kilichopangwa au kuchelewa kukamilika kwa miradi iliyokusudiwa kwa wakati.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar kuhakikisha wanatafuta washauri elekezi wa miradi ya ujenzi mapema iwezekanavyo kabla ya kuanza kazi za ujenzi kwani ushauri wao unaweza kusaidia katika kutathmini uwezo wa wakandarasi na kutatua mapema changamoto katika miradi hiyo. Mchanganuo wa miradi ya ujenzi iliyotekelezwa bila ya kuwepo kwa Mshauri elekezi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 26: Miradi ya Ujenzi iliyoanza kutekelezwa bila ya kuwepo Mshauri Elekezi**

| Jina la Mkataba wa Mradi | Jina la Mkandarasi | Jina la Mshauri elekezi | Thamani ya Mradi (Tshs.) | Tarehe ya Kuanza kwa Mradi | Tarehe ya kuajiriwa Mshauri elekezi |
|---|---|---|---|---|---|
| Mkataba wa Ujenzi wa Eneo la kusubiri,Gala na njia Ya Watembea kwa Miguu katika Bandari ya Mkokotoni | Edge Engineering and Consulting (T) Limited | Hakukua na Mshauri Elekezi | 1,106,822,520 | 21/6/2022 | -- |
| Mkataba wa kuendeleza Bandari ya Mkoani | China Railway Major Bridge Engineering Group Co. Ltd | Anova Consultant Company Limited | 5,778,594,226 | 27/6/2022 | 22/5/2023 |
| Mkataba wa Ujenzi wa Bandari ya Shumba | Comfix and Engineering Limited | -- | 5,615,114,016 | 27/6/2022 | 3/6/2023 |
| **Jumla** | | | **12,500,530,762** | | |

### 4.1.2.2 Kuchelewa kuanza kwa mradi wa ujenzi wa bandari ya Shumba

Shirika la Bandari Zanzibar lilingia mkataba wenye kumbukumbu namba SMZ/F123/W/IRB/2021-2022/44 na kampuni ya M/s Comfix Engineering Limited uliosainiwa tarehe 27 Juni, 2022 kwa thamani ya shilingi 5,615,114,016 pamoja na VAT kwa ajili ya kazi ya usanifu na ujenzi wa Bandari ya Shumba.

Kwa mujibu wa kifungu cha 20 cha Masharti Maalum ya Mkataba (SCC), ilibainishwa kuwa utekelezaji wa mradi huo utakuwa ni wa kipindi cha mwaka mmoja (1) kuanzia tarehe 11 Julai, 2022 na kukamilika tarehe 26 Juni, 2023.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa pamoja na kwamba mkataba wa ujenzi ulishasainiwa lakini hadi ukaguzi unakamilika mnamo tarehe 8 Septemba, 2023 mradi huo bado haujaanza kutekelezwa kama ilivyokubalika.

Kuchelewa kuanza kazi za ujenzi wa Bandari ya Shumba kunapelekea kuchelewa kuondosha kero inayowakabili wananchi pamoja na Shirika kushindwa kufikia malengo iliyojiwekea katika mradi huo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar kuendelea kusimamia na kufuatilia kwa karibu kazi za ujenzi wa Bandari ya Shumba ili malengo yaliyokusudiwa yaweze kufanikiwa.

### 4.1.2.3 Kumaliza muda wa dhamana ya Utendaji kazi (Performance security)

Kanuni ya 29(6) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za 2020 inasema "dhamana ya utendaji (Performance Security) itahifadhiwa na taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma hadi kukamilika kwa mkataba na itatolewa baada ya kutolewa kwa cheti cha kukubali ripoti ya mwisho au cheti cha kukamilika kwa kazi au huduma ikiwa hakuna madai yaliyowasilishwa dhidi ya mzabuni, mdhamini wa mkataba au kampuni ya udhamini".

Mnamo tarehe 27 Juni, 2022 Shirika la Bandari Zanzibar lilisaini mkataba wa shilingi 5,615,114,016 na kampuni ya M/S Comfix and Engineering Limited kwa ajili ya Usanifu na Ujenzi wa Bandari ya Shumba ambao ulitarajiwa kukamilika tarehe 26 Juni, 2023. Kwa mujibu wa mkataba huo Shirika la bandari lilipaswa kulipa malipo ya awali ya shilingi 1,731,752,064 ambapo kampuni ya M/S Comfix and Engineering Limited ilipaswa kutoa dhamana ya utendaji kazi kwa kiasi hicho hicho. Mnamo tarehe 30 Juni, 2022 Kampuni ya M/S Comfix and Engineering Limited iliwasilisha dhamana ya utendaji kazi kutoka KCB Bank Limited kwa ajili ya mkataba huo ambapo Shirika la Bandari pia limefanya malipo ya awali ya shilingi 1,731,752,064 kwa mkandarasi kama inavyotakiwa na mkataba.

Ukaguzi ulibaini kuwa dhamana ya utendaji kazi iliyoletwa na kampuni ya M/S Comfix and Engineering Limited kupitia Benki ya KCB ilimaliza muda wake tarehe 25 Juni, 2023 hata kabla ya kazi ya ujenzi kuanza.

Kumaliza muda wa dhamana ya utendaji kazi kunaweza kusababisha Shirika la Bandari Zanzibar kutorudishiwa malipo ya awali yaliyolipwa endapo kutatokea madai dhidi ya mkandarasi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar kuhakikisha unasimamia kikamilifu mchakato wa ujenzi wa bandari ili hatua za ujenzi zianze kutekelezwa kwa mujibu wa makubaliano yaliyoanishwa katika mkataba pamoja na kuhakikisha kwamba Mkandarasi anawasilisha dhamana mpya ya utendaji kazi kama inavyotakiwa katika mkataba.

### 4.1.2.4 Kutokujumuishwa kwa maoni ya Mwanasheria Mkuu katika mkataba wa ujenzi wa Bandari ya Shumba

Kanuni nambari 47(4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za 2020 inaeleza kuwa "Afisa Masuuli atakapo pokea maoni juu ya rasimu ya mkataba kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, atayajumuisha katika rasimu ya mkataba huo".

Ukaguzi ulibaini kuwa tarehe 23 Juni, 2023 Shirika la Bandari Zanzibar ilipokea barua kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali yenye kumbukumbu namba L.D902VOL.IV/5 kwa ajili ya rasimu ya mkataba wa ujenzi wa bandari ya Shumba ambayo ilijumuisha maoni sita. Miongoni mwa maoni hayo ni kama ifuatavyo:-

(a) Shirika inabidi liandae rasimu ya mkataba mpya kwa kutumia hati ya kawaida iliyotolewa na Mamlaka ya Manunuzi Zanzibar. Pia rasimu ya mkataba ieleze kazi mahususi itakayofanywa na mkandarasi na sio kubuni michoro na kujenga.

(b) Shirika linapaswa kujiridhisha iwapo mkandarasi aliyepewa kazi hiyo ana uwezo wa kukamilisha kazi hiyo kisheria na kutimiza taratibu za usajili na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar.

(c) Shirika hilo lishirikishe kikamilifu Wakala wa Majengo Zanzibar katika ujenzi huo.

Baada ya kupitia mkataba kati ya Shirika la Bandari Zanzibar na kampuni ya M/S Comfix and Engineering Limited unaohusu Usanifu na Ujenzi wa Bandari ya Shumba kwa jumla ya shilingi 5,615,114,016, ukaguzi haukupata ushahidi unaoonyesha kuwa maoni ya Mwanasheria Mkuu yameingizwa kwenye mkataba uliosainiwa.

Kutokutekelezwa kwa mapendekezo kutoka kwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa rasimu ya mikataba liyowasilishwa kunaweza kusababisha Shirika kuingia katika makubaliano ya mikataba isiyo na tija na hatimae linaweza kupata hasara isiyo ya lazima.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar kuhakikisha kuwa mikataba yote ya manunuzi inawasilishwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kabla ya kusainiwa kama inavyotakiwa na kanuni 47(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya 2020 na mapendekezo ya Mwanasheria Mkuu yanafanyiwa kazi na kuingizwa katika mikataba ili kupunguza hatari ya kuingia katika makubaliano ya mikataba ambayo haina tija kwa Serikali.

#### 4.1.2.5 Kutokuwepo kwa usimamizi mzuri wa madeni ya wadaiwa wa Shirika shilingi 1,692,860,807.5

Kifungu nambari 30(1)(2) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa Afisa Masuuli atahusika na usimamizi wa mapato ya Taasisi ya Umma na atachukua hatua zinazofaa kuhakikisha uanzishaji na uendeshaji wa mfumo bora na wa ufanisi wa ukusanyaji na wa uhifadhi wa mapato. Aidha, kanuni ya 23(1)(a) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inasisitiza ukusanyaji wa mapato kwa kueleza kuwa Afisa Masuuli atahakikisha kuwa watu wote wanaopaswa kulipa fedha yoyote kama mapato ya Serikali au stahiki yoyote ya Taasisi ya Umma wanapewa notisi ya madai au notisi yoyote ile ya madeni yanayodaiwa kwa wakati huo.

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kuwa Shirika la Bandari Zanzibar linadai jumla ya shilingi 1,692,860,807.5 zitokanazo na utolewaji wa huduma mbalimbali kwa kampuni mbalimbali pamoja na watu binafsi jambo ambalo limepelekea kutokufikiwa kwa malengo yaliokusudiwa.

Hali hii imesababishwa zaidi na kutokuwepo kwa sera za usimamizi wa madeni (receivable management policies) katika Shirika.

Aidha, ukaguzi umebaini kuwa licha ya wadaiwa hao kutokulipa madeni yao ya muda mrefu wanaendelea kupata huduma zote wanazohitaji kutoka kwa Shirika la bandari.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar kuanzisha sera za usimamizi wa madeni pamoja na kuzisimamia ili kuboresha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na madeni hayo. Mchanganuo wa baadhi ya wafanyabiashara wanaodaiwa na Shirika la Bandari Zanzibar ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 27: Wadaiwa wa Shirika la Bandari Zanzibar

| Jina la Mdaiwa | Tarehe ya Ankara | Muda wa deni tokea kutolewa Ankara (invoice) hadi tarehe 30 Juni, 2023 (Siku) | Bakaa ya deni (Tsh) |
|---|---|---|---|
| **Alghubra** | | | |
| General Journal | 30/06/2022 | | 4,497,090.00 |
| Ankara | 30/07/2022 | 335 | 2,010,660.00 |
| | 30/08/2022 | 304 | 578,940.00 |
| | 31/10/2022 | 242 | 559,606.10 |
| | 29/11/2022 | 213 | 4,112,836.00 |
| | 30/12/2022 | 182 | 2,446,872.00 |
| | 31/01/2023 | 150 | 1,715,889.70 |
| | 28/02/2023 | 122 | 1,087,164.00 |
| | 29/03/2023 | 93 | 2,053,233.00 |
| **Jumla ndogo(A)** | | | **19,062,290.80** |

| ALI SALAMA SHIPPING LINE | | | |
|---|---|---|---|
| General Journal | 30/06/2022 | | 2,078,628.00 |
| Ankara | 30/07/2022 | 335 | 435,714.30 |
| | 31/01/2023 | 150 | 647,519.00 |
| | 28/02/2023 | 122 | 565,561.95 |
| | 28/02/2023 | 122 | 6,323,850.00 |
| | 45126 | 115 | 8,046,090.00 |
| | 29/03/2023 | 93 | 1,047,100.30 |
| **Jumla Ndogo(B)** | | | **19,144,463.55** |

| AZAM MARINE PEMBA | | | |
|---|---|---|---|
| Ankara | 30/08/2022 | 304 | 4,948,922.00 |
| | 30/08/2022 | 304 | 1,698,205.00 |
| | 30/09/2022 | 273 | 5,347,132.00 |
| | 30/09/2022 | 273 | 2,344,528.00 |
| | 31/10/2022 | 242 | 1,567,427.00 |
| | 31/10/2022 | 242 | 5,220,172.00 |
| | 31/10/2022 | 242 | 664,424.00 |
| Payment | 21/11/2022 | | -78,821.00 |
| **Jumla Ndogo(C)** | | | **21,711,989.00** |
| **Jumla kuu(A+B+C)** | | | **59,918,743.35** |

Aidha, ukaguzi umebaini uwepo wa madeni ya muda mrefu ambayo yanatia shaka juu ya ulipwaji wake kutokana na wadaiwa kutokufanya juhudi za ulipaji wa madeni yao jambo ambalo limepelekea kuwepo kwa kiwango kikubwa cha fedha zinazodaiwa na Shirika. Hali hii inaweza kupelekea kukosekana kwa baadhi ya huduma muhimu ambazo zingeweza kutekelezeka iwapo fedha zinazodaiwa zingeweza kulipwa kwa wakati. Mchanganuo wa madeni ambayo yanatia shaka juu ya ulipwaji wake ni kama inavyooneakana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 28: Wadaiwa wa muda mrefu

| Jina la Mdaiwa | Tarehe iliyotolewa huduma. | Kiasi cha deni (Tshs) |
|---|---|---|
| Anna Shipping | 30/06/2022 | 94,629,415.16 |
| Azam Marine | | 52, 334, 394.25 |
| BP Ltd | | 37,608,470.35 |
| Jack Enterprises | | 156,608,868.00 |
| Kamal | | 57,357,105.75 |
| Kilimanjaro First Feries | | 29,672,626.25 |
| Nanai Co Ltd | | 41,718,154.00 |
| Saqar General Trader | | 29,686,440.00 |
| Sohar General Trader | | 173,303,007.00 |
| Tropical Air | | 91,642,505.20 |
| United Trader Enterprises Tzs | | 438,412,069.00 |
| Mansour Abeid | 27/06/2023 | 39,436,824.60 |
| K.F.F Marine Services | 22/06/2023 | 29,255,284.00 |
| Saqar General Trader | 30/03/2023 | 508,240,710.00 |
| **Jumla ndogo** | | **1,632,942,064.15** |

### 4.1.2.6 Kukosekana kwa kumbukumbu za vikao vya kamati ya misamaha na madai

Kanuni nambari 40(2) ya Kanuni za Fedha za Shirika la Bandari Zanzibar kinaeleza kuwa Mkurugenzi wa Fedha kwa kushauriana na Mkurugenzi Mkuu wanaweza kusamehe kiasi kisichozidi asilimia 25 ya deni la huduma ya tozo ya uhifadhi wa mzigo. Ikiwa msamaha ulioombwa ni zaidi ya asilimia 25 ya deni hilo, maombi hayo yatafikishwa kwa kamati ya madai na misamaha kwa kujadiliwa na kupatiwa maamuzi.

Ukaguzi umepitia taarifa mbalimbali zinazohusiana na msamaha wa tozo za uhifadhi zilizotolewa kwa wafanyabiashara tofauti na Shirika la Bandari Zanzibar na kukosa uthibitisho kuwa misamaha hiyo ilitolewa baada ya idhini ya kamati husika. Aidha, tuliona udhaifu katika udhibiti wa ndani kutokana na ukweli kuwa Mkurugenzi Mkuu na Mkurugenzi wa Fedha wamepewa uwezo wa kusamehe hadi asilimia 25 ya tozo ya uhifadhi wa mzigo. Hii inaweza kutumika kama mwanya iwapo Mkurugenzi Mkuu na Mkurugenzi wa Fedha watakuwa na mgongano wa kimaslahi katika ombi la msamaha wa kodi husika.

Aidha, ukaguzi umekosa taarifa juu ya kiasi halisi kilichosamehewa kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Hali hii inaweza kupelekea Shirika kukosa mapato kutokana na kuwepo kwa mianya ya kusamehe tozo ya uhifadhi wa mzigo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar kuweka udhibiti mzuri wa utoaji wa misamaha ya tozo ya uhifadhi mizigo ikiwa ni pamoja na kuweka vizuri kumbukumbu za taarifa zote zinazohusu misamaha hii. Aidha Shirika ni vyema likaainisha mapema sababu zinazofaa kuzingatiwa katika kutoa misahama ya tozo na misamaha mengineyo.

Mchanganuo wa baadhi ya makampuni yalioomba misamaha ya tozo ya uhifadhi mizigo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 29: Orodha ya waombaji wa misamaha ya tozo**

| Jina la kampuni. | Kiwango anachodaiwa (Tshs) | Kiwango cha asilimia iliyosamehewa (%) |
|---|---|---|
| Salalah Investment Ltd Company | 5,597,280.00 | 15 |
| Hamza Brother General Supply | 8,684,800.00 | 25 |
| Darajani General Tyres | 1,736,960.00 | 25 |
| Khamis Ali Khamis | 7,518,700.00 | Haijaainishwa |
| Abrahmani Ali Juma | 2,583,360.00 | 25 |
| Hafidh Talib Omar | 22,066,200.00 | 25 |
| Iri Clearing And Forward | 3,437,120.00 | 25 |
| Muslih Ali Ali | 24,274,660.00 | Haijaainishwa |
| Mourib And Mouhib | 14,392,940.00 | Haijaainishwa |
| Milan Heilmann | 8,163,160.00 | Haijaainishwa |
| Turky Petroleum | 43,314,750.00 | 50 |

### 4.1.2.7 Kushindwa kukusanya tozo ya mizigo na ada ya kukodisha ghala shilingi 546,795,243.75

Kifungu nambari 57(1-3) cha Sheria ya Usimamizi wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, 2004 kinataka wakati bidhaa yoyote itauzwa kwa mnada wa umma, basi mapato ya mauzo hayo yatatumika kwa utaratibu uliowekwa hapa chini katika utekelezaji wa ushuru, gharama za mauzo, kodi mbalimbali, tozo za forodha pamoja na ushuru wa bandari.

Ukaguzi ulibaini kuwa, mnada wa hadhara unaofanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) haukuzingatia utaratibu uliotajwa na Sheria, kwani Shirika la Bandari Zanzibar limekuwa halirejeshewi mapato wanayodai kutokana na mizigo iliyopigwa mnada ikiwemo gharama za kodi ya ghala na uhifadhi za mizigo. Ukaguzi umebaini kuwa kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2023, Shirika la Bandari lilikuwa linadai malipo yenye jumla ya shilingi 546,795,243.75 kutoka kwa wafanyabiashara walioshindwa kutoa mizigo yao mapema na kulazimu Mamlaka ya Mapato Tanzania kupiga mnada wa mizigo yao.

Hali hii inalifanya Shirika kushindwa kupata mapato yake stahiki licha ya kutoa huduma kwa wafanya biashara wenye mizigo husika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari Zanzibar kukaa pamoja na uongozi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania tawi la Zanzibar kwa ajili ya kujadili na kutafuta namna bora ya kutatua tatizo hili kwa maslahi ya pande zote mbili.

Mchanganuo wa Madeni yaliyoshindwa kulipwa kutokana na kupigwa mnada na Mamlaka ya Mapato Tanzania ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 30: Orodha ya madeni yaliyoshindwa kulipwa

| Namba ya Kontena | Ukubwa (ft) | Siku | Gharama za Storage (Tshs) | Gharama za Liftings (Tshs) | Jumla (Tshs.) |
|---|---|---|---|---|---|
| DFSU 773821-6 | 40 | 105 | 20,962,200 | 227,268.75 | 21,189,468.75 |
| CLHU 904320-0 | 40 | 105 | 20,962,200 | 227,268.75 | 21,189,468.75 |
| TCHU 881341-9 | 40 | 105 | 20,962,200 | 227,268.75 | 21,189,468.75 |
| AMFU 878152-0 | 40 | 105 | 20,962,200 | 227,268.75 | 21,189,468.75 |
| DSAU 949686-1 | 40 | 105 | 20,962,200 | 227,268.75 | 21,189,468.75 |
| APZU 321336-0 | 20 | 139 | 14,117,400 | 133,687.50 | 14,251,087.50 |
| DFSU 771716-8 | 40 | 139 | 28,234,800 | 227,268.75 | 28,462,068.75 |
| CMAU 698686-2 | 40 | 158 | 32,298,900 | 227,268.75 | 32,526,168.75 |
| MRSU 309393-4 | 40 | 153 | 31,229,400 | 227,268.75 | 31,456,668.75 |
| MSKU 870976-5 | 40 | 122 | 24,598,500 | 227,268.75 | 24,825,768.75 |
| TCNU 414739-8 | 20 | 210 | 21,710,850 | 133,687.50 | 21,844,537.50 |
| TCKU 207477-7 | 20 | 210 | 21,710,850 | 133,687.50 | 21,844,537.50 |
| DRYU 291366-0 | 20 | 210 | 21,710,850 | 133,687.50 | 21,844,537.50 |
| TCKU 218493-1 | 20 | 179 | 18,395,400 | 133,687.50 | 18,529,087.50 |
| DFSU 307830-4 | 20 | 169 | 17,325,900 | 133,687.50 | 17,459,587.50 |
| DFSU 619132-0 | 40 | 154 | 31,443,300 | 227,268.75 | 31,670,568.75 |
| RFCU 501377.3 | 40 | 154 | 31,443,300 | 227,268.75 | 31,670,568.75 |
| DFSU 752799-9 | 40 | 120 | 24,170,700 | 227,268.75 | 24,397,968.75 |
| FCIU 820678-6 | 40 | 120 | 24,170,700 | 227,268.75 | 24,397,968.75 |
| ESPU 801922-8 | 40 | 120 | 24,170,700 | 227,268.75 | 24,397,968.75 |
| RFSU 501643-2 | 40 | 120 | 24,170,700 | 227,268.75 | 24,397,968.75 |
| DRYU 966710-5 | 40 | 120 | 24,170,700 | 227,268.75 | 24,397,968.75 |
| DRYU 994833-4 | 40 | 111 | 22,245,600 | 227,268.75 | 22,472,868.75 |
| **Jumla** | | | | | **546,795,243.75** |

**SHIRIKA LA BANDARI PEMBA**

#### 4.1.2.8 Malimbikizo ya Madeni ya Mapato shilingi 226,165,354.96

Kifungu nambari 29(1)(b) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa "Afisa Mhasibu wa Taasisi ya Umma atahusika na kusimamia madeni ya Taasisi ya Umma".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Shirika la Bandari Tawi la Pemba linazidai Kampuni Binafsi za Usafirishaji na baadhi ya taasisi za Serikali jumla ya shilingi 226,165,354.96 kutokana na utoaji wa huduma mbali mbali bandarini. Madeni hayo ni ya muda mrefu na hakuna hatua zilizobainika na ukaguzi ambazo zimechukuliwa na Shirika katika kudai madeni hayo, jambo ambalo ni kuikosesha Serikali mapato ambayo yangetumika katika utekelezaji wa shughuli za Serikali ikiwemo miradi ya maendeleo, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Bandari Pemba kuongeza umakini katika kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kufanya ufuatiliaji wa madeni ili yaweze kuongeza mapato Serikalini. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 31: Malimbikizo ya madeni ya mapato ya muda mrefu**

| Namba | Mdaiwa | Deni halisi (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Wakala wa Barabara | 198,375.00 |
| 2. | ZIPA | 2,415,690.00 |
| 3. | GAPCO | 9,255,080.26 |
| 4. | Shirika la Meli Zanzibar | 40,675,392.20 |
| 5. | Azam Marine | 117,520,296.90 |
| 6. | Zanzibar Fast Feries | 56,100,520.60 |
| | **Jumla** | **226,165,354.96** |

*Chanzo: Orodha ya madeni ya Shirika*

### 4.1.3 SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC)

Ukaguzi wa hesabu za Shirika la Biashara la Taifa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.1.3.1 Kushindwa kutekelezwa kwa takwa la kisheria la kuchangia fedha katika Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu

Kifungu nambari 22 cha Sheria nambari 2 ya Maendeleo ya Karafuu ya 2014 kinaelezea kuwa "Vyanzo vya Fedha za Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu vitajumuisha; fedha kutoka Serikalini, michango kutoka kwa wakulima wa karafuu, wauzaji, Shirika la ZSTC na wahusika wengine wa sekta ya karafuu kama ilivyoainishwa katika Kanuni za Sheria hii ...". Aidha, kanuni ya 9 ya Kanuni ya Maendeleo ya karafuu ya 2014 inaeleza kuwa mchango wa fedha katika Mfuko wa Maendeleo ya karafuu utajumuisha; Muuzaji wa karafuu ambae atachangia asilimia 0.5 kwa kila kilo inayouzwa kwa Shirika; Shirika litachangia asilimia 1.5 kwa kila kilo inayouzwa; Mchango wa Serikali; Fedha yoyote iliyopokelewa kutoka kwa michango, misaada, au mapato kutoka kwa uwekezaji.

Wakati wa ukaguzi wangu, nilipitia barua za mawasiliano kati ya Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) na Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuhusu michango ya fedha kwa Sheria ya Maendeleo ya Karafuu. Miongoni mwa barua nilizozipitia ni barua yenye kumbukumbu namba SBT/K.M.20/4/166.VOL.1 ya tarehe 25 Septemba, 2023 kutoka Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC) kwenda Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda ambayo inaelezea changamoto zinazoukabili Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu wa kutopokea fedha zozote kutoka vyanzo vingine kama ilivyoelezwa katika Sheria hiyo.

Ukaguzi ulibaini kuwa ukiachilia mchango kutoka ZSTC hakuna mchango wowote ulioingia katika Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu kutoka maeneo mengine yaliyotajwa kwa ajili ya kuchangia tokea kusainiwa kwa sheria hio.

Kukosekana kwa michango katika Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu kunaathiri uendelevu na ufanisi wa Mfuko katika kufikia malengo yake yaliyokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar kuishauri Serikali juu ya umuhimu wa kuchangia katika Mfuko wa Maendeleo ya Karafuu kama ilivyotajwa katika Sheria ya Maendeleo ya Karafuu nambari 2 ya 2014. Aidha, Shirika linashauriwa kufanya majadiliano na wadau waliotajwa katika Sheria ya Maendeleo ya Karafuu nambari 2 ya 2014 ili kuangalia namna bora ya utekelezaji wa Sheria hiyo.

#### 4.1.3.2 Malimbikizo ya madeni yatokanayo na ukodishwaji wa majengo ya uwekezaji shilingi 233,529,493.04

Kwa mujibu wa Viwango vya Uhasibu vya Kimataifa (IAS 40) Mali ya Uwekezaji ni mali kama vile ardhi, jengo au sehemu ya jengo, au zote mbili ambayo inatumiwa na mmliki kwa madhumuni ya kupata mapato ya kukodisha au kuongezeka kwa thamani ya mali au kwa madhumuni yote mawili.

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kuwa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar linadai jumla ya shilingi 233,529,493.04 ambazo ni madeni ya muda mrefu ya wadaiwa yaliyotokana na wateja waliokodishwa majengo ya uwekezaji ya Shirika.

Hali hii inatokana na ufuatiliaji mdogo wa madeni ya kodi ya muda mrefu ya majengo ya Uwekezaji ya Shirika jambo ambalo limepelekea kuathiri malengo ya kimkakati yaliopangwa pamoja na utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Shirika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar kuongeza jitihada za ufuatiliaji na ukusanyaji wa fedha za madeni ya muda mrefu yanayotokana na kodi za majengo ya uwekezaji ili kuongeza mapato ya Shirika.

Mchanganuo wa madeni ya muda mrefu ya wadaiwa katika majengo ya uwekezaji ya Shirika ni kama yanavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 32: Madeni ya muda mrefu yatokanayo na majengo ya uwekezaji**

| Namba | Majengo yaliyokodishwa | Fedha zinazodaiwa (Tsh.) |
|---|---|---|
| 1. | Jengo la Kitega Uchumi Kinazini | 108,637,521.49 |
| 2. | Jengo la Malindi | 58,565,906.55 |
| 3. | Maghala | 66,326,065.00 |
| **Jumla** | | **233,529,493.04** |

#### 4.1.3.3 Utendaji usioridhisha wa ZSTC Tawi la Dar es Salaam na kusababisha hasara ya shilingi 168,428,564.48

Lengo mojawapo la uanzishwaji wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar ni kufanya shughuli za kibiashara kwa njia ya ushindani na yenye tija kama inavyoelezewa katika Dira ya Shirika.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa uendeshaji wa tawi la Shirika la Dar es Salaam haukuwa mzuri kutokana na kuwepo kwa hasara ya shilingi 168,428,564.48, ambapo gharama zilikuwa juu sana ikilinganishwa na mapato yaliyokusanywa. Kukosekana kwa ufanisi katika uendeshaji wa Tawi la Dar es Salaam kunaongeza gharama zisizo za lazima kwa Shirika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar kutafuta namna bora ya kuimarisha Tawi la Dar es salaam na kutumia fursa ya uwepo wa mahitaji makubwa ya bidhaa kutokana na fursa iliyopo ya idadi kubwa ya watu Tanzania Bara ukilinganisha na Zanzibar.

Mchanganuo wa mapato na matumizi ya tawi la Shirika la Dar es Salaam ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 33: Mapato na Matumizi ya Tawi la ZSTC Dar es Salaam kwa mwaka 2022/2023**

| Maelezo | Kiasi (Tshs.) |
|---|---|
| **Mapato (A)** | 549,526,925.00 |
| **Matumizi:** | |
| Ununuzi wa Malighafi | 498,999,750.61 |
| Kodi na gharama nyenginezo | 67,753,838.87 |
| Mishahara | 151,2021,900.00 |
| **Jumla ya Matumizi ( B)** | **717,955,489.48** |
| **Hasara(A-B)** | **-168,428,564.48** |

#### 4.1.3.4 Kukosekana kwa Hatimiliki kwa baadhi ya Majengo ya Shirika

Kifungu cha 64(1) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaitaka kila Taasisi ya Umma kuweka nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zote zinamilikiwa kisheria na Serikali.

Ukaguzi umebaini kuwa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar linamiliki majengo mbalimbali kisiwani Pemba ambapo baadhi ya majengo hayo hayana hatimiliki jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Hali hii inaweza kupelekea kukosekana kwa uthibitisho wa kisheria wa umiliki wa majengo hayo endapo kutatokea migogoro ya umiliki baina ya Shirika na wananchi wa maeneo husika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar kuhakikisha unasimamia mchakato wa upatikanaji wa hatimiliki za majengo yake ili kuepuka matatizo yanayoweza kutokea kuhusiana na umiliki wa majengo hayo ili kuweza kulinda mali za Serikali.

Orodha ya majengo ya Shirika ambayo hayana hatimiliki ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 34: Majengo ya ZSTC ambayo hayana Hatimiliki**

| Namba | Jina la Jengo | Eneo Liliopo |
|---|---|---|
| 1. | Kituo cha ununuzi wa karafuu | Makongeni Mtambwe |
| 2. | | Chanjaani |
| 3. | | Pandani |
| 4. | | Chonga |

**SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC) PEMBA**

### 4.1.3.5 Hali ya Uchakavu wa majengo ya Shirika

Kifungu nambari 66 (1) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba "Kutakuwa na mpango wa matengenezo ya mali utakaoandaliwa na Taasisi ya Umma unaohakikisha kwamba mali zinabaki katika ubora kwa matumizi yaliyokusudiwa".

Shirika la Biashara la Taifa Pemba linamiliki majengo katika maeneo mbalimbali yakiwemo maghala na vituo vya kununulia karafuu.

Ukaguzi umebaini kuwa majengo mengi yapo katika hali ya Uchakavu mkubwa uliosababishwa na kutokufanyiwa ukarabati kwa wakati jambo ambalo linaweza kupelekea kuzidi kuchakaa kwa majengo hayo na hatimae kubomoka na kuanguka na kuisababishia hasara Serikali jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu cha sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa Pemba kuyafanyia ukarabati kwa wakati majengo ili kuepusha athari zinazoweza kujitokeza baadae.

### 4.1.3.6 Hasara inayotokana na kupungua kwa uzito wa karafuu shilingi 254,358,500

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa upungufu wa kilo za karafuu zilizonunuliwa na Shirika na kuhifadhiwa katika maghala yake yaliyopo Chake Chake, Mkoani na Wete Pemba, ambapo imebainika wakati wa kuzipima tena karafuu hizo kwa ajili ya kuzisafirisha kwenda Makao Makuu ya ZSTC Zanzibar kwa ajili ya kufanyiwa taratibu za mauzo kuwepo kwa upungufu wa kilo 19,159.5 zenye thamani ya shilingi 254,358,500 ambao umetokana na kupungua kwa uzito wa karafuu hizo (Shrinkage) jambo ambalo hupelekea upotevu wa fedha kutokana na kutokupatikana kwa usahihi wa kilo wakati wa kununua na wakati wa kuzisafirisha.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika kubuni njia bora zaidi ya kupunguza hasara inayotokana na kunywea kwa karafuu ikiwemo kununua mashine maalum za kupima kiwango cha unyevu unaohitajika kabla ya kununua karafuu kutoka kwa wakulima kutokana na mashine zilizopo kutokufanya kazi ipasavyo. Mchanganuo wa upungufu wa kilo hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 35:Hasara inayotokana na kupungua kwa uzito wa karafuu

| Namba | Rebage/No Rebage | Grade ya Karafuu | Kilo zilizopungua kwa mwaka (A) | Bei ya karafuu kwa kilo (Tshs) (B) | Jumla ya upungufu (Tshs) (A & B) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Ghala la Chake Chake | Nzuri | 1,514.5 | 14,000 | 21,203,000 |
| | | Wastani | 2,304.5 | 13,000 | 29,958,500 |
| | | Hafifu | 2.5 | 12,000 | 30,000 |
| 2. | Ghala la Wete | Nzuri | 3,471.5 | 14,000 | 48,601,000 |
| | | Wastani | 4,295 | 13,000 | 55,835,000 |
| | | Hafifu | 371.5 | 12,000 | 4,458,000 |
| | | Mpeta | 271 | 7,000 | 1,897,000 |
| 3. | Ghala la Mkoani | Nzuri | 2,683 | 14,000 | 37,562,000 |
| | | Wastani | 4,129.5 | 13,000 | 53,683,500 |
| | | Hafifu | 63 | 12,000 | 756,000 |
| | | Mpeta | 53.5 | 7,000 | 374,500 |
| **Jumla** | | | | | **254,358,500** |

*Chanzo: Taarifa za Shirika*

#### 4.1.3.7 Dosari zilizobainika katika mashine za kupimia ubora wa karafuu

Shirika la Biashara la Taifa limenunua mashine maalumu kwa ajili ya kupimia ubora wa karafuu zinazowasilishwa na wakulima wa zao hilo kwa ajili ya kuuza.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokufanyakazi ipasavyo kwa mashine hizo kama ilivyokusudiwa ambapo imebainika kwamba mashine hizo zinapotumika kupima ubora wa karafuu hazionyeshi uhalisia wa ubora huo jambo ambalo hupelekea wapasishaji wa karafuu kutumia njia nyengine mbadala kama ilivyokuwa inatumika awali.

Aidha, imebainika baadhi ya mashine hizo kutokufanya kazi kabisa, na nyengine hufanyakazi kwa muda na baadae hugoma kufanyakazi jambo ambalo linapelekea ugumu katika upasishaji wa zao hilo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Biashara la Taifa kununua vipimo vyenye ubora na vinavyotoa matokeo sahihi.

### 4.1.4 KAMPUNI YA MWANI ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Kampuni ya Mwani Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.1.4.1 Kuchelewa kukabidhiwa vifaa vya ukulima wa mwani shilingi 1,587,600,000

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika jitihada zake za kuimarisha Sera ya Uchumi wa Buluu na kwa lengo la kuwaondoshea shida mbalimbali wananchi wa Zanzibar zikiwemo za kiuchumi kupitia mradi wa UVIKO - 19 iliamua kununua vifaa mbalimbali kwa ajili ya wakulima wa mwani wa Unguja na Pemba.

Ukaguzi ulihakiki orodha ya vifaa katika ghala la Kampuni ya Mwani vyenye thamani ya shilingi 1,587,600,000 kutoka Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kupitia fedha za ahuweni ya UVIKO 19, vifaa ambavyo vilikabidhiwa tarehe 3 Oktoba, 2022 kwa lengo la kupewa wakulima wa zao la mwani wa Unguja na Pemba. Aidha, ukaguzi ulibaini kutokukabidhiwa kwa walengwa kwa baadhi ya vifaa badala yake vimewekwa katika maghala ya Kampuni.

Kuchelewa kukabidhiwa kwa vifaa hivyo kwa wakulima wa mwani kunaweza kupelekea kutofikiwa kwa lengo la Serikali lililokusudiwa kwa wakati uliopangwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kampuni ya Mwani kuhakikisha unasimamia ipasavyo sera ya uchumi wa Buluu ikiwa ni pamoja na kuharakisha utolewaji wa vifaa hivyo kwa wakulima kama ilivyokusudiwa. Mchanganuo wa vifaa vilivyochelewa kugaiwa kwa wakulima wa mwani ni kama vinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 36: Vifaa vya ukulima wa mwani vilivyochelewa kugaiwa kwa wakulima**

| Namba | Maelezo | Idadi | Kiasi cha Fedha (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1. | Ropes 4mm | 60,000 | 4,212,000 |
| 2. | Tie-tie 1mm | 60,000 | 842,400,000 |
| 3. | Ropes 10mm | 10,000 | 324,000,000 |
| **Jumla** | | | **1,587,600,000** |

### 4.1.4.2 Changamoto zinazowakabili wakulima katika uzalishaji wa zao la Mwani

Uzalishaji wa zao la mwani unazidi kuongezeka kwa kasi baada ya wananchi kupata mwamko wa kutosha kuhusiana na zao hilo hata hivyo kumejitokeza changamoto kunakotokana na kukosekana kwa njia bora ya uanikaji wa mwani, hali iliyopelekea mwani huo kufanya unyevu unyevu unaotokana na chumvi na kuleta shida kwa waanikaji hao kuanika mara kwa mara na kupelekea kukosa kiwango cha ubora kinachotakiwa na wanunuzi. Aidha, ukaguzi umebaini uwepo wa bei ndogo wanayolipwa wakulima ukilinganisha na kazi kubwa wanayoipata katika uzalishaji wa zao hilo.

Kutokuzingatiwa kwa changamoto zinazowakabili wakulima wa zao la mwani kunaweza kupelekea kupungua ari ya uzalishaji wa zao hilo na hivyo kutokufikiwa kwa malengo yaliokusudiwa na Serikali.

Ukaguzi unaishauri Serikali kupitia Kampuni ya mwani kuhakikisha wanawapatia wakulima vifaa vya kuanikia mwani pamoja na kuongeza bei ya ununuzi wa mwani.

### 4.1.4.3 Hasara iliyopatikana kutokana na mwani ulioharibika shilingi 191,692,800 (USD 81,920)

Kampuni ya Mwani (ZASCO) ilifanikiwa kununua wastani wa tani 1,236 za mwani aina ya ULVA, mwani huo ulinunuliwa kwa bei ya shilingi 800 kwa kilo 1. Jumla ya fedha zilizotumika kwa ununuzi wa mwani ni shilingi 718,430,500 na fedha za uendeshaji kwa shughuli za ununuzi wa mwani ni shilingi 139,025,517.

Ukaguzi umebaini kwamba Kampuni ya Mwani (ZASCO) ilisafirisha mwani tani 679.8 aina ya ULVA na kuuzwa kwa Kampuni ya Nutri-san kwa thamani ya shilingi 890,004,960 sawa na USD 380,344. Aidha, ukaguzi umebaini Kampuni ya ZASCO ilipata mrejesho kutoka kwa Kampuni ya Nutri-San kuwa tani 120.47 za mwani zenye thamani ya shilingi 191,692,800 sawa na USD 81,920 kutokufikia ubora uliotakiwa kutokana na kuwa na unyevu mwingi na taka taka zinazozidi kiwango kinachotakiwa na mnunuzi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kampuni ya Mwani kuhakikisha kuwa uchakataji wa mwani unafanywa kutokana na viwango bora ili kuweza kupata faida na kuzuia uwezekano wa kuingia hasara kwa Kampuni. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 37: Hasara itokanayo na mwani ulioharibika**

| Tani zilizosafirishwa | Thamani ya fedha (USD) | Tani zilizoharibika | Pesa zilizokatwa (USD) | Tani zilizolipwa | Pesa zilizolipwa (USD) |
|---|---|---|---|---|---|
| 679.8 | 462,264 | 120.47 | 81,920 | 559.33 | 380,344 |

### 4.1.5 SHIRIKA LA MELI NA UWAKALA ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.1.5.1 Mkataba unaotekelezwa bila kuwasilishwa dhamana ya utendaji kazi (Performance Security)

Kanuni nambari 29(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya 2020 inamtaka mzabuni aliyeshinda zabuni kuwasilisha dhamana ya utendaji kazi (Performance Security) ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa mkataba wake.

Shirika la Meli la Zanzibar limeingia mkataba na kampuni ya Zanzibar Agency Tally (ZAG-TAC) kwa ajili ya Utoaji wa Huduma za Ufuatiliaji wa mwenendo wa makontena (tracing and tracking), huduma za ulinzi pamoja na uthibitishaji wa taarifa za makontena (Tallying) katika bandari ya Malindi Zanzibar.

Kifungu cha 28 cha mkataba kati ya Shirika la Meli la Zanzibar na Zanzibar Agency Tally (ZAG-TAC) kinaeleza kuwa Mtoa Huduma (ZAG-TAC) atawasilisha dhamana ya utendaji kazi kwa mwajiri (Shirika la Meli la Zanzibar) kabla ya tarehe iliyoainishwa katika barua ya kukubali zabuni hiyo. Dhamana ya utendaji kazi itatolewa katika kiasi, aina na benki au mdhamini anayekubalika kwa mwajiri, na kujumuishwa katika aina na uwiano wa sarafu ambayo bei ya mkataba inayolipwa.

Ukaguzi umebaini kuwa Mtoa huduma (ZAG-TAC) hakuwasilisha dhamana ya utendaji kazi (Performance Security) kwa Mwajiri (Shirika la Meli la Zanzibar) licha ya ukweli kuwa Mtoa Huduma bado anendelea na utekelezaji wa majukumu yake.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 28 cha mkataba baina ya Shirika la Meli la Zanzibar na Kampuni ya Zanzibar Agency Tally (ZAG-TAC) na kupelekea Shirika kukosa kidhibiti endapo Mtoa Huduma atashindwa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa mkataba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar kuzingatia miongozo ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya 2020 pamoja na masharti ya Mkataba ili kuhakikisha maslahi ya Serikali yanapatikana katika utekelezaji wa mikataba.

### 4.1.5.2 Wasiwasi juu ya Ulipwaji wa deni kutoka Kampuni ya GBP TANZANIA shilingi 1,406,195,716.28

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar limeingia katika makubaliano ya mikataba ya ukodishwaji wa meli yake ya MT UKOMBOZI na Kampuni ya GBP TANZANIA. Makubaliano hayo yalikuwa ni ya ukodishwaji meli kwa kodi ya safari (voyage charter) ambapo malipo ya ukodishwaji hulipwa kwa kuzingatia uzito wa mzigo (wa mafuta) uliobebwa katika safari husika.

Wakati wa ukaguzi wetu, ilibainika kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 kampuni ya GBP TANZANIA LTD ilikuwa inadaiwa na Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar deni lenye jumla ya shilingi 1,406,195,716.28 ambalo limebakia bila ya kulipwa kwa muda wa zaidi ya mwaka mmoja. Ukaguzi umebaini kuwa deni hili limesababishwa kutokana na kutokukubaliana baina ya Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar na kampuni ya GBP juu ya vipimo vinavyotumika katika upimaji wa uzito wa mafuta.

Uwepo wa deni hili kumesababisha Shirika kukosa fedha ambazo zingelisaidia Shirika katika uendeshaji wa kazi zake za kila siku.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar kwa kushirikiana na taasisi nyengine za Serikali ikiwemo ZURA na ZBS kukaa pamoja na Kampuni ya GBP ili kutafuta ufumbuzi wa suala hili ili hatimae fedha ya deni la Shirika iweze kukusanywa.

### 4.1.5.3 Kutokuwepo kwa mkataba baina ya Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar na kampuni ya ZALAGACO

Kanuni ya 83(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya 2020 inaeleza kuwa Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za umma itawajibika kwa usimamizi mzuri wa mkataba wa ununuzi wowote wa bidhaa, huduma au kazi za ujenzi. Aidha, kifungu nambari 63(3) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza kwamba "kukubaliwa kwa zabuni kutaidhinishwa kwa mkataba wa maandishi utakaosainiwa na pande zote mbili Mtoa huduma na Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji **...**"

Ukaguzi umebaini kuwa Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar lilikuwa likiilipa kampuni ya ZALAGACO kwa huduma mbalimbali wanazozitoa za ufungaji na ufunguaji makontena ya Shirika pasi na kuwepo kwa makubaliano halali ya mkataba kwani mkataba uliopo tayari umeshapita muda wake.

Kwa kukosekana makubaliano baina ya pande hizo mbili kuna uwezekano huduma zisitolewe kama Shirika linavyotarajia. Aidha huwa ni vigumu kwa Shirika kuweza kutatua mgogoro pindi utakapoibuka.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar kuhakikisha kunakuwepo mkataba halali baina yake na Mtoa huduma ili kuhakikisha Mtoa huduma anatoa huduma kwa mujibu wa makubaliano.

### 4.1.5.4 Malipo yaliyofanywa bila ya upatikanaji wa huduma zilizokusudiwa shilingi 32,260,000

Jumla ya shilingi 32,260,000 zililipwa kwa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar (e-GAZ) kwa ajili ya ununuzi wa Mfumo wa Uhasibu katika Shirika la Meli.

Hata hivyo hadi ukaguzi unakamilika mfumo huo ulikuwa haujakamilika wala kufanya kazi kama ilivyotarajiwa na Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar. Aidha, ilibainika kuwa hakukuwa na mkataba kati ya Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar na Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar hali iliyopelekea Shirika kushindwa kutatua changamoto ilizokabiliana nazo katika ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar uwasiliane na Wakala wa Serikali Mtandao ili kuweza kupata mfumo huo wa uhasibu na kuweza kutumika kama ilivyotarajiwa.

#### 4.1.5.5 Malipo yaliyofanyika kinyume na bajeti iliyoidhinishwa shilingi 174,865,205

Kanuni ya 22 ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za 2021 inaeleza kuwa "Afisa Masuuli hatoingia dhima au kulipa deni lolote ambalo fedha zake hazikuwemo katika bajeti".

Katika ukaguzi wetu wa Shirika la Meli na Uwakala kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ukaguzi umebaini kuwa Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar lilitumia jumla ya shilingi 174,865,205 ikiwa ni zaidi ya fedha zilizoidhinishwa katika bajeti ambapo ukaguzi umekosa ushahidi wa uwepo wa idhini ya Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika juu ya uhaulishaji wa fedha kuruhusu malipo hayo.

Kufanya matumizi zaidi ya bajeti iliyopitishwa ni kwenda kinyume na Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za 2021 na kunapelekea udhibiti dhaifu wa matumizi ya fedha za umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Meli na Uwakala Zanzibar kuimarisha udhibiti wa bajeti utakaohakikisha kunakuwepo na uwiano kati ya matumizi halisi na bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka husika. Aidha, uongozi wa Shirika uhakikishe hakuna matumizi yanayofanywa zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa pasi na kupata idhini ya Bodi ya Wakurugenzi au mamlaka nyengine husika.

Mchanganuo wa vifungu vilivyobainika kuzidi bajeti iliyoidhinishwa ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 38: Matumizi ya Shirika la Meli yaliyozidi bajeti iliyoidhinishwa**

| Maelezo | Kiasi cha Bajeti (Tsh.) | Matumizi Halisi (Tsh.) | Tofauti (Tsh.) | Asilimia ya Matumizi Halisi (%) |
|---|---|---|---|---|
| Printings & Stationeries | 24,451,600 | 32,775,120 | -8,320,520 | 134 |
| Staff Transport Office | 72,885,000 | 212,751,685 | -139,866,685 | 292 |
| Public relation | 10,000,000 | 18,000,000 | -8,000,000 | 180 |
| Donations | 6,000,000 | 24,678,000 | -18,678,000 | 411 |
| **Jumla** | **113,336,600** | **288,204,805** | **-174,865,205** | |

### 4.1.6 SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR (ZBC)

Ukaguzi wa hesabu za Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.1.6.1 Uchakavu wa jengo la Karume House

Katika kupitia na kukagua hesabu ya mwisho wa mwaka ukaguzi umebaini uwepo wa uchakavu unaolikabili jengo la Karume House ambapo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya shilingi 38,316,604 zilitumika kwa ajili ya kufanya maboresho katika maeneo mbali mbali yaliyokuwa na uchakavu. Aidha kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Shirika la Utangazaji Zanzibar lilitumia jumla ya shilingi 15,153,496 sawa na asilimia 39.55 ya fedha iliyotumika kwa mwaka uliopita.

Kutokana na tathmini iliyofanywa na ukaguzi imebaini uwepo wa upungufu wa gharama kwa asilimia 39.55 kwenye ukarabati wa jengo inayotumiwa kwa kila mwaka, hii ni kutokana na jengo hilo kuwa la zamani na linahitaji matengenezo makubwa.

Pamoja na uwepo wa upungufu wa gharama iliyotumika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuchukuwa jitihada za makusudi kupeleka ombi maalum Serikalini la kupatiwa eneo na kujengewa jengo la kisasa ambalo litaendana na hadhi ya kituo cha Kurushia Maudhui cha Serikali.

#### 4.1.6.2 Kukosekana kwa vifaa vya kisasa vya kutendea kazi

Miongoni mwa malengo ya Shirika la Utangazaji Zanzibar ni kuwa kituo kikuu cha utoaji wa habari sahihi na kwa wakati zenye kuaminika na kuleta tija kwa jamii.

Katika kufikia azma hiyo ukaguzi umebaini Shirika la Utangazaji Zanzibar linakabiliwa na changamoto ya upungufu wa vifaa pamoja na kutokuwa na vifaa vya kisasa vya kurushia maudhui, miongoni mwa vifaa hivyo ni pamoja na Gari la kurushia matangazo "Outside Broadcasting Van (OBVAN)" ambayo hutumika kurahisisha kutoa matangazo nje ya Studio za ZBC jambo ambalo limepelekea Shirika kulazimika kutumia huduma za kuomba umeme sehemu ya karibu wakati inapohitajika kutoa huduma ya matangazo nje ya studio zao.

Aidha, kwa upande wa Pemba Shirika linakabiliwa na uchakavu mkubwa wa vifaa pamoja na upungufu wa vitendea kazi ikiwemo uwepo wa gari moja ambayo haikidhi mahitaji katika shughuli za ufuatiliaji wa maudhui na utoaji wa huduma za kiofisi hasa ukizingatia Jiografia ya kisiwa cha Pemba.

Kutokana na changamoto hiyo ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Utangazaji Zanzibar kuhakikisha unaandaa na kuwasilisha Serikalini waraka maalum wa mahitaji ya vifaa vinavyohitajika ili viweze kutengewa bajeti maalum ya maendeleo kwa lengo la kupatiwa vifaa hivyo na kutatuliwa changamoto inayopelekea Shirika kutokuwa na ufanisi katika utekelezaji wake wa majukumu.

#### 4.1.6.3 Kutokuwepo kwa Mfumo madhubuti wa kuhifadhi maudhui (Media Asset Management System)

Shirika la Utangazaji ndio Chombo Kikuu cha Serikali chenye dhamana ya kukusanya habari zenye viwango, kutowa taarifa na habari na kuandaa vipindi vyenye ubora kwa jamii.

Katika kutekeleza majukumu ya ukaguzi, wakaguzi walikagua taarifa mbali mbali pamoja na mazingira ya Shirika na kubaini kutokuwepo kwa mfumo madhubuti wa kuhifadhi maudhui (Media Asset Management System), pamoja na "off site Back up" ya Maudhui ambazo ni muhimu sana katika kulisaidia Shirika kuhifadhi na kurejesha kumbukumbu za taarifa zote iwapo yatatokea majanga yasiotarajiwa kama vile mafuriko, radi, moto, umeme na mengineo.

Kutokuwepo kwa mfumo madhubuti wa kuhifadhia maudhui pamoja na "off site Back up" ni hatari kwa ZBC kwani kunauwezekano mkubwa wa kupoteza kumbukumbu muhimu za Shirika wakati majanga yanapotokezea.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa ZBC kuweka mfumo madhubuti wa kuhifadhi maudhui (media Asset Management System) pamoja na kuanzisha utaratibu wa kuwa na "off site Back up" ili iweze kutumika wakati wa dharura**.**

### 4.1.6.4 Kuvuja kwa Studio ya kutayarishia na kurushia matangazo Mkoroshoni PEMBA

Katika kupitia na kukagua mazingiza ya ZBC Pemba, ukaguzi umebaini kuwepo kwa hali isioridhisha katika jengo kogwe la Studio liliopo Mkoroshoni Pemba ambalo linatumika kutayarisha na kurushia matangazo. Wakati wa Ukaguzi unatembelea umeshuhudia studio hiyo kuvuja katika sehemu ya mitambo na kupelekea mitambo kufunikwa turubali ili kuepusha kuathirika na maji ya mvua, iwapo hatua za dharura hazitachukuliwa kunauwezekano mkubwa wa Shirika la Utangazaji ZBC na Serikali kwa ujumla kupata hasara kutokana na hali hiyo.

Kushidwa kufikia malengo ya Shirika na kuathirika kwa mitambo inayotumika kwa utangazaji ambayo imegharimu fedha nyingi za Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Utangazaji Zanzibar kulifanyia ukarabati jengo la studio hususan sehemu ya mitambo ili kuepuka hasara inyoweza kuigharimu Serikali.

### 4.1.6.5 Kukaimu katika nafasi za utumishi kinyume na utaratibu

Kwa mujibu wa kanuni nambari 20(6) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inaeleza kwamba "kwa kuzingatia masharti ya kifungu hiki hakuna nafasi ya kukaimu zaidi ya muda wa miezi kumi na mbili (12) mfululizo kutoka tarehe ya uteuzi wa kukaimu isipokuwa muhusika atathibitishwa katika wadhifa huo au mwenye dhamana atakaporejea."

Ukaguzi umebaini kwamba Shirika la Utangazaji Zanzibar limewakaimisha watumishi wawili nafasi za Utumishi kwa kipindi cha zaidi ya miaka mitatu (3) jambo ambalo ni kinyume na kanuni ya Utumishi wa Umma niliyoinakili hapo juu.

Kuendelea kuwakaimisha watumishi hao kwa zaidi ya kipindi kilichoelezwa kwa mujibu wa sheria kunapelekea kuwapunguzia hamasa na kuwavunja moyo watendaji hao katika utekelekezaji wao wa majukumu, na hivyo inaweza kusababisha kukosekana kwa ufanisi na tija iliyokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Utangazaji Zanzibar kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha watumishi hao wanathibitishwa au unaandaliwa utaratibu wa kuwateuwa watumishi wengine wenye sifa toshelevu za kushika nafasi hizo.

Mchanganuo wa watumishi waliokaimu kwa zaidi ya kipindi kilichoainishwa kwa mujibu wa sheria ni kama inavyonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 39: Watumishi waliokaimu nafasi kinyume na utaratibu**

| Namba | Nafasi Inayokaimiwa | Muda wa Kukaimu |
|---|---|---|
| 1. | Mkuu wa Kituo | 15/3/20219 mpaka sasa 2024 |
| 2. | Mkurugenzi Idara ya Masoko na Uwekezaji | 16/7/2021 mpaka sasa 2024 |

**Mapungufu katika kituo cha Utangazaji Dar es Salaam**

Shirika la Utangazaji (ZBC) linaendesha shughuli zake katika studio zake zilizoko Dar-es-Salaam kwa muda mrefu. Katika kupitia na kukagua nyaraka na mazingira ya Shirika la utangazaji ukaguzi ulitembelea katika kituo hicho na kubaini dosari mbali mbali ambazo zinachangia kupunguza ufanisi katika utekelezaji wa kazi pamoja na kushindwa kuleta ushindani wa kibiashara na mashirika au taasisi nyengine za utangazaji. Dosari zilizobainika ni kama zifuatazo: -

- Studio ya kutangazia kutokuwa na "sound proof" (sauti ya nje inaingia ndani na ya ndani inatoka nje) kutokana na ujenzi wake haukujengwa kwa madhumuni ya studio.
- Ufinyu wa nafasi katika chumba cha studio ambayo haitoshelezi mahitaji na ushindani wa kibiashara.
- Kukosekana kwa Ofisi ya Mkuu wa kituo.
- Kutokuwepo kwa sehemu ya kupokelea wageni wanaohitaji huduma ya Shirika
- Vitendea kazi havikidhi mahitaji ya Ofisi kutokana na kuchakaa sana na uchache wa vifaa hivyo jambo ambalo linapelekea kushindwa kuleta ushindani wa kibiashara.
- Kutokuwa na bajeti ya kuendesha kituo.
- Kutopatiwa masurufu (imprest) kwa matumizi ya dharura.

Kuwepo kwa dosari katika kituo hicho kunapelekea kupunguza ufanisi katika utendaji jambo ambalo linapelekea kukosa mapato ya shirika na kushindwa kumudu ushindani wa biashara katika soko la habari na utangazaji.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Utangazaji Zanzibar kuziangalia changamoto hizo kwa upana na kutafuta sehemu sahihi ya kuendeleza shughuli zake za utangazaji kwa faida ya Shirika na Serikali kwa ujumla.

### 4.1.6.7 Kukosekana kwa hatimiliki

Shirika la Utangazaji la Zanzibar linamiliki maeneo mawili ambayo ni eneo la Redio Rahaleo na eneo la Urushaji wa Maudhui Dole ambayo yanatumika kwa shughuli za urushaji matangazo mbali mbali kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa.

Katika ukaguzi wa mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kutokuwepo kwa uthibitisho unaoonesha umiliki halali wa maeneo hayo jambo ambalo linaweza kupelekea kulinyima Shirika fursa za umiliki ikiwa Shirika litashindwa kusimamia na kufuatilia kikamilifu upatikanaji wa hati miliki za eneo la Rahaleo na Dole kwa mujibu wa sheria.

Kutokuwepo kwa hati miliki za umiliki wa majengo kunapelekea kutothibitika uhalali wa maeneo hayo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Utangazaji Zanzibar kufuatilia upatikanaji wa hatimiliki ili kulinda maeneo yao yasichukuliwe na wananchi ama mamlaka nyengine za Serikali.

### 4.1.6.8 Malimbikizo ya Madeni ya muda mrefu shilingi 353,893,200

Ukaguzi umepitia na kukagua nyaraka mbali mbali ikiwemo hesabu ya mwisho wa mwaka na kubaini kwamba jumla ya taasisi 82 za Serikali na binafsi zinadaiwa na Shirika la Utangazaji (ZBC) kiasi cha shilingi 353,893,200 kutokana na huduma mbali mali walizopatiwa na Shirika hilo.

Kutolipwa kwa wakati unaostahiki madeni ya Shirika kunapelekea kusuasua kwa utekelezaji wa majukumu ya Shirika hivyo kushidwa kufikia malengo yaliowekwa kwa wakati jambo ambalo linarejesha nyuma maendeleo ya Shirika hilo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Utangazaji Zanzibar kuweka mikakati maalum na kuchukuwa hatua madhubuti katika kusimamia ulipaji wa madeni ili kufikia malengo yaliowekwa na kuongeza ufanisi kwa Shirika na Serikali kwa ujumla. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 40: Madeni yanayodaiwa na Shirika la Utangazaji Zanzibar**

| Namba | Taasisi Inayodaiwa | Deni Halisi (Tsh.) |
|---|---|---|
| 1. | Shirika la Umeme | 16,518,450.00 |
| 2. | Afisi ya Rais Fedha na Mipango | 15,674,250.00 |
| 3. | Wizara ya Afya | 13,059,500.00 |
| 4. | Baraza la Manispaa Magharibi A | 3,298,750.00 |
| 5. | Baraza la Manispaa Mjini | 18,475,250.00 |
| 6. | Mamlaka ya Maji Zanzibar | 12,660,100.00 |
| 7. | Baraza la Manispaa Magharibi B | 4,759,750.00 |
| 8. | Tume ya Utumishi Serikalini | 3,249,000.00 |
| 9. | Bodi ya Wathamini | 92,000.00 |
| 10. | Baraza la Jiji Zanzibar | 529,000.00 |
| 11. | Baraza la Mji Kati Unguja | 2,296,500.00 |
| 12. | Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda | 8,846,250.00 |
| 13. | Chuo cha Utawala wa Umma | 3,036,500.00 |
| 14. | Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa | 1,000,000.00 |
| 15. | Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa | 2,130,500.00 |
| 16. | Kamisheni ya Utalii | 100,000.00 |
| 17. | Wizara ya Elimu na Mafunzo na Amali | 15,490,300.00 |
| 18. | Baraza la Mji Kaskazini "A" | 2,043,500.00 |
| 19. | Baraza la Mji Kaskazini B | 534,750.00 |
| 20. | Afisi ya Mufti Mkuu | 310,500.00 |
| 21. | Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar | 253,000.00 |
| 22. | Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale | 4,195,000.00 |
| 23. | Mamlaka ya Mapato Zanzibar | 3,174,000.00 |
| 24. | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii | 1,909,000.00 |
| 25. | Shirika la Bandari | 465,750.00 |
| 26. | Zanzibar University | 3,027,000.00 |
| 27. | Mahakama Kuu Zanzibar | 86,250.00 |
| 28. | Wakala wa Barabara | 46,000.00 |
| 29. | Mamlaka ya Usafiri Baharini | 3,737,250.00 |

| Namba | Taasisi Inayodaiwa | Deni Halisi (Tsh.) |
|---|---|---|
| 30. | Afisi ya Rais Katiba Sheria Utumishi na Utawala Bora | 103,500.00 |
| 31. | Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi | 155,250.00 |
| 32. | Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji | 10,160,850.00 |
| 33. | Baraza la Sanaa Sensa ya Filamu na Utamaduni | 310,500.00 |
| 34. | Mamlaka ya Mafunzo ya Amali | 2,185,000.00 |
| 35. | Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi | 138,000.00 |
| 36. | Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii | 927,700.00 |
| 37. | Kamisheni ya Ardhi | 2,880,750.00 |
| 38. | Baraza la Kuwakilisha Watumiaji wa Huduma za Nishati | 490,000.00 |
| 39. | NIDA | 120,000.00 |
| 40. | TCRA | 420,000.00 |
| 41. | Wizara ya Maendeleo ya Jamii  Jinsia, Wazee na Watoto | 155,250.00 |
| 42. | Chuo Kikuu  cha Taifa cha Zanizibar | 2,162,000.00 |
| 43. | Jeshi la Kujenga Uchumi | 184,000.00 |
| 44. | Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani | 92,000.00 |
| 45. | Mahkama ya Ardhi Zanzibar | 69,000.00 |
| 46. | Tume ya Ushindani Halali wa Biashara | 46,000.00 |
| 47. | Baraza la Mji Kaskazini B | 1,302,000.00 |
| 48. | Chama cha Walimu Zanzibar | 155,250.00 |
| 49. | Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi | 1,091,250.00 |
| 50. | Halmashauri ya Wilaya ya Kusini Unguja | 103,500.00 |
| 51. | Afisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kusini | 115,000.00 |
| 52. | Shirika la Bandari Zanzibar | 293,250.00 |
| 53. | Mahakama Kuu | 172,500.00 |
| 54. | Wizara ya Maji Nishati na Madini | 3,500,000.00 |
| 55. | Umoja wa Wazazi CCM | 1,500,000.00 |
| 56. | Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira | 345,000.00 |
| 57. | Tume ya Ukimwi Zanzibar | 2,400,000.00 |
| 58. | Idara ya Utawala Bora | 4,140,000.00 |
| 59. | Shirika la Biashara la Taifa ZSTC | 310,500.00 |
| 60. | Taasisi ya Utafiti wa Kilimo | 92,000.00 |
| 61. | Shirika la Meli Zanzibar | 207,000.00 |
| 62. | Bodi ya Kondominio | 138,000.00 |
| 63. | Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikal Zanzibar | 3,938,750.00 |
| 64. | Tume ya Taifa ya Uchaguzi | 10,828,500.00 |
| 65. | Idara ya Mazingira | 345,000.00 |
| 66. | Taasisi ya Viwango Zanzibar | 2,296,000.00 |
| 67. | Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo | 2,700,800.00 |
| 68. | Baraza la Wawakilishi | 67,875,000.00 |
| 69. | Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar | 414,000.00 |
| 70. | Benki ya Watu wa Zanzibar Limited | 10,350,000.00 |
| 71. | ZPRA | 805,000.00 |
| 72. | Shirika la Bima Zanzibar | 3,888,000.00 |
| 73. | Kamisheni  ya Kukabiliana na Maafa | 552,000.00 |

| Namba | Taasisi Inayodaiwa | Deni Halisi (Tsh.) |
|---|---|---|
| 74. | Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu | 2,031,600.00 |
| 75. | ZFDA | 922,000.00 |
| 76. | Mamlaka ya Manunuzi Zanzibar | 4,564,200.00 |
| 77. | Wizara ya Mawasiliano | 10,422,000.00 |
| 78. | TAMWA | 7,450,000.00 |
| 79. | Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Idara Maalum | 3,677,500.00 |
| 80. | Taasisi ya Sayansi ya Karume | 1,769,700.00 |
| 81. | Zanzibar Connection | 9,600,000.00 |
| 82. | Bahari FM | 32,000,000.00 |
| **Jumla** | | **353,893,200** |

**SHIRIKA LA UTANGAZAJI PEMBA**

### 4.1.6.9 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 10,539,676

Kanuni nambari 57(1)(2)(b) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaeleza kuwa "Malipo yote lazima yaambatanishwe na hati ya malipo ambayo imekamilika vielelezo vyote kwa mujibu wa maelekezo ya Hazina na kuidhinishwa na Afisa Mhasibu".

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 10,539,676 zimetumika kwa matumizi mbali mbali ya Shirika la Utangazaji Pemba lakini baadhi ya vielelezo husika havikuambatanishwa katika hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo na mapokezi ya bidhaa zilizonunuliwa, aidha ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Hali hiyo imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani na uhifadhi wa vielelezo vya fedha na vielelezo vyengine vinavyohusiana na uendeshaji wa kazi za Shirika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika kuhakikisha malipo yote yanayofanyika yanaambatishwa na nyaraka za malipo husika kwa wakati ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo. Mchanganuo wa hati za malipo zenye vielelezo pungufu ni kama inavyoonekana katka jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 41: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu**

| Namba | Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| | 01/07 ya 11/07/2022 | 000259 | 4,637,136 | Mbukilage Partnership | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya uchimbaji wa kisima. |
| | 01/09 ya 05/09/2022 | T.O | 5,902,540 | | |
| **Jumla** | | | **10,539,676** | | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati za malipo.*

### 4.1.6.10 Mikataba ya ukodishaji minara ambayo haikupatikana kwa ukaguzi

Kanuni nambari 57(1)(2)(b) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaeleza kuwa "Malipo yote lazima yaambatanishwe na hati ya malipo ambayo imekamilika vielelezo vyote kwa mujibu wa maelekezo ya Hazina na kuidhinishwa na Afisa Mhasibu".

Ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Shirika la Utangazaji Pemba limeingia mikataba na taasisi mbali mbali kwa ajili ya kukodisha minara ya kurushia matangazo iliyoko Pemba, dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokuwepo kwa mikataba ya ukodishaji wa minara hiyo jambo ambalo linapelekea kushindwa kujiridhisha juu ya uhalali wa ukodishwaji huo, aidha ni kwenda na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Utangazaji Pemba kuweka kumbukumbu zote za ukodishwaji wa minara na kuziwasilisha kwa ukaguzi. Mchanganuo wa Mikataba hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 42: Mikataba ya ukodishwaji Minara ambayo haikupatikana kwa ukaguzi**

| Namba | Aliyekodishwa |
|---|---|
| 1. | Zenj FM Redio |
| 2. | Redio Nuru |
| 3. | Redio Maria |
| 4. | Redio Istiqama |
| 5. | Wizara ya Elimu |
| 6. | Radio Iman |
| 7. | BBC |
| 8. | ZBC Redio |
| 9. | Z Connect |

*Chanzo: Uchambuzi wa taarifa za Shirika*

### 4.1.6.11 Kutokuwepo ulinzi katika Mnara wa kurushia Matangazo

Kifungu nambari 58(b)(d) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza majukumu ya Afisa Masuuli wa taasisi ya umma katika kusimamia mali za Taasisi.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Shirika la Utangazaji Zanzibar linamiliki minara ya kurushia matangazo iliyopo katika maeneo mbali mbali Kisiwani Pemba ambayo hukodishwa kwa ajili kuingiza mapato katika Shirika. Dosari iliyobainika ni kutokupatiwa uthibitisho wa kuwepo kwa walinzi katika baadhi ya minara ikiwemo mnara wa kurushia matangazo uliopo katika eneo la Kichunjuu Wilaya ya Mkoani jambo ambalo linaweza kupelekea kufanyika kwa uharibifu na upotevu wa vifaa katika minara hiyo, aidha ni kinyume na kifungu nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika kuimarisha ulinzi kwa masaa 24 kwa siku pamoja na kudhibiti eneo la minara ya Kurushia matangazo.

### 4.1.6.12 Malipo kwa watoa huduma ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 12,144,827

Kwa mujibu wa kifungu nambari 23(1) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi. Aidha, kifungu nambari 23(2) kinafafanua kuwa zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Shirika la Utangazaji Pemba limefanya malipo yenye jumla ya shilingi 12,144,827 kwa wafanyabiashara mbali mbali ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kama ni watoa huduma jambo ambalo linaweza kupelekea kuikosesha serikali mapato yatokanayo na utoaji wa huduma hiyo, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha sheria nilichokinakili hapo juu. Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani kwa kutokuwa makini kwa watendaji wenye dhamana ya kusimamia malipo.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Shirika Pemba kuongeza umakini katika kusimamia sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kununua bidhaa au huduma kwa watoa huduma waliosajiliwa na Mamlaka husika. Mchanganuo wa malipo kwa wafanyabiashara ambao hawajasajiliwa na mamlaka ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 43: Malipo kwa watoa huduma ambao hawajasajiliwa na ZPPDA**

| Hati Nambari | Hundi Nambari | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 01/07 ya 11/07/2022 | 000259 | 4,637,136 | Mbukilage Partnership | Ununuzi wa vifaa vya uchimbaji wa Kisima. |
| 02/07 ya 11/07/2022 | 000260 | 364,408 | Seif Nassor Salim | Ununuzi wa viburudishaji pamoja na Toyz. |
| 05/08 ya 24/08/2022 | 000266 | 434,720 | Mums Food and Refreshments | |
| 06/08 ya 24/08/2022 | 000267 | 165,669 | Ali Nassor Abdalla | Ununuzi wa vifaa vya matengenezo. |
| 07/08 ya 24/08/2022 | 000268 | 310,354 | Nassor Said Nassor | |
| 01/09 ya 05/09/2022 | T.O | 5,902,540 | Mbukilage Partnership | Ununuzi wa vifaa vya uchimbaji wa kisima. |
| 08/05 ya 12/05/2023 | 000287 | 330,000 | Seif Nassor Salim | Ununuzi wa Toys. |
| **Jumla** | | **12,144,827** | | |

*Chanzo: Hati za Malipo na Orodha ya wafanyabiashara waliosajiliwa*

### 4.1.7 SHIRIKA LA NYUMBA ZANZIBAR (ZHC)

Ukaguzi wa hesabu za Shirika la Nyumba Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo na Ukaguzi**

#### 4.1.7.1 Kutokuchukuliwa hatua za kisheria kwa Wapangaji wenye malimbikizo ya madeni ya muda mrefu shilingi 833,023,000

Kifungu cha 33(2) na 34(4) vya Sheria nambari 6 ya Shirika la Nyumba Zanzibar ya 2014 vinalitaka Shirika la Nyumba Zanzibar kumuondosha mpangaji ndani ya nyumba na linaweza kumfikisha mahakamani kudai deni lake iwapo mpangaji atashindwa kulipa kodi ya nyumba kama ilivyokubaliwa kwenye mkataba.

Aidha, mikataba yote ya muda mfupi ya upangishaji nyumba imeeleza wazi katika vifungu vya adhabu kwamba "ikiwa kwa namna yoyote kodi haijalipwa kwa kipindi cha siku thelathini (30) kutoka tarehe ya mwisho aliyoishia kulipa kodi hiyo, Mpangishaji atalazimika kumpa mpangaji notisi ya indhari ya kufuta mkataba wa upangishaji ya siku thalathini (30), na ikiwa kodi itakuwa haijalipwa kwa kipindi cha siku 30 kutoka tarehe ya notisi hiyo, mpangishaji atalazimika kumhamisha mpangaji kupitia kwa dalali wa mahakama bila kumpa notisi nyingine na mpangishaji atampeleka mpangaji mahakamani kudai deni lake".

Ukaguzi umepitia taarifa za mapato pamoja na mikataba ya upangishaji na kubaini uwepo wa idadi kubwa ya wapangaji wenye madeni ya muda mrefu ambao bado wanaendelea kukaa kwenye nyumba za Shirika bila kuchukuliwa hatua zozote za kisheria kwa mujibu wa Sheria na mikataba ya upangishaji.

Ukaguzi umebaini kuwa sababu mojawapo ya kasoro hii ni na kuingiliwa kwa maamuzi ya uongozi wa Shirika la Nyumba Zanzibar kwa kupewa maagizo ya mamlaka nyengine za Serikali.

Kutokuchukuliwa hatua za kisheria kwa wapangaji wenye malimbikizo ya madeni ya muda mrefu kunapelekea kudhoofika kwa juhudi za Shirika katika kutoa huduma bora za makazi kwa wananchi. Aidha, kunaweza kusababisha kuongezeka kwa idadi ya wapangaji wanaokaidi kulipa malimbikizo ya madeni yao.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Nyumba Zanzibar pamoja Serikali Kuu kwa ujumla kuhakikisha kuwa huduma za upangishaji wa nyumba za Shirika zinatolewa kwa mujibu wa masharti ya Sheria nambari 6 ya Shirika la Nyumba la Zanzibar ya 2014. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 44: Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu kwa wapangaji wa nyumba za Serikali**

| Namba | Mtaa | Idadi ya Wapangaji | Idadi ya Wadaiwa | Asilimia (%) | Deni halisi linalodaiwa (Tsh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| **ENEO LA NG'AMBO YA MJI** | | | | | |
| 1. | MICHENZANI BLOCK 1 | 104 | 26 | 25 | 11,670,000 |
| 2. | MICHENZANI BLOCK 3 | 70 | 11 | 16 | 1,975,000 |
| 3. | MICHENZANI BLOCK 4 | 30 | 4 | 13 | 6,211,000 |
| 4. | MICHENZANI BLOCK 5 | 57 | 11 | 19 | 6,500,000 |
| 5. | MICHENZANI BLOCK 6 | 70 | 8 | 11 | 4,850,000 |
| 6. | MICHENZANI BLOCK 7 | 85 | 13 | 15 | 6,900,000 |
| 7. | MICHENZANI BLOCK 8 | 161 | 29 | 18 | 10,475,000 |
| 8. | MICHENZANI BLOCK 9 | 108 | 26 | 24 | 21,614,000 |
| 9. | MICHENZANI BLOCK 10 | 54 | 15 | 28 | 8,460,000 |
| 10. | MOMBASA | 92 | 24 | 26 | 17,800,000 |
| 11. | SAATENI | 32 | 15 | 47 | 15,230,000 |
| 12. | KIKWAJUNI | 98 | 27 | 28 | 20,915,000 |
| 13. | KILIMANI | 13 | 5 | 38 | 1,300,000 |
| 14. | GAMBA | 136 | 107 | 79 | 86,250,000 |
| 15. | MPAPA | 70 | 59 | 84 | 103,045,000 |
| 16. | MAKUNDUCHI | 96 | 71 | 74 | 56,330,000 |
| 17. | CHUKWANI | 2 | 2 | 100 | 4,525,000 |
| 18. | **Jumla Ndogo (A)** | **1,283** | **454** | 35 | **384,050,000** |

| ENEO LA MJI MKONGWE | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 19. | MALINDI | 69 | 37 | 54 | 65,898,500 |
| 20. | KIPONDA | 154 | 74 | 48 | 64,386,000 |
| 21. | VUGA | 34 | 11 | 32 | 60,293,000 |
| 22. | S/MUHOGO | 28 | 9 | 32 | 11,735,000 |
| 23. | DARAJANI | 44 | 10 | 23 | 18,755,000 |
| 24. | FORODHANI | 21 | 2 | 10 | 24,700,000 |
| 25. | SHANGANI | 54 | 16 | 30 | 54,207,500 |
| 26. | HURUMZI | 58 | 17 | 29 | 15,240,000 |
| 27. | BAGHANI | 9 | 4 | 44 | 1,490,000 |
| 28. | KOKONI | 16 | 6 | 38 | 6,932,500 |
| 29. | M/ WIMA | 12 | 1 | 8 | 1,000,000 |
| 30. | GIZENGA | 49 | 14 | 29 | 15,160,000 |
| 31. | MKUNAZINI | 68 | 24 | 35 | 45,620,500 |
| 32. | KAJIFICHENI | 44 | 20 | 45 | 36,340,000 |
| 33. | MCHANGANI | 46 | 6 | 13 | 7,295,000 |
| 34. | MBUYUNI | 19 | 2 | 11 | 3,220,000 |
| 35. | MLANDEGE | 14 | 2 | 14 | 780,000 |
| 36. | K/TUMBO | 11 | 6 | 55 | 6,510,000 |
| 37. | MTENDENI | 18 | 4 | 22 | 9,160,000 |
| 38. | MNAZI MMOJA | 3 | 1 | 33 | 250,000 |
| 39. | **Jumla Ndogo (B)** | **775** | **266** | 34 | **448,973,000** |
| 40. | **JUMLA KUU (A+B)** | **2,058** | **720** | 35 | **833,023,000** |

### 4.1.7.2 Kuwepo kwa idadi kubwa ya wapangaji ambao hawana mikataba halali

Kifungu nambari 1(ii) cha mikataba yote ya muda mfupi ya ukodishaji nyumba kinamtaka mpangaji kuomba kwa maandishi mkataba mpya ndani ya kipindi cha miezi mitatu kabla ya kumalizika muda wa mkataba ulio hai. Aidha, kifungu cha 8 cha mikataba yote ya muda mfupi ya ukodishaji nyumba kinaeleza mazingira yanayopelekea kuvunjika kwa mikataba hiyo ambayo ni pamoja na kukamilika kwa muda wa mkataba.

Ukaguzi umepitia orodha za mikataba ya muda mfupi ya ukodishaji nyumba za biashara na makazi kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2023 na kubaini uwepo wa idadi ya wapangaji 616 kati ya wapangaji 2,058 wa nyumba za Shirika wanaendelea kunufaika na matumizi ya nyumba za Shirika bila ya kuwa na mikataba halali ya upangishaji.

Kuwepo kwa idadi kubwa ya wapangaji ambao hawana mikataba halali ya upangishaji kunaweza kukapelekea Shirika kushindwa kuwashurutisha kisheria wapangaji hao endapo watashindwa kutekeleza masharti ya matumizi ya nyumba hizo. Aidha kunaweza kupelekea upotevu wa mapato ya Serikali. **Kiambatisho Nambari 1 Kinahusika.**

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Nyumba la Zanzibar kuhakikisha kuwa huduma za kupangisha nyumba zinatolewa kwa kufuata Sheria nambari 6 ya Shirika la Nyumba ya 2014. Aidha, Serikali iangalie namna bora ya kuwasaidia wananchi wasio na uwezo katika kuwahakikishia wanapata makaazi bora kwa gharama nafuu.

### 4.1.7.3 Kukosekana kwa sera za bima (insurance policies) kwa nyumba za biashara zenye mikataba ya upangaji wa muda mrefu (long lease contracts)

Kifungu cha 7 (ii) cha mikataba ya upangishaji nyumba wa muda mrefu kinaeleza kwamba "Mpangaji atakata bima ya mwaka kwa jengo alilopanga na atawasilisha sera ya bima hiyo (insurance policy) kwa Mpangishaji kila mwaka katika kipindi cha mkataba husika".

Katika kuthibitisha utekelezaji wa kifungu cha 7 (ii) cha mikataba ya upangishaji nyumba wa muda mrefu, ukaguzi uliomba kupatiwa nakala za sera za bima zilizokatwa na kuwasilishwa na wapangaji wa muda mrefu. Hata hivyo ukaguzi ulipatiwa bima za nyumba kwa mikataba miwili (2) kati ya mikataba 36 ya upangaji wa muda mrefu ambazo zimekatwa na kuwasilishwa na wapangaji wa muda mrefu katika shirika.

Kukosekana kwa bima za majengo kwa wapangishaji wa muda mrefu ni kwenda kinyume na mikataba ya upangishaji na kunaweza kusababisha athari za kifedha kwa Mpangaji na Mpangishaji pindi yakitokea majanga kama ya moto na matukio mengine hatarishi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Nyumba Zanzibar kuwasiliana na wapangaji wa muda mrefu kuhusu ukataji na uwasilishaji wa Bima za nyumba Shirikani.

### 4.1.7.4 Kutotenganishwa kwa thamani ya Ardhi na Majengo katika kutafuta gharama za uchakavu

Aya ya 45 ya Viwango vya Uhasibu vya Kimataifa (IAS 16) inaeleza kuwa Kila sehemu ya thamani ya Mali ya Kudumu ambayo ina thamani kubwa ikilinganishwa na thamani ya jumla ya mali hiyo, italazimika kufanyiwa uchakavu peke yake.

Aidha, aya ya 58 ya Viwango vya Uhasibu vya Kimataifa (IAS 16) inaeleza kuwa Ardhi na jengo ni mali zinazotenganishika na utafutaji wa uchakavu wao hufanyika kwa kutenganishwa hata kama vyote vimenunuliwa au kupatikana kwa pamoja.

Ukaguzi umepitia taarifa za fedha za mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2023 za Shirika la Nyumba Zanzibar na kubaini kuwa kiasi cha shilingi 3,290,829,902 za majengo kilichoonyeshwa katika taarifa ya fedha hakikutenganishwa na gharama ya ardhi kinyume na miongozo ya aya ya 58 ya Viwango vya Uhasibu vya Kimataifa (IAS 16).

Ukaguzi unahusisha dosari hii kuwa inatokana na Shirika kushindwa kufanya uthamini wa majengo yake.

Kutotenganishwa kwa thamani ya Ardhi na Majengo katika kutafuta gharama za uchakavu kunaweza kusababisha gharama za uchakavu kuwa kubwa zaidi ya uhalisia na hatimae kupelekea Taarifa ya Fedha ya mwisho wa mwaka ya Shirika kutokutoa sura sahihi na halisi.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Shirika la Nyumba Zanzibar kuboresha vizuri taarifa za Daftari la Mali na kufanya uthamini wa kitaalamu kwa majengo yake ili kuweza kujuwa thamani halisi ya Majengo na Ardhi wanayomiliki.

#### 4.1.7.5 Kushindwa kuondoa thamani ya majengo mawili yaliyobomolewa katika taarifa za mwaka wa fedha 2022/2023

Aya ya 66 ya Viwango vya Uhasibu vya Kimataifa (IAS 40) inaeleza kuwa Mali ya Uwekezaji (Investment Property) inapaswa kuondoshwa katika taarifa ya hali kifedha (statement of financial position) wakati itakapouzwa au Mali hiyo itakapoondolewa kwa kudumu katika kutumika na kwamba hakuna maslahi ya kiuchumi yanayotarajiwa kupatikana baadae kwa kuondolewa kwake.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni 2023 Shirika la Nyumba Zanzibar liliyabomoa majengo yake mawili yaliyokuwa maeneo ya Darajani Unguja na Mkungu Malofa - Chake Chake Pemba ambayo yalikuwa yakitumika kama ni Mali ya Uwekezaji (Investment Property) ili kupisha ujenzi wa majengo mapya ya uwekezaji katika maeneo hayo ya Darajani Unguja na Mkungu Malofa - Chake Chake Pemba.

Ukaguzi umebaini kuwa Shirika la Nyumba Zanzibar limeshindwa kuondoa thamani ya mwisho yaliyokuwa nayo majengo hayo *(carrying value)* katika taarifa ya hali ya fedha jambo lililosababishwa na kutokufanyiwa kwa uthamini wa majengo hayo kabla ya kubomolewa.

Kutokuondoshwa kwa thamani ya majengo hayo katika taarifa ya Hali ya Kifedha ya mwaka 2022/2023 kumepelekea thamani ya Mali za Uwekezaji zilizoonyeshwa katika taarifa ya hali ya Kifedha kuwa zaidi ya kiwango halisi cha Mali hizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Nyumba Zanzibar kufuata miongozo ya Viwango vya Uhasibu vya Kimataifa (IAS 40) katika kuondosha thamani ya mali za uwekezaji zilizobomolewa kutoka taarifa ya hali ya kifedha ya mwaka.

**SHIRIKA LA NYUMBA PEMBA**

#### 4.1.7.6 Malipo yaliyofanywa nje ya mfumo wa manunuzi shilingi 17,310,740

Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba MUUMU.BA.156/370/001/27 ya tarehe 12/08/2022 kutoka Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar kwenda kwa wakuu wa taasisi inaeleza kwamba kuanzia tarehe 15/08/2022 manunuzi yote ya Serikali yanatakiwa yafanywe kwa kutumia mfumo wa ununuzi wa kielektroniki (e-PROZ).

Ukaguzi umebaini kwamba Shirika la Nyumba Pemba limetumia jumla ya shilingi 17,310,740 kwa ajili ya manunuzi mbali mbali pasipo kutumia mfumo wa kielektroniki wa manunuzi bila ya kuwepo sababu maalum ya kufanya hivyo. Kufanya manunuzi bila kutumia mfumo ni kwenda kinyume na maelekezo ya barua niliyoitaja hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Nyumba Pemba kuhakikisha manunuzi yote yanayofanyika yanapitia katika mfumo wa manunuzi. Mchanganuo wa manunuzi yaliyofanywa nje ya mfumo wa manunuzi ni kama ufuatao:-

**Jadweli Nambari 45: Manunuzi yaliyofanyika bila ya kutumia mfumo wa kielektroniki (e-Proz)**

| Namba | Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 1/10 ya 04/10/2022 | 000350 | 980,000 | Abrahman Haji Abdalla | Malipo kwa ajili ya gharama za ufundi. |
| 2. | 3/9 ya 2/09/2022 | TT | 6,913,919.60 | Salim Hamdan Maalim | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi. |
| 3. | 16/9 ya 21/09/2022 | | 504,210 | Masoud General Supplier | Malipo kwa ajili ya matengenezo ya gari. |
| 4. | 4/4 ya 2/09/2022 | | 8,912,610 | Asaa Kheri Asaa | Malipo ya ununuzi wa vifaa vya ujenzi. |
| **Jumla** | | | **17,310,740** | | |

*Chanzo: Uchambuzi wa taarifa za Shirika*

### 4.1.7.7 Kutokununua vifaa vya kuandikia kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji shilingi 3,419,504.70

Kifungu nambari 35 cha Sheria nambari 12 ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar ya 2018 kimezitaka Taasisi zote za Serikali kupeleka kazi zake zote za Uchapaji na Mahitaji ya vifaa vya Afisi na vifaa vya kuandikia kwa wakala wa Uchapaji wa Serikali Zanzibar.

Ukaguzi umebaini kwamba Shirika la Nyumba Pemba limefanya ununuzi wa vifaa vya kuandikia vyenye thamani ya shilingi 3,419,504.70 kutoka kwa Wasambazaji bila ya kuwepo kwa ruhusa kutoka kwa Wakala kama utaratibu unavyoelekeza jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo ikiwemo kununua vifaa kwa Wakala husika au kuomba ruhusa kwa Wakala ili kuweza kununua vifaa hivyo kwa wasambazaji wengine pale inapotokezea Wakala kutokuwa na vifaa vinavyohitajika kununuliwa. Mchanganuo wa vifaa vilivyonunuliwa nje ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji Pemba ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 46: Kutonunua vifaa kutoka kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji**

| Namba | Hati Namba | Hundi Namba | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 11/12 ya 20/12/2022 | TT | 1,231,232.80 | Adult Training Centre | Ununuzi wa vifaa vya kuandikia |
| 2. | 13/9 ya 16/9/2022 | | 2,002,914.20 | Halim Enterprises | |
| 3. | 22/7 ya 27/7/2022 | | 185,357.70 | Capital Tecnology Centre | |
| **Jumla** | | | **3,419,504.7** | | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati za malipo*

#### 4.1.7.8 Hali ya Uchakavu wa majengo ya Shirika

Kifungu nambari 66(1) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba "Kutakuwa na mpango wa matengenezo ya mali utakaoandaliwa na Taasisi ya Umma unaohakikisha kwamba mali zinabaki katika ubora kwa matumizi yaliyokusudiwa".

Shirika la Nyumba Pemba linamiliki majengo katika maeneo mbalimbali yakiwemo maghala na vituo vya kuuzia karafuu.

Ukaguzi umebaini kuwa majengo mengi yapo katika hali ya Uchakavu mkubwa uliosababishwa na kutokufanyiwa ukarabati kwa wakati jambo ambalo linaweza kupelekea kuzidi kuchakaa kwa majengo hayo na hatimae kubomoka na kuanguka na kuisababishia hasara Serikali jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu cha sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Nyumba Pemba kuyafanyia ukarabati kwa wakati majengo ili kuepusha athari zinazoweza kujitokeza baadae.

#### 4.1.7.9 Kukosekana kwa hatimiliki kwa baadhi ya mali za Shirika

Kifungu nambari 64(1) cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya mwaka 2021 kinaeleza kwamba "Taasisi ya Umma itahifadhi nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zote zinamilikiwa kisheria na Serikali".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa mali nyingi za Shirika la Nyuma Pemba ambazo hazina hati miliki, miongoni mwa mali hizo ni baadhi ya majengo ya Afisi, nyumba za kupangisha pamoja na vyombo vya moto jambo ambalo linaweza kupelekea upotevu wa mali hizo kutokana na Serikali kutokuwa na umiliki halali, aidha ni kwenda kinyume na Kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Hali hii imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani pamoja na kutokuongeza umakini kwa watendaji wenye dhamana ya kusimamia utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo inayotolewa na Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika kuongeza umakini katika kufuata Sheria, Kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kuzitafutia hati miliki mali za Shirika. Orodha ya mali ambazo hazina hatimiliki ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 2.**

#### 4.1.7.10 Deni la Mapato la ukarabati wa nyumba zilizotolewa fidia shilingi 57,900,000

Kutokana na makubaliano ya vikao vilivyofanyika baina ya uongozi wa Shirika la Nyumba Pemba na wamiliki wa nyumba za fidia zilizopo katika majengo ya Nyumba za maendeleo zilizofanyiwa matengenezo "wamiliki wa nyumba za fidia wanatakiwa kuchangia gharama za matengenezo ya nyumba hizo ili kuendana na muonekano wa pamoja baina ya nyumba za Shirika na zile zilizotolewa fidia".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kufanyika kwa matengenezo ya nyumba za fidia zilizoko katika maeneo mbali mbali ili ziweze kuwa na muonekano wenye kufanana na nyumba za Shirika ikiwa ni njia mojawapo ya kuzitunza na kuziboresha nyumba hizo lakini hadi ukaguzi unakamilika imebainika wamiliki wa nyumba hizo hawajachangia gharama za matengenezo yaliyofanyika katika nyumba zao jambo ambalo ni kulibebesha Shirika mzigo mkubwa wa gharama za matengenezo na hatimae kuitia hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika kuweka sera na miongozo bora ya kushughulikia na kuzitunza nyumba za maendeleo za Shirika na zile za watu binafsi. Baadhi ya nyumba hizo ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 47: Nyumba za fidia zilizofanyiwa matengenezo**

| Namba | Namba ya Nyumba | Eneo Ilipo | Deni linalodaiwa (Tshs) | Fedha iliyolipwa (Tshs) | Bakaa ya Deni (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | BL-5/1 | Madungu | 2,000,000 | 1,200,000 | 800,000 |
| 2. | BL-5/2 | | 2,000,000 | 0 | 2,000,000 |
| 3. | BL-5/3 | | 2,000,000 | 400,000 | 1,600,000 |
| 4. | BL-5/4 | | 2,000,000 | 0 | 2,000,000 |
| 5. | BL-5/5 | | 2,000,000 | 0 | 2,000,000 |
| 6. | BL-3/3 | | 8,500,000 | 0 | 8,500,000 |
| 7. | BL-4/14 | | 8,500,000 | 0 | 8,500,000 |
| 8. | BL-4/15 | | 8,500,000 | 0 | 8,500,000 |
| 9. | BL-4/1 | Mtemani | 3,000,000 | 0 | 3,000,000 |
| 10. | BL-4/2 | | 3,000,000 | 0 | 3,000,000 |
| 11. | BL-4/4 | | 3,000,000 | 0 | 3,000,000 |
| 12. | BL-4/7 | | 3,000,000 | 0 | 3,000,000 |
| 13. | BL-4/8 | | 3,000,000 | 0 | 3,000,000 |
| 14. | BL-4/11 | | 3,000,000 | 0 | 3,000,000 |
| 15. | BL-4/12 | | 3,000,000 | 0 | 3,000,000 |
| 16. | BL-4/22 | | 3,000,000 | 0 | 3,000,000 |
| **Jumla** | | | **59,500,000** | **1,600,000** | **57,900,000** |

*Chanzo: Uchambuzi wa taarifa za madeni ya Shirika*

### 4.1.8 SHIRIKA LA MAGAZETI YA SERIKALI ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 4.1.8.1 Mapungufu yaliyobainika katika ufanisi wa utendaji wa Shirika kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023

Ukaguzi umepitia taarifa za fedha za Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar kwa mwaka fedha unaoishia Juni 30, 2023 pamoja na taarifa nyengine za utendaji za Shirika kwa lengo la kutathmini ufanisi wa Shirika katika kujiendesha. Tathmini iliyofanyika imebaini mapungufu yafuatayo:-

- **Kupungua kwa mapato ya ndani kwa mwaka fedha 2022/2023 yakilinganishwa na yale ya mwaka wa fedha uliopita**

Taarifa za fedha ya mwisho wa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 ya Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar zinaonesha kuwa Shirika lilikusanya jumla ya shilingi 886,721,666 ikilinganishwa na mapato ya shilingi 1,227,293,996 yaliyokusanywa mwaka wa fedha 2021/2022 ikiwa ni upungufu wa shilingi 340,572,330 sawa na upungufu wa asilimia 27. Mchanganuo wa ulinganisho wa mapato hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 48: Mapato ya ndani ya Shirika katika kipindi cha miaka miwili iliyopita

| Maelezo | 2022/2023 (Tshs.) | 2021/2022 (Tshs.) | Tofauti (Tshs.) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| Mapato ya matangazo | 816,420,579 | 1,178,733,831 | -362,313,252 | -30.74 |
| Mapato ya mauzo ya magazeti | 70,301,086 | 48,560,164 | 21,740,922 | 44.77 |
| **Jumla** | **886,721,666** | **1,227,293,996** | **-340,572,330** | **-27.75** |

- **Kutofikiwa kwa makadirio ya makusanyo ya ndani**

Ukaguzi umebaini kwamba kwa mwaka fedha 2022/2023 Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar limekusanya jumla ya shilingi 886,721,666.76 ikilinganishwa na makadirio ya shilingi 1,011,900,000 ambayo ni sawa na asilimia 87.63 ya makadirio kukiwa na upungufu wa shilingi 125,178,333.24 sawa na upungufu wa asilimia 12.37 ya makadirio.

- **Uwezo wa Shirika kujiendesha**

Ukaguzi umepitia taarifa za mapato na matumizi za Shirika la Magazeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 na kubaini kuwa Shirika lina uwezo mdogo wa kujiendesha kutokana na kuwa na nakisi iliyotokana na matumizi ya Shirika kuzidi mapato yaliyokusanywa ndani ya mwaka wa fedha uliokaguliwa. Mchanganuo wa mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 49: Mapato na matumizi ya Shirika kwa mwaka wa fedha 2022/2023

| Maelekezo | Kiasi (Tshs.) |
|---|---|
| Makusanyo ya ndani | 886,721,666 |
| Ruzuku (OC) | 257,894,990 |
| **Jumla ya Mapato (A)** | **1,144,616,656** |
| Matumizi ya kawaida | 1,201,292,618 |
| Ununuzi wa mali za kudumu (assets) | 82,717,440 |
| **Jumla ya Matumizi (B)** | **1,284,010,058** |
| **Tofauti ya mapato na matumizi kwa mwaka 2022/2023 (Nakisi)** | **(139,393,402)** |

Ukaguzi umebaini kuwa miongoni mwa sababu zinazopelekea kupungua kwa mapato ya Shirika yamepungua kutokana na kuwa halijawahi kupatiwa mtaji wa biashara na uwekezaji, kutokuwa na mtambo wake wa kuchapishia magazeti jambo ambalo linalipelekea shirika kuchapisha magazeti yake kwa kampuni binafsi kwa gharama kubwa. Aidha, Shirika linakabiliwa na tatizo la kuongezeka kwa madeni hasa ya Taasisi za Umma jambo linalifanya Shirika kukosa mapato ambayo yangesaidia katika kutekeleza majukumu yake kiufanisi.

Kuendelea kupungua kwa mapato ya ndani pamoja na kutokufikia malengo ya makusanyo ya ndani ya Shirika kunapelekea Shirika kukosa mapato ambayo yangesadia kutekeleza majukumu yake ya kila siku.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar kuwa na mpango madhubuti wa ukusanyaji wa madeni ya wadaiwa wao ili kuhakikisha yanalipwa kwa wakati. Aidha, Uongozi wa Shirika ushirikiane na Mamlaka zenye kuhusika na mfumo wa malipo wa Serikali (ZanMalipo) ili waweze kutatua chanagamoto za mfumo zinazosababisha wateja kushindwa kulipa madeni yao kwa urahisi.

### 4.1.8.2 Changamoto katika ugawaji na uuzaji wa magazeti

Ukaguzi umepitia taarifa za ugawaji na uuzaji wa magazeti katika Shirika la Magazeti Zanzibar kwa upande wa Zanzibar na kubaini kuwa magazeti mengi yanabakia kila siku bila kuuzwa hali inayosabibisha Shirika kuendelea kukusanya mapato madogo yanayotokana na mauzo ya magazeti au kukosa matangazo mengi kutokana na magazeti kutosambazwa maeneo ya kutosha.

Aidha, ukaguzi umekosa taarifa za mauzo ya magazeti kwa upande wa Tanzania Bara kutokana na kutokuwepo kwa usimamizi mzuri katika Afisi zake za Dar es Salaam.

Ukaguzi umebaini kuwa sababu zinazopelekea changamoto katika uuzaji wa magazeti ya Shirika ni kulazimika kuchapisha magazeti mengi kutokana na sera ya Mchapaji wa magazeti ya Shirika kutokuchapisha magazeti chini ya nakala 3,000. Aidha, sababu nyengine ni Kuendelea kupungua kwa wasomaji wa magazeti katika jamii pamoja na kuongezeka kwa ushindani katika soko la magazeti nchini hali hii inayopelekea magazeti mengi kubakia bila kuuzwa.

Kuwepo kwa changamoto katika ugawaji na uuzaji wa magazeti ya Shirika kunapelekea Shirika kuendelea kulipa fedha nyingi kwa ajili ya gharama za uchapishaji ambazo haziendani na mauzo husika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika kuangalia namna bora ya ugawaji na uuzaji wa magazeti ili kupunguza gharama za uchapishaji ikiwa pamoja na uwezekano wa kuchapisha magazeti wenyewe badala ya kuchapisha kwa kampuni binafasi. Mchanganuo wa taarifa za ugawaji, uuzaji na bakaa ya magazeti kwa upande wa Zanzibar ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 50: Takwimu za mgawanyo wa Magazeti**

| Mwezi | Idadi ya Magazeti yaliyogaiwa | Idadi ya Magazeti yaliyouzwa | Idadi ya Magazeti yaliyobakia bila kuuzwa | Asilimia ya Magazeti Yaliyobakia |
|---|---|---|---|---|
| Julai, 2022 | 31,344 | 14,036 | 12,940 | 41.3 |
| Agosti, 2022 | 28,182 | 14,067 | 9,525 | 33.8 |
| Septemba, 2022 | 27,396 | 12,930 | 8,724 | 31.8 |
| Octoba, 2022 | 27,172 | 13,620 | 9,062 | 33.4 |
| Novemba, 2022 | 26,022 | 12,598 | 9,150 | 35.2 |
| Disemba, 2022 | 26,644 | 12,211 | 10,065 | 37.8 |
| Januari, 2023 | 27,392 | 12,568 | 10,234 | 37.4 |
| Februari, 2023 | 24,468 | 11,223 | 9,159 | 37.4 |
| Machi, 2023 | 22,714 | 12,395 | 5,951 | 26.2 |
| April, 2023 | 25,952 | 13,081 | 8,590 | 33.1 |
| Mei, 2023 | 30,585 | 14,674 | 11,321 | 37.0 |
| Juni, 2023 | 14,235 | 9,343 | | 0.0 |
| **Jumla** | **312,106** | **152,746** | **104,721** | **33.6** |

*Chanzo: Taarifa ya Ugawaji, mauzo na bakaa ya magazeti kwa mwaka 2022/2023 ya Shirika kwa Zanzibar*

#### 4.1.8.3 Uwepo wa madeni makubwa yanayotokana na taasisi za umma, shilingi 2,036,324,994

Ukaguzi umepitia taarifa za madeni ya Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar kwa taasisi mbalimbali za Umma na kubaini kuwa taasisi nyingi za umma hazilipi madeni yao kwa wakati hali inayopelekea Shirika kukosa mapato ambayo yangesaidia katika kutekeleza majukumu ya Shirika kiufanisi.

Kuwepo madeni makubwa yanayotokana na taasisi za umma kunapelekea Shirika kukosa fedha za kujiendesha katika shughuli zake za kila siku.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar kuzidisha juhudi katika kufuatilia madeni yake katika taasisi za umma ikiwa ni pamoja na kuomba msaada kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya kupata fedha zake kutoka taasisi mbali mbali za umma zinazodaiwa na Shirika. Orodha ya madeni hayo ni kama yalivyoambatishwa katika **Kiambatisho Nambari 3**.

### SHIRIKA LA MAGAZETI YA SERIKALI PEMBA

#### 4.1.8.4 Malimbikizo ya madeni ya mapato shilingi 89,902,540

Kifungu nambari 29(1)(b) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa "Afisa Mhasibu wa Taasisi ya Umma atahusika na kusimamia madeni ya Taasisi ya Umma."

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Shirika la Magazeti Pemba linazidai Taasisi mbali mbali za Umma madeni yenye jumla ya shilingi 89,902,540 yatokanayo na kuzipatia taasisi hizo huduma za magazeti, ambapo madeni hayo ni ya muda mrefu na hakuna hatua zilizochukuliwa na Shirika katika kuyadai jambo ambalo ni kulikosesha Shirika fedha kwa ajili ya shughuli za uendeshaji ikiwemo uchapishaji wa magazeti.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika kuongeza umakini katika kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo ikiwemo kuchukua hatua stahiki za kufuatilia ulipwaji wa madeni hayo. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama yanavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 51: Madeni ya mapato ya muda mrefu**

| Namba | Jina Mdaiwa/Taasisi | Deni halisi la Mapato (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi | 4,879,500.00 |
| 2. | Afisi ya Baraza la Mji wa Mkoani. | 4,208,500.00 |
| 3. | Afisi ya Makamo wapili wa Rais Pemba | 1,349,000.00 |
| 4. | Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais K/Sheria Pemba. | 2,698,000.00 |
| 5. | Wizara ya Afya, Ustawi wa jamii, /J/W/W/Pemba | 3,163,500.00 |
| 6. | Idara ya Uratibu Madawa ya Kulevya Pemba | 728,000.00 |
| 7. | Afisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mkoani Pemba | 4,010,620.00 |
| 8. | Wizara ya Nchi,O/R/T/M/na Vikosi vya SMZ | 2,743,500.00 |
| 9. | Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi Pemba | 2,329,500.00 |
| 10. | Afisi ya Baraza la Mji wa Chake Chake Pemba | 2,672,000.00 |
| 11. | Wizara ya Uwezeshaji Pemba | 749,000.00 |
| 12. | Afisi ya Maadili ya Viongozi Pemba | 1,343,000.00 |
| 13. | Afisi ya Kamisheni ya Utalii Pemba | 1,421,500.00 |
| 14. | Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Pemba | 1,808,000.00 |
| 15. | Wizara ya Habari, Vijana, na Michezo Pemba | 1,046,000.00 |
| 16. | Idara ya Usimamizi wa Mazingira (ZEMA) Pemba | 1,737,000.00 |
| 17. | Idara ya Mazingira Pemba | 1,189,000.00 |
| 18. | Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba | 1,279,000.00 |
| 19. | Muhasibu Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba. | 1,457,000.00 |
| 20. | Afisa Mipango Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba | 1,421,000.00 |

| Namba | Jina Mdaiwa/Taasisi | Deni halisi la Mapato (Tshs) |
|---|---|---|
| 21. | Afisa Utumishi Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba | 1,086,500.00 |
| 22. | Mkuu wa Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale Pemba | 1,421,000.00 |
| 23. | Afisa Mdhamini Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba | 329,040.00 |
| 24. | Mkuu wa Idara ya Habari Maelezo Pemba | 1,048,000.00 |
| 25. | Afisi ya Mufti Pemba | 608,000.00 |
| 26. | Afisi ya Mkuu wa Mkoa Kusini Pemba | 6,605,500.00 |
| 27. | Afisi ya Rais MBLM Pemba | 2,675,500.00 |
| 28. | Jeshi la Kujenga Uchumi | 1,150,400.00 |
| 29. | Wizara ya Kilimo, Maliasili Pemba | 4,176,000.00 |
| 30. | Mkoa wa Kaskazini Pemba | 4,572,800.00 |
| 31. | Mkuu wa Wilaya ya Micheweni Pemba | 5,120,000.00 |
| 32. | Afisi ya Mkuu wa Wilaya ya Wete Pemba | 8,931,470.00 |
| 33. | Afisi ya Mkuu wa Wilaya ya Chake Chake Pemba | 2,562,900.00 |
| 34. | Afisi ya Wilaya Ndogo Kojani | 1,049,000.00 |
| 35. | Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda Pemba | 2,814,500.00 |
| 36. | Baraza la Mji Wete Pemba. | 362,500.00 |
| 37. | Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale Pemba. | 1,369,040.00 |
| 38. | Mahakama Chake Chake Pemba | 1,542,000.00 |
| 39. | Halmashauri ya Wilaya ya Micheweni Pemba. | 1,770.00 |
| 40. | TAMWA | 244,000.00 |
| **Jumla** | | **89,902,540** |

*Chanzo: Uchambuzi wa madeni ya mapato ya shirika.*

### 4.1.8.5 Hati za malipo zilizokosekana kwa Ukaguzi

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Shirika la Magazeti Pemba limefanya malipo mbali mbali kwa ajili ya shughuli za uendeshaji. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa hati za malipo za miezi 8 kuanzia mwezi wa Julai, 2022 hadi mwezi wa Febuari, 2023 kwa ajili ya ukaguzi ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo yaliyofanyika ambapo ni kwenda kinyume na kanuni nambari 166(2)(f) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021. Hali hii imesababishwa na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani pamoja na mshika fedha kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu ya utunzaji wa nyaraka za malipo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika la Magazeti Pemba kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo ikiwemo kutayarisha na kuzitunza hati za malipo pamoja na vielelezo vyake.

### 4.1.8.6 Kutokutumika kwa vifaa vya Shirika

Kifungu nambari 27(1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza "Afisa Mhasibu wa Taasisi ya Umma anawajibika kusimamia masuala ya fedha za Taasisi ya Umma na kwa madhumuni hayo atachukua hatua muafaka za kuendeleza matumizi bora ya rasilimali za umma na kuzuia viashiria hatarishi vya kifedha katika mfumo wa usimamizi wa fedha za umma"

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwepo kwa vifaa vya Shirika la Magazeti Pemba vilivyoletwa kutoka Makao Makuu ya Shirika Unguja lakini hadi ukaguzi huu unakamilika vifaa hivyo bado havijaanza kutumika ambapo ni miaka 2 tokea vifaa hivyo kuwasilishwa katika Shirika Pemba, vifaa wenyewe ni Camera 1 aina ya NIKON na Photocopy 1 aina ya image Runner 2530i jambo ambalo linaweza kupelekea kuharibika kwa vifaa hivyo kutokana na kutokutumika kwa muda mrefu na hatimae kuitia hasara Serikali, aidha ni kwenda kinyume na kifungu nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Shirika kuongeza umakini katika kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo inayotolewa na Serikali ikiwemo kuvitumia vifaa hivyo ili kuweza kufikia lengo lililokusudiwa pamoja

# SURA YA TANO









# 5.0 MAMLAKA ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umebainisha taarifa ya michango ya vyanzo vya mapato vya Mamlaka za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, utendaji wa mwaka kwa kila chanzo cha mapato pamoja na kubainisha dosari za kiutendaji zilizojitokeza wakati wa ukaguzi na kushauri njia za utatuzi wa dosari hizo.

## 5.1 TAARIFA ZA UKAGUZI WA MAMLAKA ZA SERIKALI

Ukaguzi huu umefanywa kwa kuzingatia misingi ya ukaguzi ya kitaifa na kimataifa ambapo mambo mbalimbali yamebainishwa ambayo yanahitaji kushughulikiwa na Serikali, Baraza la Wawakilishi pamoja na  Uongozi wa taasisi husika ili kuhakikisha ufanisi katika utendaji wa shughuli za taasisi hizo unaimarika. Matokeo na mapendekezo ya ukaguzi yameainishwa kupitia Mamlaka za Serikali ya Mapinduzi zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kama ifuatavyo:-

### 5.1.1 MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI ZANZIBAR (ZURA)

Ukaguzi wa hesabu za Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.1.1.1 Kukosekana kwa Hatimiliki  ya Ardhi ya ZURA - Chake Chake Pemba

Uhakiki wa nyaraka za umiliki za Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar ulibaini kuwa ardhi inayotumiwa na kumilikiwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar imekosa uthibitisho wa umiliki wa ardhi yake iliyoko Wilaya ya Chake Chake. Hali hii inaonyesha kuwa Mamlaka ya Udhibiti wa huduma za maji na Nishati Zanzibar haina uthibitisho wa umiliki ardhi hiyo kisheria na endapo kama kutatokea mgogoro wa umiliki wa ardhi hiyo, Mamlaka ya Udhibiti wa huduma za Maji na Nishati inaweza kushindwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar kuharakisha mchakato wa upatikanaji wa hati miliki ya Ardhi iliyoko Chake Chake Pemba ili kuepuka matatizo yanayoweza kutokea kuhusiana na umiliki wa ardhi hiyo na hivyo kuweza kulinda mali za Serikali.

#### 5.1.1.2 Kutofanyiwa maboresho kwa Daftari la kutunza mali za kudumu za Mamlaka

Kifungu nambari 58(c) cha Sheria nambari 6 ya Afisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kuwa Taasisi ya Umma inapaswa kuhifadhi na kuboresha mara kwa mara Daftari la kutunzia mali za kudumu kwa kujumuisha mali mpya zilizonunuliwa na kuondosha taarifa za mali zilizouzwa.

Katika ukaguzi wa Mamlaka ya udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati nilibaini kuwa Mamlaka haikufanya maboresho taarifa za mali zilizonunuliwa katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Kutokufanyiwa maboresho Daftari la kutunzia mali za kudumu kunapelekea udhaifu katika kulinda mali za Serikali dhidi ya upotevu, matumizi mabaya, uharibifu, wizi na matumizi yasiyoruhusiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar kufanyia maboresho daftari la mali za kudumu kwa kujumuisha taarifa zote muhimu kwa mujibu wa matakwa ya Sheria nambari 6 ya Afisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021.

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA MAJI NA NISHATI PEMBA**

### 5.1.1.3 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 40,258,400

Kanuni ya 57(1)(2)(b) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaeleza kuwa malipo yote lazima yaambatanishwe na hati ya malipo ambayo imekamilika vielelezo vyote kwa mujibu wa maelekezo ya hazina na kuidhinishwa na Afisa Mhasibu.

Ukaguzi umebaini kuwa jumla ya shilingi 40,258,400 zimetumika kwa ajili ya malipo mbali mbali ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Pemba lakini baadhi ya vielelezo havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutokuambatanisha vielelezo vya malipo kwa wakati katika hati za malipo kunaweza kupelekea kutokuthibitika kwa uhalali wa malipo husika jambo ambalo ni kwenda kinyume na Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka kuambatanisha vielelezo vyote husika katika hati za malipo mara tu baada ya malipo kukamilika. Mchanganuo wa hati za malipo zenye vielelezo pungufu ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 52: Hati za malipo zenye vielelezo pungufu**

| Hati Namba | Hundi Namba | Thamani (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 15/10 ya 20/10/2022 | - | 28,831,600 | New Home Furniture | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa samani za Afisi. |
| 30/6 ya 26/06/2023 | TT | 11,426,800 | Saleh Decoration | |
| **Jumla** | | **40,258,400** | | |

*Chanzo: Hati za malipo*

### 5.1.1.4 Kukosekana kwa thamani halisi ya fedha ya Ununuzi wa Mapazia shilingi 6,210,000

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Pemba imenunua mapazia mapande 10 kwa thamani ya shilingi 6,210,000 sawa na shilingi 621,000 kwa kila pande moja.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa thamani halisi ya fedha iliyotumika ukilinganisha na bidhaa iliyonunuliwa hali inayoonyesha fedha iliyotumika kwa ununuzi huu ni kubwa sana jambo linalopelekea uwezekano wa uwepo wa matumizi mabaya ya fedha za umma. Kufanya ununuzi usiozingatia thamani ya fedha ni kwenda kinyume na kanuni ya 46 ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka kuhakikisha wanafanya ununuzi wa bidhaa kulingana na bei na ubora wa bidhaa. Mchanganuo wa ununuzi ambao hauendani na uhalisia ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 53: Ununuzi wa Mapazia ambao hauendani na uhalisia**

| Hati Namba | Hundi Namba | Thamani ya Hati (Tshs) | Thamani ya Mapazia (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 30/6 ya 26/06/2023 | TT | 11,426,800 | 6,210,000 | Saleh Decoration | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa samani za Afisi. |
| **Jumla** | | **11,426,800** | **6,210,000** | | |

### 5.1.1.5 Kutokufuatwa kwa Mfumo wa Manunuzi Ipaswavyo

Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba MUUMU.BA.156/370/001/27 ya tarehe 12/08/2022 kutoka Mamlaka ya Ununuzi wa Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar kwenda kwa wakuu wa taasisi inaeleza kwamba kuanzia tarehe 15/08/2022 manunuzi yote ya Serikali yanatakiwa yafanywe kwa kutumia mfumo wa ununuzi wa kielektroniki (e-Proz).

Baada ya kufanya ukaguzi wa kina juu ya matumizi ya mfumo wa ununuzi ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati imemuacha mtoa huduma wa shilingi 14,950,000 na kumchagua wa shilingi 18,160,000 kwa ajili ya ununuzi wa mapazia kwa matumizi ya Afisi ya Mamlaka Pemba pamoja na samani za Afisi za Afisi ya Mamlaka Unguja hivyo kuweka tofauti ya shilingi 3,210,000 ambazo ni kuitia hasara Serikali. Hali hii inaonyesha Mamlaka kutokufuata kikamilifu matakwa ya mfumo wa ununuzi kwa kumuacha mtoa huduma mwenye bei ndogo na kumchagua mwenye bei kubwa bila ya kuainisha sababu mahsusi za kufanya hivyo.

Kumzawadia mtoa huduma mwenye bei ya juu na kumuacha mwenye bei ndogo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 pamoja na matakwa ya barua niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka Makao Makuu kuhakikisha wanafuata kikamilifu matakwa ya Sheria ya Ununuzi pamoja na mfumo wa ununuzi. Mchanganuo wa ununuzi ambao haukufuata mfumo wa manunuzi ipaswavyo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 54: Kutokufuatwa kwa Mfumo wa Manunuzi Ipaswavyo**

| Hati Namba | Hundi Namba | Thamani ya Hati (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 30/6 26/06/2023 | TT | 11,426,800 | Saleh Decoration | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa samani za Afisi. |
| **Jumla** | | **11,426,800** | | |

## 5.1.2 MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI ZANZIBAR (ZMA)

Ukaguzi wa hesabu za Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

### 5.1.2.1 Kushindwa kuweka kumbukumbu za Wafanyakazi (Majalada) katika Masjala ya Siri

Kanuni nambari 52(4) ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya 2014 inahitaji Majalada yote ya watumishi wa umma kuhifadhiwa katika masjala ya siri na hayatoruhusika kupewa mtumishi yeyote isipokuwa kwa ruhusa ya Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi.

Ukaguzi umepitia mfumo wa masjala wa Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar na kubaini kuwa Mamlaka inahifadhi majalada ya wafanyakazi katika Afisi ya Mkurugenzi wa Rasilimali Watu na Utawala badala ya kuhifadhiwa katika masjala ya siri kinyume na matakwa ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya 2014.

Kushindwa kuweka Majalada ya watumishi wa Mamlaka katika Masjala ya Siri kunaweza kusababisha upotevu au uvujaji wa baadhi ya taarifa za wafanyakazi kutoka kwenye majalada yao.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar kuchukua juhudi za makusudi katika kutafuta eneo kwa ajili ya Masjala ya siri ili kuweza kuhifadhi nyaraka zote za siri za Mamlaka kwa usalama zaidi kama inavyotakiwa na Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014.

### 5.1.2.2 Dosari zilizobainika katika Mchakato wa Ajira Mpya

Mamlaka ya Usafiri wa Baharini Zanzibar ilifanya mchakato wa ajira za wafanyakazi tisa (9) wa kudumu katika mwaka wa fedha wa 2022/2023 ili kujaza nafasi za Afisa wa Usajili wa Meli Daraja la II, Afisa wa Ukaguzi Daraja la II na Afisa Msaidizi wa Usalama Daraja la II. Mchakato wa ajira ulihusisha uchunguzi wa awali kwa waombaji 117 kulingana na sifa zinazohitajika kupitia usaili wa maandishi uliofuatiwa na usaili wa mahojiano ya ana kwa ana.

Ukaguzi ulipitia mchakato wa ajira hiyo na kubaini kwamba waombaji wawili kwa nafasi za Afisa wa Ukaguzi Daraja la II na Afisa Msaidizi wa Usalama Daraja la II ambao walipata alama za juu katika usaili wa maandishi na usaili wa mahojiano ya ana kwa ana (kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa na kamati iliyochaguliwa ya ajira) hawakuajiriwa licha ya ukweli kwamba walipata alama za juu na walikuwa na sifa zote zinazohitajika kama ilivyoelezwa katika tangazo la kazi (Jadweli namba 4 hapo chini linataja sifa zilizohitajika za waombaji). Kulingana na ripoti ya Kamati iliyochaguliwa ya ajira, waombaji hao wawili walifaulu katika nafasi ya kwanza na ya pili katika usaili waliofanyiwa.

Zaidi ya hayo, ilibainika kwamba waombaji hao hawakuajiriwa kutokana na kutokuwasilisha Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi, jambo ambalo ukaguzi unahisi lilipaswa kushughulikiwa mwanzoni mwa mchakato wa ajira katika hatua za awali za kuchuja maombi. Hata hivyo ukaguzi umebaini kuwa waombaji hao waliruhusiwa kuendelea na usaili ngazi zote hadi mwisho wa mchakato na kupata alama za juu na baadaye hawakuchaguliwa (kwa ajira) kutokana na kutokuwasilisha Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.

Ukaguzi unaona kuwa hali hiyo imetokana na kutokuwepo kwa umakini na uangalifu katika hatua za mchakato wa ajira.

Kuwepo kwa dosari zilizotajwa hapo juu kunaweza kusababisha migogoro au kufanya maamuzi yasiyo ya haki ambayo hayakuzingatia sifa za waombaji, kwani waombaji wote wawili walipaswa kuondolewa katika mchakato huo mwanzoni kabisa ikiwa hawakuwasilisha Vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi.

Ukaguzi unashauri Uongozi wa Mamlaka ya Usafiri wa Baharini kuhakikisha kuwa mchakato wa ajira unafanyika kwa umakini na uangalifu unaostahili na kwa kuzingatia miongozo ya utumishi wa umma ili kuepusha upendeleo na migogoro katika mchakato mzima wa ajira. Mchanganuo wa maelezo ya sifa zilizohitajika kwa ajili ya maombi ya nafasi hizo ni kama yanavyooneka katika jedwali hapo chini:-

**Jadweli Nambari 55: Sifa za Waombaji wa nafasi za kazi katika ZMA**

| **Nafasi I** | **Afisa Mkaguzi wa Meli Daraja la II** |
|---|---|
| Sifa za Mwombaji | Awe mwenye cheti cha umahiri daraja la II (Certificate of Competence Class II) na kuendelea; au mwenye elimu ya Shahada ya kwanza na kuendelea katika fani ya Masuala ya Baharini/ Usafirishaji wa Baharini/Usanifu wa Majini/Usalama wa Baharini/ Uhandisi wa Meli, au fani inayolingana na hiyo kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. |
| **Nafasi II** | **Msaidizi Usalama wa Meli Daraja la III** |
| Sifa za Mwombaji | Awe mwenye elimu ya cheti katika fani ya Masuala ya Baharini/Usafirishaji wa Baharini/ Usalama wa Baharini/ Elimu ya Mafunzo ya awali ya Baharini, "Basic Mandotary Certificate" au fani inayolingana na hiyo kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. |

*Chanzo: Job announcement https://www.zma.go.tz/zma/Job_Opportunities_ Annoucement.pdf*

Mchanganuo wa maelezo ya waombaji waliokataliwa, nafasi waliyoomba na alama walizopata ni kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini:-

**Jadweli Nambari 56: Waombaji walioshinda na kukataliwa katika Mchakato wa Ajira**

| | **Alama katika Usaili wa Maandishi** | **Alama katika Usaili wa Ana kwa ana** | **Wastani wa Alama** | **Nafasi** |
|---|---|---|---|---|
| **Afisa Mkaguzi Meli Daraja la II** | | | | |
| Fahad Omar Ali | 84 | 72 | 78 | 2 |
| Qualification: | Degree in Maritime Transport and Nautical Science | | | |
| Other Qualification: | Mandatory Course | | | |
| **Afisa Msaidizi Usalama wa Meli Daraja la III** | | | | |
| Saumu Ibrahim Mtikuwe | 43 | 40 | 41.5 | 1 |
| Qualification: | Certificate | | | |
| Other Qualification: | Mandatory Rating | | | |

*Chanzo: Ripoti ya Mchakato wa ajira iliyoandaliwa na kamati ya ajira*

### 5.1.2.3 Manunuzi yaliyofanywa nje ya mfumo wa manunuzi wa kielektroniki (e-Proz) shilingi 160,290,815

Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar kupitia barua ya tarehe 12/8/2022 yenye kumbukumbu namba MUUMU.BA.156/370/01/27 iliwaagiza Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Idara Maalum, Wakuu wa Mashirika ya Umma, Wakuu wa Mamlaka na Taasisi zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwamba kuanzia tarehe 15/08/2022 manunuzi yote ya Serikali yawe yanafanywa kwa kutumia mfumo wa manunuzi wa kielektroniki wa Serikali (e-Proz). Aidha, Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar imesisitiza kuwa changamoto yoyote itakayojitokeza katika matumizi ya mfumo huo iwasilishwe kwa Mamlaka haraka iwezekanavyo kwa ajili ya utatuzi wake.

Ukaguzi umepitia taarifa za utekelezaji wa kitengo cha manunuzi, taarifa kutoka katika mfumo wa e-Proz (RFQ Report) pamoja na hati za malipo mbalimbali za Mamlaka ya Usafiri Baharini na kubaini kuwa, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar imefanya manunuzi yenye jumla ya shilingi 354,119,365; kati ya hizo, manunuzi ya shilingi 160,290,815 hayakufanywa kupitia mfumo huo ambapo ni kinyume na maelekezo ya manunuzi yaliyotolewa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar.

Ukaguzi umebaini kuwa dosari hii imetokana na Maafisa wa Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar kutokuwa na ufahamu wa kutosha wa matumizi ya mfumo huo licha ya jitihada zilizochukuliwa na Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar kuomba kupewa mafunzo maalum kwa ajili ya matumizi bora ya mfumo huo.

Kuwepo kwa Manunuzi yaliyofanywa nje ya mfumo wa manunuzi wa Kielektroniki wa Serikali kunaweza kusababisha kupata taarifa isiyo sahihi juu ya ununuzi wote unaofanywa na taasisi za Umma na kunaweza kuathiri utayarishaji na utoaji wa taarifa kwa fedha za Serikali.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya Usafirii Baharini Zanzibar kuwasilisha changamoto zote wanazokabiliana nazo katika utumiaji wa mfumo wa e-Proz kwa Mamlaka husika ili kuhakikisha kuwa malengo ya uanzishaji wa mfumo huo yanafikiwa ili kuzuia uwepo wa mianya ya kufanya manunuzi nje ya Mfumo wa manunuzi wa Kielektroniki wa Serikali jambo ambalo litaweza kupelekea kuingiza hasara Serikali.

Machanganuo wa manunuzi yaliyofanywa nje ya mfumo wa e-Proz ni kama yanavyoonekana katika Jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 57 : Manunuzi yaliyofanyika nje ya Mfumo wa e-Proz

| Namba | Maelezo | Kiasi (Tshs.) |
|---|---|---|
| 1. | Procurement of ICT equipment | 18,576,904.50 |
| 2. | Procurement of Stationary | 20,495,750.00 |
| 3. | Submission of printing works | 6,693,000.00 |
| 4. | Preparation of internal training for board of director and management | 8,000,000.00 |
| 5. | Water well drilling | 3,000,000.00 |
| 6. | Procurement of Safety Gear | 11,674,800.00 |
| 7. | Procurement of ICT equipment | 6,150,000.00 |
| 8. | Procurement of Stationary | 19,527,603.00 |
| 9. | Procurement of receipt books and files | 6,470,000.00 |
| 10. | Generator and motor vehicle services and purchase of fire extinguishers | 1,875,000.00 |
| 11. | Procurement of life Jackets | 4,370,000.00 |
| 12. | Procurement of printer for seafarers' books | 25,481,420.00 |
| 13. | Procurement of receipt books and files | 7,118,500.00 |
| 14. | Motor vehicle insurance | 9,196,837.50 |
| 15. | Procurement of Manifest and paper for printing control numbers | 2,650,000.00 |
| 16. | Services of motor vehicles | 2,444,000.00 |
| 17. | Procurement of ICT equipment | 6,567,000.00 |
| **Jumla** | | **160,290,815** |

*Chanzo: Taarifa za utekelezaji za kitengo cha Manunuzi cha ZMA*

#### 5.1.2.4 Kushindwa kuthibitisha usahihi wa gharama za Mali za kudumu (PPE) zilizoainishwa katika taarifa ya fedha ya mwaka, shilingi 1,517,043,603

Aya ya 26 na 27 za Viwango vya Kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS 17) zinazitaka mali za kudumu kutambuliwa kwa gharama yake ya ununuzi, na kwa mali ya kudumu inayopatikana kwa njia isiyo ya biashara (non-exchange transaction), gharama yake ipimwe kwa kuangalia thamani yake halisi siku ya ununuzi.

Ukaguzi umepitia taarifa ya fedha za Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar na kukokotoa upya thamani za mali za kudumu (PPE) zenye thamani ya jumla ya shilingi 1,517,043,603 zilizoainishwa katika Taarifa ya Hali ya Fedha ya Mamlaka (Statement of Financial Position) ya tarehe 30 Juni 2023 ili kuthibitisha usahihi wake.

Ukaguzi ulishindwa kuthibitisha usahihi wa thamani ya mali za kudumu (PPE) za Mamlaka kutokana na kukosa vyanzo vya thamani zilizotumika za mali hizo kulikotokana na kukosekana kwa taarifa zenye kujitosheleza kwenye daftari la Mali za Kudumu la Mamlaka.

Kukosekana kwa vyanzo vya thamani za mali za kudumu za Mamlaka kunapelekea taarifa za fedha za Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar kutoonesha sura sahihi na halisi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar kufanya uthamini wa mali zake za kudumu ili kupata misingi ya vipimo vya thamani ya mali hizo (measurement basis) kunakoenda sambamba na kuendelea kutunza na kuboresha daftari la mali za Kudumu la Mamlaka.

**MAMLAKA YA USAFIRI BAHARINI PEMBA**

#### 5.1.2.5 Kutokufunguliwa kwa Hesabu ya Matumizi ya Kawaida

Mamlaka ya Usafiri Baharini Pemba inawajibu wa kuendesha na kusimamia shughuli za Mamlaka kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya kifedha.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Mamlaka ya Usafiri Baharini haijafungua hesabu ya matumizi ya kawaida ili kuweza kuendesha shughuli zake za kiofisi kwa ufanisi zaidi hali ambayo inapelekea matumizi yote ya Mamlaka Pemba kufanyika Afisi kuu ya Mamlaka iliyoko Unguja.

Kutokufunguliwa kwa hesabu ya matumizi ya kawaida ya Mamlaka kwa upande wa Pemba ni kwenda kinyume na Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 na pia kunaweza kupunguza ufanisi katika utendaji kazi wa Mamlaka kwa upande wa Pemba.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Usafiri Baharini Pemba kwa kushirikiana na Afisi ya Rais Fedha na Mipango Pemba kufungua hesabu ya matumizi ya kawaida katika Tawi la Pemba.

#### 5.1.2.6 Uwepo wa Upungufu wa Watumishi

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mamlaka ya Usafiri Baharini Pemba ina upungufu wa watumishi muhimu ambao wangaliwezesha Mamlaka kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Upungufu huu unaathiri utendaji wa jumla wa Mamlaka ikiwa ni pamoja na utoaji duni wa huduma, mrundikano wa majukumu, na kupunguza hamasa ya utendaji kazi kwa watumishi waliopo.

Hali hii inaweza kupelekea ucheleweshwaji wa utoaji huduma kwa taasisi za umma na jamii kwa ujumla na pia inaweza kupelekea kuikosesha mapato Serikali.

Kutokupewa nafasi za uajiri kwa mujibu wa nafasi zilizowazi ni kwenda kinyume na kanuni nambari 6(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kulipa kipaombele suala la uajiri ili kupunguza changamoto za kiutendaji zinazoikabili taasisi husika.

Mchanganuo wa upungufu wa watumishi ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 58: Upungufu wa Watumishi

| Namba | Kada | Waliopo | Mahitaji | Upungufu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Muhasibu | 0 | 1 | 1 |
| 2. | Afisa utumishi | 0 | 1 | 1 |
| 3. | Afisa manunuzi | 0 | 1 | 1 |
| 4. | Afisa masjala | 0 | 1 | 1 |
| 5. | Mshika fedha | 0 | 1 | 1 |
| 6. | Mkaguzi wa meli | 0 | 1 | 1 |
| **Jumla** | | **0** | **6** | **6** |

*Chanzo: Mpango wa rasilimali watu.*

### 5.1.2.7 Uhaba wa Vyombo vya Usafiri

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Mamlaka ya Usafiri Baharini Pemba inamiliki gari moja na vespa mbili ambazo zilikuwa zinatumika katika Afisi ya Mkoani. Vyombo hivi kwa sasa haviko katika hali inayoridhisha.

Hadi ukaguzi unakamilika, Afisi zote za Mamlaka Pemba ambazo ni Mkoani, Wesha na Wete hazina vyombo vya usafiri kwa ajili ya kazi za kila siku zinazohusu ufuatiliaji na utoaji wa taaluma juu ya athari ya utumiaji wa bandari bubu zilizopo katika maeneo tofauti. Hali hii inaathiri utendaji kazi wa Mamlaka kwa kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi unaotegemewa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka kutenga fedha za kutosha za bajeti kwa ajili ya ununuzi wa vyombo vya usafiri.

### 5.1.2.8 Upatikanaji mdogo wa mapato yatokanayo na utoaji wa leseni za vyombo vya uvuvi

Kwa mujibu wa Sheria namba 3 ya mwaka 2009 ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya Usafiri Baharini kifungu namba 5(1)(e) Mamlaka ya Usafiri Baharini ina jukumu la kusajili na kutoa leseni za vyombo vya baharini vikiwemo vya uvuvi.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba utoaji wa leseni kwa vyombo vya uvuvi unafanywa na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kupitia Idara yake ya Uvuvi kinyume na matakwa ya sheria ya uanzishwaji wa Mamlaka bila ya Mamlaka kuonekana kuchukua juhudi zozote za ufuatiliaji wa suala hili. Hali hiyo inapelekea Mamlaka ya Usafiri Baharini kukosa mapato yatokanayo na utoaji wa leseni hizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka kukaa pamoja na Uongozi wa Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi ili kuhakikisha sheria ya Mamlaka inatekelezwa. Aidha, Mamlaka ichukuwe juhudi za makusudi za kuwaelimisha wavuvi ili kujua ni taasisi gani kisheria inahusika na utowaji wa leseni za uvuvi.

### 5.1.3 MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR (ZAA)

Ukaguzi wa hesabu za Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.1.3.1 Kutowasilishwa katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kwa Tozo ya Usalama (Safety Fee) inayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) kwa niaba ya Mamlaka, shilingi 684,050,000

Kwa mujibu wa Sheria nambari 2 ya Kodi za Huduma za Bandari na Viwanja vya Ndege ya 1999 (Port Service Charge Act no.2, 1999), abiria yeyote anaesafiri ndani ya Tanzania kupitia viwanja vya ndege, anapaswa kutozwa shilingi 2,000 na wale wanaosafiri nje ya Tanzania kutozwa USD 9. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, Mamlaka ya Mapato Zanzibar, huzikusanya fedha hizo kupitia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango na baadae kuziwasilisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege.

Katika kupitia Bajeti ya Mamlaka ya Viwanja vya ndege Zanzibar ya mwaka wa fedha 2022/2023, ukaguzi umebaini kwamba, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 406,215,357 kutokana na tozo ya usalama (safety fee).

Ukaguzi ulipitia Ankara za madai zenye thamani ya shilingi 684,050,000 ambazo Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ilizituma kwenda Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa ajili ya kurejeshewa fedha za tozo ya usalama wa abiria za Viwanja vya Ndege zilizokusanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar. Hata hivyo fedha hizo hazikuwasilishwa katika Mamlaka ya Viwanja vya ndege Zanzibar. Aidha ukaguzi umebaini kwamba kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa tozo hizo hazijawasilishwa katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar na kupelekea Mamlaka kuidai Afisi ya Rais, Fedha na Mipango jumla ya shilingi 1,257,606,000 zinazotokana na deni la tozo ya usalama wa abiria.

Kutokuwasilishwa kwa tozo ya usalama kwa Mamlaka ya Viwanja vya ndege kunapunguza uwezo wa Mamlaka katika kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato hayo katika uwezo wa kuboresha usalama wa abiria.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya ndege Zanzibar kuendelea na jitihada za kuishawishi Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuwasilisha mapato yanayotokana na tozo ya usalama wa abiria kama inavyotakiwa na Sheria.

Mchanganuo wa bajeti na makusanyo halisi yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar kwa niaba ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 59: Bajeti na Makusanyo halisi ya tozo ya Usalama wa Abiria ya ZAA**

| Aina ya Tozo | Bajeti ya mwaka wa fedha 2022/2023 (Shs.) | Fedha zilizokusanywa 2022/23 (Shs.) | Fedha zilizowasilishwa ZAA (Shs.) |
|---|---|---|---|
| Tozo ya usalama wa abiria | 406,215,357 | 684,050,000 | 0 |
| **Jumla** | **406,215,357** | **684,050,000** | **0** |

### 5.1.3.2 Kutowasilishwa katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kwa Tozo ya Huduma kwa abiria (Passenger Service Charge) inayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) kwa niaba ya Mamlaka

Kwa mujibu wa Sheria nambari 2 ya Kodi za Huduma za Bandari na Viwanja vya Ndege ya 1999 (Port Service Charge Act no.2, 1999), abiria yeyote anaesafiri ndani ya Tanzania kupitia Viwanja vya Ndege, anapaswa kutozwa shilingi 10,000 na wale wanaosafiri nje ya Tanzania kuchajiwa USD 40 kwa ajili ya tozo ya huduma kwa abiria (Passenger Service Charge). Kwa mujibu wa sera za kimataifa za usafiri wa Anga (International Civil Aviation Organization Policies), fedha zote zinazokusanywa kupitia huduma za abiria, zinatakiwa zirudishwe kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege husika kwa ajili ya kuboresha huduma za Viwanja vya Ndege kwa ajili ya abiria wanaotumia viwanja hivyo.

Ukaguzi umebaini kwamba tozo ya huduma kwa abiria haijawahi kuwasilishwa kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kama zinavyoelekeza sera za kimataifa za usafiri wa anga.

Kutowasilishwa katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kwa tozo ya huduma kwa abiria kunaweza kuzorotesha matengenezo na maboresho ya huduma za viwanja vya ndege vya Zanzibar kwa ajili ya abiria wanaotumia viwanja hivyo jambo linaloweza kupelekea uwezekano wa kushuka hadhi kwa Viwanja vya Ndege vya Zanzibar kwa mujibu wa viwango za kimataifa za usafiri wa anga.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kupita Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuishawishi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango juu ya umuhimu wa kurejesha fedha za makusanyo ya tozo ya huduma kwa abiria katika Mamlaka ya Viwanja vya ndege Zanzibar ili ziweze kusaidia katika kuboresha huduma za Viwanja vya Ndege kwa ajili ya abiria wanaotumia viwanja hivyo.

### 5.1.3.3 Malipo ya kukodi mabasi manne kwa ajili ya wafanyakazi bila ya kuzingatia thamani ya fedha (Value for money), shilingi 237,600,000

Kwa mujibu wa kifungu nambari 37(c)(e) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016, inelezea kwamba ununuzi na uondoshaji wa mali za Umma unatakiwa kufanywa kwa mujibu wa misingi ya kuwepo ushindani na kuhakikisha thamani ya fedha (Value for Money) inapatikana pamoja na kuzingatia hali ya uchumi na ufanisi.

Ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar imekodi mabasi manne (4) kwa ajili ya wafanyakazi wake kwa gharama za shilingi 237,600,000 kwa mwaka ambazo ni sawa na wastani wa shilingi 4,950,000 kwa mwezi kwa kila basi bila ya kuzingatia thamani halisi ya fedha zinazolipwa kwa Mkodishaji.

Utaratibu wa Mamlaka kukodi mabasi hayo bila ya kuzingatia thamani halisi ya fedha inaibua wasiwasi kuhusu matumizi bora ya fedha za umma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kufanya tathmini ya kina kabla ya kuanza na utaratibu wa kukodi mabasi kwa ajili ya wafanyakazi wake na kuja na namna ya uboreshaji wa huduma za usafiri kwa wafanyakazi kwa kuzingatia thamani halisi ya fedha (Value for Money), hali ya uchumi na ufanisi.

#### 5.1.3.4 Kutokuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Viwanja vya Ndege

Kifungu nambari 20 cha Sheria nambari 9 ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ya 2011 (Aerodrome Act), kinahitaji kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Viwanja vya Ndege (Airport Development Fund) utakaojumuisha fedha zitakazoamuliwa kwa pamoja na Waziri anaeshuhulika na Viwanja vya Ndege pamoja na Waziri anehusika na masuala ya Fedha. Kwa mujibu wa kifungu hicho, fedha zinazowekwa katika Mfuko huo zinatakiwa zitumike kwa ajili ya uwekezaji, uendelezaji au ujenzi wa Viwanja vya Ndege.

Ukaguzi umebaini kwamba Mfuko wa Maendeleo ya Viwanja vya Ndege haujawahi kuanzishwa tangu kusainiwa kwa Sheria hiyo ya Viwanja vya Ndege mwaka 2011.

Kutokuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Viwanja vya Ndege ni kwenda kinyume na Sheria ya Viwanja wa Ndege jambo ambalo linapelekea kukosekana kwa fedha maalum zinazotengwa na Serikali kwa ajili ya uwekezaji, uendelezaji au ujenzi wa viwanja vya ndege Zanzibar.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kuhakikisha unafanya ufuatiliaji ikiwa ni pamoja na kufanya vikao kwa lengo la kujadili namna bora ya kuweza kuhuisha mfuko ulioasisiwa katika sheria ili kuhakikisha utekelezaji wa shughuli za uwekezaji, uendelezaji au ujenzi wa viwanja vya ndege Zanzibar.

#### 5.1.3.5 Kutokuwepo kwa Sera na Miongozo ya Uendeshaji na Usimamizi wa Mamlaka

Kwa mujibu wa viwango bora vinavyokubalika vya uendeshaji na usimamzi wa Viwanja vya Ndege, ni muhimu kuandaa sera na miongozo itakayofafanua na kuweka kumbukumbu za viwango vya utendaji na taratibu ambazo ni muhimu kwa ajili ya kupunguza vihatarishi katika usimamizi na uendeshaji wa wafanyakazi wa Mamlaka.

Lengo kuu la kuwepo sera katika usimamizi na uendeshaji wa Mamlaka ni kuweka usawa katika shughuli za utendaji ndani ya Mamlaka na katika Idara zote. Uwepo wa sera na miongozo ya uendeshaji na usimamizi wa shughuli za Mamlaka kunaongeza nguvu za udhibiti wa ndani katika usimamizi wa shughuli za kila siku za Mamlaka.

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Viwanja vya Ndege haina miongozo na sera za uendeshaji na usimamizi wa shughuli zake muhimu ikiwemo:

a. Sera ya usimamizi wa mali (Asset Management Policy),
b. Kanuni za Fedha (Financial Regulations),
c. Kanuni za Utumishi (Staff Regulations),
d. Sera za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT Policies).

Kutokuwepo kwa sera na miongozo ya uendeshaji na usimamizi wa Mamlaka kunaweza kupelekea kuongezeka kwa vihatarishi vinavyoikabili Mamlaka katika usimamizi bora wa shughuli za kiutendaji za Mamlaka.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kuweka kipaombele katika uanzishaji wa sera na miongozo inayogusa maeneo muhimu ya uendeshaji wa Mamlaka ikiwemo usimamizi wa mali, usimamizi wa fedha, usimamizi wa rasilimali watu na usimamizi wa teknolojia ya habari na mawasiliano. Aidha ni vyema kwa uongozi wa Mamlaka kuhakikisha kuwa miongozo hiyo inaendana na viwango bora vinavyokubalika vya sekta ya Viwanja vya Ndege na inaendana na matakwa ya kisheria.

### 5.1.3.6 Kutokuwepo kwa usimamizi mzuri wa madeni ya Mamlaka

Kifungu nambari 30(1)(2) vya Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa Afisa Masuuli atahusika na usimamizi wa mapato ya Taasisi ya Umma na atachukua hatua zinazofaa kuhakikisha uanzishaji na uendeshaji wa mfumo bora na wa ufanisi wa ukusanyaji na wa uhifadhi wa mapato. Aidha, Kanuni ya 23(1)(a) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inasisitiza ukusanyaji wa mapato kwa kueleza kuwa Afisa Masuuli atahakikisha kuwa watu wote wanaopaswa kulipa fedha yoyote kama mapato ya Serikali au stahiki yoyote ya Taasisi ya Umma wanapewa notisi ya madai au notisi yoyote ile ya madeni yanayodaiwa kwa wakati huo.

Ukaguzi umebaini kuongezeka kwa madeni yanayodaiwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kwa ongezeko lenye jumla ya shilingi 2,945,599,832 kutokana na kuwepo wadaiwa wenye jumla ya shilingi 10,407,989,440 katika mwaka 2022/2023 ikilinganishwa na wadaiwa wenye jumla ya shilingi 7,462,389,608 kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Ukaguzi umebaini kuwa hali hii imesababishwa zaidi na kutokuwepo kwa sera nzuri ya usimamizi wa madeni (Receivable Management Policies) katika Mamlaka.

Kukosekana kwa usimamizi mzuri wa madeni ya wadaiwa wa Mamlaka kunaathiri mtiririko wa fedha za Mamlaka jambo linaloweza kupelekea Mamlaka kushindwa kukimu mahitaji ya fedha kwa muda mfupi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kuanzisha sera za usimamizi wa madeni ili kuboresha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na madeni hayo.

Mchanganuo wa madeni ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 60: Madeni wadaiwa wa Mamlaka ya ZAA**

| Kiasi cha Wadaiwa hadi kufikia tarehe 30, Juni 2023 (Tshs.) | Kiasi cha Wadaiwa Hadi tarehe 30 Juni 2022 (Tshs.) | Kiasi cha Ongezeko la Wadaiwa (Tshs.) |
|---|---|---|
| 10,407,989,440 | 7,462,389,608 | 2,945,599,832 |

*Chanzo: Taarifa za Fedha za Mamlaka ya Viwanja vya Ndege za 30 Juni, 2023.*

**MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE PEMBA**

### 5.1.3.7 Kutokukamilika kwa Ufungaji wa Taa za kuongozea Ndege (Approach light)

Kwa mujibu wa miongozo ya kimataifa ya usimamizi wa viwanja vya ndege ANNEX 14 inaeleza kwamba Taa za kuongozea ndege (Approach light) ni taa ambazo zinatakiwa kuwepo katika kiwanja cha ndege kwa lengo la kumuongoza rubani katika njia sahihi wakati wa kutua.

Ukaguzi umebaini kwamba katika Kiwanja cha Ndege cha Pemba runway 2 Kusini na runway 20 Kaskazini kunatakiwa kuwepo taa 17 kila upande. Hadi ukaguzi huu unakamilika mnamo mwezi wa Disemba, 2023 runway 2 ni taa 15 pekee zinafanya kazi na hivyo kuweka tofauti ya taa 2 ambazo hazifanyi kazi na runway 20 zipo taa 11 zinafanya kazi na kuweka upungufu wa taa 6 ambazo hazifanyi kazi. Hali hii ikiendelea inaweza kusababisha kutokea kwa ajali pale ambapo itatokezea taa nyengine zaidi kuharibika na hivyo rubani kushindwa kuona vyema.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Pemba kuchukua jitihada za haraka za kuziweka taa hizo ili kuondoa usumbufu kabla hazijasababisha madhara kwa watumiaji wa uwanja huo, aidha ukaguzi unashauri kuimarisha ulinzi na kuweka uzio ulio imara.

### 5.1.4 MAMLAKA YA MAJI ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Mamlaka ya Maji (ZAWA) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.1.4.1 Kutokufikiwa kwa malengo katika ukusanyaji wa mapato shilingi 7,799,113,594.02

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Mamlaka ya Maji Zanzibar ilipanga kukusanya Jumla ya shilingi 10,870,491,200 kutokana na vyanzo vyake vya ndani vya mapato.

Nimebaini kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 Mamlaka ya Maji Zanzibar ilikusanya jumla ya shilingi 3,071,377,605.98 ambayo ni sawa na asilimia 28.25 ya makadirio kukiwa na upungufu wa makusanyo ya mapato yenye jumla ya shilingi 7,799,113,594.02 sawa asilimia 71.75 ya makadirio.

Kutokufikiwa kwa malengo ya ukusanyaji wa mapato ya Mamlaka kama ilivopangwa katika bajeti yake ya mwaka kunapelekea Mamlaka kukosa fedha za uendeshaji na kupelekea kuathiri huduma ya upatikanaji maji kwa wananchi na hatimae kupelekea kutofikiwa kwa malengo ya Mamlaka katika usambazaji wa huduma za maji katika maeneo yote ya mijini na vijijini nchini kwa ufanisi.

Unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar kuongeza nguvu katika kusimamia ukusanyaji wa mapato kwa kuhakikisha uanzishwaji na uendeshaji wa mfumo bora na wa ufanisi wa ukusanyaji na uhifadhi wa mapato ili kuwezesha Mamlaka kufikia malengo yake iliyojiwekea. Aidha nashauri Mamlaka iendeleze mikakati ya kufunga mita za maji kwa wateja ambao wanatumia huduma ya maji.

#### 5.1.4.2 Uwepo wa changamoto za mitandao ya maji katika shehia

Kifungu nambari 5(1)(e) cha Sheria nambari 4 ya Maji ya 2006 kinaeleza kazi ya Mamlaka ya Maji Zanzibar ni kusimamia uzalishaji na usambazaji wa maji kwa wananchi kwa misingi endelevu.

Ukaguzi umebaini kuwa hadi kufikia mwezi Disemba, 2023 Mamlaka ya Maji Zanzibar imekuwa ikikabiliwa na changamoto katika kutimiza wajibu wake kwenye utoaji wa huduma za maji safi, usambazaji wa maji wa kuaminika kutokana na mitandao ya maji kuwa ya zamani na mfumo wa usambazaji maji usiokidhi mahitaji ya watumiaji wa huduma za maji. Aidha ukaguzi umebaini kuwa kuna shehia 11 za Unguja ambazo hazipati maji kwa ukamilifu kutokana na sababu za uchakavu wa mitandao na mifumo ya usambazaji maji.

Kuwepo kwa maeneo (Shehia) ambazo mtandao wa maji hautoshelezi mahitaji ya watumiaji wa huduma ya maji ipasavyo kunasababisha kukosekana kwa huduma za maji safi na salama katika Shehia husika na kupelekea uzoroteshaji wa shulighuli za kiuchumi za wananchi pamoja na ukosefu wa mapato kwa Mamlaka ya Maji Zanzibar.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar kukamilisha mtandao wa maji kwa maeneo ambayo wa maji haujitoshelezi ili kuhakikisha uwepo wa huduma endelevu za usambazaji wa maji safi na salama kwa Wananchi wote nchini. Aidha, ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar kwa kushirikiana na Wizara ya Maji, Nishati na Madini kuongeza uwekezaji katika kuboresha na kukamilisha mtandao wa maji nchini ili kuongeza uzalishaji wa maji pamoja na miundombinu ya usambazaji maji ili kukidhi ongezeko la mahitaji ya maji katika shehia mbalimbali nchini. Mchanganuo wa shehia ambazo zinakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa huduma za maji safi na salama ni kama zinavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 61: Shehia ambazo zina changamoto za mtandao wa maji kwa upande wa Wilaya za Mjini Unguja**

| Namba | Jimbo | Shehia | Changamoto |
|---|---|---|---|
| 1. | Malindi | Shangani | Mtandao haujitoshelezi |
| | | Mkunazini | |
| | | Kiponda | |
| 2. | Kikwajuni | Miembeni | |
| | | Muembe shauri | |
| 3. | Chumbuni | Karakana | |
| | | Muembe Makumbi | |
| | | Banko | |
| 4. | Jangombe | Kidongo Chekundu | |
| | | Kwa alinato | |
| 5. | Mpendae | Mpendae | Maji machafu |

*Chanzo cha taarifa: kutoka idara ya operesheni za kiufundi*

### 5.1.4.3 Dosari katika matumizi ya Mfumo unganishi wa usimamizi wa uvujaji wa maji "Intergrated leakage Management System (ILMS)"

Katika mwaka wa fedha 2021/22 Mamlaka ya maji (ZAWA) ilinunua mfumo unganishi wa usimamizi wa uvujaji wa maji "Intergrated leakage Management System (ILMS)" kwa malengo makuu matano ambayo ni; kuyatambua maeneo ya wateja wa maji (Customer mapping), Udhibiti wa uvujaji wa maji kutoka kwenye miundombinu ya Maji (Leakage management), Kutambua kiwango cha maji (water quality), Ufanyaji maombi ya wateja wa maji (Customer Application) pamoja na Usimamizi wa kiwango cha maji ya tanki (Water tank level Management (Monitoring).

Ukaguzi umebaini kwamba mpaka kufikia mwezi wa Disemba 2023, Mamlaka ya Maji Zanzibar imefanikiwa kutumia mfumo wa ILMS katika lengo moja tu (1) ambalo linatumika kwa ajili ya Kutambua maeneo ya wateja wa maji (Customer mapping) huku kukiwa kumebakia dhamira au malengo manne (4) ambayo Mamlaka bado haijaanza kuyafanyia kazi ambayo ni; Udhibiti wa uvujaji wa maji kutoka kwenye miundo mbinu ya maji (Leakage management), Kutambua kiwango cha maji(water quality), Maombi ya wateja wa maji (Customer Application) na Usimamizi wa kiwango cha maji ya tanki (Water tank level Management (Monitoring).

Kutokamilika kwa matumizi ya mfumo wa (ILMS) katika dhamira nne (4) zilizosalia kunapelekea Mamlaka kutofikia malengo ya ununuzi wa mfumo huo ambapo hatimae kunaweza kupelekea kukosekana kwa thamani halisi ya fedha (Value for Money) ya ununuzi wa mfumo huo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar kuharakisha matumizi ya mfumo kwenye dhamira ya udhibiti wa uvujaji wa maji kutoka kwenye miundo mbinu (Leakage management) kutakoenda sambamba na ukamilishaji wa dhamira zote zilizobakia ili kuweza kufanikisha malengo ya ununuzi wa mfumo huo.

### 5.1.4.4 Kutokuwepo kwa sera ya utoaji huduma kwa mkopo (Credit policy)

Mamlaka ya Maji Zanzibar katika kutekeleza majukumu yake ya kukuza na kuendeleza utoaji wa huduma za maji Zanzibar huwa inatoa huduma zake kwa kutoza ada mbalimbali ambazo hupelekea Mamlaka kuzidai kampuni, mahoteli na wananchi ambao wanaopokea huduma kutoka kwa Mamlaka.

Uwepo wa sera ya utoaji huduma kwa mkopo (credit policy) husaidia taasisi kubainisha ni wateja gani wanastahiki kupewa huduma kwa mkopo au huduma gani inastahiki kutolewa kwa mkopo na pia inabainisha hatua zitakazochukuliwa na taasisi katika ukusanyaji wa madeni ya wanaodaiwa.

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Maji Zanzibar haina sera ya utoaji huduma kwa mkopo (credit policy) licha ya ukweli kuwa Mamlaka kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 ilikuwa na wadaiwa wenye jumla ya shilingi 53,490,152,833.

Kutokuwepo kwa Sera ya madeni kunaweza kupelekea kuongezeka kwa madeni ya wadaiwa wa Mamlaka na hatimae kunaweza kupelekea Mamlaka kupoteza mapato yanayotokana na vyanzo vyake vya mapato vya ndani.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar kuharakisha uandaaji wa sera za utoaji huduma kwa mkopo ili kuongeza usimamizi mzuri wa madeni yake na kuhakikisha kuwa wadaiwa wa Mamlaka wanalipa madeni yao kwa wakati ili fedha za Mamlaka zinazotokana na wadaiwa ziweze kusaidia shughuli za Uendeshaji za Mamlaka.

### 5.1.4.5 Kutokufanyika kwa uhakiki wa madeni ya wadaiwa shilingi 53,490,152,833

Mamlaka ya Maji Zanzibar imeweka utaratibu wa kufunga mita za maji kwa baadhi ya maeneo yanayopata maji kwa ajili ya kupima matumizi ya maji kwa mteja, na kwa yale maeneo ambayo bado hayajafungiwa Mamlaka imeweka utaratibu wa ulipaji wa bili ya maji ya shilingi 4,000 kwa mwezi kwa kila mteja anaepata huduma ya maji. Kwa mujibu wa taarifa za fedha za mwisho wa mwaka za Mamlaka ya Maji Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Mamlaka ilikuwa na wadaiwa (wateja wanaopata huduma ya maji ya Mamlaka) wenye jumla ya deni la shilingi 53,490,152,833 kwa upande wa Unguja na Pemba.

Ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka haijafanya uhakiki wa madeni ya waidaiwa ili kujiridhisha usahihi wa madeni hayo hasa ikizingatiwa kuwa kuna baadhi ya wateja wanaleta malalamiko katika Mamlaka juu ya kupata bili ya deni la maji hali ya kuwa wamekosa huduma ya maji katika kipindi husika.

Kutofanyiwa uhakiki wa madeni ya wadaiwa wa Mamlaka kunapelekea kuwepo kwa taarifa za madeni ya wadaiwa wa Mamlaka zilizokosa uhalisia na usahihi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar uhakikishe unafanya uhakiki wa madeni ya wateja wa maji ili kuepusha taarifa za fedha za mwisho wa mwaka za Mamlaka kuonyesha taarifa za wadaiwa wa Mamlaka zisizokuwa sahihi na halisi.

### 5.1.4.6 Kukosekana kwa hatimiliki (title deeds) kwa maeneo yanayotumiwa na Mamlaka ya Maji kwa uzalishaji na usambazaji maji

Kifungu nambari 41 cha Sheria nambari 4 ya Maji ya 2006 kinakataza kufanyika shughuli za ujenzi wa makaazi ya kudumu au ya muda mfupi katika maeneo ya vianzio vya maji na maeneo ya usambazaji wa maji.

Ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka ya Maji Zanzibar kwa upande wa Unguja inamiliki maeneo 28 kati ya maeneo hayo ni maeneo 5 tu ndio yaliyo na hati miliki (ambayo ni Welezo Matangini, Chuini, Gulioni, Mtoni-base camp na Muembe Madema) na maeneo 23 bado hayana hati miliki.

Kukosekana kwa hati miliki kwa maeneo ambayo Mamlaka ya Maji Zanzibar inayatumia kwa ajili shughuli za uzalishaji na usambazaji maji kunaweza kupelekea migogoro ya ardhi baina ya Mamlaka ya Maji na wananchi wa maeneo husika, uvamizi wa maeneo ambayo yanamilikiwa na Mamlaka ya maji na kunaweza kupelekea hasara ya kulipia fidia mara mbili.

Kukosekana kwa nyaraka za umiliki kumepelekea kushindwa kuthibitisha mali hizo kama zinamilikiwa kisheria na Mamlaka ya Maji Zanzibar. Hii inamaanisha kwamba Mamlaka ya Maji Zanzibar haimiliki mali hizo kisheria na endapo kutakuwa na kesi ya kushtakiwa Mamaka inaweza kushindwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar kuongeza juhudi katika kutafuta hati miliki kwa maeneo wanayotumia kwa ajili ya uzalishaji na usambazaji maji ili kupata nguvu za kisheria na kulinda mali za Serikali kutokana na uvamizi.

**MAMLAKA YA MAJI (ZAWA) PEMBA**

### 5.1.4.7 Malimbikizo ya Madeni ya muda mrefu shilingi 197,719,439

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mamlaka ya Maji Pemba inadaiwa jumla ya shilingi 197,719,439 zinazotokana na uwepo wa deni linalodaiwa na watoa huduma mbali mbali. Uwepo wa madeni ya muda mrefu katika Taasisi za Umma yanayodaiwa kutokana na huduma iliyotolewa yanatoa kiashiria cha kwamba Afisa Mhasibu wa Taasisi za Umma ameshindwa kusimamia ulipwaji wa madeni hayo kwa wakati kutokana na kukosekana kwa sera au muongozo wa ulipwaji wa madeni kwa wanufaika.

Kutokulipa madeni kwa wakati kunawakatisha tamaa watoa huduma na wasambazaji wa bidhaa na kunaweza kusababisha washindwe kuihudumia Mamlaka kwa mkopo hivyo Mamlaka kushindwa kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Ni muhimu kudumisha mahusiano mema ya kiutendaji kati ya Mamlaka na wadau wake, wakiwemo watoa huduma na bidhaa, kwa kuhakikisha Mamlaka inatimiza wajibu wake kwa kulipa madeni kwa wakati.

Kutokulipwa madeni kwa wakati ni kwenda kinyume na kifungu nambari 29(1)(b) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Maji Pemba kuchukuwa juhudi za makusudi kuhakikisha kwamba kunakuwa na sera ya usimamizi wa madeni ili kuepukana na uwepo wa madeni makubwa ambayo hayatoweza kulipika. Aidha, madeni yote yalipwe ili kuepusha uwezekano wa kuwepo kwa migogoro baina ya serikali na wananchi. Kipaumbele cha ulipaji kiwekwe kwenye madeni yaliyodumu kwa muda mrefu ikiwa ni pamoja na kufanya uhakiki wa usahihi wa madeni kabla ya kuyalipa. Mchanganuo wa malimbikizo ya madeni ya muda mrefu ni kama yanavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

### Jadweli Nambari 62: Malimbikizo ya Madeni ya Muda Mrefu

| Mdai (Supplier) | Huduma Iliyotolewa | Kiasi cha Fedha kinachodaiwa (Tshs) |
|---|---|---|
| Sapphire Engineering (T) Limited | Mashine ya Kusukumia Maji | 56,111,000 |
| Midodoni Hardware | Vifaa mbali mbali vya Maji Safi | 26,451,150 |
| Suleiman Nassor Suleiman | Changarawe za Visima | 21,400,000 |
| Broad Mind Company Ltd | Mashine ya Kusukumia Maji | 20,650,000 |
| Nassor Said Nassor | Vifaa vya Maji na Umeme | 18,016,789 |
| Suleiman Seif Rashid | Machine ya kusukumia maji | 11,615,000 |
| Mohammed Abdallah Rashid | Uchimbaji mtaro –W/Afya | 11,530,000 |
| Maroo Master General Supply | Vifaa vya umeme | 9,860,000 |
| Salim Hamdan Maalim | Vifaa vya ujenzi | 3,665,000 |
| Misufini Stationery Center | Vifaa vya kuandikia | 6,849,000 |
| Misali Sunset Beach | Huduma ya chakula | 4,210,000 |
| Nourbhai Auto services | Vifaa vya magari | 2,575,000 |
| Khamis Hassan Mgau | Ujenzi wa kibanda | 2,300,000 |
| Kikwajuni Zanzibar Solar | Machine ya kusukumia Maji | 2,100,000 |
| Khamis Sultan Said | Vifaa vya maji safi | 386,500 |
| **Jumla** | | **197,719,439** |

*Chanzo: Idara ya uhasibu.*

### 5.1.4.8 Kukosekana kwa Hati za Umiliki wa Ardhi na Majengo

Kwa mujibu wa kifungu nambari 64(1) cha Sheria nambari 6 ya Afisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kuwa Taasisi ya Umma itahifadhi nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zote zinamilikiwa kisheria na Serikali.

Ukaguzi umebaini kwamba baadhi ya mali za kudumu zinazomilikiwa na Mamlaka ya Maji Pemba zikiwemo majengo na maeneo yaliyojengwa visima vya maji yamekosa hati za umiliki hivyo ukaguzi kushindwa kuthibitisha umiliki halali wa mali husika. Kukosekana kwa hati ya umiliki wa mali hizo kunaweza kujitokeza kwa migogoro ya ardhi na kuweza kupelekea kuingia hasara kwa Serikali kwa kushindwa katika mashauri ya migogoro hiyo. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 64(1) cha Sheria ya Afisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma nambari 6 ya 2021.

Ukaguzi unaishauri Serikali kuhakikisha inachukuwa juhudi za makusudi ili kuzitambua na kuziwekea hati miliki mali zote zinazomilikiwa na Serikali ili kuepusha kujitokeza kwa mizozo baina ya Serikali na Jamii.

### 5.1.4.9 Kutowekewa Uzio Sehemu ya Kuhifadhia Vifaa

Kwa mujibu wa kifungu nambari 58(d) cha Sheria nambari 6 ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kuwa "Afisa Masuuli wa Taasisi ya Umma atakua na jukumu la kuhakikisha utaratibu wa kuhifadhi unawekwa ili kuondoa wizi, hasara, kupotea na matumizi mabaya.

Baada ya kupitia maeneo mbalimbali yanayomilikiwa na Mamlaka ya Maji Pemba, ukaguzi umebaini kuwepo kwa vifaa vya maji ikiwemo bomba za maji na ''Tee Compling" ambavyo vimehifadhiwa katika eneo la wazi kwa Sharifu Ali ambalo halijajengewa uzio. Hali hii inaweza kupelekea wizi, hasara, kupotea na matumizi mabaya ya mali na hivyo kuitia hasara Serikali.

Kutokujengwa kwa uzio katika eneo la kuhifadhia vifaa ni kwenda kinyume na kifungu nambari 58(d) cha Sheria nambari 6 ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 .

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka kuhakikisha kwamba wanaweka mikakati madhubuti katika utunzaji na uhifadhi wa vifaa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa uzio (fence) katika eneo la kuhifadhia vifaa la Sharifu Ali ili kuepukana na wizi na uharibifu wa vifaa hivyo.

### 5.1.4.10 Mazingira yasiyoridhisha ya Uhifadhi wa Vifaa vya Ghalani pamoja na Mali Nyengine

Kwa mujibu wa kifungu nambari 58(d) cha Sheria nambari 6 ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kuwa "Afisa Masuuli wa Taasisi ya Umma atakua na jukumu la kuhakikisha utaratibu wa kuhifadhi unawekwa ili kuondoa wizi, hasara, kupotea na matumizi mabaya.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa mazingira yasiyoridhisha ya uhifadhi wa vifaa vya ghalani pamoja na mpangilio usioridhisha wa vifaa hivyo vikiwa ghalani. Aidha, ukaguzi umebaini uwepo wa mashine za kusukumia maji (Water pump) 11, mtambo (gari) wa kuchimbia visima pamoja na mtambo wa kusafishia visima (Compressor) ambayo imewekwa sehemu isiyosalama kutokana na kupigwa na mvua na jua, hali ambayo inaweza kupelekea mitambo hiyo kuchakaa haraka na kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi unaotakiwa na pia inaweza kupelekea kutokea kwa uharibifu, upotevu au wizi wa mali hizo na hivyo kuitia hasara Mamlaka na Serikali kwa ujumla.

Uhifadhi wa vifaa katika mazingira yasiyoridhisha na mpangilio wa vifaa hivyo usioridhisha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Maji Pemba kuhakikisha wanafanya juhudi za makusudi ili kupata ghala yenye nafasi ya kutosha itakayowezesha kuhifadhi na kudhibiti vyema mali za Mamlaka, aidha ukaguzi unaishauri Mamlaka kuhakikisha kuwa mashine zote zilizowekwa nje ya ghala zinahifadhiwa katika sehemu salama.

### 5.1.4.11 Uhaba wa upatikanaji wa Huduma ya Maji Safi na Salama

Mamlaka ya Maji Tawi la Pemba inalo jukumu la kuhakikisha linaweka mtandao imara wa upatikanaji wa maji safi na salama katika maeneo yote ya Kisiwa cha Pemba.

Ukaguzi umebaini kwamba uzalishaji wa maji wa Mamlaka ya Maji Pemba unategemea maji kutoka kwenye visima ambapo wastani wa visima 22 havikuweza kufanya kazi kikamilifu katika nyakati tofauti katika robo ya mwisho ya mwaka wa fedha 2022/2023 kati ya visima 134 kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo kuungua mota za pampu za kusukumia maji kutokana na hitilafu ya mfumo wa umeme pamoja na sababu mbalimbali za kiufundi.

Kutokuwepo kwa huduma ya maji safi na salama ya uhakika ni kwenda kinyume na Sheria Nambari 4 ya Maji ya mwaka 2006.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka kuhakikisha inachukua juhudi za makusudi za utafutaji wa nishati mbadala na pia kuweka vidhibiti umeme (Stabilizer/UPS) katika visima vya maji ili kuepusha kuungua kwa mota kunakotokana na kupanda na kushuka kwa umeme na vile vile kuendelea kuvifanyia ukarabati visima vyote ambavyo havizalishi maji ya kutosha na kurekebisha pampu zote ili kuboresha huduma hio.

Mchanganuo wa wastani wa upungufu wa uzalishaji wa maji kwa robo ya mwisho ya mwaka 2022/2023 ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 63: Wastani wa Uzalishaji Maji kwa Robo ya Nne ya 22/23**

| Wilaya | Mahitaji ya Maji (1pd) | Uzalishaji wa Maji (1pd) | Upungufu (1Pd) | Asilimia ya Upungufu (%) |
|---|---|---|---|---|
| Mkoani | 21,743,372 | 12,482,400 | 9,260,972 | 42.59 |
| Chake Chake | 21,943,978 | 15,750,000 | 6,193,978 | 28.23 |
| Wete | 23,942,632 | 15,424,147 | 8,518,485 | 35.58 |
| Micheweni | 19,864,019 | 8,282,400 | 11,581,619 | 58.30 |
| **Jumla** | **87,494,001** | **51,938,947** | **35,555,054** | **40.64** |

### 5.1.4.12 Kutokuwepo kwa Maabara ya Upimaji wa Ubora wa Maji

Kwa mujibu wa Kanuni ya Maji ya mwaka 2007 inaitaka Mamlaka ya Maji ihakikishe ubora wa maji unazingatia viwango vilivyowekwa na Shirika la Afya Dunia (WHO).

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Maji Pemba haina maabara kwa ajili ya kupimia ubora wa maji ili kuweza kujiridhisha na usafi na usalama wa maji yanayotumika.

Kukosekana kwa maabara ya kupima ubora wa maji ni kwenda kinyume na kanuni niliyoitaja hapo juu.

Hali hii imetokana na Mamlaka kutokufuata kikamilifu matakwa ya Sheria za kitaifa na kimataifa hali ambayo inaweza ikapelekea kutokea kwa maradhi ya mripuko ikiwemo kipindupindu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya Maji Pemba kuhakikisha wanatenga bajeti kwa ajili ya ujenzi wa Maabara ya kisasa ya kupima ubora wa maji kabla ya kuwafikia watumiaji.

### 5.1.4.13 Kutokuwepo kwa Mfumo Rasmi wa Uingizaji Dawa za Kutibu Maji Katika Matangi ya Kuhifadhia Maji (Clorination Plant)

Kwa mujibu wa Kanuni ya Maji ya mwaka 2007 inaitaka Mamlaka ya Maji ihakikishe ubora wa maji unazingatia viwango vilivyowekwa na Shirika la Afya Dunia (WHO).

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Maji Pemba haina mfumo rasmi wa uingizaji dawa za kutibu maji katika matangi ya kuhifadhi na kusambazia maji kwenda kwa watumiaji jambo ambalo ni kwenda kinyume na kanuni ya Maji ya mwaka 2007 pamoja na matakwa ya Shirika la Afya Duniani.

Hali hii imetokana na Mamlaka Kutokufuata kikamilifu matakwa ya Sheria za kitaifa na kimataifa jambo ambalo linaweza likapelekea kutokea kwa maradhi ya mripuko.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya Maji Pemba kuhakikisha upatikanaji wa mfumo mpya na wa kisasa wa kuingiza dawa za kutibu maji katika matangi ya kuhifadhi na kusambazia maji kwenda kwa watumiaji.

### 5.1.4.14 Kutokuwasilishwa kwa Mkato wa Income Tax katika Mamlaka Husika shilingi 37,259,724

Kwa mujibu wa kifungu nambari 84(1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato ya 2004 (iliyorekebishwa mwaka 2019) kinaeleza kuwa "Kila Wakala wa kuzuia kodi atalipa kwa kamishna wa kodi ndani ya siku saba (7) baada ya tarehe ya mwisho ya kila mwezi kodi yoyote ile aliyozuia".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mamlaka ya Maji Pemba inadaiwa jumla ya shilingi 37,259,724 na Mamlaka ya Mapato Tanzania ikiwa ni kodi za wafanyakazi (PAYE) tokea mwaka 2016. Hali hii inaashiria udhibiti wa ndani usioridhisha pamoja na Mamlaka kutofuata kikamilifu matakwa ya Sheria jambo ambalo linaweza kupelekea kuitia hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Maji kufuata Sheria, Kanuni na Miongozo ya Serikali kikamilifu ili kuepukana na uwezekano wa kulipa deni pamoja na adhabu hivyo kuitia hasara Serikali. Mchanganuo wa fedha za kodi ya mapato (PAYE) ambazo hazijawasilishwa Mamlaka ya Mapato Tanzania ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 64: Deni la Kodi ya Mapato (PAYE) Ambalo Halijawasilishwa TRA

| Namba | Tarehe | Maelezo | Kiasi (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1. | 30/05/2016 | Commissioner of Income Tax. | 6,381,325 |
| 2. | 28/06/2016 | | 6,334,202 |
| 3. | 04/08/2016 | | 6,124,280 |
| 4. | 05/09/2016 | | 6,124,280 |
| 5. | 30/09/2016 | | 6,102,184 |
| 6. | 03/11/2016 | | 6,193,453 |
| **Jumla** | | | **37,259,724** |

### 5.1.4.15 Malipo yaliyofanywa kwa njia ya Fedha Taslimu shilingi 8,955,000

Kanuni ya 58(1) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaeleza kwamba malipo yote ya matumizi ya Taasisi za Kibajeti na Serikali za Mitaa lazima yafanywe kwa kutumia njia za kielektroniki.

Mamlaka ya Maji Pemba imefanya malipo yenye thamani ya shilingi 8,955,000 kwa ajili ya ununuzi na upatikanaji wa huduma mbalimbali. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni Mamlaka kutokutumia mfumo wa kibenki na badala yake kufanya matumizi kwa njia ya mfumo wa fedha taslim jambo ambalo huenda likapelekea uwepo wa viashiria vya matumizi mabaya ya fedha za umma au kujitokeza kwa udanganyifu unaotokana na ulipwaji wa malipo kwa watumishi wasiostahiki.

Kufanya matumizi kwa njia ya fedha taslimu ni kwenda kinyume na Kanuni ya Usimamizi ya Fedha za Umma ya 2021. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka kuhakikisha kwamba malipo yote yanafanyika kwa njia ya mfumo wa kibenki kwa lengo la kuhakikisha Serikali inapata mapato yatokanayo na kodi ya zuio kwa watoa huduma mbalimbali pamoja na uwezekano wa matumizi yasiyoridhisha ya fedha za umma. Mchanganuo wa malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 65: Malipo Yaliyofanyika kwa Njia ya Fedha Taslimu**

| Hati Namba | Hundi Namba | Thamani (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 14/8 ya 17/8/2022 | | 660,000 | Mamlaka ya Maji Pemba | Malipo ya nauli na posho la safari kikazi. |
| 11/9 ya 28/9/2022 | | 2,370,000 | | Malipo ya nauli na posho la safari kikazi. |
| 27/10 ya 13/10/2022 | | 490,000 | | Malipo ya nauli na posho safari kikazi. |
| 37/10 ya 13/10/2022 | | 1,435,000 | | Ikiwa ni malipo ya nauli na posho safari kikazi. |
| 55/10 ya 21/10/2022 | | 2,000,000 | | Malipo ya deni la wasimamizi wa vituo |
| 54/10 ya 21/10/2022 | | 2,000,000 | | Malipo ya deni la wasimamizi wa vituo vya maji kwa mwezi Januari, 2021. |
| **Jumla** | | **8,955,000** | | |

*Chanzo: Hati za malipo*

### 5.1.4.16 Kutokusomwa kwa Mita za Maji 1627

Kwa mujibu wa kifungu nambari (50)(2) cha Sheria nambari 4 ya Maji ya mwaka 2006 kinaeleza kwamba "Wateja watalipa Ankara zao za maji kulingana na vikundi vyao" Vilevile kifungu nambari 30(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma za mwaka 2016 kinaelezea "Afisa Mhasibu atachukuwa hatua zinazofaa kuhakikisha uanzishaji na uendeshaji wa mfumo bora na wa ufanisi wa ukusanyaji na uhifadhi wa mapato".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 ni mita za maji 3,445 pekee ndio zilizosomwa kati ya mita 5072 hivyo mita 1,627 hazikuweza kusomwa. Aidha, imebainika kuwa mita hizo husomwa kwa kutumia P.O.S ambazo zina uwezo mdogo wa kupiga picha hivyo kupelekea msoma mita kushindwa kuzituma taarifa katika mfumo wa malipo ya maji.

Vile vile ukaguzi umebaini uwepo wa baadhi ya mita katika mfumo lakini hazipo katika maeneo husika kutokana na kuharibika au kung'olewa na wateja kwa kukosa huduma ya maji. Hadi ukaguzi huu unakamilika Mamlaka ya Maji Pemba haijanunua vifaa vya kusomea mita ambavyo vitawawezesha kusoma mita kwa wakati na ufanisi zaidi, vifaa hivyo ni kama vile simu zenye uwezo na zinazoendana na matakwa ya mfumo wa malipo ya maji.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Maji Pemba kununua vifaa vya kisasa ili kuongeza kasi ya usomaji wa mita za maji na kuweza kusaidia katika kuongeza ukusanyaji wa mapato. Aidha, uongozi wa Mamlaka unashauriwa kuzihakiki mita zote kwa kulinganisha mita zilizomo katika mfumo na mita zilizofungwa kwa wateja pamoja na kuzitambua mita za wateja wanaopata huduma ya maji na wale wasiopata kwa lengo la kuepuka kuwabambikizia wateja wao madeni.

### 5.1.4.17 Kutokusajiliwa kwa Visima Binafsi 3,786

Kwa mujibu wa kifungu nambari 50(2) cha Sheria nambari 4 ya Maji ya 2006 inaeleza "Wateja watalipa Ankara zao kulingana na vikundi vyao". Vilevile kifungu nambari 30(2) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma za mwaka 2016 kinaelezea "Afisa Mhasibu atachukuwa hatua zinazofaa kuhakikisha uazishaji na uendeshaji wa mfumo bora na wa ufanisi wa ukusanyaji na uhifadhi wa mapato."

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa visima binafsi 3,799 katika Kisiwa cha Pemba. Kati ya visima hivyo visima vilivyosajiliwa ni visima 13 hivyo uwepo wa utofauti wa visima 3,786 ambavyo havijasajiliwa pamoja na kwamba mchakato wa kuvitambua visima hivyo umeshakamilika. Hali hii inaweza kupelekea uchimbaji wa visima kiholela unaoweza kupelekea upatikanaji wa maji ya chumvi na pia ni kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na usajili wa visima binafsi.

Kutokuvisajili visima vya maji binafsi ni kwenda kinyume na vifungu vya Sheria kama nilivyovinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Maji kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha visima vyote binafsi vinasajiliwa kwa wakati na kurahisisha upatikanaji wa taarifa za wateja na ufuatiliaji wa mapato.

### 5.1.4.18 Malimbikizo ya madeni ya maji ya muda mrefu shilingi 22,626,068,954.31

Mamlaka ya Maji Pemba ina jukumu kubwa la kuhakikisha linatoa huduma ya maji safi na salama sehemu mbalimbali katika jamii ya Zanzibar, kutokana na huduma inayotolewa wananchi wa Zanzibar hutakiwa kuchangia shilingi 4000 kwa mwezi kwa wale ambao hawakufungiwa mita za maji. Aidha, kwa wale waliofungiwa mita hizo watapaswa kuchangia huduma hiyo kwa kadri ya matumizi yatakavyofanywa na muhusika.

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ukaguzi umebaini uwepo wa malimbikizo ya madeni ya shilingi 22,626,068,954.31 yanayodaiwa kutoka kwa wananchi kisiwani Pemba.

Hali hii imetokana na Mamlaka ya Maji kutokuwashajihisha na kuwahamasisha wanufaika wa huduma ya maji kuweza kulipa madeni yao kwa kadri ya hali inavyoruhusu ili kupunguza uwezekano wa uwepo wa deni kubwa ambalo hawatoweza kulilipa na pia kupelekea Mamlaka kushindwa kufikia malengo waliyojipangia.

Kutokukusanywa kwa madeni ya maji ni kwenda kinyume na kifungu nambari 29(1)(b) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Maji Zanzibar kuchukuwa jitihada za makusudi za kulihakiki upya deni hilo ili kwa wale watakaobainika wanatumia huduma ya maji kuweza kufungiwa mita maalum za malipo (pre paid meter) na wale watakaobainika hawana huduma za maji deni lao kuwasilishwa Serikalini kwa lengo la kuombewa kibali maalum cha kuweza kusamehewa na hatimae kulifuta.

Aidha, uongozi wa Mamlaka ya Maji Pemba unashauriwa kuhakikisha wanaandaa mpango madhubuti utakaowezesha upatikanaji na usambazaji wa mita za maji za kulipia kabla (Pre-Paid meters). Mchanganuo wa malimbikizo ya madeni ya muda mrefu ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 66: Malimbikizo ya Madeni ya Muda Mrefu**

| Nam. | Aina ya Malipo | Kiasi Kinachodaiwa (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Wateja wa Kilimo (Agriculture) | 69,609,607.34 |
| 2. | Wateja wa Majumbani (Domestic) | 20,467,208,080.08 |
| 3. | Wateja wa Taasisi ( Institution) | 1,275,479,238.82 |
| 4. | Wateja wa Biashara (Commercial) | 813,772,028.07 |
| **Jumla** | | **22,626,068,954.31** |

### 5.1.5 MAMLAKA YA KUKUZA UWEKEZAJI ZANZIBAR (ZIPA)

Ukaguzi wa hesabu za Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.1.5.1 Dosari zilizojitokeza katika manunuzi ya ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 13.5 iliyoko Micheweni

Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) iliingia mkataba na Wakala wa Barabara Zanzibar tarehe 15 Agosti, 2022 kwa ajili ya ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilometa 13.5 kwa kiwango cha "prima coat" katika Maeneo Huru ya Kiuchumi ya Micheweni. Mkataba ulikuwa na kiasi cha shilingi 6,984,145,000 kwa muda wa miezi sita kutoka tarehe ya kuanza kwa kazi katika maeneo yote yaliyotengwa kwa kazi za ujenzi.

Hata hivyo, baada ya ukaguzi kupitia hati za malipo, mpango wa manunuzi na ripoti ya utekelezaji wa manunuzi kwa mwaka 2022/2023 umebaini dosari zifuatazo zinazohusiana na manunuzi ya ujenzi huo:-

- **Manunuzi yamefanyika nje ya mpango wa Manunuzi wa mwaka**

Ukaguzi ulipitia mpango wa manunuzi wa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 na kubaini kuwa manunuzi ya ujenzi huo hayakuwa yamepangwa kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha. Aidha, majibu ya awali ya uongozi yalisema kuwa manunuzi hayo yalipangwa kufanyika katika mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2022. Hata hivyo ukaguzi ulipojiridhisha kupitia mpango wa manunuzi uliowasilishwa na Uongozi wa Mamlaka kwa ajili ya ukaguzi wa mwaka wa fedha 2021/2022 umebaini kuwa manunuzi hayo pia hayakuwemo katika mpango huo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 42(7) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 ambayo inakataza kutekeleza ununuzi nje ya mpango wa ununuzi isipokuwa katika hali za dharura na za haraka.

- **Mchakato wa ununuzi ulitekelezwa na kukamilishwa bila idhini ya Bodi ya Zabuni ya Mamlaka**

Ukaguzi umepitia kumbukumbu za vikao vya bodi ya zabuni (minutes) kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 na kubaini kuwa, mchakato mzima wa ununuzi huu haukupata idhini ya bodi ya zabuni ya Mamlaka.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 28(1) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 ambayo inataja majukumu ya Bodi ya Zabuni ambayo ni pamoja na kuidhinisha taratibu za ununuzi, kuhakikisha kwamba kabla ya kuidhinishwa ununuzi unalingana na mpango wa ununuzi pamoja na kuidhinisha nyaraka za zabuni na mkataba.

- **Kutokuratibiwa kwa mchakato wa ununuzi na Kitengo cha Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma**

Kupitia mahojiano na majadiliano na Kitengo cha Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma cha Mamlaka, tulibaini kuwa ununuzi wa mradi huu, haukuratibiwa wala kusimamiwa na kitengo hicho, badala yake kitengo kimekuwa kikipokea taarifa za utekelezaji wa mradi huu kutoka kwa maofisa wanaohusika na Mradi huo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 29(a)(p) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 ambavyo inahitaji Kitengo cha Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kusimamia na kuratibu kazi zote za ununuzi na uondoshaji wa mali za taasisi isipokuwa kutoa hukumu na kutoa zabuni.

- **Kushindwa kukamilika mradi (kazi ya ujenzi) kwa wakati kama ilivyotakiwa na mkataba shilingi 12,927,128,073.42**

Kwa mujibu wa Masharti Maalum ya Mkataba Kifungu cha 1, kipindi cha kukamilisha kazi zote kilikuwa ni miezi sita (6) kutoka tarehe ya kuanza kwa kazi katika maeneo yote yaliyotengwa kwa kazi ya ujenzi. Aidha, kwa mujibu wa ratiba ya kazi iliyowekwa kwenye mkataba, mradi ulipaswa kukamilika ifikapo tarehe 30 Desemba, 2022. Hata hivyo, hadi mwisho wa mwaka wa fedha 2022/2023, mradi ulikuwa haujakamilika. Kutokana na hali hiyo, Mamlaka iliamua kuvunja mkataba na Wakala wa Barabara Zanzibar licha ya kwamba shilingi 4,004,377,562 sawa na asilimia 57.3 ya kiasi cha mkataba tayari ilikuwa imeshalipwa.

Aidha, wakati wa ziara ya kutembelea kwenye eneo la Mradi iliyofanyika mwezi Desemba, 2023 ukaguzi ulibaini kuwa mradi huu alikabidhiwa mkandarasi mwengine M/S IRIS CONSTRUCTION AND TRADE LIMITED kupitia mkataba uliosainiwa tarehe 10 Agosti, 2023 kwa Ujenzi wa barabara ya kilomita 13.5 kwa kiwango cha lami kwa kiasi cha mkataba cha USD 5,265,632.62 (sawa na shilingi 12,927,128,073.42 pamoja na VAT). Hadi tunakamilisha ukaguzi wetu mnamo tarehe 7 Januari, 2024, mradi ulikuwa bado unaendelea.

Kuwepo kwa dosari zilizobainika katika manunuzi ya mradi wa ujenzi wa barabara katika maeneo Huru ya Kiuchumi Micheweni kunaibua wasiwasi juu ya uwazi, haki, na uwajibikaji katika mchakato wa ununuzi huo jambo linalopelekea kuchelewa kukamilika kwa Mradi huo kama inavyotarajiwa na hatimaye kunaweza kusababisha kukosekana kwa Thamani ya Fedha (Value for Money) katika utekelezaji wa Mradi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar kuhakikisha kuwa manunuzi yote yanayofanywa na Mamlaka yanatokana na mpango wa manunuzi wa mwaka ulioidhinishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu nambari 42(1), (2), (4), (5), (6) na (7) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016. Aidha uongozi wa Mamlaka uhakikishe kuwa Kitengo cha Ununuzi na Uondoaji wa mali pamoja na Bodi ya Zabuni vyote zinashirikishwa kikamilifu katika mchakato mzima wa manunuzi ili kuongeza uwazi, uwajibikaji, haki na ustawi sambamba na kuhakikisha kupatikana thamani ya fedha (value for money) katika manunuzi.

### 5.1.5.2 Kushindwa kutekeleza Mapendekezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Utayarishaji wa Mikataba ya Manunuzi

Kanuni ya 47(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma, 2020 inaeleza kuwa Mkataba wowote unaohusu manunuzi ambao thamani yake ipo juu ya *minor value* kwa mujibu wa njia za manunuzi au kiwango cha chini utaidhinishwa na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya kusainiwa na pande husika.

Aidha, kanuni ya 47(4) ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za 2020 inaeleza kuwa “Afisa Masuuli baada ya kupokea maoni ya rasimu ya mkataba kutoka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, atajumuisha maoni hayo katika rasimu ya mkataba”.

Katika mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 ukaguzi ulibaini kuwa Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar iliomba maoni ya kisheria kutoka kwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa rasimu za mikataba mbalimbali. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwa baada ya Mamlaka kupokea mapendekezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, baadhi ya mapendekezo hayakutekelezwa na Mamlaka. Maelezo ya mapendekezo hayo ni kama yalivyofafanuliwa hapo chini: -

a) Baada ya Kupitia barua yenye kumbukumbu nambari DB.135/142/01/E-124 ya tarehe 10 Mei, 2023 kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuwasilisha rasimu ya mikataba kati ya Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar na kampuni ya M/S SKARS BUILDING COMPANY LIMITED ZANZIBAR kwa ajili ya zabuni za Ukarabati wa Ukuta na Mgahawa (SMZ/F0109/ W/OQ/2022-23/31), ukaguzi ulibaini kuwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilitoa mapendekezo kumi (10) ya kurekebishwa rasimu ya mkataba wa Ukarabati wa Mgahawa kabla ya kusainiwa. Hata hivyo baada ya kupitia mkataba uliosainiwa ukaguzi uligundua kuwa mapendekezo mawili hayakutekelezwa ambayo ni:-

- Pendekezo la 6: Kifungu cha 7 cha SCC kinachohusiana na malipo ya awali *(Advance payment)* kifungu hicho kisomeke *Not Applicable.*
- Pendekezo namba 8: Rasimu isomeke taarifa kamili za benki za mkandarasi. Pamoja na mambo mengine taarifa hizo zijumuishe Jina la benki, Nambari za Akaunti na Jina la tawi la benki.

b) Baada ya kupitia barua yenye kumbukumbu nambari DB.135/142/01/131 ya tarehe 23 Januari, 2023 kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuwasilisha rasimu ya mkataba kati ya Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar na kampuni ya M/S BITZ COMPANY LIMITED kwa ajili ya zabuni ya Ununuzi wa “Server” (ZIPA)(SMZ/F0109/G/NCB /2022-2023/27), ukaguzi ulibaini kuwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilitoa baadhi ya mapendekezo ya kurekebisha rasimu ya mkataba wa Ununuzi wa Server kabla ya kutia saini. Hata hivyo, baada ya kupitia mkataba uliosainiwa tulibaini kuwa mapendekezo mawili hayakutekelezwa ambayo ni:-

- Pendekezo namba 5: Muda wa mkataba ujulikane na uainishwe katika fomu ya mkataba.
- Pendekezo namba 7: Kifungu cha 9.1 cha SCC. Ofisi inashauri dhamana ya utekelezaji kazi *(performance Security)* iwepo na iwe ni asilimia kumi (10%) ya bei ya mkataba na iwe dhamana ya benki isiyo na masharti *(Unconditional bank Guarantee)*. Aidha, Afisi inashauri muda wa kurejesha *performance Security* kwa *Supplier* ni baada ya kumalizika kwa muda wa dhima wa bidhaa (Warranty period).

c) Baada ya kupitia barua yenye kumbukumbu nambari DB.135/142/01/123 ya tarehe 19 Januari, 2023 kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuwasilisha rasimu ya mkataba kati ya Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar na kampuni ya M/S CLASSIC SOLUTION PARTNERSHIP kwa ajili ya zabuni ya ununuzi wa Vifaa vya Kuandika (SMZ/F0109/G/OQ/2022-2023/09), ukaguzi ulibaini kuwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilitoa baadhi ya mapendekezo ya kurekebisha rasimu ya mkataba wa ununuzi wa Vifaa vya Kuandikia kabla ya kusainiwa. Hata hivyo, baada ya kupitia mkataba uliosainiwa tuligundua kuwa mapendekezo matatu (3) yaliyotolewa hayakutekelezwa ambayo ni:-

- Pendekezo namba 6. Katika Masharti Maalum ya Mkataba kiwepo kifungu kinachohusiana na utatuzi wa migogoro, kifungu hicho kielezee kwamba, mgogoro wowote utakaojitokeza na kushindwa kutatuliwa kwa njia ya mazungumzo utatuliwe katika Mahakama ya Biashara ya Zanzibar. Hivyo mwenendo wa shauri utaendeshwa kwa mujibu wa mahkama.

- Pendekezo namba 7: suala la utekelezaji kazi (performance Security) lizingatiwe na iwe dhamana isiyo na masharti (Unconditional Bank Guarantee).
- Pendekezo namba 10: Rasimu inapaswa kusomeka taarifa kamili za benki za msambazaji. Pamoja na mambo mengine, taarifa hizo zijumuishe Jina la benki, namba za akaunti na jina la tawi la benki.

Kutokutekelezwa kwa mapendekezo kutoka kwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa rasimu za mikataba zilizowasilishwa kunaweza kukasababisha Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar kuingia katika makubaliano ya mikataba isiyo na tija na hatimae Mamlaka inaweza kupata hasara isiyo ya lazima.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar kuhakikisha kuwa mikataba yote ya manunuzi inawasilishwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu kabla ya kusainiwa kama inavyotakiwa na Kanuni nambari 47(1) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za 2020 na mapendekezo ya Mwanasheria Mkuu yanafanyiwa kazi ili kupunguza hatari ya kuingia katika makubaliano ya mikataba ambayo haina faida kwa Serikali.

### 5.1.5.3 Kutokuwepo kwa bodi hai ya wakurugenzi kwa zaidi ya miezi kumi na miwili

Kifungu nambari 17 cha Sheria nambari 14 ya Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar ya 2018 inaeleza Uwezo na kazi mbalimbali za bodi ya wakurugenzi ya Mamlaka ambazo zinalenga kusaidia katika kusimamia shughuli za kila siku za Mamlaka.

Katika kipindi cha ukaguzi, ukaguzi ulibaini kuwa bodi ya wakurugenzi ya Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar haikuwa hai kwa kipindi chote cha mwaka wa fedha. Hii ina maana kwamba Mamlaka haikukidhi matakwa ya kisheria yaliyoainishwa katika kifungu cha 8(1) cha Sheria nambari 14 ya Mamlaka ya Kukuza na Kulinda Uwekezaji Zanzibar ya 2018.

Kutokuwepo kwa bodi ya Wakurugenzi kunapelekea kutokuwepo kwa usimamizi juu ya utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka (ya ufanyaji wa maamuzi ya kimkakati) yanayotokana na Bodi ya Wakurugenzi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar kutafuta ushauri juu ya hali hiyo kutoka kwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu jinsi Mamlaka inavyoweza kupata kazi za uangalizi (oversight functions) bila Bodi ya Wakurugenzi. Aidha, Uongozi wa Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar uchukue juhudi katika kuharakisha uteuzi wa Bodi mpya ya Wakurugenzi.

### 5.1.5.4 Kutokuwepo kwa Kamati hai ya Ukaguzi wa Ndani

Kifungu nambari 118(3) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 inazitaka Mashirika ya Umma kuanzisha Kamati za Ndani za Ukaguzi zinazotoa taarifa kwa chombo husika cha uongozi.

Ukaguzi umebaini kuwa kamati ya ukaguzi ya Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar haikuwa hai katika kipindi chote cha mwaka wa fedha 2022/2023 kutokana na kutokuwepo kwa Bodi ya Wakurugenzi. Hii imetokana na kuwa sehemu kubwa ya wajumbe wa kamati ya Ukaguzi wanatokana na wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Mamalaka.

Kutokuwepo kwa kamati hai ya ukaguzi kunasababisha kukosekana kwa chombo cha uangalizi wa shughuli za Mamlaka pamoja na kukosekana kwa tathmini ya mfumo wa udhibiti wa ndani na mfumo wa usimamizi wa vihatarishi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar kushawishi vyombo vinavyohusika na uteuzi wa wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, kuharakisha uteuzi huo ili kuwa na kamati ya ukaguzi iliyo hai.

### 5.1.5.5 Kutokuwepo kwa Mkataba wa usambazaji wa Mafuta

Kwa mujibu wa Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya 2016, mkataba ni makubaliano yanayofanywa kati ya taasisi ya ununuzi na mzabuni kutokana na taratibu za manunuzi. Aidha, kifungu nambari 63(3) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza kwamba "kukubaliwa kwa zabuni kutaidhinishwa kwa mkataba wa maandishi utakaosainiwa na pande zote mbili Mtoa huduma na Taasisi ya Ununuzi na Uondoshaji ....."

Ukaguzi umepitia taarifa ya utekelezaji wa manunuzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 za Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar na kubaini kuwa Mamlaka inanunua mafuta (petroli na dizeli) kutoka kwa wauzaji mbalimbali bila kuwepo mkataba rasmi wa ununuzi wa mafuta.

Kutokuwepo kwa mkataba rasmi wa ununuzi wa mafuta kati ya Mtoa huduma na Mamlaka kunaweza kusababisha kukosekana kwa masharti halali yanayobana pande husika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar kufanya makubaliano ya kimkataba na wasambazaji wa mafuta ili kurasimisha mauziano kati yao.

**MAMLAKA YA KUKUZA UWEKEZAJI (ZIPA) - PEMBA**

### 5.1.5.6 Kukosekana kwa Mpango Kazi na Mpango wa Ununuzi wa Mwaka

Kifungu nambari 41(2) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza "Taasisi zinazohusika na bajeti ya Serikali zitawasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali bajeti zao za mwaka na zitajumuisha Mpango kazi na mpango wa ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Pemba hawakutayarisha mpango kazi na mpango wa ununuzi wa mwaka wa fedha 2022/2023 hali ambayo inapelekea kushindwa kufanya tathmini ya utekelezaji wa shughuli zake za robo mwaka na mwaka na pia inaweza kupelekea ununuzi wa bidhaa ambazo hazikuhitajiwa. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha sheria niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka kuhakikisha wanaandaa mpango kazi na mpango wa ununuzi wa mwaka kama sheria inavyoelekeza.

### 5.1.5.7 Kutokuwepo kwa mkataba wa ununuzi wa mafuta shilingi 14,804,840

Kwa mujibu wa kifungu nambari 42(2) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza kwamba "Taasisi ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma itapanga mpango wake wa ununuzi na uondoshaji kwa kutumia vigezo vinavyokubalika na hususan utazingatia kutumia mfumo wa mikataba maalumu (framework contract) kwa namna inavyohitajika kutoa huduma bora, zenye gharama nafuu na kwa njia inayoweza kubadilika kwa bidhaa zinazohitajika kila mara au zinazojirudia kila baada ya muda".

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 14,804,840 zimelipwa na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Pemba kwa kituo cha mafuta cha Chake Petrol Station kwa ajili ya ununuzi wa mafuta bila ya kuwepo kwa mkataba. Hali hii inaweza kupelekea kutokupata huduma iliyo bora na ya uhakika pamoja na uwezekano wa kutokea kwa ununuzi holela wa mafuta. Aidha, ni kwenda kinyume na kifungu nambari 42(2)(b) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka kuhakikisha wanafunga mikataba kwa ununuzi wa bidhaa zote wanazotumia kila mara au zinazojirudia kila baada ya muda kama sheria inavyoolekeza. Mchanganuo wa ununuzi wa mafuta hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 67: Mafuta yaliyonunuliwa bila ya Mkataba**

| Hati Namba | Hundi Namba | Aliyelipwa | Thamani (Tshs) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 17/9 ya 22/9/2023 | 000006 | Zanzibar Petroleum | 452,840 | Malipo ya ununuzi wa mafuta kwa ajili ya matumizi ya Ofisi. |
| 1/8 ya 1/8/2022 | 000001 | | 1,794,000 | |
| 7/3 ya 15/3/2023 | 000023 | Chake Petrol station | 10,465,000 | |
| 8/11 ya 23/11/2022 | 000010 | | 598,000 | |
| 3/1 ya 9/1/2023 | T.T | | 897,000 | |
| 10/1 ya 24/1/2023 | | | 598,000 | |
| **Jumla** | | | **14,804,840** | |

*Chanzo: Hati za malipo*

### 5.1.5.8 Malimbikizo ya madeni ya muda mrefu USD 122,750 (wastani wa shilingi 319,150,000)

Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Pemba imesajili jumla ya miradi 41 ambayo inajishughulisha na shughuli mbalimbali ikiwemo biashara ya hoteli, usafirishaji, kilimo na viwanda.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba kati ya miradi iliyosajiliwa ni miradi 13 pekee ambayo imefanya malipo huku ikiwacha miradi 28 bila ya kufanya malipo yenye thamani ya USD 122,750 sawa na wastani wa shilingi 319,150,000.

Hali hii inaweza kudhoofisha maendeleo ya Mamlaka na kupelekea kutokufikia malengo iliyojiwekea. Kutokukusanya mapato ya usajili wa miradi kwa wakati ni kwenda kinyume na Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Pemba kuhakikisha wanafuatilia ipaswavyo ukusanyaji wa mapato yatokanayo na ada za wawawekezaji na pia iwaelimishe wawekezaji juu ya umuhimu wa ulipaji wa kodi kwa wakati.

### 5.1.6 MAMLAKA YA UNUNUZI NA UONDOAJI WA MALI ZA UMMA ZANZIBAR (ZPPDA)

Ukaguzi wa hesabu za Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifza na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

**MAMLAKA YA UNUNUZI NA UONDOAJI WA MALI ZA UMMA PEMBA**

### 5.1.6.1 Uwepo wa Uhaba wa Wataalamu

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Pemba ina upungufu wa wataalamu hususan wahandisi na wakaguzi katika fani ya ununuzi. Wataalamu hawa ni muhimu katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka ili kuhakikisha uwepo wa uwazi, usawa na thamani halisi ya fedha (Value for Money) katika mchakato mzima wa ununuzi na uondoaji kwa mujibu wa sheria na taratibu za ununuzi na uondoaji wa mali za umma katika taasisi zote za Serikali.

Kutokufanya uajiri kwa mujibu wa nafasi zilizowazi ni kwenda kinyume na kanuni nambari 6(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka kuhakikisha wanaendelea kuomba kibali cha uajiri kutoka Tume ya Utumishi Serikalini vyenginevyo ihakikishe inapata watumishi wa kuhamisha kutoka Taasisi nyengine za Umma ili kuziba pengo la ukosefu wa wataalamu.

#### 5.1.6.2 Uhaba wa Vyombo vya Usafiri

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Pemba ina uhaba mkubwa wa vyombo vya usafiri kwa ajili ya shughuli zake za kila siku ambapo kulingana na hali halisi ya kazi zake inahitaji kupata usafiri wa kutosha na wa uhakika ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Aidha, ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka inamiliki gari moja ambayo mara nyingi huazimwa na ofisi nyengine kwa ajili ya kufanya shughuli mbali mbali za kiserikali ikiwemo ziara za viongozi wakuu. Kukosekana kwa usafiri wa uhakika kunapelekea kupungua kwa ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za Mamlaka. Kukosekana vitendea kazi vya kutosha ikiwemo vyombo vya usafiri ni kwenda kinyume na Sheria nambari 2 ya Utumishi wa Umma ya 2011.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya ununuzi wa vyombo vya usafiri.

### 5.1.7 MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI (VTA)

Ukaguzi wa hesabu za Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.1.7.1 Upungufu wa vifaa vya kufanyia mitihani kwa vitendo

Ukaguzi umebaini kwamba Vituo vya Mafunzo ya Amali ambavyo vipo chini ya Mamlaka ya Vyuo vya Amali Zanzibar vina upungufu wa vifaa vya kufanyia mitihani kwa vitendo kwa ajili ya wanafunzi wa vituo hivyo ambao wanalazimika kufanya mitihani yao ya nadharia na ya vitendo. Hata hivyo ili wanafunzi waweze kufaulu mitihani yao wanatakiwa kufanya mitihani ya vitendo zaidi ya mitihani ya nadharia. Hata hivyo ukaguzi umebaini kuwa vifaa vya kufanyia mitihani ya vitendo ni vichache ukilinganisha na wingi wa wanafunzi.

Uchache wa vifaa vya kufanyia mitihani ya vitendo kunapelekea kutofanyika baadhi ya mafunzo ya vitendo na hata baadhi ya mitihani ya vitendo. Aidha kunapelekea vyuo hivyo kutumia muda mrefu kwa kufanyia mitihani wanafunzi wachache na wengine kusubiria hadi kumalizika kwa idadi ya wanafunzi wote.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Vyuo vya Amali Zanzibar kujipanga vizuri na kununua vifaa vya kutosha vya kufanyia mitihani ya vitendo ili kuwaondolea usumbufu wanafunzi kukaa na kusubiri kwa muda mrefu kwa siku za mitihani.

### 5.1.7.2 Kukosekana kwa hati miliki za majengo yanayomilikiwa na Taasisi

Uhakiki wa nyaraka za umiliki umebaini kwamba majengo yanayomilikiwa na Mamlaka ya Vyuo vya Amali Zanzibar hayana uthibitisho wa umiliki halali wa majengo hayo kutokana na kukosekana kwa hati za umiliki (Tittle Deeds) wakati wa ukaguzi ili kuthibitisha uhalali wa umiliki huo.

Kukosekana kwa hati za umiliki wa majengo kunapelekea Mamlaka kukosa uhalali wa kisheria wa umiliki wa majengo hayo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Vyuo vya Amali Zanzibar kufuatilia hati za majengo yake yote ili kuepuka matatizo yanayoweza kutokea kuhusiana na umiliki wa majengo hayo.

**MAMLAKA YA MAFUNZO YA AMALI PEMBA**

### 5.1.7.3 Uwepo Mashine za Boti Zilizotelekezwa kwa Muda Mrefu

Kwa mujibu wa kifungu nambari 61(2) cha Sheria nambari 6 ya Afisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba "Afisa Masuuli atahakikisha kwamba mali za umma zinatumika kwa tija na manufaa kulingana na jukumu litakalotekelezwa".

Ukaguzi umebaini uwepo wa mashine mbili (2) kubwa za boti katika Chuo cha Mafunzo ya Amali Daya ambazo zilipatikana mwaka 2020 kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wakati wa ufunguzi wa chuo hicho kama msaada kutoka kwa wafadhili wa mradi wa ALSD II kwa madhumuni ya kufundishia wanafunzi wanaojifunza fani ya uvuvi kwa vitendo. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokutumika kwa mashine hizo kwa muda mrefu hali inayopelekea kutokufikia kwa malengo yaliyokusudiwa.

Kutokutumika kwa mashine hizo ni kuwakosesha wanafunzi wa fani ya uvuvi fursa ya kujifunza zaidi kwa vitendo pamoja na kuondoa nia njema ya Serikali ya kuwapatia wananchi wake elimu ya uvuvi itakayoweza kuwasaidia kuimarisha uchumi wa nchi hasa kupitia uchumi wa buluu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Pemba kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha mashine hizo zinatumika kwa ufanisi ili kuleta tija iliyokusudiwa.

### 5.1.7.4 Upungufu wa Mashine za Kisasa za Kufundishia

Mamlaka ya Mafunzo ya Amali imeanzishwa kwa lengo la kukuza taaluma ya ujuzi kwa vijana kwa kuwapatia mafunzo ya Elimu ya Ufundi, utakaowaweka katika nafasi ya kuweza kuajiriwa Serikalini, katika sekta binafsi au kujiajiri wao wenyewe na kuweza kuongeza kipato chao na pato la Taifa kwa ujumla.

Ukaguzi umebaini kutokufikiwa kwa lengo hili kutokana na upungufu mkubwa wa mashine za kisasa za kufundishia kwa vitendo katika fani za ufundi wa magari, kilimo, ushoni useremala, ujenzi, ufundi bomba, umeme na fani nyenginezo zinazofundishwa na Vyuo vya Mafunzo ya Amali vilivyopo Daya na Vitongoji hali inayopelekea wanafunzi kuendelea kujifunza kwa njia ya nadharia (Theory) pekee na hivyo kutokufikiwa kikamilifu malengo ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali.

Kukosekana kwa vifaa vya kisasa vya kufundishia kwa vitendo ni kutokufikiwa kwa lengo la kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka kuhakikisha wanatenga fedha za kutosha katika bajeti zao za mwaka ili kuweza kufanya ununuzi wa vifaa vyote muhimu vinavyohitajika.

#### 5.1.7.5 Kutokukamilika kwa Ujenzi wa Uzio Katika Chuo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji

Kifungu nambari 58(d) cha Sheria nambari 6 ya Afisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kuwa Afisa Masuuli wa Taasisi ya Umma atakuwa na jukumu la kuhakikisha utaratibu wa kuhifadhi unawekwa ili kuondoa wizi, hasara, kupotea na matumizi mabaya.

Baada ya kupitia maeneo mbalimbali yanayomilikiwa na Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Pemba, ukaguzi umebaini kutokukamilika kwa ujenzi wa uzio katika Chuo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji. Hali hii inaweza kupelekea uvamizi na uharibifu mkubwa wa mali za Serikali ikiwemo Majengo ya Chuo hicho pamoja na mali zilizomo ndani yake.

Kutokukamilishwa kwa ujenzi wa uzio wa Chuo cha Mafunzo ya Amali Vitongoji ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu pamoja na vifungu vya 29(a) na 112(2)(e) vya Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016. Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka kuhakikisha kwamba wanatenga fedha za kutosha katika bajeti yao ya mwaka zitakazowezesha majengo yote yanayomilikiwa na Mamlaka kujengewa uzio.

#### 5.1.7.6 Uchakavu wa Magari yanayotumiwa na Mamlaka

Kifungu nambari 69(1)(2) cha Sheria nambari 6 ya Afisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba "Kutakuwa na mpango wa uondoaji wa mali wa mwaka utakaoandaliwa na kila taasisi ya Umma na kuwasilishwa katika Afisi ya Msajili wa Hazina. Taasisi ya Umma itaomba ruhusa kutoka katika ofisi kwa ajili ya kuondoa mali za Umma".

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Pemba inakabiliwa na tatizo la usafiri lililotokana na uchakavu wa magari yake ambayo yameshatumika kwa muda mrefu sasa bila ya kuuzwa au kununuliwa gari nyengine. Hali hii inapelekea magari hayo kuharibika mara kwa mara na kuigharimu Mamlaka fedha nyingi kwa ajili ya matengenezo.

Kutokuondolewa na kununuliwa magari mapya ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kuhakikisha wanatenga fedha za kutosha katika bajeti zao za mwaka kwa ajili ya ununuzi wa gari za Afisi.

#### 5.1.7.7 MAMLAKA YA HIFADHI NA UENDELEZAJI MJI MKONGWE ZANZIBAR (ZSTDA)

Ukaguzi wa hesabu za Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.1.7.8 Kutotambuliwa kwa taarifa za Makusanyo ya Mapato na Matumizi ya Bustani ya Forodhani katika Hesabu ya Mamlaka

Kanuni nambari 26(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za 2021 inaeleza kwamba Hazina ndio chombo pekee chenye mamlaka ya kuanzisha chanzo kipya cha mapato kwa ajili ya kukusanywa na Taasisi ya Umma. Aidha, kanuni nambari 29(1)(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 zinaeleza kuwa kwa njia yoyote ile makusanyo yanayopokewa na Taasisi ya kibajeti yanapaswa kuwasilishwa katika Mfuko Mkuu wa Hazina kwa ujumla wake na matumizi ya mapato yaliyopokelewa yatahitaji ruhusa husika kuwa ni matumizi ya Serikali.

Ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe inakusanya mapato kutokana na Bustani ya Forodhani ambayo yanaingia katika hesabu ya benki iliyoko PBZ yenye namba 0404302000 na jina la Forodhani Park, ambapo Mkurugenzi wa Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe ni sehemu ya uidhinishaji wa matumizi ya mapato hayo. Hata hivyo mapato hayo pamoja na matumizi yake hayakutambuliwa katika hesabu za mwisho wa mwaka za Mamlaka kwa mwaka wa fedha 2022/2023, na ukaguzi haukupatiwa uthibitisho wa ruhusa ya matumizi ya mapato hayo kutoka kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Kutokutambuliwa kwa mapato na matumizi ya fedha zinazotokana na Bustani ya Forodhani katika hesabu za mwisho wa mwaka za Mamlaka pamoja na kutokuwasilishwa kwa mapato hayo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ni kwenda kinyume na Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 pamoja na Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za 2021.

Aidha, kukosekana kwa uthibitisho wa ruhusa ya matumizi ya mapato hayo kutoka kwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali kunapelekea kukosekana kwa uhalali wa matumizi hayo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe kuhakikisha kwamba unasimamia na kutekeleza uingizwaji wa taarifa za mapato na matumizi yatokanayo na Bustani ya Forodhani katika hesabu za mwisho wa mwaka za Mamlaka ili kuepuka kujitokeza kwa hesabu hiyo kutokuonesha sura sahihi na halisi kulingana na miongozo ya ufungaji wa mahesabu wa Kitaifa na Kimataifa. Aidha, kuhakiksha kunakuwa na usimamizi imara katika kufuta matakwa ya kisheria kama ilivyobainishwa hapo juu.

### 5.1.7.9 Kutotambuliwa kwa taarifa za Makusanyo ya Mapato na Matumizi ya Bustani ya Forodhani katika Hesabu ya Mamlaka

Kanuni nambari 26(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za 2021 inaeleza kwamba Hazina ndio chombo pekee chenye mamlaka ya kuanzisha chanzo kipya cha mapato kuweza kukusanywa na Taasisi yeyote ya umma.

Ukaguzi umebaini kwamba Bustani ya Forodhani inakusanya mapato ambayo yanaingia katika hesabu namba 0404302000 inayosomeka kwa jina la Forodhani Park ambapo Mkurugenzi wa Mamlaka ya Mji Mkongwe ni sehemu ya uidhinishaji wa matumizi ya mapato hayo hata hivyo mapato hayo Pamoja na matumizi yake hayakutambuliwa katika hesabu za Mamlaka kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Aidha, kanuni nambari 29(1) ya kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za 2021 kinaeleza kuwa kwa njia yoyote ile makusanyo yanayopokewa na Taasisi ya kibajeti yanapaswa kuwasilishwa katika mfuko Mkuu wa Hazina na matumizi ya mapato hayo yanahitaji ruhusa ya kuwa ni matumizi ya Serikali. Ukaguzi haukuweza kupatiwa uthibitisho wa ruhusa ya matumizi ya mapato hayo kutoka Hazina.

Kutokutambliwa kwa mapato na matumizi ya fedha za Bustani ya Forodhani katika hesabu ya Mamlaka ni Kwenda kinyume taratibu za ufungaji wa hesabu.

Aidha kutowasilishwa kwa mapato hayo katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ni kwenda kinyume na kanuni nilizozinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe kuhakikisha unayatambua mapato na matumizi ya Bustani katika hesabu za mwisho wa mwaka ili kuweza kuonesha sura sahihi na halisi ya hesabu zilizotayarishwa na kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

### 5.1.7.10 Matumizi yaliyofanyika zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa katika vifungu husika shilingi 446,759,632.42

Kifungu nambari 31(3) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaelekeza kuwa Afisa Mhasibu atachukua hatua za kutumia ndani ya bajeti iliyotengwa na kuzuia matumizi ya ziada, na kuwasilisha taarifa kwa Waziri anayehusika, Bodi ya usimamizi na Hazina ya Serikali.

Ukaguzi umepitia taarifa za hesabu ya mwisho wa mwaka za Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe na kubaini uwepo wa matumizi yaliyofanyika zaidi ya bajeti iliyopangwa jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Kufanya matumizi ya fedha ambayo yamezidi bajeti katika vifungu husika kunapelekea kuathiri utekelezaji wa shughuli nyingine za Mamlaka.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe kuhakikisha kwamba matumizi ya fedha yanayofanywa na Mamlaka yanafuata bajeti husika ili kuwa na nidhamu katika utekelezaji wa matumizi ya Mamlaka. Aidha, uongozi wa Mamlaka uhakikishe hakuna matumizi yanayofanywa zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa pasi na kupata idhini ya Bodi ya Wakurugenzi au Mamlaka nyengine husika. Mchanganuo wa vifungu vilivyobainika kuzidi bajeti iliyoidhinishwa ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 68: Matumizi yaliyofanyika zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa katika vifungu husika**

| Huduma iliyotolewa | Fedha iliyopangwa (Tshs) | Fedha iliyotumika (Tshs) | Tofauti (Tshs) |
|---|---|---|---|
| Suplies and consumables Goods | 285,200,000 | 568,450,842.66 | 283,250,842.66 |
| Routine, Maintenance and Repair | 41,500,000 | 91,852,150 | 50,352,150 |
| Other Payment | 12,600,000 | 125,756,639.76 | 113,156,639.76 |
| **Jumla** | | | **446,759,632.42** |

### 5.1.7.11 MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI ZANZIBAR (ZAECA)

Ukaguzi wa Hesabu za Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar mwaka wa fedha 2022/2023 kwa umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

### 5.1.7.12 Ucheleweshwaji wa kupelekwa fedha kwenda Mfuko Mkuu wa Hazina shilingi 512,198,804.97

Kwa mujibu wa kifungu nambari 30(3) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa Afisa Masuuli atachukua hatua zinazofaa kuhakikisha kwamba mapato yote yanayapokelewa yanawekwa vizuri au yanawekwa katika hesabu ya benki ya Mfuko Mkuu wa Hazina mara tu baada ya kukusanywa.

Ukaguzi umepitia taarifa za fedha za mwisho wa mwaka za Mamlaka pamoja na taarifa za kibenki za hesabu za Mamlaka zenye namba 0724961001 na 0724961002 zilioko Benki ya Watu wa Zanzibar zenye jina la ZAECA Revenue na kubaini kuwepo kwa ucheleweshwaji wa kupeleka fedha zilizopatikana na Mamlaka kwenda katika Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali baada ya kesi husika kufanyiwa maamuzi ambapo uhaulishaji wa fedha hizo zilivuka mwaka wa fedha.

Kuwepo kwa ucheleweshaji wa kupelekwa fedha zilizokusanywa na Mamlaka kwenda Mfuko Mkuu wa Hazina ni kwenda kinyume na Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016.

Ukaguzi unaushuri uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar kuhakikisha kuwa unasimamia uwasilishaji wa fedha zote zinazokusanywa katika Mfumko Mkuu wa Hazina kwa wakati na kwa mujibu wa Sheria ili kuepuka kujitokeza kwa viashiria vya ubadhirifu wa fedha za Umma. Mchanganuo wa fedha zilizocheleshwa kuwasilishwa Hazina ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 69: Malipo ya fedha kwenda Mfuko Mkuu wa Hazina

| Maelezo | Tarehe ya Kupelekwa Hazina | Muda wa ucheleshwaji (Miezi) | Kiasi (Tsh) |
|---|---|---|---|
| Fedha zilizopatikana katika mwaka 2021/2022 | 31/12/2023 | 18 | 315,679,589.64 |
| Fedha zilizopatikana katika mwaka 2022/2023 | 03/11/2023 | 4 | 196,519,215.33 |
| **Jumla Kuu** | | | **512,198,804.97** |

*Chanzo: Taarifa za fedha za Kibenki za Mamlaka, 2022/2023*

### 5.1.7.13 Kukosekana kwa udhibiti na Utunzaji wa gari

Ukaguzi umebaini kuwepo kwa magari ambayo yameshaanza kuharibika na mengine ambayo yameshachakaa hali iliyosababishwa na utunzaji wa magari hayo usioridhisha.

Aidha, ukaguzi umebaini gari hizo zimehifadhiwa katika eneo la wazi ambalo halikuwekwa maalumu kwa ajili ya kuhifadhi gari hizi dhidi ya mabadiliko ya hali ya hewa, hali iliyopelekea gari hizo kuchakaa na kuharibika.

Kuwepo kwa uhifadhi usio mzuri wa gari kunaweza kupelekea kuisababishia Serikali hasara ikiwa gari hizo zilipatikana zikiwa katika hali nzuri na ikitokea kesi itashinda basi zitashindwa kurejeshwa kwa wahusika hivyo Serikali inaweza kubeba gharama za matengenezo ya gari hizo.

Ukaguzi unaushuri uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar kuzingatia matakwa ya Sheria katika kusimamia mali zinazopatikana na Mamlaka katika utekelezaji wa majukumu yake pamoja na kuzingatia uhifadhi bora wa mali hizo dhidi ya uharibifu unaoweza kujitokeza.

### 5.1.7.14 Kushindwa kuthibitisha uwepo wa ongezeko la mali za ghalani zilizoainishwa katika Taarifa za Fedha za Mwisho wa Mwaka

Muongozo nambari 2 (2022/2023) wa kufunga hesabu za mwaka wa fedha 2022/2023 sehemu ya 7(c) ya Ufafanuzi wa Taarifa za Fedha (Disclosures) inaeleza kwamba Taasisi zitalazimika "kufanya Stock taking ya mali za mpito (Current Asset), na kuziainisha mali hizo zilizopo hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 kwa kuainisha bakaa ya "Inventories" na "Receivables".

Katika kipindi cha ukaguzi, ukaguzi uliomba ripoti ya "Stock Taking" kuweza kuvitambua vifaa vilioainishwa ili kuweza kujiridhisha juu ya thamani ya vifaa ilioanishwa katika Taarifa za fedha za mwisho wa mwaka 2022/2023 ambapo Mamlaka waliainisha bakaa la mali za ghalani (Inventory) la jumla ya shilingi 8,408,120. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi iliainisha bakaa ya mali za ghalani (Inventories) yenye thamani ya shilingi 6,962,580 na kupelekea uwepo wa ongezeko la mali zenye thamani ya shilingi 1,445,540 kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa taarifa za kuhesabu mali za ghalani zilizopelekea uwepo wa ongezeko la mali zilizonunuliwa ambazo hazikubainishwa katika daftari la mali za ghalani pamoja na kukosekana kwa ripoti ya uhakiki wa mali za ghalani.

Pamoja na uwepo wa dosari hizo ukaguzi umeshindwa kuthibitisha uhalali wa taarifa iliyowasilishwa katika ufungaji wa hesabu kwa mwaka wa fedha 2022/2023 jambo ambalo limepelekea kushindwa kutoa maoni sahihi ya ufungaji wa hesabu uliyowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi kuhakikisha unatekeleza miongozo ya Ufungaji wa Hesabu ili taarifa za hesabu ya mwisho wa mwaka ziweze kuonyesha sura sahihi na halisi pamoja na kuweza kufahamu idadi ya mali zilizopo, gharama za mali hizo, mahala zilipo, pamoja na hali ya uchakavu ili kuweza kutoa taarifa za kuziondosha katika vitabu vya hesabu Mali zilizopitwa na muda wa matumizi.

#### 5.1.7.15 Manunuzi yaliyofanywa nje ya Mfumo wa Manunuzi (e-Proz) shilingi 84,530,901

Kupitia barua ya tarehe 12/8/2022 yenye kumbukumbu nambari MUUMU.BA.156/370/01/27 Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar ilitoa agizo kwa Makatibu Wakuu, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Idara Maalumu, Wakuu wa Mashirika, Mamlaka na Taasisi Zinazojitegemea Zanzibar kuwa kuanzia tarehe 15/8/2022 Manunuzi yote ya Serikali yatapaswa kufanyika kupitia mfumo wa ununuzi mtandao (e-Proz).

Katika kupitia hati za malipo yaliofanywa na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar, ukaguzi ulibaini kwamba manunuzi ya jumla ya shilingi 84,530,901 yalifanywa na ZAECA bila ya kuzingatia utumiaji wa mfumo wa ununuzi mtandao kama ambavyo imeelekezwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma Zanzibar.

Ufanyaji wa manunuzi nje ya mfumo wa manunuzi kunaweza kupelekea Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kushindwa kujiridhisha juu ya ufanisi wa watoa huduma waliotumiwa na ZAECA na hatimae kupelekea ZAECA kupata huduma kutoka kwa wasambazaji wasiokuwa na sifa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar kuhakikisha kuwa manunuzi yote yanafanyika kwa kuzingatia utumiaji wa mfumo wa Manunuzi (e-Proz). Mchanganuo wa manunuzi yaliyofanyika nje ya mfumo wa mununuzi ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 70: Manunuzi yaliofanyika nje ya Mfumo wa Manunuzi**

| Hati Namba | Alielipwa | Kiasi (Tsh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 06/10 ya 06/10/2022 | Director General | 200,000 | Ununuzi wa Viburudishaji |
| 05/12 ya 2/12/2022 | Kamishna Vyuo vya Mafunzo | 15,000,000 | Malipo ya ukarabati wa ofisi |
| 47/01 ya 18/01/2023 | Rashid Mohamed Soud | 1,841,600 | Malipo kwa ajili ya kukodi magari |
| 68/01 ya 27/01/ 2023 | Director General | 2,000,000 | Malipo kwa ajili ya Mafunzo mbali mbali |
| 80/01 ya 31/01/ 2023 | | 494,600 | |
| 81/01 ya 31/01/2023 | | 395,000 | |
| 17/02 ya 21/02/2023 | | 90,000 | Ununuzi wa vifaa vya kompyuta |
| 08/03 ya 06/03/2023 | Ali Suleiman Foodstuff Enterprises | 288,120 | Ununuzi wa Mabuli |

| Hati Namba | Alielipwa | Kiasi (Tsh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 17/03 ya 10/03/2023 | Mustafa Hassan Issa | 442,000 | Ununuzi wa chakula na viburudishaji |
| 20/04 ya 12/04/2023 | Director General | 4,530,000 | |
| 35/06 ya 16/06/2023 | 4 Peoples General Supplier | 10,565,821 | Malipo kwa ajili ya matumizi mbalimbali kwa mafunzo ya BIC |
| 36/06 ya 16/06/2023 | 3R and 2N supplier | 25,000,000 | |
| 39/06 ya 20/06/2023 | Zanzibar Quality Tailoring Ltd | 5,703,600 | |
| 50/06 ya 20/06/2023 | 3R and 2N supplier | 17,230,160 | |
| 93/06 ya 22/06/2023 | Adam S. Suleiman | 750,000 | |
| **Jumla** | | **84,530,901** | |

### 5.1.7.16 Malipo yaliyolipwa kinyume na utaratibu shilingi 34,191,000

Kanuni nambari 58(1) ya Kanuni ya Usimamizi wa fedha za Umma ya 2021 inaeleza kuwa "Malipo yote kwa Taasisi za kibajeti, Mamlaka za Serikali za mitaa lazima yafanyike kwa njia ya Kibenki". Aidha, kifungu nambari 40 cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa manunuzi yote yanatakiwa kufanyika kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa kisheria.

Ukaguzi ulipitia taarifa za fedha, hati za malipo na vielelezo vilivyofanyiwa malipo na kubaini uwepo wa dosari mbalimbali zitokanazo na kufanyika kwa malipo yenye thamani ya shilingi 34,191,000 kinyume na utaratibu. Miongoni mwa dosari hizo ni kama zifuatazo:-

- Kufanyika kwa malipo katika hesabu ya mtumishi anaetambulika kwa jina la **Kudura Ramadhan Hassan** ambapo ukaguzi ulibaini Mamlaka humlipa mtumishi huyo kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa mafunzo na programu mbalimbali, vile vile mtumishi huyo hutoa fedha kwenye akaunti yake aliyoingiziwa na kumlipa mtu mmoja moja kwa njia ya fedha taslim jambo ambalo ni kwenda kinyume na utaratibu wa malipo ya fedha za Serikali.
- Kufanyika kwa malipo ya fedha taslim jambo ambalo hupelekea kuikosesha Serikali mapato yanayotokana na kodi juu ya huduma inayotolewa.
- Kufanyika kwa malipo nje ya mfumo wa manunuzi na kupelekea kuikosesha Serikali mapato ya kodi ya watoa huduma wanayotakiwa kukatwa.
- Kukosekana kwa kumbukumbu sahihi za taarifa ya matumizi na vielelezo halali vilivyofanyiwa matumizi jambo ambalo linapelekekea kushindwa kuthibitisha uhalali wa malipo yaliyofanyika.
- Kukosekana kwa uhalali wa vielelezo vinavyowasilishwa ambavyo haviendani na thamani halisi ya fedha aliyoingiziwa kwenye akaunti yake.

Kutokufuatwa kwa kanuni na miongozo ya usimamizi wa fedha kunaweza kupelekea upotevu wa fedha za umma unaotokana na kuingiziwa mtumishi fedha ya Serikali kwenye akaunti yake binafsi kutekeleza malengo ya Serikali kinyume na utaratibu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar kuhakikisha shughuli zote zilizopangwa zinasimamiwa na kutekelezwa kwa mujibu wa utaratibu ili kuweza kuhalalisha malipo yanayofanyika. Malipo hayo ni kama yanavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 71: Malipo yaliyolipwa kinyume na utaratibu**

| Hati ya Malipo | Aliyelipwa | Kiasi (Tsh.) |
|---|---|---|
| E05PV220000029 ya 12/4/2023 | Kudura Ramadhan Hassan | 12,400,000 |
| E05PV220000030 ya 12/4/2023 | | 8,495,000 |
| E05PV220000038 ya 06/6/2023 | | 5,000,000 |
| E05PV2200000420 ya 16/6/2023 | | 2,696,000 |
| E05PV220000049 ya 23/6/2023 | | 5,600,000 |
| **Jumla** | | **34,191,000** |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati za Malipo, 2022/2023*

**MAMLAKA YA KUZUIA RUSHWA NA UHUJUMU UCHUMI PEMBA**

### 5.1.7.17 Kukosekana kwa mpango kazi na mpango wa ununuzi

Kifungu nambari 41(2)(c) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kuwa Taasisi zinazohusika na bajeti ya Serikali zitawasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali bajeti zao za mwaka na zitajumuisha; Mpango kazi na mpango wa ununuzi.

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Mkoa wa Kusini na Kaskazini Pemba haikutayarisha mpango kazi na mpango wa ununuzi wa mwaka wa fedha 2022/2023 hali ambayo inapelekea kushindwa kufanya tathmini ya utekelezaji wa shughuli zake za robo mwaka na mwaka na pia inaweza kupelekea ununuzi wa bidhaa zisizohitajika.

Kutokuandaliwa kwa mpango kazi na mpango wa ununuzi wa mwaka ni kwenda kinyume na kifungu nambari 41(2)(c) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka kutayarisha mpango kazi na mpango wa ununuzi kama sheria inavyoelekeza ili kuepuka manunuzi holela na yasiyo na tija na Serikali.

### 5.1.7.18 Kutokuwepo kwa hesabu ya matumizi ya kawaida

Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Mkoa Kaskazini Pemba inawajibu wa kuendesha na kusimamia shughuli za Mamlaka kwa mujibu wa sheria, kanuni na miongozo mbalimbali ya kifedha.

Ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka haina hesabu ya matumizi ya kawaida kwa ajili ya kuendesha shughuli zao za kila siku, hali ambayo inapelekea matumizi yote ya Afisi za Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Mkoa wa Kusini na Kaskazini Pemba kufanyika Makao Makuu ya Mamlaka ilioko Unguja. Hali hii inapunguza ufanisi wa kiutendaji wa Mamlaka.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka kushirikiana na Afisi ya Rais Fedha na Mipango Pemba kuhakikisha wanafungua hesabu ya matumizi ya kawaida (Recurrent Account) katika Afisi za Mamlaka za Mikoa. Kukosekana kwa hesabu ya kawaida katika Afisi ya Mamlaka ni kwenda kinyume na Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016.

### 5.1.7.19 Watumishi kutokufanyiwa tathmini ya utendaji kazi

Kwa mujibu wa kanuni nambari 93(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya 2014 inaeleza kwamba Kila taasisi ya umma italazimika kumfanyia tathmini ya utendaji wa kazi mtumishi wake kila mwaka.

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Mkoa wa Kusini Pemba haikuwafanyia watendaji wake tathmini ya utendaji kazi. Hali ambayo inaweza kupelekea watumishi kukosa stahili zao muhimu ikiwemo nyongeza ya mwaka au kupandishwa cheo.

Kutokufanyiwa tathmini ya utendaji kazi watumishi ni kwenda kinyume na Kanuni ya Utumishi wa Umma niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Kusini Pemba kuwafanyia watendaji wake tathmini ya utendaji kazi ya mwaka ili waweze kupata nyongeza ya mwaka ya mshahara.

### 5.1.8 MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI

Ukaguzi wa hesabu za Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.1.8.1 Kukosekana kwa hatimiliki ya eneo la kiwanja linalomilikiwa na Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani.

Kifungu nambari 64(1) cha sheria nambari 6 ya Afisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba "Taasisi ya Umma itahifadhi nyaraka zinazothibitisha kuwa mali zote zinamilikiwa kisheria na Serikali".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani inamiliki eneo la kiwanja kilichopo Chuini Unguja ambacho hakina hatimiliki inayo thibitisha umiliki halali wa eneo hilo pamoja na mipaka yake.

Kukosekana kwa hatimiliki kwa maeneo ya Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kunaweza kupelekea uvamizi wa maeneo, migogoro ya ardhi pamoja na kushindwa kuthibitisha umiliki halali wa mali hayo na hatimaye kuitia hasara Serikali kwa kulipa fidia mara mbili.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kuongeza juhudi katika kutafuta hatimiliki ya maeneo yake ili kupata nguvu za kisheria na kulinda mali za Serikali kutokana na uvamizi.

#### 5.1.8.2 Dosari ya kutokuwasiliana kwa mifumo ya ZODLAP, ZTMS na mfumo mama wa Mamlaka (ZARSTA)

Lengo la Serikali ni kuzitaka taasisi zote kuhakikisha wanatekeleza shughuli zote za makusanyo ya mapato kwa njia ya mifumo na kuhama katika analogi kwa lengo la kurahisisha na kudhibiti upotevu wa mapato katika Serikali.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani inatumia mifumo tofauti kwa lengo la ukusanyaji na kudhibiti mapato, dosari iliyobainika ni kutoweza kuwasiliana kwa mifumo hiyo, Makosa yanayotokana na vyombo vya moto yanayohusishwa na faini ya papo kwa papo kupitia mfumo wa **ZTMS** ambapo "control number" hutolewa kwa ajili ya malipo na pale ambapo "control number" inapomaliza muda bila ya kufanyiwa malipo, mfumo wa **ZARSTA** hutumika kutoa control number nyengine na kufanya malipo kwa mfumo wa **ZARSTA** hivyo mifumo hiyo hukinzana na kupelekea deni kubakia katika mfumo wa **ZTMS** na kusababisha mizozo baina ya askari na wamiliki wa vyombo.

Kutokuunganishwa kwa Mifumo ya ukusanyaji mapato na mfumo mama kunaweza kupelekea kutokupatikana kwa takwimu sahihi ya mapato yaliyokusanywa kwa mwaka husika, usumbufu kwa wamiliki wa vyombo vya usafiri barabarani ambapo pia hupelekea kuibuka kwa migogoro baina ya taasisi na wapewa huduma.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka kuhakikisha mifumo inayotumika katika ukusanyaji mapato inaunganishwa na mfumo mama ili kuondoa changamoto zinazojitokeza pamoja na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji na upatikanaji wa taarifa sahihi za mapato.

**MAMLAKA YA USAFIRI NA USALAMA BARABARANI PEMBA**

### 5.1.8.3 Malipo yaliyofanywa nje ya mfumo wa manunuzi shilingi 13,758,907

Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba MUUMU.BA.156/370/001/27 ya tarehe 12/08/2022 kutoka Mamlaka ya Ununuzi wa Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar kwenda kwa wakuu wa taasisi inaeleza kwamba kuanzia tarehe 15/08/2022 manunuzi yote ya Serikali yanatakiwa yafanywe kwa kutumia mfumo wa ununuzi wa kielektroniki (e-PROZ).

Ukaguzi umebaini kwamba Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani imetumia jumla ya shilingi 13,758,907 kwa ajili ya manunuzi mbalimbali pasipo kutumia mfumo wa kielektroniki wa manunuzi bila ya kuwepo sababu maalum ya kufanya hivyo. Kufanya manunuzi bila kutumia mfumo ni kwenda kinyume na maelekezo ya barua niliyoitaja hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka kuhakikisha manunuzi yote yanayofanyika yanapitia katika mfumo wa manunuzi. Mchanganuo wa manunuzi yaliyofanywa nje ya mfumo wa manunuzi ni kama ufuatao:-

**Jadweli Nambari 72: Manunuzi yaliyofanywa nje ya mfumo wa manunuzi**

| Hati Namba | Hundi Namba | Thamani (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 01/12 ya 20/12/2022 | TT | 353,907 | AMOS Industries Ltd | Malipo ya ununuzi wa maji |
| 03/09 ya 28/09/2022 | 000021 | 1,495,000 | Ole Filling Station | Malipo ya ununuzi wa mafuta ya dizeli kwa matumizi ya Afisi ya Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Pemba. |
| 01/10 ya 13/10/2022 | 000022 | 1,495,000 | | |
| 02/11 ya 22/11/2022 | 000023 | 1,495,000 | | |
| 03/01 ya 17/01/2023 | TT | 1,495,000 | | |
| 02/02 ya 21/02/2023 | | 1,495,000 | | |
| 03/01 ya 17/01/2023 | | 1,495,000 | | |
| 02/02 ya 21/02/2023 | | 1,495,000 | | |
| 02/03 ya 29/03/2023 | | 1,490,000 | | |
| 03/05 ya 19/05/2023 | | 1,450,000 | | |
| **Jumla** | | **13,758,907** | | |

### 5.1.8.4 Uwepo wa Upungufu wa Watumishi

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Pemba ina upungufu wa watumishi muhimu ambao wangaliwezesha Mamlaka kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Upungufu huu unaathiri utendaji wa jumla wa Mamlaka ikiwa ni pamoja na utoaji duni wa huduma, mrundikano wa majukumu, na kupunguza hamasa ya utendaji kazi kwa watumishi waliopo.

Kwa sasa barua zinazoingia zinapokelewa na Msaidizi Afisa Utumishi na utunzaji wa kumbukumbu za ghalani unafanywa na Afisa Msaidizi Usafirishaji. Hali hii inaweza kupelekea ucheleweshwaji wa utoaji huduma kwa taasisi za umma na jamii kwa ujumla na pia inaweza kupelekea kuikosesha mapato Serikali.

Kutokupewa nafasi za uajiri kwa mujibu wa nafasi zilizowazi ni kwenda kinyume na kanuni nambari 6(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kulipa kipaombele suala la uajiri ili kupunguza changamoto za kiutendaji zinazoikabili taasisi husika. Mchanganuo wa upungufu wa watumishi ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 73: Upungufu wa Watumishi**

| Namba | Kada | Waliopo | Mahitaji | Upungufu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Afisa manunuzi | 0 | 1 | 1 |
| 2. | Afisa Takwimu | 0 | 1 | 1 |
| 3. | Mhandisi wa Komputa | 0 | 1 | 1 |
| 4. | IT | 0 | 1 | 1 |
| 5. | Mtunza ghala | 0 | 1 | 1 |
| 6. | Mwangalizi wa ofisi | 0 | 1 | 1 |
| 7. | Afisa mapokezi | 0 | 1 | 1 |
| 8. | Katibu muhtasi | 0 | 1 | 1 |
| 9. | Karani masjala | 0 | 1 | 1 |
| 10. | Walinzi | 0 | 2 | 2 |
| 11. | Afisa Ukaguzi wa magari | 0 | 2 | 2 |
| 12. | Afisa upasishaji madereva | 0 | 2 | 2 |
| 13. | Afisa usalama barabarani | 0 | 4 | 4 |
| 14. | Afisa upasishaji mitihani | 0 | 1 | 1 |
| **Jumla** | | **0** | **20** | **20** |

*Chanzo: Mpango wa rasilimali watu.*

### 5.1.9 MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA

Ukaguzi wa hesabu za Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 5.1.9.1 Mapato yaliyokusanywa nje ya mfumo shilingi 70,989,688

Kwa mujibu wa Muongozo nambari 2 (2022/23) – wa kufunga hesabu za mwaka wa fedha 2022/23 sehemu ya 6 Mapato ya kodi (Tax Revenue) na yasio ya kodi (Non Tax Revenue) inataka mapato yote yanayokusanywa na Taasisi kutokana na vyanzo mbalimbali Maafisa Masuuli wahakikishe taarifa za makusanyo ya Mapato ya Kodi (Tax Revenue) na yasio ya kodi (Non Tax Revenue) ziwe zimeingizwa katika mfumo wa ukusanyaji wa mapato wa IFMIS pamoja na kufanyiwa Usuluhishi (Reconciliation) kwa fedha zilizohamishiwa katika Hesabu ya Mfuko Mkuu wa Serikali na taarifa za IFMIS pamoja na kuhakikisha fedha zote zimehamishwa ndani ya mfumo kutoka katika Vote kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali.

Katika kufanya mapitio ya hesabu za benki za Mamlaka, hesabu nambari 406448000 yenye jina Uendeshaji wa Miradi ya Kidimni na hesabu nambari 0827932001 yenye jina Mamlaka ya Kudhibiti Dawa za Kulevya Zanzibar, ukaguzi ulibaini kwamba Mamlaka ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi 70,989,688 kupitia vyanzo vyake mbalimbali vya mapato bila ya kuzingatia utumiaji wa mfumo wa ukusanyaji wa mapato wa IFMIS.

Ukusanyaji wa mapato nje ya mfumo unaweza kupelekea kukosekana kwa usahihi katika Taarifa za Fedha za Mwisho wa Mwaka zinazoandaliwa na Mamlaka na hatimae kupelekea kuathiri maamuzi ya watumiaji wa Taarifa hizo.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kuhakikisha makusanyo yote yanafanyika kupitia mfumo uliowekwa na Serikali. Aidha ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha unazisimamia na kuzifuatilia Taasisi zote zinazokusanya mapato nje ya mfumo ili kuweza kujua changamoto inayowakabili kwa lengo la kuchukuwa hatua za haraka za utatuzi wa changamoto hizo ikiwemo Taasisi hizo kuunganishwa na Mfumo Mkuu wa Serikali ili kuweza kupata taarifa kamili na sahihi za ukusanyaji wa mapato kwa mwaka. Mchanganuo wa mapato yaliyokusanywa nje ya mfumo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 74: Mapato yaliokusanywa nje ya Mfumo wa IFMIS**

| Chanzo | Nambari ya Hesabu | Kiasi (Tsh) |
|---|---|---|
| Miradi ya Mamlaka | 406448000 | 34,068,854 |
| | 0827932001 | 36,920,834 |
| | **Jumla** | **70,989,688** |

### 5.1.9.2 Kushindwa kuthibitisha uwepo wa mali za ghalani za jumla ya shilingi 52,059,922.59 zilizoainishwa katika Taarifa za Fedha za Mwisho wa Mwaka

Muongozo nambari 2 (2022/23) – wa kufunga hesabu za mwaka wa fedha 2022/23 sehemu ya 7(c) ya Ufafanuzi wa Taarifa za Fedha (Disclosures) inaeleza kwamba Taasisi zitalazimika "kufanya Stock taking ya mali za mpito (Current Asset), na kuziainisha mali hizo zilizopo hadi kufikia 30 Juni 2023 kwa kuainisha bakaa ya Inventories na Receivables".

Katika kipindi cha ukaguzi, ukaguzi uliomba ripoti ya stock taking kuweza kuvitambua vifaa vilioainishwa ili kuweza kujiridhisha juu ya thamani ya vifaa ilioanishwa katika Taarifa za fedha za mwisho wa mwaka 2022/2023 ambapo Mamlaka waliainisha bakaa la mali za ghalani (Inventory) la jumla ya shilingi 52,059,922.59. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya iliainisha bakaa ya mali za ghalani (Inventories) yenye thamani ya shilingi 87,049,814.70 ambapo imebainika ni pungufu kwa thamani ya shilingi 34,989,892 kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kukosekana kwa taarifa za uondoshwaji wa mali zenye thamani ya shilingi 34,989,892 pamoja na kukosekana kwa ripoti ya hesabu za mali zenye thamani ya shilingi 52,059,922.59 iliyoripotiwa katika hesabu ya mwisho wa mwaka wa fedha 2022/2023.

Pamoja na uwepo wa dosari hizo ukaguzi umeshindwa kuthibitisha uhalali wa taarifa iliyowasilishwa katika ufungaji wa hesabu kwa mwaka wa fedha 2022/2023 jambo ambalo limepelekea kushindwa kutoa maoni sahihi ya ufungaji wa hesabu iliyowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

Kushindwa kutambua thamani ya shilingi 34,989,892 ya mali zilizoondoshwa kwenye vitabu vya hesabu kwa mwaka wa fedha 2021/2022 pamoja na thamani halisi ya fedha ya shilingi 52,059,922.59 iliyobainishwa katika vitabu vya hesabu kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umetia shaka juu ya usahihi wa taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka zilizowasilishwa na Mamlaka kuonyesha sura sahihi na halisi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kuhakikisha unatekeleza miongozo ya Ufungaji wa Hesabu ili taarifa ya hesabu ya mwisho wa mwaka ziweze kuonyesha sura sahihi na halisi pamoja na kuweza kufahamu idadi ya mali zilizopo, gharama za mali hizo, mahala zilipo, pamoja na hali ya uchakavu ili kuweza kutoa taarifa za kuziondosha katika vitabu vya hesabu Mali zilizopitwa na muda wa matumizi.

### 5.1.9.3 Kukosekana kwa Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi (Risk Management Framework)

Kwa mujibu wa kanuni nambari 154, 155 na 156 za Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021, Afisa Masuuli wa Taasisi ya Umma anapaswa kutengeneza, kutekeleza na kuimarisha Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi (Risk Management Framework). Aidha, Afisa Masuuli anapaswa kuhakikisha kuwa ripoti za usimamizi wa vihatarishi (risk management reports) zinawasilishwa katika kamati ya ukaguzi angalau mara nne (4) kwa mwaka.

Ukaguzi umebaini kuwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya bado haina Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi (Risk management Framework) sambamba na kukosa kuwasilishwa ripoti za usimamizi wa vihatarishi katika kamati ya ukaguzi. Hali hii inaweza kupelekea Mamlaka kushindwa kutambua na kuingiza katika mikakati na mipango ya Taasisi vihatarishi vilivyopo na vinavyoweza kuwepo katika utendaji kazi wa Taasisi hiyo ikiwemo vihatarishi vya kisheria (legal risks), vihatarishi vya uhalifu mitandaoni (cyber security risks), na vihatarishi vya mazingira ya utendaji kazi (operational risks).

Kutokuanzisha, kutekeleza na kuimarisha Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi ni kwenda kinyume na kanuni nambari 154, 155 na 156 za Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kuhakikisha unaanzisha, unatekeleza na kuimarisha Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi (Risk Management Framework) kwa mujibu wa Kanuni kama zilivyonakiliwa hapo juu.

### 5.1.9.4 Kuchelewa kukamilika kwa mradi wa ujenzi

Katika ukaguzi wa 2022/2023 Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar kupitia Miradi ya Maendeleo ilipanga kukamilisha jengo na huduma nyengine za jengo ambapo Mamlaka ilipanga bajeti ya shilingi 5,000,000,000 fedha yote hii ni kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Ukaguzi wa Mradi wa kukamilisha jengo umefanywa kwa lengo la kuangalia hali halisi ya utekelezaji wa mradi pamoja na tija inayopatikana kutokana na mradi huo. Aidha, ukaguzi umekagua taratibu mbali mbali zinazohusiana na utekelezaji wa mradi ikiwa ni pamoja na kupima kiwango cha ufanisi kilichofikiwa kutokana hatua zilizochukuliwa kwa lengo lililokusudiwa katika utekelezaji wa mradi huo.

Kupitia Taarifa za Fedha za Mwisho wa Mwaka 2022/2023, ukaguzi ulibaini kwamba kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Mamlaka ilifanya malipo ya jumla ya shilingi 2,075,254,873 kwa ajili ya kuendeleza shughuli za mradi wa Ujenzi. Mnamo tarehe 2 Februari 2024 ukaguzi ulitembelea maeneo mbalimbali ya mradi na kubaini kuwa mkandarasi ameshindwa kukamilisha kazi kwa wakati kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba pamoja na makubaliano wa muda nyongeza, ambapo kwa mujibu wa barua ya tarehe 8 Machi 2023 kuhusiana na nyongeza ya mkataba wa Ujenzi yenye kumbukumbu nambari MKKDK/U.10/VOL.2/… kwenda kwa kampuni ya M/S AZHAR Construction Co. Ltd ujenzi ulitakiwa kukamilika tarehe 30 Novemba 2023 huku muda wa uangalizi ukiwa ni mwaka mmoja, aidha hadi ukaguzi unafanya kikao cha kufunga Ukaguzi tarehe 05/2/2024 shughuli za Ujenzi zilikua bado zinaendelea ikiwemo ukarabati wa maeneo mbalimbali kama upakaji rangi jengo la Mnara wa mbao na kushindwa kufunga milango pamoja na CCTV Camera kwa jengo la Kidimni na shughuli za usafishaji wa eneo kwa Kidimni na Mnara Mbao.

Kushindwa kukamilisha kwa makubaliano ya utekelezaji wa miradi kwa wakati kunaweza kusababisha uwepo wa matumizi ya ziada ambayo sio ya msingi yanayoweza kusababishwa na kuongezeka kwa gharama za utekelezaji wa mradi huo kunakosababishwa na mfumko wa bei ya vifaa vya ufundi. Aidha, kunaweza kupelekea kushindwa kunufaika na kipindi cha uangalizi kilichowekwa (Defect Liability Period)

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar kufanya ufuatiliaji wa vipengele vyote vya mikataba ili kuweza kufikia viwango vya ubora wa kazi iliyokusudiwa, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba mradi unatekelezwa ndani ya muda uliopangwa kwa kuhakikisha bajeti iliyopo inatosha ndipo ifunge mkataba.

### 5.1.9.5 Dosari katika mradi wa Ujenzi Kidimni

Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 inataka manunuzi yote kufanyika kwa kuzingatia thamani halisi ya fedha (Value For Money).

Kupitia Taarifa za Fedha za Mwisho wa Mwaka Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya iliainishwa malipo ya jumla ya shilingi 3,141,798,476 kwa ajili ya maboresho na Ujenzi kwa kituo cha Kidimni ikiwa ni utekelezaji wa mkataba nambari SMZ/C0401/W/ICB/2021-2/21 uliosainiwa tarehe 16 Machi 2022 baina ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar na mkandarasi M/S AZHAR Construction Co. Ltd.

Kupitia ziara ya Ukaguzi kwenye maeneo ya mradi, ukaguzi ulibaini uwepo wa dosari mbalimbali katika utekelezaji wa mradi huo ikiwemo kuharibika kwa maeneo mbalimbali ya majengo yaliojengwa ikiwemo tiles za kingo za chini ya kuta kabla ya hata majengo hayo kuanza kutumika.

Kuwepo kwa dosari hizi katika miradi ya ujenzi kunaweza kupelekea kukosekana kwa uimara wa majengo pamoja na kushindwa kuzingatia thamani halisi ya fedha katika ujenzi uliojengwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar kuhakikisha unaboresha na kusimamia ipasavyo majengo yaliojengwa na kuhakikisha majengo yote yamejengwa kwa ubora unaotakiwa katika maeneo yote ya mradi kabla kukamilisha malipo kwa mkandarasi.

### 5.1.9.6 Uhifadhi usioridhisha wa vielelezo vya dawa za kulevya zilizokamatwa

Kifungu cha 50(e) cha Sheria nambari 8 ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar ya 2021 inaitaka Mamlaka kutunza vyema vifaa vilivyozuiliwa ili kuepuka uwezekano wa kupotea, kuibiwa, kusinyaa, kushuka kwa ubora au thamani yake.

Ukaguzi ulifanya ziara katika maeneo ya kuhifadhia dawa za kulevya yaliofanikiwa kukamatwa (Kidimni) na kubaini kwamba Mamlaka imeshindwa kuanzisha utaratibu mzuri wa uhifadhi wa dawa hizo hali inayoweza kupelekea upotevu wa madawa hayo (Kuibiwa) na hata kuhatarisha usalama wa wanaohusika katika uhifadhi wa dawa hizo.

Miongoni mwa dosari zilizobainika ni pamoja na;

- Kukosekana kwa 'CCTV Camera' katika jengo na chumba cha uhifadhi wa dawa za kulevya.
- Uhifadhi usioridhisha wa dawa za kulevya zilizokamatwa kutokana na kuchanganya dawa zinazotakiwa kuangamizwa pamoja na vielelezo vinavyohifadhiwa.
- Uwepo wa vifungashio vya kuhifadhia dawa za kulevya vilivyochanika hali inayopelekea dawa hizo kupotea.

Uwepo wa uhifadhi usioridhisha wa dawa za kulevya unaweza kuhatarisha usalama wa wahusika wanaosimamia uhifadhi wa dawa za kulevya lakini pia kunaweza kupelekea upotevu wa dawa za kulevya na kushindwa kubaini muhusika wa upotevu huo kutokana na kutokuepo kwa uhifadhi mzuri pamoja na CCTV camera.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar kuhakikisha wanaboresha njia za uhifadhi wa dawa za kulevya ili kuepusha kujitokeza kwa vitendo vya ukosefu wa maadili kwa baadhi ya watumishi kuweza kutumika kupoteza ushahidi au kufanya utoroshaji wa dawa hizo kwa maslahi binafsi.

### 5.1.9.7 Malimbikizo ya Madeni ya muda mrefu shilingi 55,421,635

Ukaguzi umepitia na kukagua nyaraka mbali mbali ikiwemo hesabu ya mwisho wa mwaka na kubaini kwamba jumla ya taasisi 2 za Serikali zinaidai Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar kiasi cha shilingi 55,421,635 kutokana na huduma mbali mali alizopatiwa na taasisi hizo.

Kutokana na uwepo wa deni hilo ukaguzi umefanya tathmini ya kina na kubaini kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Mamlaka ilikuwa ikidaiwa jumla ya shilingi 10,296,505 na Mfuko wa Maendeleo – JKU pamoja na Shirika la Bima la Zanzibar.

Aidha kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ukaguzi umebaini uwepo wa ongezeko la deni hilo na kufikia jumla ya shilingi 55,421,635 inalotokana na Mamlaka kuendelea kupatiwa huduma na taasisi hizo bila ya kuonyesha juhudi za kupunguza ukuaji wa deni hilo ambalo limeongezeka kwa wastani wa asilimia 438.26

Kuendelea kuongezeka kwa deni hilo kunaweza kupelekea kusuasua kwa utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka hivyo kuzotesha utekelezaji wa mpango waliojipangia na hatimae kutokufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar kuweka mikakati maalum na kuchukuwa hatua madhubuti katika kusimamia ulipaji wa madeni ili kufikia malengo yaliowekwa na kuongeza ufanisi kwa Mamlaka na Serikali kwa ujumla.

### 5.1.9.8 Dosari zilizobainika katika utekelezaji wa Sheria

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya inaendelea na utekelezaji wa majukumu yake kama yalivyotajwa katika Sheria nambari 8 ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya 2021, katika vifungu mbalimbali ambapo katika utekelezaji wa kazi hizo ukaguzi umebaini uwepo wa kesi mbalimbali zilizoripotiwa, kuwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka pamoja na kuchukuliwa hatua za Mahkama kama ifuatavyo:-

- Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya kesi 498 ziliripotiwa ambapo kesi 354 majalada yake yamefikishwa Mahkamani na kesi 72 bado zinaendelea na hatua za upelelezi, kesi 41 vielelezo vyake havikutambulika kuwa ni dawa za kulevya na kesi 31 zimefungwa na Mkurugenzi wa Mashtaka.
- Uwepo wa ongezeko la kesi zilizofikia 498 ukilinganisha na kesi zilizoripotiwa mwaka uliopita ambazo zilikuwa kesi 312. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 59.6 ya ongezeko la kesi zote.

Aidha, katika hatua za upelelezi wa Tuhuma mbalimbali zilizowakabili watuhumiwa wa dawa za kulevya ukaguzi umebaini uwepo wa tuhuma 103 ambazo ziliendelea kuchukuliwa hatua mbali mbali za ukusanyaji wa vielelezo, uchukuwaji wa maelezo ya mashahidi, pamoja na upitiaji wa taarifa zinazohusiana na tuhuma hizo ili kuweza kuwasilishwa Mahkamani kwa ajili ya kutolewa hukumu. Miongoni mwa tuhuma hizo ni kama zilivyobainshwa katika jadweli liliopo hapo chini:-

**Jadweli Nambari 75: Idadi ya Tuhuma katika hatua ya upelelezi hadi Oktoba, 2023**

| Aina ya Dawa | Jumla ya Kesi | Mamlaka | Mkurugenzi wa Mashtaka | Mkemia | Zilizofungwa na DPP |
|---|---|---|---|---|---|
| Heroin | 25 | 10 | 1 | 5 | 9 |
| Kokeni | 2 | - | - | 2 | |
| Bangi | 74 | 34 | 8 | 10 | 22 |
| Valium | 1 | 1 | - | - | |
| Mirungi | 1 | 1 | - | - | - |
| **Jumla** | **103** | **46** | **9** | **17** | **31** |

Pamoja na uwepo wa tuhuma 103 zinazoendelea katika hatua mbalimbali za uchunguzi ukaguzi umebaini hadi kufikia Oktoba, 2023 jumla ya majalada 286 ya kesi za dawa za kulevya yamefikishwa katika Mahkama mbalimbali za Unguja na Pemba. Mchanganuo wa majalada hayo ni kama unaonekana katika jadweli kama ifuatayo:-

**Jadweli Nambari 76: Idadi ya majalada ya kesi zilizofikishwa Mahkamani hadi Oktoba 2023**

| Mahkama Unguja | Idadi | Mahkama Pemba | Idadi |
|---|---|---|---|
| Mahkama Kuu Tunguu | 111 | Mahkama Kuu Chake Chake | 7 |
| Mahkama ya Mkoa-Vuga | 85 | Mahkama ya Mkoa Wete | 8 |
| Mahkama ya Mkoa-Mwera | 25 | Mahkama ya Mkoa Chake Chake | 18 |
| Mahkama ya Mkoa-Mahonda | 32 | -- | -- |
| **Jumla** | **253** | | **33** |

Katika ufuatiliaji wa mwenendo wa mashauri ya kesi Mahkamani ukaguzi umebaini jumla ya kesi 354 ziliripotiwa Mahkamani ambapo kati ya kesi hizo jumla ya kesi 206 ziliachiwa huru kutokana na sababu mbalimbali zilizopelekea watuhumiwa kutokuwa na kesi ya kujibu na hatimae Mahkama kuamuru watuhumiwa hao kuachiwa huru kwa mujibu wa taratibu za kimahakama. Aidha, jumla ya kesi 122 bado zinaendelea na hatua ya kujiridhisha kutokana na vielelezo vilivyowasilishwa Mahkamani pamoja na hatua za kuwasikiliza mashahidi. Vile vile jumla ya kesi 26 zilitolewa hukumu kwa watuhumiwa kuweza kutiwa hatiani ima kwa kulipa fidia, kutumikia kifungo au mambo yote mawili kwa pamoja.

Kutokana na idadi kubwa ya kesi zilizoachiwa huru ukaguzi umebaini pamoja na uwepo wa sababu nyenginezo suala la upatikanaji wa shahidi huru, utambuzi wa watuhumiwa, watuhumiwa kutokupewa haki, mashahidi kushindwa kufika mahkamani huwenda ikawa ni kichocheo pekee kilichopelekea kukosekana kwa nguvu ya kisheria na hatimae Mahkama kuamuru kuwaachia huru watuhumiwa.

Pamoja na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ikiwemo kufanya maboresho na mapitio mapya ya Sheria nambari 8 ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya 2021 ukaguzi unaushauri ni vyema suala la upatikanaji wa shahidi huru kutizamwa kwa upana wake kwani ni miongoni mwa sababu zinazopelekea idadi kubwa ya kesi kuachiwa huru hivyo ni vyema shahidi huru kutumika wakati wa upekuzi wa madawa ya kulevya kwa watuhumiwa. Mchanganuo wa mwenendo wa kesi hizo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 77: Hatua za kesi zilizofikishwa Mahkamani hadi Oktoba,2023**

| Aina ya dawa | Jumla ya kesi | Zilizoachwa huru | | Zinazoendelea Mahkamani | | Zilizopata hatia | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Unguja | Pemba | Unguja | Pemba | Unguja | Pemba |
| Heroine | 146 | 63 | 24 | 38 | 10 | 6 | 5 |
| Kokeni | 4 | 2 | - | 1 | - | 1 | - |
| Bangi | 201 | 105 | 10 | 57 | 15 | 5 | 9 |
| Mirungi | 1 | - | - | 1 | - | - | - |
| Valium | 2 | 1 | 1 | - | - | - | - |
| **Jumla** | **354** | **171** | **35** | **97** | **25** | **12** | **14** |
| | | **206** | | **122** | | **26** | |

**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA PEMBA**

### 5.1.9.9 Kukosekana kwa usafiri wa uhakika wa ufuatiliaji wa kazi za Mamlaka za utoaji taaluma kwa Wananchi

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Pemba inalojukumu la kutembelea katika skuli na shehia mbalimbali ili kutoa taaluma kwa wanafunzi, vijana na jamii kwa ujumla juu ya athari za dawa za kulevya na kufuatilia taarifa za utumiaji, uuzaji, usambazaji na usafirishaji wa dawa hizo.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Mamlaka inamiliki gari moja ambayo ni chakavu na inayoigharimu Mamlaka fedha nyingi kwa ajili ya matengenezo hali inayoweza kupelekea kuzorota kwa shughuli nyengine muhimu za Mamlaka. Kukosekana kwa usafiri wa uhakika kunaweza kusababisha kutokutolewa elimu kwa wakati kwa wanafunzi, vijana na jamii hali inayoweza kupelekea Mamlaka kushindwa kufikia lengo lililokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Pemba kuhakikisha wanatenga fedha za kutosha kwa lengo la kununua vyombo vya usafiri ili kuweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

### 5.1.9.10 Kukosekana kwa usiri katika utekelezaji wa Majukumu ya Mamlaka

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Afisi ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Pemba siyo tu kwamba imezungukwa na taasisi nyengine bali imo katika jengo moja na Afisi ya Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu pamoja na Afisi ya Tume ya Haki za Binadamu.

Hali hii inaweza kupelekea kukosekana kwa usiri katika utekelezaji wa majukumu yao ambapo kwa uhalisia wa kazi zake inahitaji kuwepo katika Afisi iliyojitenga na ofisi nyengine ili kuweza kufanya kazi zake ipaswavyo na kwa ufanisi mkubwa zaidi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kuhakikisha wanapeleka pendekezo maalum Serikalini la kupatiwa Afisi ya faragha ili kuweza kutekeleza majukumu yao kwa usiri mkubwa.

### 5.1.9.11 Kukosekana kwa vifaa vya kisasa vya ukaguzi wa dawa za kulevya

Kwa mujibu wa kanuni nambari 126 ya Kanuni ya utumishi wa umma ya mwaka 2014 inaeleza kwamba "Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi atalazimika kuhakikisha kuwa mtumishi anaefanya kazi katika mazingira yanayohitaji vifaa maalum vya kutendea kazi anapatiwa vifaa hivyo".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Pemba haina vifaa vya kisasa, mfumo mzuri na imara wa ukaguzi wa mizigo na abiria katika bandari na uwanja wa ndege Pemba ili kuweza kubaini dawa za kulevya zinazoingia au kutoka katika kisiwa cha Pemba. Hali hii inaweza kupelekea watu wasiowaadilifu kuingiza au kutoa dawa za kulevya katika kisiwa cha Pemba kwa urahisi. Ukaguzi unaishauri Serikali kupitia Mamlaka kuhakikisha inaipatia vitendea kazi vyenye ubora na vya kisasa ili kuweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

# SURA YA SITA







# 6.0 UKAGUZI WA WAKALA ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umebainisha taarifa ya michango ya vyanzo vya mapato vya Wakala wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, utendaji wa mwaka kwa kila chanzo cha mapato pamoja na kubainisha dosari za kiutendaji zilizojitokeza wakati wa kaguzi na kubainisha njia za utatuzi wa dosari hizo.

## 6.1 TAARIFA ZA WAKALA WA SERIKALI KWA MWAKA 2022/2023

Ukaguzi huu umefanywa kwa kuzingatia misingi ya ukaguzi ya kitaifa na kimataifa ambapo mambo mbali mbali yamebainishwa ambayo yanahitaji kushughulikiwa na Serikali, Baraza la Wawakilishi pamoja na Uongozi wa taasisi husika ili kuhakikisha ufanisi katika utendaji wa shughuli za taasisi hizo unaimarika. Matokeo na mapendekezo ya ukaguzi yameainishwa kupitia ripoti hii ya Wakala wa Serikali zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kama ifuatavyo:-

### 6.1.1 WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR (ZAGPA)

Ukaguzi wa hesabu za Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar (ZAGPA) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 6.1.1.1 Malipo yaliyofanywa kwa njia ya Fedha Taslimu shilingi 286,955,157

Kanuni ya 58(1) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaeleza kwamba malipo yote ya matumizi ya Taasisi za Kibajeti na Serikali za Mitaa lazima yafanywe kwa kutumia njia za kieletroniki.

Wakala wa Serikali wa Uchapaji imefanya malipo yenye thamani ya shilingi 286,955,157 kwa ajili ya ununuzi na upatikanaji wa huduma mbalimbali. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni Wakala kutokutumia mfumo wa kibenki na badala yake kufanya matumizi kwa njia ya mfumo wa fedha taslimu jambo ambalo huenda likapelekea uwepo wa viashiria vya matumizi mabaya ya fedha za umma au kujitokeza kwa udanganyifu unaotokana na ulipwaji wa malipo kwa watumishi wasiostahiki.

Kufanya matumizi kwa njia ya fedha taslimu ni kwenda kinyume na Kanuni ya Usimamizi ya Fedha za Umma ya 2021.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala kuhakikisha kwamba malipo yote yanafanyika kwa njia ya mfumo wa kibenki kwa lengo la kuhakikisha Serikali inapata mapato yatokanayo na kodi ya zuio kwa watoa huduma mbali mbali pamoja na uwezekano wa matumizi yasiyoridhisha ya fedha za umma. Mchanganuo wa malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha taslimu ni kama unavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 4.**

#### 6.1.1.2 Hati za malipo zenye vielelezo pungufu shilingi 440,490,855

Kanuni ya 57(1)(2)(b) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2021 inaeleza kuwa "Malipo yote lazima yaambatanishwe na hati ya malipo ambayo imekamilika vielelezo vyote kwa mujibu wa maelekezo ya Hazina na kuidhinishwa na Afisa Mhasibu".

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 440,490,855 zimetumika kwa matumizi mbalimbali ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji lakini baadhi ya vielelezo husika havikuambatanishwa katika hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo na mapokezi ya bidhaa zilizonunuliwa, aidha ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Hali hiyo imetokana na kutokuwepo kwa udhibiti wa ndani na uhifadhi wa vielelezo vya fedha na vielelezo vyengine vinavyohusiana na uendeshaji wa kazi za Wakala.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali wa Uchapaji kuhakikisha malipo yote yanayofanyika yanaambatishwa na vielelezo vya malipo husika kwa wakati ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo. Mchanganuo wa hati za malipo zenye vielelezo pungufu ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 78: Malipo kwa ajili ya shughuli mbali mbali yenye vielelezo pungufu**

| Hati Namba | Kiasi (Tsh.) | Aliyelipwa |
|---|---:|---|
| 2/7 ya 05 Julai 2022 | 450,000 | Wakala wa Serikali wa Uchapaji |
| 9/7 ya 06 Julai 2022 | 2,772,000 | Wakala wa Serikali wa Uchapaji |
| 14/7 ya 6 Julai 2022 | 6,664,000 | Quality Trader |
| 6/8 ya 9 Agosti 2022 | 1,530,000 | Wakala wa Serikali wa Uchapaji |
| 33/8 ya 33 Agosti 2022 | 5,000,000 | Jaman Printers Ltd |
| 36/8 ya 22 Agosti 2022 | 1,581,250 | Richland Trading |
| 38/8 ya 22 Agosti 2022 | 4,346,856 | BK Enterprises |
| 41/8 ya 22 Agosti 2022 | 115,000 | Wakala wa Serikali wa Uchapaji |
| 43/8 ya 22 Agosti 202 | 1,600,000 | Mohammed Suprise Supllies |
| 17/10 ya 5 Oktoba 2022 | 28,025,000 | Raprek & Technology |
| 19/10 ya 6 Oktoba 2022 | 31,144,330 | Tanzania Printing Services Ltd |
| 33/10 ya 5 Oktoba 2022 | 5,915,000 | Mohamed Enterprise & Suppliers |
| 36/10 ya 19 Oktoba 2022 | 4,346,856 | BK Enterprises |
| 2/11 ya 28 Oktoba 2022 | 4,241,144 | Transpaper (T) Ltd |
| 27/11 ya 10 Novemba 2022 | 15,000,000 | Double Two General Supply |
| 29/1 ya 13 Januari 2023 | 4,851,000 | Multicolor Printers |
| 4/2 ya 2 Februari 2023 | 2,336,627 | Ali Suleiman Food Stuff Enterprises |
| 24/2 ya 17 Februari 2023 | 588,000 | FA Stationary & Printing |
| 34/2 ya 21 Februari 2023 | 8,070,588 | Muha Copy and Stationary |
| 35/2 ya 21 Februari 2023 | 8,632,500 | JAMANA Printers Ltd |
| 36/2 ya 21 Februari 2023 | 4,416,000 | New Home Furniture |
| 15/3 ya 2 Machi 2023 | 12,348,000 | SBK Secretarial Services |
| 18/3 ya 3 Machi 2023 | 76,291,460 | Tanzania Printing Servies |
| 19/3 ya 3 Machi 2023 | 11,637,500 | Multi color Printers |
| 28/3 ya 8 Machi 2023 | 25,591,270 | TPS |
| 31/3 ya 8 Machi 2023 | 710,000 | Said Mtuma Faki |
| 35/3 ya 9 Machi 2023 | 270,000 | Mwalimu Pongwa Kwao |
| 41/3 ya 10 Machi 2023 | 11,721,568 | Muha Copy and Stationary |
| 50/3 ya 15 Machi 2023 | 30,499,300 | Maxon Paper Converter |
| 64/3 ya 28 Machi 2023 | 11,721,570 | Muha Copy and Stationary |
| 70/3 ya 29 Machi 2023 | 36,317,630 | Double Two General Supply |

| Hati Namba | Kiasi (Tsh.) | Aliyelipwa |
|---|---|---|
| 3/5 ya 27 Aprili 2023 | 12,322,060 | Muha Copy and Stationary |
| 4/5 ya 28 Aprili 2023 | 15,080,000 | Computer World(T) Limited |
| 16/5 ya 12 Mei 2023 | 4,083,200 | Maxons Paper Converters Ltd |
| 18/5 ya 4 Mei 2023 | 350,000 | Jamal Khamis Juma |
| 20/5 ya 4 Mei 2023 | 18,158,815 | Double Two General Supply |
| 47/5 ya 17 Mei 2023 | 12,180,000 | Maxons Paper Converters Ltd |
| 73/5 ya 30 Mei 2023 | 6,080,778 | Transfer (T) Ltd |
| 74/5 ya 30 Mei 2023 | 12,341,553 | Transfer (T) Ltd |
| 75/5 ya 30 Mei 2023 | 1,160,000.00 | Raptek Technology & Services |
| **Jumla Kuu** | **440,490,855** | |

### 6.1.1.3 Kutokufuatwa kwa taratibu za manunuzi shilingi 652,800,686.2

Kwa mujibu wa kanuni nambari 57(1) ya Kanuni ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya mwaka 2020 imeweka katazo kwa Taasisi ya Ununuzi ya Umma kutogawa manunuzi kwa lengo la kukwepa kutoa zabuni za ndani au za nje ya nchi.

Ukaguzi umebaini Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar umefanya manunuzi yenye thamani ya shilingi 652,800,686 kwa ajili ya ununuzi wa malighafi kutoka kwa wasambazaji mbalimbali. Dosari zifuatazo zimebainika katika ukaguzi:-

- Kutokutangazwa kwa zabuni ya wazi ili kumpata mtoa huduma mwenye uwezo na kwa bei nafuu.
- Kufanya matumizi kwa njia ya kugawa manunuzi (splitting Tender) jambo ambalo ni kinyume na kanuni nambari 57(1) ya Kanuni ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya mwaka 2020.

Kutokana na dosari zilizobainishwa hapo juu zinapelekea kufanya matumizi kusikozingatia nidhamu ya matumizi jambo ambalo huwenda ikapelekea kukosekana kwa ufanisi wa matumizi ya fedha yaliyofanyika na hatimae kuisababishia hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali wa Uchapaji kuhakikisha unazingatia matakwa ya Kanuni ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya mwaka 2020. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama yanavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 79: Manunuzi yaliofanywa kwa njia ya kuvunjwavunjwa**

| Hati Namba | Aliyelipwa | Thamani (Tsh.) |
|---|---|---|
| 3/7 ya 5 Julai 2022 | Wakala wa Serikali wa Uchapaji | 375,000 |
| 22/7 ya 11 Julai 2022 | Maxon Paper Converter | 42,480,000 |
| 24/7 ya 11 Julai 2022 | Pluto Trader | 34,966,020 |
| 29/7 ya 13 Julai 2022 | Maxon Paper Converter | 12,168,874 |
| 37/7 ya 20 Julai 2022 | BK Enterprises | 4,346,856 |
| 12/8 ya 9 Agosti 2022 | MAK Solutions Ltd | 14,160,000 |
| 22/8 ya 11 Agosti 2022 | Pluto Traders Ltd | 16,400,000 |
| 23/8 ya 12 Agosti 2022 | Computer World (T) Limited | 5,900,000 |

| Hati Namba | Aliyelipwa | Thamani (Tsh.) |
|---|---|---|
| 25/8 ya 12 Agosti 2022 | MAS General Supply | 955,800 |
| 38/8 ya 22 Agosti 2022 | BK Enterprises | 4,346,856 |
| 31/9 ya 22 Septemba 2022 | BK Enterprises | 4,346,856 |
| 36/10 ya 19 Oktoba 2022 | BK Enterprises | 4,346,856 |
| 2/11 ya 2 Oktoba 2022 | Transpaper (T) Ltd | 4,241,144 |
| 14/11 ya 2 Novemba 2022 | Double Two General Supply | 59,077,200 |
| 28/11 ya 9 Novemba 2022 | Double Two General Supply | 33,031,294 |
| 29/11ya 10 Novemba 2022 | Double Two General Supply | 38,165,600 |
| 51/11ya 22 Novemba 2022 | BK Enterprises | 4,346,856 |
| 36/12 ya 24 Disemba 2022 | Melisha Media Ltd | 5,635,000 |
| 40/1 ya18 Januari 2023 | BK Enterprises | 4,346,856 |
| 19/3 ya 3 Machi 2023 | Multi color Printers | 11,637,500 |
| 27/3 ya 8 Machi 2023 | JAMINA Enterprises | 43,859,600 |
| 28/3 ya 8 Machi 2023 | TPS | 25,591,270.20 |
| 41/3 ya 10 Machi 2023 | Muha Copy and Stationary | 11,721,568 |
| 43/3 ya 10 Machi 2023 | Suleiman M Suleiman | 370,000 |
| 50/3 ya 15 Machi 2023 | Maxon Paper Converter | 30,499,300 |
| 52/3 ya 16 Machi 2023 | BK Enterprises | 4,346,856 |
| 64/3 ya 28 Machi 2023 | Muha Copy and Stationary | 11,721,570 |
| 67/3 ya 21 Machi 2023 | Maxons Paper Converters Ltd | 32,120,400 |
| 6/4 ya 4 Aprili 2023 | MUHA COPY AND STATIONARY | 14,008,235 |
| 7/4 ya 4 Aprili 2023 | MAXON PAPER CONVERTER | 29,301,600 |
| 18/4 ya 13 Aprili 2023 | Muha Copy | 14,008,235 |
| 27/4 ya 17 Aprili 2023 | BK Enterprises | 4,346,856 |
| 31/4 ya 19 Aprili 2023 | Maxons Paper | 32,632,830 |
| 3/5 ya 27 Aprili 2023 | Muha copy and Stationary | 12,322,060 |
| 16/5 ya 12 Mei 2023 | Maxons Paper Converters Ltd | 4,083,200 |
| 20/5 ya 4 Mei 2023 | Double Two Converters Ltd | 18,158,815 |
| 46/5 ya 16 Mei 2023 | BK Enterprises | 4,346,856 |
| 47/5 ya 17 Mei 2023 | Maxons Paper Converters Ltd | 12,180,000 |
| 48/5 ya 17 Mei 2023 | Tecnopro Africa Limited | 19,137,680 |
| 73/5 ya 30 Mei 2023 | Transfer (T) Ltd | 6,080,778 |
| 74/5 ya 30 Mei 203 | Transfer (T) Ltd | 12,341,553 |
| 27/6 ya 20 Juni 2023 | BK Enterprises | 4,346,856 |
| **Jumla** | | **652,800,686.2** |

### 6.1.1.4 Uhaba wa rasilimali watu kulikopelekea malipo ya shilingi 11,490,000

Kifungu cha 7(1) cha sheria ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji kinaeleza kwamba katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria hii, Wakala utatoa huduma za Uchapaji na Bohari Kuu ya vifaa vya Afisi na kuandikia.

Katika kipindi cha Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ukaguzi ulifanya mapitio ya hati za malipo na kubaini jumla ya shilingi 11,490,000 ililipwa kutokana na Uhaba wa rasilimali watu ikiwa ni kwaajili ya kusaidia kazi za kiwandani.

Uhaba wa rasilimali watu kunapelekea kuongezeka kwa gharama za uendeshaji kwa Wakala aidha ajira za mikataba ya muda mfupi kwa ajili ya Kusaidia shughuli za kiwandani zinahatarisha usalama wa taarifa nyeti zinazowasilishwa kwa Wakala kwa ajili ya uchapaji kutokana na waajiriwa kuanza kazi kabla ya kupatiwa mafunzo ya kiusalama na mafunzo mengine muhimu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala kufanya jitihada za kufanya uajiri kwa nafasi zenye Uhaba ili kuweza kuongeza nguvu katika kufanikisha utoaji wa huduma bora ya Wakala, pia kuhakikisha waajiriwa wote wanaotumika katika eneo la kiwanda wanapatiwa mafunzo stahiki kabla ya kuanza kazi husika. Mchanganuo wa malipo yaliyofanyika ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 80: Hati za malipo kwa ajili ya ukodishaji wa gari na ufungaji wa Faiba**

| Hati Namba | Alielipwa | Kiasi (Tsh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 10/10 ya 06/10/2022 | Wakala wa Serikali wa Uchapaji | 840,000 | Malipo kwa ajili ya wafanyakazi wa mkataba |
| 13/10 ya 06/10/2022 | | 400,000 | |
| 22/11 ya 08/11/2022 | | 1,780,000 | |
| 32/1 ya 13/01/2023 | | 1,750,000 | |
| 22/3 ya 07/3/2023 | | 1,760,000 | |
| 60/3 ya 28/03/2023 | | 1,760,000 | |
| 30/4 ya 30/04/2013 | | 1,440,000 | |
| 70/5 ya 30/05/2023 | | 1,760,000 | |
| **Jumla** | | **11,490,000** | |

**WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI PEMBA**

### 6.1.1.5 Uwepo wa Upungufu wa Watumishi

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wakala wa Serikali wa Uchapaji Pemba ina upungufu wa watumishi muhimu ambao wangaliwezesha Wakala kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Upungufu huu unaathiri utendaji wa jumla wa Wakala ikiwa ni pamoja na utoaji duni wa huduma, mrundikano wa majukumu, na kupunguza hamasa ya utendaji kazi kwa watumishi waliopo.

Hali hii inaweza kupelekea ucheleweshwaji wa utoaji huduma kwa taasisi za umma na jamii kwa ujumla na pia inaweza kupelekea kuikosesha mapato Serikali.

Kutokupewa nafasi za uajiri kwa mujibu wa nafasi zilizowazi ni kwenda kinyume na kanuni nambari 6(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kulipa kipaombele suala la uajiri ili kupunguza changamoto za kiutendaji zinazoikabili taasisi husika.Mchanganuo wa upungufu wa watumishi ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 81:Upungufu wa Watumishi**

| Namba | Kada | Waliopo | Wanaohitajika | Upungufu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Afisa Utumishi | 0 | 1 | 1 |
| 2. | Afisa Muhasibu | 0 | 1 | 1 |
| 3. | Afisa IT | 0 | 1 | 1 |
| 4. | Mshika Fedha | 0 | 1 | 1 |
| 5. | Walinzi | 2 | 4 | 2 |
| 6. | Afisa Manunuzi | 0 | 1 | 1 |
| **Jumla** | | **2** | **9** | **7** |

*Chanzo: Mpango wa rasilimali watu*

### 6.1.1.6 Ufinyu wa nafasi katika ghala ya kuhifadhia vifaa Gombani

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Afisi ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji Pemba inatoa huduma ya kuuza na kuhifadhi vifaa vya kuandikia katika ghala lililopo Gombani ambalo halina nafasi ya kutosha kulingana na mzigo wa vifaa unaowekwa katika ghala hiyo hali ambayo inaweza kusababisha kuharibika kwa vifaa hivyo kutokana na mrundikano.

Uwekwaji wa vifaa katika sehemu isiyoridhisha ni kwenda kinyume na Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala kutafuta eneo litakalokidhi mahitaji kwa ajili ya kuhifadhi vifaa ili kuepukana na uwezekano wa kujitokeza kwa uharibifu wa vifaa vinavyonunuliwa kwa ajili ya utoaji wa huduma kwa wananchi.

### 6.1.1.7 Kutokufikiwa kwa malengo ya mauzo katika Duka la Wakala

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wakala wa Serikali wa Uchapaji Pemba ilikadiriwa kukusanya shilingi 17,526,366.66 zinazotokana na mauzo ya vifaa vya kuandikia na machapisho kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 Wakala ilifanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi 12,568,775 ambacho ni sawa na asilimia 71.71 ya makadirio. Hali hii inapelekea Wakala kushindwa kufikia malengo yake iliyojiwekea.

Kutokufikia malengo ya mauzo yaliyowekwa ni kwenda kinyume na kifungu nambari 30(2) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 pamoja na Sheria nambari 12 ya Uanzishwaji wa Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar ya 2018.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Serikali wa Uchapaji Pemba kuhakikisha wanajitangaza zaidi kwa lengo la kupata wateja wa kutosha na kufikia malengo iliyojiwekea.

### 6.1.1.8 Ukosefu wa Vyombo vya Usafiri

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wakala wa Serikali wa Uchapaji Pemba haina gari kwa ajili ya kubeba na kusambaza mizigo ya Afisi inayoletwa kutoka makao makuu ya Wakala Unguja hali ambayo inailazimu Afisi ya Wakala kukodi au kuazima gari kwa ajili ya kubeba mizigo hiyo kutoka bandarini hadi katika ghala la Afisi lililopo Gombani na kutoka ghalani Gombani kwenda katika duka la Wakala lililopo Chake Chake hali ambayo inapelekea kupungua kwa ufanisi katika utendaji wa kazi wa Wakala. Kukosekana kwa vyombo vya usafiri kunaweza kupelekea uwezekano wa kuongezeka kwa gharama za uendeshaji na upotevu wa vifaa hivyo.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 41(1)(a) cha Sheria nambari 2 ya Utumishi wa Umma ya 2011.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala kutenga fedha za kutosha katika bajeti zao za mwaka kwa ajili ya ununuzi wa gari.

### 6.1.1.9 Kutokuingizwa kwa vifaa katika Duka la Wakala wa Uchapaji kutoka Unguja

Ukaguzi umebaini kwamba hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 Wakala wa Serikali wa Uchapaji Pemba hawakupokea bidhaa yoyote kutoka Afisi Kuu Unguja kwa ajili ya mauzo kwa upande wa bohari. Hali hii inaweza kupelekea Wakala kupunguza imani kwa Taasisi za Umma na watu binafsi kutokana na kutopatikana kwa vifaa katika duka la Wakala.

Kutokuingizwa kwa bidhaa katika duka la Wakala ni kwenda kinyume na Sheria nambari 12 ya mwaka 2018 ya uanzishwaji wa Wakala wa Serikali wa Uchapaji ambayo inaitaka Wakala kufanya uuzaji wa bidhaa na vifaa vya kuandikia kwa taasisi binafsi na za Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala kuhakikisha wanafanya jitihada za makusudi kuhakikisha wanaleta mzigo wa kutosha ili kuweza kufanya biashara inavyotakiwa.

#### 6.1.1.10 Kutokutekelezeka kwa Bajeti ya Matumizi

Wakala wa Serikali wa Uchapaji Pemba iliidhinishiwa kutumia jumla ya shilingi 219,756,730 kwa ajili ya kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 kiasi cha shilingi 2,500,000 zimeingizwa na kutumika kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 1.14 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya gharama za uendeshaji wa shughuli za kiafisi.

Hali hii inapelekea Wakala kushindwa kufanya shughuli zake za kiutendaji kwa ufanisi unaotakiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala kushirikiana na Afisi Kuu ya Wakala Unguja kuhakikisha Afisi ya Wakala Pemba inaingiziwa fedha za kutosha kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji wa Afisi.

### 6.1.2 WAKALA WA MIUNDOMBINU YA TEHAMA ZANZIBAR (ZICTIA)

Ukaguzi wa hesabu za mwaka wa fedha 2022/2023 kwa Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA Zanzibar umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 6.1.2.1 Dosari katika uandaaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka

Kwa mujibu wa miongozo ya ufungaji Hesabu ya IPSAS Cash Basis 1.3.26 inaeleza kwamba, taarifa za awali za mapato na matumizi pamoja na taarifa nyenginezo za fedha kutolewa mchanganuo wake katika taarifa za uchanganuzi (Notes of the financial statement). Aidha, IPSAS Cash Basis 1.3.25 (b) kinasisitiza taarifa za Hesabu kuwasilishwa kwa kuzingatia usahihi na usawa.

Ukaguzi ulipitia taarifa za fedha za mwaka 2022/2023 zilizowasilishwa na Wakala na kubaini uwepo wa baadhi ya vifungu vilivyoainishwa katika taarifa ya mapato na matumizi ya fedha (Statement of Cash Receipts and Payments) pamoja na taarifa ya mtiririko wa fedha (Statement of Cashflow) zilibainisha uwepo wa kifungu cha mapato mengineyo (other receipts) chenye jumla ya shilingi 4,227,531,817 ambazo hazijabainishwa mchanganuo wake katika taarifa zilizoainishwa katika maelezo ya taarifa ya fedha (Notes of the Financial Statement).

Uandaaji wa Taarifa za Fedha za Mwisho wa mwaka bila ya kuzingatia miongozo ya ufungaji wa Hesabu ya IPSAS Cash Basis inaweza kupelekea kuathiri maamuzi ya watumiaji wa Taarifa za Fedha.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA kufanyia mapitio Taarifa zake za fedha za mwisho wa mwaka na kuhakikisha taarifa zinaandaliwa kwa kuzingatia usawa na usahihi.

#### 6.1.2.2 Tofauti iliyojitokeza katika taarifa za fedha shilingi 2,672,032,699

IPSAS Cash Basis 1.3.27 inaeleza kwamba, taarifa za fedha za mwisho wa mwaka zitalazimika kuwa zenye kueleweka, taarifa zenye usahihi, zilizokamilika, zisizo na makosa, zenye uwiano kwa vipindi tofauti na pia ambazo zitaweza kuthibitishwa.

Ukaguzi ulipitia Taarifa za Fedha za Mwisho wa Mwaka 2022/2023 na kubaini jumla ya shilingi 4,063,749,680.39 ziliripotiwa katika taarifa hizo na shilingi 6,735,811,870.87 ziliripotiwa katika daftari Kuu la Mapato na kupelekea uwepo wa tofauti katika taarifa za fedha jumla ya shilingi 2,672,032,699 jambo ambalo limetia shaka juu ya uwepo wa tofauti hiyo ambapo hadi ukaguzi unamalizika maelezo ya tafauti hiyo hayajapatikana.

Kushindwa kuainisha makusanyo ya jumla ya shilingi 2,672,032,699 katika taarifa za fedha za mwisho wa mwaka kunaweza kupelekea kuathiri maamuzi ya watumiaji wa Taarifa za Fedha za Mwisho wa Mwaka kwa kushindwa kubaini kiasi halisi cha fedha kilichokusanywa.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA kuhakikisha unazifanyia mapitio taarifa za fedha za mwisho wa mwaka kwa kulinganisha na taarifa zilizomo katika daftari la mapato ili kuweza kuhakikisha upatikanaji wa taarifa zilizokamilika na zenye usahihi.

Hali halisi wa mapato kwa mujibu wa Cash book ni kama inayoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 82: Orodha ya bili zilizolipwa kwa mujibu wa daftari la mapato**

| Taarifa ya mapato kwa Tanzania shilingi | | | |
|---|---|---|---|
| **Tarehe** | **Jina** | **Nambari ya bili** | **Kiasi kilicholipwa (Tshs)** |
| 07/06/2022 | Katibu Mkuu Wizara ya Maji Nishati (Michenzani Mall) | 188 | 3,961,500 |
| 07/06/2022 | Commissioner ZRA | 189 | 36,320,400 |
| 07/08/2022 | M/Mtendaji Mamlaka ya M/Amali (Vitongoji) | 191 | 9,269,000 |
| 18/7/2022 | The Institute Of Public (IPA) | 193 | 11,536,800 |
| 19/7/2022 | Katibu Mkuu Wizara ya Elimu Na M/Amali (Elimu FM) | 195 | 5,448,800 |
| 26/7/2022 | Kamishna Bodi ya Mapato Zanzibar (Gombani PBA) | 196 | 7,521,000 |
| 08/03/2022 | Kamishna Idara ya Michezo (Viwanja Vya Mpira) | 199 | 9,960,000 |
| 08/04/2022 | Dhiabu Moh'd Dhiabu wa Mbeleo | 200 | 6,000,000 |
| 08/09/2022 | Wakala wa Maendeleo ya Viwanda SMIDA | 201 | 4,665,000 |
| 08/09/2022 | Chief Executive Officer Zanztel (AUG) | 202 | 34,951,122 |
| 08/11/2022 | Mamlaka ya Viwanja Vya Ndege (Terminal III) | 205 | 15,092,000 |
| 29/8/2022 | Taasisi ya Elimu Zanzibar | 208 | 3,076,250 |
| 09/05/2022 | Megha Engineering | 211 | 12,000,000 |

| Taarifa ya mapato kwa Tanzania shilingi | | | |
|---|---|---|---|
| **Tarehe** | **Jina** | **Nambari ya bili** | **Kiasi kilicholipwa (Tshs)** |
| 09/07/2022 | Estim Enterprises Ltd | 212 | 17,629,500 |
| 09/07/2022 | Chief Executive Officer Zantel (Sept) | 213 | 34,967,427 |
| 09/07/2022 | Katibu Mkuu Wizara ya M/Jamii Zanzibar (Sebleni) | 215 | 6,618,250 |
| 15/9/2022 | Kamishna Zimamoto (Ofisi Kuu) | 217 | 6,710,250 |
| 16/9/2022 | M/Mtendaji Mamlaka ya M/Amali (Beit-El-Rais) | 218 | 4,749,500 |
| 19/9/2022 | M/Mtendaji Kampuni ya Uvuvi (Ofisi za ZAFICO) | 219 | 2,265,500 |
| 21/9/2022 | M/Mkuu Taasisi ya Utafiti (Kizimbani) | 221 | 3,478,261 |
| 21/9/2022 | Mkurugenzi Mtendaji Mfuko Wa Barabara (Ofisi ya Mfuko) | 222 | 1,345,500 |
| 26/9/2022 | Zanzibar Bureau Of Standards (ZBS) | 223 | 3,184,279 |
| 26/9/2022 | Mrajis Bodi ya Kondonominia (Sensa) (Shangani) | 225 | 3,363,000 |
| 30/9/2022 | Mkurugenzi Matrekta (Mbweni) | 226 | 2,687,650 |
| 30/9/2022 | M/Mtendaji Idara Ya Kilimo (Mbweni) | 227 | 4,408,000 |
| 10/04/2022 | Ofisi ya Wakala wa Vipimo Pemba | 229 | 3,473,000 |
| 10/04/2022 | Wakala Wa Usalama/ Barabarani Pemba (M/Usafiri PBA) | 230 | 3,343,500 |
| 10/04/2022 | Karakana Kuu ya Magari - Pemba (Ofisi Kuu) | 231 | 4,266,250 |
| 10/04/2022 | Usajili Wa Biashara na Mali - Pemba (Ofisi Kuu) | 232 | 2,570,750 |
| 10/06/2022 | M/Mtendaji Mamlaka ya M/Amali (Makunduchi) | 234 | 8,630,750 |
| 10/06/2022 | Chief Executive Officer Zantel (OC) | 235 | 34,967,427 |
| 17/10/2022 | Mkuu wa Skuli ya Sheria Zanzibar | 240 | 3,126,000 |
| 27/10/2022 | Mkurugenzi Salem Contruction | 246 | 16,663,500 |
| 28/10/2022 | Management & Development Health PBA | 247 | 5,272,750 |
| 11/02/2022 | Wakala Wa Usajili Wa Matukio | 248 | 19,377,500 |
| 11/02/2022 | Wakala Wa Usajili Wa Matukio | 249 | 3,967,500 |
| 11/10/2022 | Kamishna Bodi Ya Mapato Zanzibar | 250 | 8,320,250 |
| 11/10/2022 | Kamishna Bodi Ya Mapato Zanzibar | 251 | 5,313,000 |
| 11/11/2022 | Taasisi Ya Utafiti Wa Mifugo | 253 | 4,248,300 |
| 14/11/2022 | Wakala Wa Majengo Zanzibar | 254 | 3,082,000 |
| 15/11/2022 | Wakala Wa Matukio Ya Kijamii | 255 | 4,105,500 |
| 16/11/2022 | Shirika La Bima Zanzibar | 258 | 6,755,000 |

| Taarifa ya mapato kwa Tanzania shilingi | | | |
|---|---|---|---|
| **Tarehe** | **Jina** | **Nambari ya bili** | **Kiasi kilicholipwa (Tshs)** |
| 17/11/2022 | Katibu Mkuu Wizara Ya Afya | 259 | 4,105,500 |
| 21/11/2022 | Mkurugenzi Mtendaji Zura | 260 | 3,777,750 |
| 23/11/2022 | Katibu Mkuu W/Watoto | 261 | 3,887,000 |
| 25/11/2022 | Mkurugenzi Baraza Ka Jiji | 262 | 2,314,000 |
| 28/11/2022 | Mkurugenzi Mtendaji ZEMA | 263 | 1,385,750 |
| 29/11/2022 | Mkurugenzi Idara ya M/Mifugo | 264 | 4,324,000 |
| 12/01/2022 | Mthamini Mkuu wa Serikali | 265 | 2,345,000 |
| 12/03/2022 | Katibu Mkuu Wizara ya Afya | 266 | 30,479,400 |
| 12/05/2022 | Quality Building Contractor Ltd Kitogani | 267 | 345,000 |
| 12/06/2022 | Kamishna Bodi ya Mapato Zanzibar | 275 | 13,978,250 |
| 14/12/2022 | Wakala Wa Huduma za Matrekta Pemba | 276 | 3,620,100 |
| 12/08/2022 | Chief Executive Officer Zantel (Nov,2022) | 277 | 34,967,427 |
| 12/08/2022 | Chief Executive Officer Zantel (Dec,2022) | 278 | 34,967,427 |
| 13/12/2022 | Mratibu Wakala wa Barabara Pemba | 282 | 3,851,400 |
| 14/12/2022 | Quality Building Constractor Ltd Kitogani | 283 | 9,188,500 |
| 14/12/2022 | Rans Company Ltd – Dimani | 284 | 66,907,000 |
| 14/12/2022 | | 286 | 17,249,400 |
| 14/12/2022 | CRJE (East Africa Ltd) – DSM | 287 | 31,079,400 |
| 14/12/2022 | | 288 | 22,235,700 |
| 14/12/2022 | Salem Contruction Ltd Dsm | 291 | 7,969,500 |
| 01/03/2023 | Zmux July- Dec,2022 | 292 | 69,000,000 |
| 01/04/2023 | Viettel Tanzania Plc (April- March,2023) | 293 | 87,000,000 |
| 01/04/2023 | Htt Infraco Limited (July - Dec,2022) | 294 | 175,917,644 |
| 01/04/2023 | Chief Executive Officer Zanztel (July June2023) | 295 | 367,500,000 |
| 01/10/2023 | The Institute Of Public (Ipa) | 296 | 34,610,400 |
| 01/10/2023 | Chief Executive Officer Zantel (Jan- 2023) | 297 | 34,967,427 |
| 01/10/2023 | Wcfc (Hospital) Limited | 299 | 77,878,500 |
| 24/01/2023 | Mazrui Building Contractors Ltd | 301 | 17,549,400 |
| 24/01/2023 | Tume ya Ushindani wa Biashara -Pemba | 303 | 1,610,000 |
| 30/01/2023 | Mamlaka ya Udhibiti Nishati Zura | 304 | 3,120,750 |

| Taarifa ya mapato kwa Tanzania shilingi | | | |
|---|---|---|---|
| **Tarehe** | **Jina** | **Nambari ya bili** | **Kiasi kilicholipwa (Tshs)** |
| 30/01/2023 | Tupo Pamoja Zanzibar | 306 | 3,000,000 |
| 30/01/2023 | Limbani Wete Hub | 307 | 4,000,000 |
| 30/01/2023 | Mamlaka ya Huduma ya Nishati (ZURA) | 308 | 2,179,250 |
| 02/07/2023 | Idara ya Habari Maelezo | 310 | 1,500,000 |
| 02/07/2023 | Zanzibar Water Authority (ZAWA) | 312 | 5,397,187 |
| 02/07/2023 | Zanzibar Housing Corporation (ZHC) | 313 | 3,691,800 |
| 13/02/2023 | Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha | 320 | 8,322,000 |
| 13/02/2023 | Mkuu Wa Kikosi Cha Valantia | 321 | 7,000,000 |
| 21/02/2023 | Zanzibar Housing Corporation (ZHC) | 347 | 3,691,800 |
| 21/02/2023 | Zanzibar Housing Corporation (ZHC) | 349 | 9,237,375 |
| 21/02/2023 | Bodi ya Mikopo Elimu ya Juu Zanzibar | 350 | 2,413,000 |
| 27/02/2023 | Commissioner ZRA | 351 | 36,320,400 |
| 27/02/2023 | | 352 | 36,474,300 |
| 27/02/2023 | Karume Institute of Science and Technology (KIST) | 371 | 6,130,350 |
| 14/03/2023 | Zanzibar Fisheries and Marine Resources Research (ZAFIRI) | 378 | 2,332,155 |
| 27/02/2023 | The State University of Zanzibar (SUZA) | 389 | 66,587,400 |
| 15/03/2023 | Meneja Mkuu Shirika la Umeme Zanzibar | 390 | 4,910,000 |
| 24/03/2023 | Mkuu wa Kikosi cha Valantia | 392 | 7,000,000 |
| 28/03/2023 | Karume Institute of Science and Technology (KIST) | 393 | 3,083,270 |
| 13/04/2023 | Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini "A" | 402 | 2,556,522 |
| 14/04/2023 | Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Mali Asili na Mifugo | 403 | 17,226,270 |
| 14/04/2023 | Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Ofisi za Maruhubi | 404 | 6,002,713 |
| 18/042023 | Mkurugenzi Mkuu Tume ya Ushindani Halali Zanzibar | 405 | 1,610,000 |
| 18/042023 | Group Six International Ltd (GSI) | 420 | 36,891,400 |
| 05/04/2023 | Katibu Mkuu Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwekezaji Zanzibar | 421 | 5,855,500 |
| 05/04/2023 | The State University of Zanzibar (SUZA) | 425 | 22,148,775 |
| 15/03/2023 | Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Jozani | 442 | 8,737,126 |
| 18/05/2023 | Mkurugenzi Mtendaji Taasisi ya Elimu Zanzibar | 447 | 2,621,500 |
| 14/06/2023 | Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini "A" | 452 | 2,433,809 |

| Taarifa ya mapato kwa Tanzania shilingi | | | |
|---|---|---|---|
| **Tarehe** | **Jina** | **Nambari ya bili** | **Kiasi kilicholipwa (Tshs)** |
| 15/06/2023 | Mkaguzi Mkuu wa Elimu Zanzibar | 453 | 3,567,400 |
| 30/06/2023 | Htt Infraco Limited (Jan - Juni 2023) | 456 | 176,250,000 |
| **Jumla Ndogo Tsh. (A)** | | | **2,056,008,388** |
| **Taarifa za Mapato kwa fedha za Kigeni** | | | |
| **Tarehe** | **Jina** | **Nambari ya Bili** | **Kiasi kilicholipwa (USD)** |
| 07/05/2022 | Chief Executive Officer Zantel (July) | 187 | 15,000 |
| 07/06/2022 | Zanzibar Social Security Fund (ZSSF) | 190 | 3,825 |
| 18/7/2022 | Zanzibar Electricity Corporation (ZECO) | 192 | 1,530 |
| 16/8/2022 | China Medical Team (CMT) | 206 | 4,600 |
| 12/06/2022 | Managing Director Zanlink | 268 | 17,920 |
| 12/06/2022 | Managing Director Zanlink | 269 | 124,200 |
| 12/06/2022 | Managing Director Zanlink | 270 | 49,680 |
| 12/06/2022 | Managing Director Zanlink | 271 | 24,840 |
| 12/06/2022 | Mic Tanzania Limited Plc Tigo | 272 | 320,784.20 |
| 12/06/2022 | Management & Development For Health (MDH) | 273 | 5,175 |
| 01/11/2023 | Zanzibar Connecting Company | 298 | 13,378 |
| 01/11/2023 | Zanzibar Airport Authority (ZAA) | 315 | 15,075 |
| 01/11/2023 | Zanzibar Airport Authority (ZAA) | 322 | 15,075 |
| 01/11/2023 | Zanzibar Airport Authority (ZAA) | 323 | 15,075 |
| 01/11/2023 | Zanzibar Utility Regulatory Authority Zura | 330 | 16,500 |
| 01/11/2023 | People's Bank of Zanzibar Ltd (PBZ) | 336 | 2,880 |
| 01/11/2023 | People's Bank of Zanzibar Ltd (PBZ) | 337 | 8,640 |
| 20/03/2023 | Account Payable Finance Mic Tanzania PLC | 340 | 207 |
| 20/03/2023 | Zanzibar Social Security Fund | 343 | 15,300 |
| 27/02/2023 | Chief Executive Officer Zantel (February, 2023) | 353 | 15,000 |
| 27/02/2023 | Chief Executive Officer Zantel (March,2023) | 354 | 15,000 |
| 28/02/2023 | Zanzibar Ports Corporation (ZPC) | 357 | 3,918.75 |
| 28/02/2023 | | 358 | 4,743.75 |
| 28/02/2023 | | 359 | 4,743.75 |
| 28/02/2023 | | 360 | 4,743.75 |

| Taarifa ya mapato kwa Tanzania shilingi | | | |
|---|---|---|---|
| **Tarehe** | **Jina** | **Nambari ya bili** | **Kiasi kilicholipwa (Tshs)** |
| 28/02/2023 | Zanzibar Shipping Corporation | 365 | 3,960 |
| 03/02/2023 | Zanzibar State Trading Corporation (ZSTC) | 366 | 2,070 |
| 03/02/2023 | | 367 | 2,070 |
| 03/02/2023 | | 368 | 2,070 |
| 03/02/2023 | | 369 | 2,070 |
| 03/03/2023 | Zanzibar Electricity Corporation | 372 | 1,453.50 |
| 03/08/2023 | Managing Director Zanlink Limited | 376 | 24,840 |
| 03/08/2023 | Managing Director Zanlink Limited | 377 | 133,750 |
| 15/03/2023 | Zanzibar Road Transport Safety Authority | 381 | 6,969 |
| 15/03/2023 | | 382 | 6,969 |
| 15/03/2023 | | 383 | 6,969 |
| 15/03/2023 | People's Bank Of Zanzibar Ltd (Pbz) | 407 | 6,624 |
| 27/04/2023 | Zanzibar Utility Regulatory (Zura) | 408 | 4,125 |
| 05/04/2023 | Chief Executive Officer Zantel (April,2023) | 422 | 15,000 |
| 05/04/2023 | China Medical Team (Cmt) | 423 | 2,300 |
| 05/04/2023 | Zanzibar Social Security Fund (Zssf) | 424 | 4,398.75 |
| 05/10/2023 | Mic Tanzania Limited Plc Tigo | 427 | 728,379.25 |
| | Managing Director Zanlink | 429 | 144,900 |
| 05/11/2023 | Zanzibar Shipping Corporation (Shipco) | 433 | 1,138.50 |
| 05/11/2023 | Zanzibar Housing Corporation (Zhc) | 434 | 1,811.25 |
| 05/11/2023 | Deep Sea Fishing Authority (Dspa) | 438 | 14,250 |
| 05/12/2023 | Chief Executive Officer Zantel (May,2023) | 440 | 15,000 |
| 15/05/2023 | Managing Director Zanlink | 444 | 84,146.63 |
| 15/05/2023 | | 445 | 4,140 |
| 15/05/2023 | | 446 | 82,146.64 |
| 26/06/2023 | Karume Institute Of Science And Technology | 455 | 1,552.50 |
| | **Jumla Ndogo (USD)** | | **2,020,937.22** |
| | **Jumla ndogo (Tsh.) (B)** | **1USD = Tsh. 2,315.66** | **4,679,803,483** |
| | **Jumla Kuu (A+B)** | | **6,735,811,870.87** |

*Chanzo: Taarifa za mapato ziliozowasilishwa na Msimamizi wa mapato wa Wakala*

### 6.1.2.3 Uwepo wa deni la shilingi 2,605,582,800 ambalo halijalipwa

Ukaguzi ulipitia Taarifa za Fedha za Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA pamoja na Ankara zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi na kubaini uwepo wa deni la shilingi 2,605,582,800 kwa taasisi za Serikali ambalo halijalipwa ,deni ambalo mbali na jitihada zilizochukuliwa na Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA kwenda kwa wateja waliowapatia huduma halijalipwa.

Kutokulipwa kwa deni hilo kunaweza kuathiri malengo ya ukusanyaji wa Mapato ya Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA .

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA kuhakikisha wanachukua jitihada za makusudi kwa taasisi hizo juu ya ulipaji wa madeni kwa wakati.

Mchanganuo wa deni ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 83: Orodha ya Deni kwa mujibu wa Ankara**

| Tarehe | Jina | Nambari ya Bili | Deni (Tsh.) |
|---|---|---|---|
| 29/7/2022 | M/Mkuu Mamlaka ya Maji (Marekebisho Mradi) | 197 | 37,077,500 |
| 08/03/2022 | Kamishna Idara ya Michezo (Viwanja vya Mpira) | 199 | 20,244,750 |
| 17/8/2022 | Katibu Mkuu Wizara ya Biashara na Viwanda (Kinazini) | 207 | 4,290,075 |
| 31/8/2022 | Mamlaka Ya Viwanja Vya Ndege (Terminal III) | 209 | 17,710,000 |
| 09/02/2022 | Katibu Mtendaji Maji Nishati (Ofisi Ya Crc) | 210 | 3,921,500 |
| 20/9/2022 | M/Mkuu Mamlaka Ya Viwanja Vya Ndege (Terminal III) | 220 | 17,710,000 |
| 26/9/2022 | Katibu Mkuu Ofisi Ya Rais (Uwekaji Wa Lan) | 224 | 13,386,000 |
| 30/9/2022 | Mkurugenzi Matrekta (Mbweni) | 226 | 3,850,100 |
| 30/9/2022 | M/Mtendaji Idara Ya Umwagiliaji Maji (Mbweni) | 228 | 5,336,000 |
| 25/10/2022 | Mkurugenzi Idara Ya M/Ualimu | 243 | 1,138,500 |
| 25/11/2022 | Mkurugenzi Baraza La Jiji | 262 | 2,251,500 |
| 01/02/2023 | Kampuni Ya Bench Mark Dsm | 289 | 4,807,000 |
| 01/02/2023 | Ofisi Ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar | 290 | 5,669,500 |
| 23/01/2023 | Taasisi Ya Viwango Zanzibar | 302 | 1,610,000 |
| 23/01/2023 | Ofisi Ya Mkurugenzi Wa Mashtaka | 309 | 6,808,000 |
| 02/07/2023 | Idara Ya Habari Maelezo | 310 | 3,939,500 |
| 20/02/2023 | Mic Tanzania Limited Plc Tigo | 339 | 6,621,700 |
| 03/03/2023 | Katibu Mkuu Wizara Ya Afya Zanzibar | 374 | 3,542,000 |
| 16,03/2023 | Meneja Mkuu Shirika La Umeme Zanzibar | 391 | 10,137,250 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 29/03/2023 | Kamishna Mkuu Uhamiaji Tanzania (Miaka Miwili) | 396 | 99,360,000 |
| 27/04/2023 | Afisa Mdhamini Ofisi Ya Makamo Wa Pili Pemba | 411 | 11,321,750 |
| 27/04/2023 | Mkaguzi Mkuu Wa Elimu Zanzibar | 426 | 4,174,500 |
| 05/12/2023 | Zmux --January - June 2,023, | 441 | 69,000,000 |
| 06/07/2023 | Meneja Mkuu Shirika La Umeme Zanzibar | 451 | 63,145,000 |
| 15/06/2023 | Mkaguzi Mkuu Wa Elimu Zanzibar | 453 | 4,174,500 |
| 22/06/2023 | Mratib Mamlaka Ya Mafunzo Ya Amali Pemba | 454 | 4,370,000 |
| **Jumla** | | | **425,596,625** |
| **Tarehe** | **Jina** | **Nambari ya Bili** | **Deni (USD)** |
| 18/7/2022 | Zanzibar Utility Regulatory (ZURA) | 194 | 4,743.75 |
| 10/11/2022 | Com.Net Compant Ltd | 237 | 14,283.00 |
| 10/11/2022 | Com.Net Compant Ltd | 238 | 14,283.00 |
| 17/10/2022 | Zanzibar Fisheries And Marine | 239 | 1,207.50 |
| 12/06/2022 | Mic Tanzania Limited Plc Tigo | 272 | 320,784.20 |
| 12/06/2022 | Zanzibar Water Authority (ZAWA) | 312 | 5,175.00 |
| 12/06/2022 | Director G. Z'bar Road Transport (ZANROAD) | 314 | 6,969.00 |
| 09/02/2023 | Z'bar Investment Promotion Authority (ZIPA) | 316 | 4,398.00 |
| 09/02/2023 | Zanzibar Airport Authority (ZAA) | 323 | 17,336.00 |
| 13/02/2023 | Tanzania Telecommunication Corporation | 324 | 76,848.00 |
| 13/02/2023 | Tanzania Telecommunication Corporation | 325 | 97,881.00 |
| 13/02/2023 | Tanzania Telecommunication Corporation | 326 | 15,369.00 |
| 13/02/2023 | Zanzibar Water Authority (ZAWA) | 331 | 5,175.00 |
| 13/02/2023 | Zanzibar Water Authority (ZAWA) | 332 | 5,175.00 |
| 13/02/2023 | Zanzibar Water Authority (ZAWA) | 333 | 5,175.00 |
| 20/03/2023 | Account Payable Finance Mic Tanzania Plc | 340 | 207.00 |
| 21/02/2023 | Zanzibar Investiment Promotion Authority (ZIPA) | 344 | 4,398.75 |
| 21/02/2023 | Zanzibar Investiment Promotion Authority (ZIPA) | 345 | 4,398.75 |
| 21/02/2023 | Zanzibar Investiment Promotion Authority (ZIPA) | 346 | 4,398.75 |
| 21/02/2023 | Zanzibar Housing Corporation (ZHC) | 348 | 1,811.25 |
| 21/02/2023 | Zanzibar Housing Corporation (ZHC) | 349 | 1,811.25 |
| 27/02/2023 | Alfa Care Group Limited | 355 | 1,139.54 |
| 27/02/2023 | Alfa Care Group Limited | 356 | 1,139.54 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 27/02/2023 | Zanzibar Electricity Corporation (ZECO) | 373 | 1,759.50 |
| 15/03/2023 | Zanzibar Broadcasting Corporation (ZBC) | 384 | 9,660.00 |
| 15/03/2023 | Zanzibar Broadcasting Corporation (ZBC) | 385 | 9,660.00 |
| 15/03/2023 | Zanzibar Broadcasting Corporation (ZBC) | 386 | 9,660.00 |
| 28/03/2023 | Zanzibar Broadcasting Corporation (ZBC) | 394 | 9,660.00 |
| 28/03/2023 | Zanzibar Water Authority (ZAWA) | 395 | 5,175.00 |
| 29/03/2023 | Zanzibar Electricity Corporation (ZECO) | 397 | 1,759.00 |
| 04/11/2023 | Zanzibar Investiment Promotion Authority (ZIPA) | 400 | 2,673.75 |
| 27/04/2023 | Zanzibar Bureau Of Standards (ZBS) | 409 | 1,656.00 |
| 27/04/2023 | Zanzibar Revenue Authority (ZRA) | 410 | 18,630.00 |
| 27/04/2023 | Zanzibar Airport Authority (ZAA) | 412 | 17,336.25 |
| 27/04/2023 | Zanzibar Airport Authority (ZAA) | 413 | 17,336.25 |
| 27/04/2023 | Zanzibar State Trading Corporation (ZSTC) | 414 | 2,070.00 |
| 27/04/2023 | Zanzibar Investiment Promotion Authority (ZIPA) | 415 | 3,536.25 |
| 27/04/2023 | Zanzibar Investiment Promotion Authority (ZIPA) | 416 | 3,536.25 |
| 27/04/2023 | Zanzibar Investiment Promotion Authority (ZIPA) | 417 | 3,536.25 |
| 27/04/2023 | Zanzibar Investiment Promotion Authority (ZIPA) | 418 | 4,398.75 |
| 27/04/2023 | Zanzibar Road Transport Safety Authority | 419 | 6,969.00 |
| 27/04/2023 | Zanzibar Housing Corporation (ZHC) | 434 | 1,811.25 |
| 05/11/2023 | Zanzibar Ports Corporation (ZPC) | 439 | 4,743.75 |
| 05/12/2023 | Chief Executive Officer Zantel (May,2023) | 440 | 15,000.00 |
| 15/05/2023 | Managing Director Zanlink | 444 | 84,146.63 |
| 15/05/2023 | Managing Director Zanlink | 445 | 4,140.00 |
| 15/05/2023 | Managing Director Zanlink | 446 | 82,146.64 |
| 31/05/2023 | The Public Helth Laboratory (PHL) | 449 | 3,750.00 |
| 25/05/2023 | Mandlethu | 450 | 1,000.00 |
| 26/06/2023 | Karume Institute of Science andTechnology | 455 | 1,552.50 |
| **Jumla (USD)** | | | **941,410.3** |

*Chanzo: Taarifa za madeni na mapato zilizowasilishwa na Msimamizi wa mapato*

### 6.1.2.4 Kushindwa kukusanya jumla ya shilingi 44,007,687 kutokana na usimamizi usioridhisha wa Mkataba baina ya Wakala na TTCL

Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA waliingia katika makubaliano ya mkataba na Tanzania Telecommunications Corporation Limited (TTCL) ambapo utekelezaji wake ulianza rasmi mnamo tarehe 1 Septemba, 2022 kwa ajili ya kupatiwa huduma ya Fiber (Zanzibar Submarine Fiber Network) kwa ada ya USD 432,000 kwa mwaka kwa huduma za kutoka Dar es Salaam kuja Zanzibar, na jumla ya USD 129,257.4 kwa huduma za kutoka Tanga kwenda Pemba na kufanya jumla ya malipo yote kuwa ni USD 561,257.

Ukaguzi ulibaini Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA waliwasilisha Ankara yenye thamani ya USD 190,098 ambayo ni sawa na shilingi 440,076,870 kwa kutumia kiwango kilichotolewa na BoT tarehe 30 Juni, 2023 cha shilingi 2,315 kwa TTCL kwa ajili ya kuweza kufanyiwa malipo pamoja na uwasilishwaji wa bili hizo kwa TTCL. Aidha, hakukua na malipo yoyote yaliofanikiwa kufanywa au kupokelewa na Wakala hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 ambapo Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA hawakuweza kuchukua hatua yoyote kwa TTCL pamoja na ucheleweshwaji wa malipo hayo, ambapo kwa mujibu wa sehemu ya 13.3 ya mkataba inaeleza kwamba endapo kutakua na ucheleweshwaji wa malipo kwa zaidi ya siku 30 kuanzia tarehe ya kuwasilishwa kwa bili, Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA atalazimika kuhakikisha anawasilisha taarifa ya ukumbusho wa deni kwa awamu mbili kwa TTCL kabla ya kujumuisha asilimia 10 ya deni ikiwa ni fidia ya ucheleweshwaji wa malipo.

Kushindwa kusimamia vyema vifungu vya mkataba kunaweza kupeleka upotevu wa mapato, aidha kushindwa kukumbushia deni kwa TTCL kunapelekea Wakala kushindwa kudai nyongeza ya asilimia 10 inayotokana na kucheleweshwa kwa malipo.

Ukaguzi unaushauri Uongozi wa Wakala kuhakikisha unasimamia vyema matakwa ya mkataba kwa manufaa ya Wakala na Serikali kwa ujumla. Mchanganuo wa deni ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 84: Mchanganuo wa deni pamoja na asilimia kumi ilioshindwa kujumuishwa katika deni**

| Namba | Nambari Ankara | Kiasi (USD) | Kiasi kilichoshindwa kudaiwa (Asilimia kumi ya bili katika USD) | Kiasi kilichoshindwa kudaiwa (Asilimia kumi katika Tsh iliobadilishwa kupitia Rate ya BoT 30/06/2022 1USD=TZS 2,315) | Miezi iliotolewa Ankara |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 324 | 76,848 | 7,684.8 | 17,790,312 | Julai – Septemba 2022 |
| 2. | 325 | 97,881 | 9,788.1 | 22,659,451.5 | Oktoba – Disemba 2022 |
| 3. | 326 | 15,369 | 1,536.9 | 3,557,923.5 | Malipo ya mwaka ya huduma ya O & M |
| **Jumla** | | **190,098** | **19,009.8** | **44,007,687** | |

### 6.1.2.5 Kutokulipwa kwa kiasi cha shilingi 859,233,085 kutoka kwa Mteja TTCL

Kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba baina ya Wakala wa Miundmbinu ya TEHAMA na Tanzania Telecommunications Corporation Limited (TTCL) ambapo utekelezaji wake ulianza rasmi mnamo tarehe 1 Septemba, 2022 kwa ajili ya kupatiwa huduma ya Faiba (Zanzibar Submarine Fiber Network). Mkataba uliainisha kuwa ada ya mwaka kwa huduma zinazotolewa na Wakala kwa TTCL ni USD 561,257 ambapo USD 432,000 ni kwa ajili ya huduma kutoka Dar es Salaam kuja Zanzibar na Dola za Marekani 129,257.4 kwa huduma kutoka Tanga kwenda Pemba.

Ukaguzi ulibaini kwamba hadi kufikia tarehe 30 Juni 2022 Wakala waliwasilisha bili zenye thamani ya USD 190,098 ambayo ni sawa na shilingi 440,076,870 kwa kutumia kiwango kiliotolewa na BoT tarehe 30 Juni 2022 ya shilingi 2,315, ambayo ilikuwa ni kuanzia Julai 2022 hadi Disemba, 2022 kwa huduma za Faiba na kwa M/S O & M waliwasilisha bili ya mwaka na kushindwa kuwasilisha bili kwa miezi iliobakia yenye thamani ya USD 371,159 ambayo ni sawa na shilingi 859,233,085.

Kushindwa kulipwa kwa bili kwa huduma wanazowapatia TTCL kunapelekea Wakala kushindwa kukusanya mapato kupitia huduma iliyotolewa kwani kiasi kingeleiweza kutumika kwa shughuli za uendeshaji wa shughuli za Maendeleo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala kuhakikisha kwamba unafatilia fedha zake kutokana na huduma walizowapatia TTCL. Mchanganuo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 85: Kiasi kilichoshindwa kudaiwa (Unbilled Amount)**

| Kiasi kilichostahiki kudaiwa kwa mujibu wa Mkataba | | Kiasi kilichodaiwa kwa mujibu wa makubaliano ya Mkataba | | Kiasi kilichoshindwa kudaiwa kwa mujibu wa Mkataba | |
|---|---|---|---|---|---|
| Dola ya Marekani | Shilingi ya Tanzania | Dola ya Marekani | Shilingi ya Tanzania | Dola ya Marekani | Shilingi ya Tanzania |
| 561,257 | 1,299,309,955 | 190,098 | 440,076,870 | 371,159 | 859,233,085 |

### 6.1.2.6 Malipo yenye vielelezo pungufu shilingi 89,032,790

Kifungu nambari 34(1) cha Sheria, Nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinamtaka Afisa Mhasibu kuweka kumbukumbu zinazohusiana na masuala ya fedha za Idara, taasisi za biashara au taasisi za kikatiba kulingana na masharti na viwango na kanuni ya 55(1) pamoja na kanuni ya 57(2) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inataka malipo yote yanayofanywa na taasisi ya Serikali kuhakikisha yanaambatanishwa na marejesho yaliokamilika.

Ukaguzi umebaini kwamba Wakala ilifanya matumizi ya jumla ya shilingi 89,032,790 kwa matumizi mbalimbali bila ya kuzingatia upatikanaji wa marejesho ya kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kukosekana kwa marejesho ya malipo yaliotajwa hapo juu kumepelekea ukaguzi kushindwa kuthibitisha uhalali wa malipo yaliofanywa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala kuhakikisha kwamba malipo yote yanayofanywa yanawekewa viambatanisho halali vya matumizi yaliyofanyika. Mchanganuo wa malipo hayo unaonekana katika Jedwali lifuatalo:-

### Jadweli Nambari 86:Hati za malipo zenye vielelezo pungufu

| Nambari ya Hati | Kiasi Kilicholipwa (shs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 2/7 ya 8-Julai-2022 | 3,660,000 | Wakala wa Mkonga | Malipo kwa ajili ya safari ya kikazi Tanga kwenda kufanya marekebisho ya Mkongo njia ya Tanga Pemba |
| 3/7 ya 8-Julai-2022 | 9,205,396 | Wakala wa Mkonga | Malipo baada ya saa za kazi kwa wafanyakazi wa Wakala |
| 13/10 ya 13-Okt-2022 | 900,000 | Wakala wa Mkonga | Malipo ya fedha kwa ajili ya kupatiwa posho walinzi watatu wanaofanya kazi ya Ulinzi |
| 21/10 ya 17-Okt-2022 | 630,000 | Wakala wa Mkonga | Malipo ya fedha kwa ajili ya safari ya Dar es salaam kikazi kwa mk Ufundi ndg Frank N Kagoma |
| 22/10 ya 17-Okt-2022 | 790,000 | Wakala wa Mkonga | Malipo ya fedha kwa ajili ya safari ya Dar es salaam kikazi kwa mtendaji Mkuu Ndg Shukuru A. Suleiman |
| 24/10 ya 18-Okt-2022 | 150,000 | Wakala wa Mkonga | Malipo ya kukodi gari na wachukuzi wa kubeba nguzo |
| 26/10 ya 18-Okt-2022 | 2,400,000 | Stone Town Trader Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya marejesho ya gharama za wino zilizotumika katika kazi za Wakala wa miundombinu ya Tehama Zanzibar |
| 31/10 ya 31-Okt-2022 | 560,000 | Wakala wa Mkonga | Malipo ya fedha kwa ajili ya marejesho ya gharama ya upakaji rangi kwenye jengo la Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wakala wa miundombinu ya Tehama Zanzibar |
| 12/11 ya 25-Nov-2022 | 680,000 | Saidi Hadadi Makame | Malipo ya fedha kwa ajili ya kukodi gari na wachukuzi wa kubeba nguzo |
| 15/11 ya 30-Nov-2022 | 250,000 | Wakala wa Mkonga Zanzibar | Malipo ya fedha kwa ajili ya marejesho ya fedha zilizotumika kwa ajili ya ununuzi wa betri ya gari SMZ 501 B |
| 6/12 ya 6-Dise-2022 | 270,000 | Wakala wa Mkonga Zanzibar | Marejesho ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa wino kwa matumizi ya Ofisi ya Mhasibu |
| 4/1 ya 5-Jan-2023 | 2,950,000 | Saidi Hadadi Makame | Malipo ya fedha kwa ajili ya uchukuzi na usambazaji wa nguzo 254 pamoja na uunganishaji mkonga wa mawasiliano katika hospitali za wilaya sita (6) na mkoa moja (1) kwa upande wa Unguja |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 5/1 ya 6-Jan-2023 | 570,000 | Miriam Stanley Mwaitumile | Malipo ya fedha kwa ajili ya malipo ya upambaji wa banda katika Tamasha la Tisa la Biashara (9 Zanzibar Shoopping Festival) |
| 9/1 ya 6-Jan-2023 | 630,000 | Wakala wa Mkonga Zanzibar | Malipo ya fedha kwa ajili ya safari ya kikazi kwa nd Muhamed Juma Muhamed |
| 13/1 ya 13-Jan-2023 | 1,065,000 | Wakala wa Mkonga Zanzibar | Malipo ya fedha kwa ajili ya safari ya kikazi Dar es salaam kwa Mkurugenzi Mtendaji wakala wa miundombinu ya TEHAMA Zanzibar |
| 22/1 ya 23-Jan-2023 | 170,000 | Said Hadadi Makame | Malipo ya fedha kwa ajili ya kukodi gari na wachukuzi wa kubeba nguzo |
| 3/2 ya 3-Feb-2023 | 600,000 | Wakala wa Mkonga Zanzibar | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho la walinzi wawili |
| 6(B)/2 ya 10-Feb-2023 | 1,931,950 | Island Refregeration & Electricity | Bakaa la malipo ya Ununuzi wa vifaa vya matengenezo ya vipoza hewa |
| 12/2 ya 14-Feb-2023 | 300,000 | Wakala wa Mkonga Zanzibar | Malipo ya fedha kwa ajili ya kukodi gari na wachukuzi kubeba nguzo |
| 13/2 ya 14-Feb-2023 | 120,000 | Wakala wa Mkonga Zanzibar | Malipo ya fedha kwa ajili ya kukodi gari na wachukuzi kubeba nguzo |
| 14/2 ya 14-Feb-2023 | 230,000 | Haroub & sons decoration | Marejesho ya fedha zilizotumika kwa ajili ya matengenezo madogo ya ofisi |
| 14/2 ya 15-Feb-2023 | 5,439,448 | Mwinyi Building Contractors Ltd | Bakaa ya malipo ya awamu ya kwanza (50%) ya kazi ya upakaji wa rangi katika majengo ya Ofisi za ZICTIA |
| 24/2 ya 24-Feb-2023 | 1,108,270 | Azam Marine Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya kukodi gari kubeba nguzo |
| 1(A)/4 ya 31-Machi-2023 | 588,235 | Azam Marine | Malipo ya kukodi gari kwa ajili ya kubeba mzigo Unguja kwenda Pemba |
| 10/5 ya 9-Mei-2023 | 1,200,000 | Wakala wa Mkonga Zanzibar | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho maalum kwa walinzi mwezi Machi na April |
| 11/5 ya 9-Mei-2023 | 2,550,000 | Wakala wa Mkonga Zanzibar | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho la kujikimu na nauli Pemba |
| 19/5 ya 22-Mei-2023 | 1,098,000 | Wakala wa Mkonga Zanzibar | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho la kujikimu na nauli ya kwenda Dar es salaam kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala wa Miundombinu ya TEHAMA |
| 20(A)/5 ya 26-Mei-2023 | 1,950,000 | Chukwani Catering Supplier | Malipo ya fedha kwa ajili ya kugharamia chakula kitakachotumika katika mafunzo kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ya Mswada wa Sheria ya kuanzishwa kwa shirika la mawasiliano Zanzibar |
| 2/6 ya 7-Juni-2023 | 7,698,429 | Double Plus Company Ltd | Malipo ya fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya kuandikia (stationary) |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3/6 ya 7-Juni-2023 | 3,170,185 | Rahisi Auto Spare | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya matengenezo ya majenereta (betri) |
| 11/6 ya 13-Juni-2023 | 9,367,608 | Kheri Mohd Mhema | Malipo kwa ajili ya malipo mbalimbali yanayohusiana na uunganishaji wa Mkonga |
| 16/6 ya 20-Juni-2023 | 100,000 | Saidi Hadadi Khamis | Malipo ya fedha kwa ajili ubebaji wa vifaa vya mkonga katika gari la Azam |
| 21/6 ya 21-Juni-2023 | 7,413,726 | Kheri Mohd Mhema | Malipo kwa ajili ya malipo mbalimbali yanayohusiana na uunganishaji wa Mkonga |
| 19-Oktoba-2022 (Dola) | 6,252,282 | AFRINIC | Malipo ya fedha kwa ajili ya kulipia IP Block mpya tulizoziomba kutoka AFRINIC |
| 07-Machi-2023 (Dola) | 694,698 | AFRINIC | Malipo ya fedha kwa ajili ya malipo ya Ada ya mwaka kwa AFRINIC |
| 1/7 ya 30-Juni-2022 (Pemba) | 9,514,563 | Iddi Mohammed Salim | Malipo ya fedha kwa huduma ya kutengeneza vyumba vya aluminium katika Ofisi za ZICTIA iliopo jengo la ZSSF Tibirinzi Chake Chake Pemba |
| 1/8 ya 11-Agos-2022 (Pemba) | 640,000 | Wakala wa Mkonga Pemba ChakeChake | Malipo ya fedha za nauli na posho la safari kikazi kwenda Unguja mratibu Wakala wa Mkonga Pemba, ndg. Abbass Fadhil Abbass |
| 3/3 ya 23-Feb-2023 (Pemba) | 1,005,000 | Wakala wa Mkonga Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho na nauli kwa mratibu wa Wakala wa Mkonga Pemba kwenda Unguja kikzi kushiriki kikao cha kuwasilisha makadirio ya bajeti ya mwaka 2023/2024 |
| 2/5 ya 15-Mach-2023 (Pemba) | 1,180,000 | Wakala wa Mkonga Pemba | Malipo ya fedha kwa ajili ya posho na nauli kwa Mratibu wa Wakala wa Mkonga Pemba kwenda Unguja kikazi kushiriki kikao cha kujadili na kupitia bajeti ya Shirika la Mawasiliano Zanzibar |
| **Jumla** | 89,032,790 | | |

### 6.1.2.7 Malipo yaliofanywa kwa njia ya Fedha Taslim (Cash Payment) shilingi 39,925,000

Kanuni Namba 58 ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inataka matumizi yote kufanyika kwa mfumo wa Kielektroniki.

Ukaguzi ulibaini kwamba Wakala ilifanya matumizi ya jumla ya shilingi 39,925,000 kwa njia ya fedha taslim (Cash) bila ya kuzingatia mfumo wa ulipaji wa Kielekroniki.

Kufanya malipo kwa njia ya fedha taslimu kunaweza kupelekea kujitokeza kwa upotevu wa fedha za umma kunakotokana na kushindwa kuzuia tozo za kodi mbalimbali na kuisababishia Serikali hasara.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala kuhakikisha kwamba hakuna malipo yanayofanywa kwa njia ya fedha taslimu. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama unavyoonekana katika Jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 87: Malipo yaliofanywa kwa fedha Taslim

| Hati namba | Aliyelipwa | Kiasi kilicholipwa (Tsh) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1/7 ya 8/7/2022 | Wakala wa Mkonga | 200,000 | Malipo kwa ajili ya ununuzi wa chakula. |
| 2/7 ya 8/7/2022 | | 3,660,000 | Malipo ya kwa ajili posho mbalimbali. |
| 20/10 ya 17/10/2022 | | 3,000,000 | |
| 5/12 ya 5/12/2022 | | 1,590,000 | |
| 5/12 ya 5/12/2022 | | 1,590,000 | |
| 8/4 ya 13/12/2022 | | 360,000 | |
| 12/4 ya 13/4/2023 | | 1,700,000 | |
| 13/4 ya 14/4/2023 | | 3,750,000 | |
| 20B/4 ya 26/5/2023 | | 18,975,000 | |
| 20/6 ya 26/6/2023 | | 4,600,000 | |
| 22/6 ya 30/6/2023 | | 500,000 | |
| **Jumla** | | **39,925,000** | |

#### 6.1.2.8 Ongezeko la matumizi kwa baadhi ya vifungu vya bajeti shilingi 932,427,527

Kanuni ya 20(1) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaelezea kwamba uhaulishaji wa fedha za vifungu usizidi asilimia kumi na tano (15%) ya kiasi chote cha programu husika.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya taarifa za fedha za mwisho wa mwaka kwa kulinganisha bajeti na Matumizi halisi yailioidhinishwa na kubaini uwepo wa ziada ya matumizi ya shilingi 932,427,527 kwa matumizi yaliyofanyika bila ya kuzingatia kiasi kilichoidhinishwa katika bajeti.

Kufanya matumizi ya ziada kwa baadhi ya programu kunaweza kuathiri shughuli nyenginezo zilizotengewa bajeti na hatimae kupunguza ufanisi wa utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala kuhakikisha matumizi yote yanafanyakia kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa na endapo italazimika kufanya uhaulishaji ni vyema kufuatwa taratibu zilizoainishwa katika sheria nambari 12 ya usimamizi wa fedha za umma ya 2016 na kanuni zake. Hali halisi ni kama inavyonekana katika jadweli hapo chini: -

## Jadweli Nambari 88: Mlinganisho wa matumizi na bajeti iliyoidhinishwa

| Kifungu | Maelezo | Makadirio (Tshs) | Matumizi halisi (Tshs) | Ongezeko la matumizi (Tshs) | Asilimia ya Ongezeko (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| 6112246 | Purchase of Fiber Equipments | 230,480,500 | 370,997,736 | 140,517,236 | 61 |
| 6112227 | Purchase of Moving camera | 6,000,000 | 7,205,882 | 1,205,882 | 20 |
| 2209003 | Tuition Fees | 6,200,000 | 18,976,040 | 12,776,040 | 206 |
| 2206025 | Burial Activities | 2,100,000 | 2,900,000 | 800,000 | 38 |
| 2206001 | Stationery Supplies | 14,000,000 | 16,374,429 | 2,374,429 | 17 |
| 2206001 | Sitting Allowance | 79,927,500 | 97,743,400 | 17,815,900 | 22 |
| 2204001 | Petrol | 77,795,000 | 158,000,000 | 80,205,000 | 103 |
| 2202003 | Gift | 500,000 | 4,600,000 | 4,100,000 | 820 |
| 2202001 | Security services | 20,000,000 | 115,500,000 | 95,500,000 | 478 |
| 2201012 | Fiber Network Maintainance | 29,000,000 | 135,863,294 | 106,863,294 | 368 |
| 2112616 | Special Allowance | 1,500,000 | 17,600,000 | 16,100,000 | 1073 |
| 2112610 | Over time | 103,000,000 | 120,590,704 | 17,590,704 | 17 |
| 2112606 | Transport Allowance | 12,600,000 | 17,688,570 | 3,888,300 | 40 |
| 2821022 | Tax Refund | - | 432,690,742 | 432,690,742 | Haimo katika bajeti |
| **Jumla** | | **583,103,000** | **1,516,730,797** | **932,427,527** | |

### 6.1.3 WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII

Ukaguzi wa hesabu za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 6.1.3.1 Kutofanyika kwa usuluhishi wa Kibenki katika ukusanyaji wa Mapato shilingi 65,624,894

Wakala wa Matukio ya Kijamii Zanzibar ina jukumu la kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi ikiwemo utoaji wa vitambulisho, vyeti vya kuzaliwa pamoja na huduma nyenginezo ambapo kwa mujibu wa utaratibu Wakala ana wajibu wa kutoza ada ya huduma inayotolewa kwa mujibu wa Sheria ya Uanzishwaji wa Wakala.

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ukaguzi umebaini uwepo wa dosari mbalimbali katika ukusanyaji wa ada za huduma zinazotolewa ambapo zimepelekea kujitokeza kwa tofauti ya fedha inayokusanywa kupitia malipo yanayolipwa vituoni pamoja na yale yanayolipwa moja kwa moja kupitia benki. Miongoni mwa dosari hizo ni kama ifuatavyo:-

- Kutokufanyika kwa usuluhishi wa kibenki kwa malipo yanayolipwa benki na malipo yanayolipwa vituoni jambo ambalo limepelekea kujitokeza kwa utofauti mkubwa baina ya mapato yaliyopo benki na mapato yaliyokusanywa vituoni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini.
- Uwepo wa miamala ya kifedha inayolipwa moja kwa moja benki bila ya kutumia nambari ya udhibiti "Control Number" hivyo kupelekea kuonekana hesabu ya benki kuwa ni kubwa tofauti na mapato halisi yanayokusanywa vituoni.
- Uwepo wa malipo yanayolipwa vituoni kwa kutumia nambari za udhibiti "Control Number" na kuingia katika mfumo wa ZanMalipo ambapo taarifa zake hazionekani katika mfumo wa CRVS.
- Kutokuunganishwa baina ya Mfumo wa CRVS na Mfumo wa ZanMalipo ambapo mifumo yote inatumika kukusanya mapato na kutoa taarifa za mapato tofauti kwa kila mwezi.

Pamoja na uwepo wa dosari hizo ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Matukio ya Kijamii Zanzibar kuhakikisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato inaunganishwa na kusomana ili kuondosha changamoto za uwepo wa tofauti wa taarifa za makusanyo pamoja na kuhakikisha kunakuwa na usuluhishi wa kibenki wa kila mwezi kwa mapato yote yanayokusanywa na benki pamoja na mapato yanayokusanywa kwenye mifumo ya Wakala.Mchanganuo wa utofauti ya taarifa za mapato ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 89: Tofauti ya Taarifa za mapato baina ya taarifa za benki na taarifa za makusanyo ya Vituo**

| Namba | Mwezi | Taarifa za fedha za Kibenki (Bank statement) (Tsh.) | Taarifa za Makusanyo katika Vituo (Tsh.) | Tofauti (Tsh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Agosti | 144,017,315 | 113,854,316 | 30,162,999 |
| 2. | Septemba | 154,040,499 | 154,006,500 | 33,999 |
| 3. | Oktoba | 176,961,999 | 157,641,000 | 19,320,999 |
| 4. | Novemba | 119,644,499 | 119,614,500 | 29,999 |
| 5. | Disemba | 94,133,999 | 94,089,500 | 44,999 |
| 6. | Februari | 105,785,049 | 105,543,050 | 241,999 |
| 7. | Machi | 107,320,900 | 100,439,000 | 6,881,900 |
| 8. | Aprili | 49,588,500 | 49,525,000 | 63,500 |
| 9. | Mei | 85,524,000 | 76,679,500 | 8,844,500 |
| **Jumla** | | | | **65,624,894** |

### 6.1.3.2 Kutokufanya kazi kwa Mfumo wa Usajili wa Wageni

Kwa mujibu wa Sheria Nambari 3 ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar ya 2018 inaitaka Wakala kufanya usajili wa wageni wanaoingia nchini ambao si Wazanzibari.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uwepo wa wageni wanaoingia nchini kutoka kwenye mataifa mbalimbali ambapo hakuna kumbukumbu iliyowasilishwa katika ukaguzi inayoonesha wageni hao wamesajiliwa kwa mujibu wa matakwa ya kifungu nambari 48 cha Sheria nambari 3 ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar ya 2018.

Pamoja na uwepo wa majibu yaliyowasilishwa na Wakala wa Matukio ya Kijamii kwa barua yenye kumbukumbu namba ZCSRA/U.60/99/VOL.I/2 ya tarehe 15 Oktoba 2021 inayobainisha ya kwamba Wakala imetayarisha kanuni za wageni na kuziwasilisha kwa Mhe. Waziri mwenye dhamana kwa ajili ya kusainiwa na kuanza kufanya kazi ukaguzi umepata shaka juu ya majibu hayo kutokana na barua hiyo kuwa na wastani wa miaka mitatu ya fedha bila ya kufanyiwa kazi na kuanza kutekeleza agizo la kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Uanzishwaji wa Wakala wa Matukio ya Kijamii Zanzibar.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Matukio ya Kijamii Zanzibar kuchukuwa jitihada za makusudi za kufuatilia utekelezaji wa barua niliyoinakili hapo juu kwa lengo la kuanza usaili wa wageni pamoja na uzalishaji wa vitambulisho maalum vya makaazi kwa mujibu wa sheria.

### 6.1.3.3 Manunuzi yaliyofanyika nje ya Mpango wa Manunuzi shilingi 81,939,033

Kwa mujibu wa kifungu nambari 42(7) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 inaeleza kwamba "kutakuwa na mapango wa manunuzi wa taasisi ambao manunuzi yake yatafuata mpango huo, hakuna manunuzi yatakayofanywa nje ya mpango huo, isipokuwa kwa kufanya manunuzi haraka na hali ya dharura".

Ukaguzi umebaini Wakala wa Matukio ya Kijamii imefanya manunuzi nje ya mpango wa manunuzi jambo ambalo ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria ya Manunuzi niliyoianisha hapo juu. Kufanya manunuzi kwa kutozingatia mpango wa manunuzi kunaweza kupelekea kuathiri utekelezaji wa bajeti na hatimae kutokufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Matukio ya Kijamii Zanzibar kuhakikisha unaandaa Mpango wa Manunuzi na kuuwasilisha kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali ili kupata idhini ya matumizi kwa mujibu wa sheria. Mchanganuo wa manunuzi hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 90: Manunuzi yaliyofanyika nje ya Mpango wa Manunuzi**

| Namba | Nambari ya Hati | Kiasi (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 44/11 ya 22/11/2022 | 10,290,000 | Zan IT Solution | Ununuzi wa kompyuta za afisi. |
| 2. | 15/11 ya 15/11/22 | 8,600,000 | ZECO | Ununuzi wa umeme kwa matumizi ya Afisi. |
| 3. | 1/10 ya 17/10/22 | 8,600,000 | ZECO | |
| 4. | 1/1 ya 12/1/2023 | 8,600,000 | ZECO | Ununuzi wa umeme kwa matumizi ya Afisi |
| 5. | 28/3 ya 23/3/2023 | 8,000,000 | ZECO | |
| 6. | 8/4 ya 14/4/2023 | 1,864,360 | ZECO | |
| 7. | 12/6 ya 16/6/23 | 8,000,000 | ZECO | |
| 8. | 13/6 ya 16/6/2023 | 2,784,673 | ZECO | |
| 9. | 19/5 ya 8/5 /2023 | 1,000,000 | ZECO | |
| 10. | 28/5 ya 19/5/2023 | 7,000,000 | ZECO | |
| 11. | 16/8 ya 3/8/2022 | 8,600,000 | ZECO | |
| 12. | 5/9 ya 14/9/2022 | 8,600,000 | ZECO | |
| **Jumla** | | **81,939,033** | | |

### 6.1.3.4 Malipo kwa watoa huduma ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma shilingi 177,132,000

Kifungu nambari 23(1) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kinaeleza kwamba "kulingana na masharti ya sheria hii mtu, kampuni au taasisi haitawasilisha zabuni au vyenginevyo kushiriki katika manunuzi ya Umma isipokua chombo kiwe kimesajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi. Aidha kifungu namba 23(2) kinafafanua kuwa zabuni kutoka kwa mtu, kampuni au chombo ambacho hakijasajiliwa haifai na hakitazingatiwa na taasisi ya ununuzi".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar imefanya malipo yenye jumla ya shilingi 177,132,000 kwa wafanyabiashara ambao hawajasajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma kama watoa huduma jambo ambalo ni kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na usajili huo, aidha ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kununua bidhaa au huduma kwa wafanyabiashara au watoa huduma waliosajiliwa na Mamlaka husika. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 91: Watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Manunuzi**

| Hati Namba | Hundi Namba | Aliyelipwa | Kiasi cha Fedha (Tsh.) | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 16/09/2022 | TISS | IRIS Co. ltd | 57,132,000 | Ununuzi wa TESLN papers. |
| 17/04/2023 | | | 120,000,000 | |
| **Jumla** | | | **177,132,000** | |

**AFISI YA WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII PEMBA**

### 6.1.3.5 Uwepo wa upungufu wa Watumishi

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wakala wa Matukio ya Kijamii Pemba ina upungufu wa watumishi muhimu ambao wangaliwezesha Wakala kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Upungufu huu unaathiri utendaji wa jumla wa Wakala ikiwa ni pamoja na utoaji duni wa huduma, mrundikano wa majukumu, na kupunguza hamasa ya utendaji kazi kwa watumishi waliopo.

Hali hii inaweza kupelekea ucheleweshwaji wa utoaji huduma kwa taasisi za umma na jamii kwa ujumla na pia inaweza kupelekea kuikosesha mapato Serikali.

Kutokupewa nafasi za uajiri kwa mujibu wa nafasi zilizowazi ni kwenda kinyume na kanuni nambari 6(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kulipa kipaombele suala la uajiri ili kupunguza changamoto za kiutendaji zinazoikabili taasisi husika. Mchanganuo wa upungufu wa watumishi ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 92: Upungufu wa Watumishi**

| Namba | Kada | Waliopo | Wanaohitajika | Tofauti |
|---|---|---|---|---|
| | Mtunza Ghala | 0 | 2 | 2 |
| | Afisa Masjala | 0 | 1 | 1 |
| | Muhudumu | 0 | 1 | 1 |
| | Wasaidizi Maafisa Usajili Wilaya ya Micheweni | 7 | 9 | 2 |
| | Wasaidizi Maafisa Usajili Wilaya ya Wete | 7 | 9 | 2 |
| **Jumla** | | **14** | **22** | **8** |

*Chanzo: Mpango wa Rasilimali watu wa Wakala*

#### 6.1.3.6 Uwepo wa ufinyu wa nafasi za kufanyia kazi

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Afisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii – Pemba haina nafasi ya kutosha kwa ajili ya watumishi wake hali iliyopelekea chumba kimoja kukaa watumishi wa kada tofauti jambo ambalo linaweza kupunguza hamasa na ari ya utendaji kazi kwa watumishi hao na hivyo Wakala kutokufanya kazi kwa ufanisi unaotarajiwa na pia uwepo wa uwezekano wa kuvuja kwa taarifa za siri za Wakala.

Aidha, ukaguzi umebaini kwamba mazingira ya utoaji wa huduma kwa wananchi katika Afisi ya Wakala Wilaya ya Wete hairidhishi kwani wananchi wanaokwenda kupatiwa huduma katika Afisi hiyo hawana sehemu nzuri ya kupatiwa huduma na hivyo kulazimika kuweka foleni nje ya Afisi katika dirisha dogo lililotengwa kwa ajili ya utoaji wa huduma ya vyeti vya kuzaliwa hali ambayo inapelekea wananchi kuwepo katika kipindi kigumu pindipo mvua ikinyesha au wakati wa jua kali.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 2 ya Utumishi wa Umma ya 2011.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Matukio ya Kijamii Pemba kuchukua jitihada za makusudi ili kuhakikisha kwamba Wakala inapata eneo la kutosha ili kuwaweka watumishi wake katika mazingira rafiki.

### 6.1.4 WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO

Ukaguzi wa hesabu za Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 6.1.4.1 Kutowasilishwa kwa Mpango wa Manunuzi katika Taasisi ya Mamlaka ya Manunuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma

Kifungu 42(1) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016 kinaitaka taasisi ya ununuzi kuandaa na kuwasilisha Mpango wake wa Manunuzi wa mwaka wa bajeti kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma katika tarehe itakayoelezwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali.

Ukaguzi umebaini kuwa Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo kwa mwaka wa bajeti 2022/2023 haijawasilisha Mpango wake wa Manunuzi katika Mamlaka ya Manunuzi na Uondoaji wa Mali za Umma kama Sheria Nambari ya Ununuzi na Uondoshaji wa mali za Umma ya 2016 inavyoelekeza. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu nilichokinakili hapo juu.

Kutowasilishwa kwa mpango wa manunuzi wa Wakala katika Mamlaka ya Manunuzi kutapelekea kufanya manunuzi ambayo hayajapata idhini za Mamlaka ya Manunuzi jambo ambalo litapelekea kufanya manunuzi kinyume na Sheria na Kanuni za Manunuzi.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala uhakikisha kuwa kitengo cha manunuzi kinafuata sheria na miongozo iliyowekwa kwa lengo la kufanikisha malengo waliyojiwekea.

### 6.1.4.2 Mapungufu yaliyobainika katika daftari linaloonyesha mienendo ya safari katika vyombo vya moto (log book)

Kanuni ya 124(2) ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya 2014 inaeleza kwamba "Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi atahakikisha vyombo vyote vinavyotumika katika Taasisi yake vinakuwa na buku linaloonyesha matumizi ya chombo kwa safari husika".

Ukaguzi umebaini kuwa Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo Zanzibar haijaandaa daftari maalum linaloonyesha mienendo ya safari ya vyombo hivyo hali inayopelekea kushindwa kujiridhisha juu ya matumizi ya mafuta yanayonunuliwa na kutumika jambo ambalo linapelekea kujitokeza kwa ugumu wa kujua muda sahihi wa kuweza kufanyiwa matengenezo ya chombo husika, aidha ni kwenda kinyume na kanuni niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo kuhakikisha unaanzisha daftari maalum (buku) la kurikodia mwenendo wa vyombo vya moto ili kuepusha hasara inayoweza kujitokeza kutokana na kuchelewa kufanyiwa matengenezo ya vyombo hivyo kwa kukosekana kwa taarifa ya mwenendo wa matumizi yao.

**WAKALA WA SERIKALI WA HUDUMA ZA MATREKTA NA ZANA ZA KILIMO PEMBA**

### 6.1.4.3 Uwepo wa Upungufu wa Watumishi

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo Pemba ina upungufu wa watumishi muhimu ambao wangaliwezesha Wakala kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Upungufu huu unaathiri utendaji wa jumla wa Wakala ikiwa ni pamoja na utoaji duni wa huduma, mrundikano wa majukumu, na kupunguza hamasa ya utendaji kazi kwa watumishi waliopo. Hali inayoweza kupelekea ucheleweshwaji wa utoaji huduma kwa taasisi za umma na jamii kwa ujumla na pia ni kuikosesha mapato Serikali.

Kutokufanya uajiri kwa mujibu wa nafasi zilizowazi ni kwenda kinyume na kanuni nambari 6(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kulipa kipaombele suala la uajiri ili kupunguza changamoto za kiutendaji zinazoikabili taasisi husika. Mchanganuo wa upungufu wa watumishi ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 93: Upungufu wa Watumishi**

| Namba | Kada | Waliopo | Wanaohitajika | Upungufu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Wahudumu | 1 | 4 | 3 |
| 2. | Mwangalizi | - | 1 | 1 |
| 3. | Msaidizi Afisa Manunuzi | - | 1 | 1 |
| **Jumla** | | **1** | **6** | **5** |

*Chanzo: Mpango wa Rasilimali Watu wa Wakala*

### 6.1.4.4 Kutokununuliwa likizo ya mtumishi aliyesitishwa kwenda likizo

Kwa mujibu wa kanuni ya 58 (1)(e) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inaeleza kwamba "Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi anaweza kumruhusu mtumishi wa umma aliezuiliwa likizo lake, kwenda likizo wakati wowote udhuru aliyozuiliwa utakapomalizika na kama miezi sita imepita tokea mtumishi huyo azuiliwe likizo lake na udhuru aliozuiliwa likizo hilo bado unaendelea, Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi anaweza kuinunua likizo hilo la mtumishi huyo kwa thamani ya mshahara wa mwezi mmoja bila ya posho".

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wakala wa Serikali wa Huduma za Matrekta na Zana za Kilimo Pemba imeshindwa kumpatia likizo Afisa Manunuzi kwa mwaka uliopita ambapo alistahiki kwenda likizo tarehe 07/10/2022 bila ya kuinunua likizo yake kama kanuni inavyoelekeza.

Kufanya hivyo inaweza kupelekea kupungua kwa ufanisi wa utendaji kwa mtumishi husika kutokana na kufanya kazi kwa muda mrefu bila ya kupumzika pamoja na kupungua ari na hamasa ya ufanyaji kazi kulikotokana na kutokupewa.

Kutokumpatia likizo mtumishi na kutokuinunua likizo hio ni kumnyima haki yake ya msingi na pia ni kwenda kinyume na kanuni ya Utumishi wa Umma niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala kufuata kikamilifu Sheria, Kanuni na Miongozo yote inayohusiana na utumishi wa umma ili kujenga mazingira mazuri baina ya uongozi na watumishi wao na kuongeza utendaji kazi kwa ufanisi ziadi.

### 6.1.5 WAKALA WA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI ZANZIBAR (ZFDA)

Ukaguzi wa hesabu za Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 6.1.5.1 Dosari katika ununuzi wa vifaa vya Maabara

Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar ilipangiwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 4.4 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya Maabara ikiwemo vifaa vya uchunguzi wa chakula, dawa, vipodozi na vifaa tiba ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imesaini hati ya makubaliano na Kampuni ya M/S Globe Cooperation & ESTEC yenye kumbukumbu nambari SMZ/H011/NCB/2022-2023/7/Lot/01 ya mwezi wa Aprili, 2023 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya Maabara kwa lot 1, na 5 kwa thamani ya Euro 803,803.16 na Lot namba 2, 6 na 7 kwa thamani ya USD 732,646.54.

Ukaguzi umebaini dosari zifuatazo:-

- Kukosekana kwa Mchanganuo wa Kifedha uliobainishwa katika kila mgawanyo wa kazi (Lot) zilizopangwa ambapo ni kwenda kinyume na kanuni ya 46 ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021.
- Kukosekana kwa ushindani wa bei ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 74(1) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.
- Kutokufuatwa kwa maagizo na maelekezo ya Mwanasheria Mkuu ambapo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 63(3) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.

Kutokana na dosari nilizozibainisha hapo juu ukaguzi umeshindwa kupata tathmini halisi juu ya mchakato wa ununuzi wa vifaa vya Maabara kwa kuzingatia thamani halisi ya fedha pamoja na upatikanaji wa tija iliyokusudiwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar kuhakikisha unazingatia na kutekeleza misingi ya kisheria iliyowekwa katika kufanya ununuzi wa huduma au bidhaa ili kuepuka kuingiza hasara Serikali pamoja na kutokufikiwa kwa malengo yaliyopangwa.

**WAKALA WA CHAKULA DAWA NA VIPODOZI PEMBA**

### 6.1.5.2 Uwepo wa Upungufu wa Watumishi

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi Pemba ina upungufu wa watumishi muhimu ambao wangaliwezesha Wakala kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Upungufu huu unaathiri utendaji wa jumla wa Wakala ikiwa ni pamoja na utoaji duni wa huduma, mrundikano wa majukumu, na kupunguza hamasa ya utendaji kazi kwa watumishi waliopo.

Hali inayoweza kupelekea ucheleweshwaji wa utoaji huduma kwa taasisi za umma na jamii kwa ujumla na pia ni kuikosesha mapato Serikali.

Kutokufanya uajiri kwa mujibu wa nafasi zilizowazi ni kwenda kinyume na kanuni nambari 6(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kulipa kipaombele suala la uajiri ili kupunguza changamoto za kiutendaji zinazoikabili taasisi husika. Mchanganuo wa upungufu wa watumishi ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 94: Upungufu wa Watumishi**

| Namba | Kada | Watumishi Waliopo | Watumishi Wanaohitajika | Upungufu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Katibu Muhtasi wa Mkurugenzi | 0 | 1 | 1 |
| 2. | Mtunza Ghala | 0 | 1 | 1 |
| 3. | Afisa Mipango | 0 | 1 | 1 |
| 4. | Mkaguzi wa Ndani | 0 | 1 | 1 |
| **Jumla** | | 0 | **4** | **4** |

*Chanzo: Mpango wa rasilimali watu*

### 6.1.5.3 Kukosekana kwa vibali vya bidhaa zinazoingizwa kupitia Bandari ya Wete

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba baadhi ya bidhaa zinazoingia kisiwani Pemba kupitia Bandari ya Wete ambazo hupakizwa katika magari yanayokuja na meli ya Seastar I kutokea Unguja hazina vibali vya ZFDA kwa ajili ya uthibitisho wa ukaguzi wa bidhaa hizo dhidi ya ubora wake. Aidha, ukaguzi umebaini kwamba watendaji katika kitengo cha uchunguzi hawana vifaa vya kutosha vya kukaguwa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje ya kisiwa cha Pemba.

Kutokukaguwa bidhaa inayoingizwa au inayotolewa ndani ya nchi inaweza kupelekea uingizwaji wa bidhaa mbovu na kusababisha athari kubwa kwa watumiaji pamoja na kuikosesha mapato Serikali.

Kukosekana kwa vibali vya bidhaa zinazoingizwa kisiwani Pemba na kutokukaguliwa bidhaa hizo ni kwenda kinyume na kifungu nambari 19(1)(d) cha Sheria nambari 2 ya Uanzishwaji wa Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi ya 2006.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Pemba kuhakikisha inafanya ukaguzi kwa bidhaa zote zinazoingizwa kwa ajili ya kulinda usalama wa watumiaji. Mchanganuo wa bidhaa zilizoingia kisiwani Pemba kupitia Bandari ya Wete na kukosa vibali vya ukaguzi ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 95: Bidhaa ambazo zimekosa Vibali vya Ukaguzi

| Namba | Tarehe | Namba ya Gari | Bidhaa Ambazo Zimekosa Kibali | Wakala |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 22/9/2023 | Z397 JW | Mchele 250 polo | Salum Nyuki |
| 2. | | Z396 JW | Dumu za mafuta 400 | |
| 3. | | Z400 JW | Unga 200 polo | |
| 4. | | Z403 JW | Sukari 200 polo | Juma Pwagu |
| 5. | | Z763 LH | Dumu za mafuta 400 | |
| 6. | | Z758 JW | Unga 200pkcts | |
| 7. | | Gari 3 | Mchele 250 polo na Sukari 200 polo | |
| 8. | 29/9/2023 | Gari 4 | Mchele 250 polo<br>Unga 200 polo | Juma Moh'd Abdallah |
| 9. | | Gari 1 | Box mchanganyiko. | Khamis Faki Omar |
| 10. | 6/10/2023 | Gari 3 | Sukari 200 polo na Mchele 250 polo | Salum Nyuki |
| 11. | | | Mchanganyiko food stuff | |
| 12. | 7/10/2023 | Gari 2 | Dumu za mafuta 400 | Abdalla Said Salum |
| 13. | | | Mchanganyiko food stuff | |
| 14. | 27/10/2023 | Gari 4 | Mchele 250 polo | Salum Abdallah Suba |
| 15. | | | Unga 200 polo | |
| 16. | | | Sukari 200 polo | |
| 17. | | | Mafuta dumu 400 | |
| 18. | 3/11/2023 | Gari 2 | Mchele 250 polo<br>Sukari 200 polo | Juma Moh'd |
| 19. | | Gari 3 | Food stuff mchanganyiko | Salum Nyuki |
| 20. | | | Mchele 250 polo | |
| 21. | | | Sukari 200 polo | |
| 22. | 4/11/2023 | Gari 1 | Chumvi 700 polo | Maryam Othman |
| 23. | | Gari 1 | Tomato paste 450 box | Juma Pwagu |
| 24. | 10/11/2023 | Gari 5 | | Salum Nyuki |
| 25. | | Gari 3 Z759 LH | | Salum Abdalla Suba |
| 26. | | Z763 LH | | |
| 27. | | Z394 JW | | |
| 28. | 17/11/2023 | Z239 JW | Mchele 200 polo | Juma Moh'd |
| 29. | | Z755 LH | Mchele 200 polo | |
| 30. | | Z763 LH | Unga 200 polo | Salum Suba |
| 31. | | Z762 LH | Mafuta 1000 dumu<br>Pampers 20 polo | Khelef Kassim |
| 32. | | Z396 JW | Sukari 100 polo<br>Mchele 250 polo | Salum Nyuki |
| 33. | | Z403 JW | Pampers 100 polo | Juma Moh'd |
| 34. | | Z398 JW | Mchele 250 polo | |
| 35. | 17/11/2023 | Z402 JW | | Salum Suba |
| 36. | | Z759 LH | Mchele 400polo | |
| 37. | | Z394 JW | | |

| Namba | Tarehe | Namba ya Gari | Bidhaa Ambazo Zimekosa Kibali | Wakala |
|---|---|---|---|---|
| 38. | 18/11/2023 | Z858 LV | Mchele 250 polo | Umea |
| 39. | | Z587 LV | Sukari 250 polo | |
| 40. | | T378 DZR | Mchele 250 polo | Salum Nyuki |
| 41. | | Z830 LP | Tomatoes 200 polo | |
| 42. | | T874 DAQ | Pempas 50 bxs<br>Buiscuites 10 bxs | |
| 43. | | Z985 DG | Unga ngano 250 polo | Hamid |
| 44. | | T366DZR | Unga ngano150 polo | |
| 45. | 24/11/2023 | Z756 LH | Mchele 400 polo | Juma Mohd |
| 46. | | Z755 LH | Mchele 400 polo | |
| 47. | | Z754 LH | Mchele 400 polo | |
| 48. | | Z395 JW | Mchele 200 polo | |
| 49. | | Z396 JW | Mchele 200 polo | |
| 50. | | Z757 LH | Mchele 400 polo | |
| 51. | | Z759 LH | Mchele 400 polo | |
| 52. | | Z400 JK | Mchele 200 polo | Juma Pwagu |
| 53. | | Z394 JW | Mchele 200 polo | Salum Suba |
| 54. | | Z763 LH | Unga 300 polo | |
| 55. | | Z762 LH | Mchele 400 polo | |
| 56. | | Z760 LH | Sukari 50 polo<br>Mchele 300 polo<br>Unga 50 polo | Salum Nyuki |

*Chanzo : Ukaguzi wa bidhaa na ZFDA POS billing system*

#### 6.1.5.4 Kukosekana kwa Maabara ya Vipimo vya Bidhaa

Miongoni mwa majukumu ya msingi ya Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi ni kukagua bidhaa zinazoingizwa kutoka nje ya Kisiwa cha Pemba na kufanya vipimo vya uchunguzi kwa bidhaa zitakazotiliwa shaka katika ubora wake.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi Pemba haina Maabara kwa ajili ya kuchunguza ubora wa chakula, dawa na vipodozi hali ambayo inapelekea sampuli ya bidhaa kusafirishwa kwenda makao makuu ya Wakala Unguja kwa ajili ya uchunguzi.

Kitendo cha kupeleka sampuli ya bidhaa Unguja kwa ajili ya kufanya uchunguzi kinapelekea kuongezeka kwa gharama za uendeshaji na hatimae kuchelewa kupatikana huduma ya chakula bora na salama kwa jamii.

Ukaguzi unaishauri Serikali kuandaa mpango wa dharura wa kujenga Maabara ya Kisasa kwa ajili ya Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi Pemba ili kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kutoa huduma bora kwa wananchi.

### 6.1.6 WAKALA WA MAJENGO ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Wakala wa Majengo Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

### 6.1.6.1 Kutonunuliwa kwa vifaa vya ujenzi vyenye thamani ya shilingi 11,580,000

Ukaguzi umefanya mapitio ya makubaliano ya mkataba wenye kumbukumbu namba SMZ /NO1/W/DP/2002/2003/01 uliosainiwa mwezi wa Febuari, 2023 baina ya M/S KMKM marine Engineering and General Trading Co.ltd na Wakala wa Majengo Zanzibar kwa ajili ya ukarabati wa jengo la Afisi ya Wakala wa Majengo lililopo Amani.

Kutokana na mapitio ya mchanganuo wa bei (BOQ) ilibainisha uwepo wa vifaa mbali mbali ambavyo vilipaswa kununuliwa na kutumika kwa ajili ya ukarabati wa jengo hilo, dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokununuliwa na kutumika kwa baadhi ya vifaa vilivyobainishwa katika (BOQ) jambo ambalo limetia shaka juu ya uhalali wa makisio ya gharama ya ukarabati wa ujenzi yaliyoainishwa na hatimae kutokujulikana kwa matumizi halisi ya fedha iliyotumika kwa ajili ya ukarabati uliofanyika.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Majengo ya Serikali kuongeza umakini katika ukadiriaji wa vifaa ili kuepusha kujitokeza kwa makadirio madogo au makadirio makubwa ambayo hayaendani na uhalisia na hatimae kupelekea kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma. Mchanganuo wa vifaa na gharama ya fedha iliyokuwa haikutumika kununulia mahitaji hayo ni kama ilivyobainishwa katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 96: Vifaa ambavyo havijanunuliwa na havikutumika katika ujenzi**

| Namba | Aina ya bidhaa | Kiwango | Kiasi kwa kila moja (Tsh.) | Jumla kwa BOQ (Tsh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | **Element No. 4 "Door"**<br>(b) Hardwood; Mkongo including 6mm thick glazing for top. | 5 | 750,000 | 3,750,000 |
| 2. | **Element, No. 8 "Fitting and funiture"** | | | |
| 3. | Office Table for one person | 1 | 675,000 | 675,000 |
| 4. | Supply and fix revolving type office chairs with black/grey fabric backing | 2 | 375,000 | 750,000 |
| 5. | Supply and fix type guest chair with black /grey | 1 | 630,000 | 630,000 |
| 6. | Supply and fix type meeting chair with black /grey | 5 | 600,000 | 3,000,000 |
| 7. | Supply and fix steel cabinet including drawer with password locks Dubai quantity or equal | 1 | 1,125,000 | 1,125,000 |
| 8. | Supply and fix table for meeting room 14 people | 1 | 600,000 | 600,000 |
| 9. | Supply and fix office steel cabinet including drawer steel filing cabinet Dubai quantity or equal | 2 | 375,000 | 700,000 |
| 10. | Supply and fix steel waiting chair | 1 | 300,000 | 300,000 |
| **Jumla** | | | | **11,850,000** |

### 6.1.6.2 Malimbikizo ya Madeni ya muda mrefu shilingi 1,703,907,400

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wakala wa Majengo Zanzibar inazidai Taasisi mbali mbali za Serikali kutokana na huduma iliyozitoa zenye thamani ya shilingi 1,703,907,400.

Uwepo wa madeni ya muda mrefu katika Taasisi za Umma yanayodaiwa kutokana na huduma iliyotolewa yanatoa kiashiria cha kwamba Afisa Mhasibu wa Taasisi za Umma ameshindwa kusimamia ulipwaji wa madeni hayo kwa wakati kutokana na kukosekana kwa sera au muongozo wa ulipwaji wa madeni kwa taasisi za umma.

Kutokulipa madeni kwa wakati kunawakatisha tamaa watoa huduma na wasambazaji wa bidhaa na kunaweza kusababisha washindwe kutoa huduma kwa ufanisi jambo ambalo linaweza kupelekea kudumaza mahusiano mema ya kiutendaji baina ya taasisi za Serikali.

Kutokulipwa madeni kwa wakati ni kwenda kinyume na kifungu nambari 29(1)(b) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016.

Ukaguzi unawashauri Maafisa Masuuli wa Taasisi za Umma kuchukuwa juhudi za makusudi kuhakikisha kwamba kunakuwa na sera ya usimamizi wa madeni ili kuepukana na uwepo wa madeni makubwa ambayo hayatoweza kulipika. Aidha, ukaguzi unaishauri Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali (PAC) kuwakutanisha viongozi Wakuu wa Taasisi zinazodaiwa ili kujadili mustakbali wa urudishwaji wa madeni yanayodaiwa kwa lengo la kuiwezesha Wakala wa Majengo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Mchanganuo wa malimbikizo ya madeni ya muda mrefu ni kama yanavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 97: Malimbikizo ya Madeni ya Muda Mrefu

| Namba | Jina la Mdaiwa | Kiasi cha Deni (Tshs) |
|---|---|---|
| **Taasisi za Unguja zinazodaiwa** | | |
| 1. | Bohari Dawa Maruhubi | 20,500,000 |
| 2. | Vyuo vya Amali Makunduchi | 132,000,00 |
| 3. | Afisi ya Utumishi na Utawala Bora, Chuo cha Sheria | 26,590,000 |
| 4. | Jeingo la kulelea watoto Mazizini | 18,000,000 |
| 5. | Idara ya Uhamiaji Mazizini | 88,032,500 |
| 6. | Idara ya Uhamiaji Kivunge | 11,623,000 |
| 7. | ZSTC Gulioni | 4,000,000 |
| 8. | Afisi ya kazi na Uwekazaji - Migombani | 4,500,000 |
| 9. | Jengo la Udhibiti ya Madawa ya Kulevya – Kidimni | 65,000,000 |
| 10. | Ukarabati wa jengo la Mufti la Mazizini | 19,200,000 |
| 11. | Ujenzi wa Mabaara Binguni | 31,395,000 |
| 12. | Ujenzi wa jengo la ZBS | 27,000,000 |
| 13. | ZRA utiaji rangi Mazizini | 4,500,000 |
| 14. | ZRA undaaji wa BOQ ya utiaji rangi – Mazizini | 800,000 |
| 15. | TRA drawing ya Karume Airport Custom Office | 34,500,000 |
| 16. | Soko la Chuini | 100,000,000 |
| 17. | Soko la Jumbi | 80,000,000 |
| 18. | Soko la Kwerekwe | 150,000,000 |
| 19. | Hospitali ya Chake Chake | 36,721,600 |
| 20. | Ukarabati wa nyumba ya Uhamiaji Mkoa Kaskazini Pemba | 7,000,000 |
| 21. | Utiaji rangi nyumba za - Tibirinzi | 5,523,000 |
| 22. | Utiaji rangi nyumba za Mkoani | 4,500,000 |
| | **Jumla Ndogo** | **739,517,100** |
| **Taasisi za Pemba zinazodaiwa** | | |
| 23. | Ujenzi wa soko la wajasiriamali Wilaya ya Micheweni | 144,000,000 |
| 24. | Wajasiriamali Kifumbi Kai Wete | 171,000,000 |
| 25. | Wajasiriamali Michakaini – Chake Chake | 150,300,00 |

| | | |
|---|---|---|
| 26. | Wajasiria mali Kipitacho – Mkoani | 150,300,000 |
| 27. | Ujenzi wa soko Macho mane | 92,700,000 |
| 28. | Ujenzi wa stand kinowe – micheweni | 93,870,000 |
| 29. | Ujenzi wa gardeni Mwana mashungi | 125,100,000 |
| 30. | Ujenzi wa soko Mtambile | 52,380,000 |
| | **Jumla Ndogo** | **829,500,300** |
| | **AFISI YA RAIS – TAMISEMI** | |
| 31. | Ujenzi wa Afisi na Maakazi Wilaya ya Mkoani | 94,500,000 |
| 32. | Ukarabati wa jengo lililopo Madungu | 18,900,000 |
| 33. | Ukarabati wa nyumba iliyopo fletini, Machomanne – Chake Chake | 8,160,000 |
| | **Jumla Ndogo** | **121,560,000** |
| | **Jumla Kuu** | **1,690,577,400** |

Aidha, pamoja na uwepo wa madeni yanayodaiwa kutokana na huduma iliyotolewa kwa taasisi za umma ukaguzi umebaini uwepo wa madeni mengineyo yanayotokana na baadhi ya taasisi au wananchi kuishi katika majengo yanayomilikiwa na Wakala wa Majengo Zanzibar kinyume na makubaliano ya mikataba jambo ambalo limepelekea uwepo wa baadhi ya nyumba kukaliwa bila ya uwepo wa mikataba halali na baadhi yake kuwa na madeni endelevu. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 98: Majengo ya Wakala yanayokaliwa bila ya Malipo

| Namba | Nyumba Namba | Mtaa iliyopo | Alipangishwa | Deni Analodaiwa (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | SH/KX/54J | Mazizini | Abdalla Zubeir Marzuk | 1,100,000 |
| 2. | SH/KS/ 50M | Mazizini | Riziki Yussuf Haji | 400,000 |
| 3. | - | Saateni | Jumuiya ya Changamoto | 1,200,000 |
| 4. | - | Makunduchi | Makame Mshimba Mbarouk | 7,000,000 |
| 5. | | Saateni | Hassan Khamis Burhan | 3,300,000 |
| 6. | SH/KS/29M | Mazizini | Nassir Ahmed Abdul-razk | 330,000 |
| 7. | 2302C | Vuga | Muhamed H. Ismail | Hana mkataba |
| 8. | S.49 | Mazizini | Zainab Ahmada Salum | Haina mkataba |
| 9. | 026/KS/MZ/61 | Mazizini | Salum muhisin Malik | Hana mkataba |
| 10. | SH/KS47AM | Mazizini | Ramadhani Ali Kimara | Hana mkataba |
| 11. | SH/KS/23M | Mazizini | Mussa Mohammed Mussa | Hana mkataba |
| 12. | SH/KS/28 | Mazizini | Abdalla Suleiman Said | Hana mkataba |
| | | **Jumla** | | **13,330,000** |

**WAKALA WA MAJENGO PEMBA**

### 6.1.6.3 Malimbikizo ya deni litokanalo na ukodishaji wa nyumba shilingi 49,725,000

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba jumla ya shilingi 49,725,000 ni fedha za malimbikizo ya mapato zinazotokana na huduma ya ukodishaji wa nyumba za kuishi zilizo chini ya usimamizi wa Wakala wa Majengo Pemba kwa wananchi na Taasisi za umma lakini fedha hizo hazijalipwa kwa kipindi kirefu na kubakia kama deni. Hali hii inapelekea Wakala kutokufikia malengo yake iliyojiwekea na pia ni kuikosesha Serikali mapato ambayo yangeliweza kutumika kwa shughuli za maendeleo na kuboresha huduma za kijamii.

Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala kuhakikisha kwamba wanaweka sera madhubuti za ufuatiliaji wa madeni yanayotokana na kodi za nyumba ikiwa ni pamoja na kuimarisha vipengele vya mikataba ili kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa wakati. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama unavyoonekana katika jadwali hapo chini:-

**Jadweli Nambari 99: Malimbikizo ya Deni la Ukodishaji wa Nyumba**

| Wilaya | Jina la Mpangaji | Nambari ya Nyumba | Mahali Ilipo | Kodi kwa Mwezi | Jumla ya Deni |
|---|---|---|---|---|---|
| Wete | Kamanda wa KMKM | SMZ – 5 | Uzunguni | 60,000 | 3,360,000 |
| | Wizara ya Afya 2 | SMZ - 9B | | 50,000 | 2,800,000 |
| | Mrajis wa Mahkama 2 | SMZ - 9A | | 50,000 | 2,750,000 |
| | Raya Mkoko Hassan | SMZ - 8 A | | 25,000 | 75,000 |
| | Wizara ya Afya 3 | SMZ - 9D | | 50,000 | 2,800,000 |
| | Wizara ya Afya 4 | SMZ - 10A | Vuga | 60,000 | 3,360,000 |
| | Wizara ya Afya 5 | SMZ - 10B | | 60,000 | 3,360,000 |
| | Wizara ya Afya 7 | SMZ - 10D | | 60,000 | 3,360,000 |
| | Wizara ya Afya 6 | SMZ - 10C | | 60,000 | 3,360,000 |
| | Wizara ya Afya 8 | SMZ - 10E | | 60,000 | 3,360,000 |
| | Wizara ya Afya 9 | SMZ - 10F | | 60,000 | 3,360,000 |
| **Jumla ya Deni Wilaya ya Wete (A)** | | | | | **31,945,000** |
| Chake Chake | Wizara ya Afya 13 | SMZ - 5 | Tenis Court | 60,000 | 3,360,000 |
| | Wizara ya Afya 18 | SMZ - 7 | | 60,000 | 3,360,000 |
| | Wizara ya Afya 14 | SMZ - 6 | | 60,000 | 3,360,000 |
| | Wizara ya Afya 16 | SMZ - 11 | Madungu | 60,000 | 3,360,000 |
| | Wizara ya Afya 17 | SMZ - 12 | | 60,000 | 3,360,000 |
| | Tabia Issa Mselem | SMZ – 9 | | 60,000 | 980,000 |
| **Jumla ya Deni Wilaya ya Chake (B)** | | | | | **17,780,000** |
| **Jumla Kuu (A+B)** | | | | | **49,725,000** |

*Chanzo: Taarifa kutoka kitengo cha fedha*

### 6.1.6.4 Ukosefu wa usafiri katika utekelezaji wa kazi za Wakala

Wakala wa Majengo Pemba inajukumu la kutoa ushauri elekezi, kukarabati na kujenga majengo kwa Taasisi za Umma na binafsi kwa lengo la kuongeza pato la taasisi na Serikali kwa ujumla.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wakala wa Majengo Pemba haina gari kwa ajili ya kusafirishia vifaa vya ujenzi kutoka sehemu moja kwenda nyengine hali ambayo inapelekea Wakala kukodi gari kwa gharama kubwa ili kuweza kufanikisha utekelezaji wa kazi ilizojipangia.

Kukosekana kwa usafiri wa gari ya kubebea vifaa kunapelekea Wakala kushindwa kufanya kazi zake kwa ufanisi na pia kuongeza gharama za uendeshaji, jambo ambalo ni kwenda kinyume na Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Majengo Pemba kuhakikisha wanatenga fedha za ununuzi wa gari katika bajeti zao za mwaka.

### 6.1.6.5 Kutokuuzwa au Kufanyiwa Matengenezo Kwa Vyombo Chakavu

Kwa mujibu wa kifungu nambari 66 cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba Kutakuwa na mpango wa matengenezo wa mali utakaoandaliwa na Taasisi ya Umma unaohakikisha kwamba mali zinabaki katika ubora kwa matumizi yaliyokusudiwa. Aidha, kifungu cha 69(1)(2) kinaeleza kuwa Kutakuwa na mpango wa uondoaji wa mali wa mwaka utakaoandaliwa na kila Taasisi ya umma na kuwasilishwa katika Afisi ya Msajili wa Hazina. Taasisi ya Umma itaomba ruhusa kutoka katika Ofisi kwa ajili ya kuondoa mali za Umma.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wakala wa Majengo ya Serikali – Pemba inamiliki gari aina ya Canter Ton 1.5 yenye namba za usajili SMZ 124B ambayo ni mbovu na ipo gereji kwa muda mrefu sasa bila ya kutengenezwa au kuuzwa pamoja na vespa star SMZ 258C ambayo haijafanyiwa matengenezo kwa muda mrefu sasa hivyo kushindwa kutumika na kuleta tija kama ilivyokusudiwa. Hali hii inaweza kupelekea vyombo hivyo kushuka thamani jambo ambalo linaweza kupelekea Serikali kushindwa kunufaika navyo wakati ingeweza kunufaika iwapo Wakala ingeamua kuvifanyia matengenezo au kuviondoa mapema inavyowezekana.

Kutokuuzwa au Kufanyiwa Matengenezo kwa vyombo chakavu ni kwenda kinyume na vifungu nambari 66 na 69(1)(2) vya Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala kuhakikisha wanaweka mpango mzuri wa matumizi ya mali zake ikiwa ni pamoja na mali zilizochakaa au kuharibika kwa muda mrefu kuziombea ruhusa kutoka Afisi ya Msajili wa Hazina kwa ajili ya kuuzwa.

### 6.1.6.6 Kutokupasishwa kwa Vyombo vya Usafiri

Kwa mujibu wa kanuni 124(5) ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2014, Mkuu wa Taasisi anatakiwa kuhakikisha kuwa vyombo vya usafiri vya Serikali vilivyo chini ya mamlaka yake vinapasishwa na kukatiwa bima.

Ukaguzi umebaini kuwa Afisi ya Wakala wa Majengo Pemba inamiliki vyombo mbalimbali vya usafiri ikiwemo gari, piki piki na vespa ambapo vyombo hivyo vyote vinatumika bila ya kupasishwa na Mamlaka husika. Hali hii imetokana na Afisi ya Wakala kuwa na uwelewa mdogo juu ya Utaratibu wa matumizi wa vyombo vya Serikali. Pamoja na uwelewa mdogo wa kanuni za utumishi wa Umma

Kutokuvipasisha vyombo vya usafiri kunaweza kuiweka Wakala kwenye hatari ya kupata hasara kubwa pale vyombo hivyo vinapopata ajali na pia ni kwenda kinyume na kanuni ya 124(5) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Majengo Pemba kufuata Sheria na Kanuni kikamilifu. Mchanganuo wa vyombo hivyo ni kama unavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

**Jadweli Nambari 100: Vyombo vya usafiri ambavyo havijapasishwa**

| Namba | Aina ya Chombo | Namba ya Chombo |
|---|---|---|
| 1. | Gari | SMZ 631 B |
| 2. | Pikipiki | SMZ 1594c |
| 3. | | SMZ 1768C |
| 4. | Vespa | SMZ 258C |

### 6.1.7 WAKALA WA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI

Ukaguzi wa hesabu za Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**WAKALA WA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI PEMBA**

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 6.1.7.1 Ufinyu wa Nafasi Katika Afisi ya Wakala

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Pemba ina ufinyu wa nafasi za kufanyia kazi ambapo watumishi wa Idara ya Kemikali na Mazingira, Idara ya Sayansi ya Makosa ya Jinai na Vinasaba, pamoja na Idara ya Udhibiti Ubora na Viwango wanatumia ofisi moja kwa ajili ya kutelekeza majumu yao ya kila siku hali ambayo inaweza kuzorotesha na kupunguza ufanisi wa kazi za Wakala. Hali hii inaweka uwezekano wa kuvuja kwa taarifa za siri za Wakala.

Kukosekana kwa nafasi ya kutosha ya kufanyia kazi katika Afisi ya Wakala ni kwenda kinyume na Sheria nambari 11 ya Ajira ya 2005 pamoja na Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Pemba kuhakikisha wanachukuwa jitihada za makusudi katika kuwatafutia watendaji wake sehemu nyengine iliyo sahihi, salama na inayoweza kuwatosha kwa ajili ya kufanya kazi zao za kila siku ili kuleta ufanisi mzuri.

#### 6.1.7.2 Kushindwa kukusanya deni la muda mrefu shilingi 35,730,000

Ukaguzi umebaini kwamba Afisi ya Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali - Pemba, inazidai Afisi za Jeshi la Polisi za Mkoa wa Kaskazini na Kusini Pemba pamoja na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya jumla ya shillingi 35,730,000 kutokana na kuwapatiwa huduma ya uchunguzi wa sampuli, DNA na madawa ya kulevya ambapo deni hilo limeanzia tokea mwaka 2013.

Hadi ukaguzi huu unakamilika deni hilo bado halijakusanywa licha ya Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuchukua hatua ya kuwaandikia barua wadaiwa hao ya kuwaomba kulipa madeni yao. Wakala ilitoa barua tarehe 15/8/2023 kwenda kwa Jeshi la Polisi Mkoa wa Kaskazini Pemba na barua ya tarehe 30/8/2023 kwenda kwa Jeshi la Polisi Mkoa wa Kusini Pemba pamoja na barua ya tarehe 15/8/2023 kwenda kwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Madawa ya Kulevya Pemba.

Pamoja na uwepo wa jitihada zilizochukuliwa za kuwapatia barua za madeni wahusika hao hadi ukaguzi unakamilika hakukuwa na dalili za ulipwaji wa deni husika.

Ukaguzi unaishauri Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali ya Baraza la Wawakilishi kufanya kikao cha pamoja cha kuzikutanisha Taasisi hizo ili kupatikana muafaka wa kufanyika malipo yanayodaiwa kwa muda mrefu.

Mchanganuo wa deni hilo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 101: Deni Ambalo Halijakusanywa kwa Kipindi Kirefu

| Namba | Mwaka | Deni la Polisi Mkoa Kusini Pemba | Deni la Polisi Mkoa Kaskazini Pemba | Mamlaka ya kudhibiti na kupambana na madawa ya kulevya Pemba | Jumla (Tsh) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 2013 | 690,000 | 870,000 | - | 1,560,000 |
| 2. | 2014 | 660,000 | 810,000 | - | 1,470,000 |
| 3. | 2015 | 870,000 | 1,050,000 | - | 1,920,000 |
| 4. | 2016 | 1,260,000 | 840,000 | - | 2,100,000 |
| 5. | 2017 | 3,510,000 | 2,070,000 | - | 5,580,000 |
| 6. | 2018 | 2,790,000 | 1,920,000 | - | 4,710,000 |
| 7. | 2019 | 2,370,000 | 1,020,000 | - | 3,390,000 |
| 8. | 2020 | 3,130,000 | 450,000 | - | 3,580,000 |
| 9. | 2021 | 3,520,000 | 1,380,000 | - | 4,900,000 |
| 10. | 2022 | 930,000 | 510,000 | - | 1,440,000 |
| 11. | 2023 | 2,500,000 | 1,200,000 | - | 3,700,000 |
| 12. | 2023 | - | - | 1,380,000 | 1,380,000 |
| **Jumla** | | **22,230,000** | **12,120,000** | **1,380,000** | **35,730,000** |

*Chanzo: Orodha ya madeni kutoka kitengo cha fedha*

### 6.1.8 WAKALA WA KARAKANA KUU YA MAGARI ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 6.1.8.1 Dosari katika utayarishaji wa Hesabu za Mwisho wa mwaka

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ukaguzi umepitia taarifa za fedha zilizotayarishwa na kuwasilishwa na Wakala na kubaini uwepo wa dosari mbali mbali ambazo zimepelekea kutokuonyesha sura sahihi na halisi ya hesabu zilizowasilishwa.

Miongoni mwa dosari hizo ni kama zifuatavyo:

- Kutokubainishwa kwa mishahara yenye jumla ya shilingi 1,030,189,053 katika hesabu za mwisho wa mwaka ambapo ni kwenda kinyume na muongozo wa ufungaji wa hesabu kwa taasisi za Umma kipengelea namba 1.7 (IPSAS)
- Kutokuwasilishwa kwa taarifa ya hesabu kwa ajili ya kupitiwa na kutolewa maoni kwa kamati ya ukaguzi na kitengo cha ukaguzi wa ndani ili kuweza kubainishwa dosari zilizopo kabla ya kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi. Jambo ambalo ni kwenda kinyume na kanuni ya 149(1)(m) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021.
- Kujitokeza kwa upotoshwaji wa taarifa za salio la hesabu ya mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo jumla ya shilingi 68,120,326 zilibainika kuwa ni salio anzia kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na sio shilingi 77,121,256 zilizoripotiwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 jambo ambalo ni kwenda kinyume na miongozo ya ufungaji wa hesabu IPSAS Cash Basis 1.3.27 pamoja na kanuni ya 127 ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Karakana Kuu ya Magari kuhakikisha unafuata miongozo ya ufungaji na utayarishaji wa hesabu za mwisho wa mwaka ikiwemo kuziwasilisha hesabu hizo kwa mkaguzi wa ndani kwa lengo la kuzipitia na kuzitolea ushauri kabla ya kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi ili kuepusha kujitokeza kwa dosari nyingi wakati wa ukaguzi.

#### 6.1.8.2 Kukosekana kwa makadirio ya mapato ya shilingi 55,340,658

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ukaguzi umefanya mapitio ya taarifa za fedha za mapato na matumizi kwa lengo la kupima ufanisi wa ukusanyaji wa mapato unaotokana na vyanzo mbali mbali vya kibajeti. Kutokana na tathmini iliyofanyika imebainika kutokukadiriwa kwa mapato kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na kubainishwa katika hesabu za mwisho wa mwaka jambo ambalo ukaguzi umetia shaka juu ya usahihi wa mapato ya shilingi 55,340,658 yaliyobainishwa katika taarifa ya hesabu ya mwisho wa mwaka ambayo hayakukadiriwa kwa mujibu wa utaratibu wa ufungaji wa hesabu.

Kutokana na dosari hiyo ukaguzi umeshindwa kutathmini hali halisi ya makusanyo kupitia makadirio ambayo hayakuanishwa mwanzoni mwa mwaka wa fedha 2022/2023 jambo ambalo ni kwenda kinyume na kanuni ya 28(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Karakana Kuu ya Magari kuweka makadirio ya mapato ili kuweza kupima na kutathmini uwezo wa ukusanyaji wa mapato kupitia vyanzo vya mapato vilivyobainishwa na Wakala wa Karakana Kuu ya Magari.

#### 6.1.8.3 Dosari katika uwasilishaji wa taarifa za fedha shilingi 12,066,650

Ukaguzi ulifanya mapitio ya taarifa za fedha za Wakala wa Karakana Kuu ya Magari zitokanazo na ruzuku inayopokelewa kwa kipindi cha Julai, 2022 hadi Juni, 2023 na kubaini jumla ya shilingi 357,904,600 zimepokelewa ikiwa ni ruzuku ya uendeshaji wa shughuli zilizopangwa na Karakana Kuu ya Magari.

Katika taarifa za hesabu za Wakala zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi zimebainisha jumla ya shilingi 369,971,250 ni fedha iliyopokewa kwa ajili ya matumizi ya shughuli za uendeshaji zilizopangwa na kupelekea uwepo wa tofauti ya shilingi 12,066,650 jambo ambalo linapelekea kutokuonesha sura sahihi na halisi ya taarifa za hesabu zilizowasilishwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Karakana Kuu ya Magari kuongeza umakini katika uandaaji na utayarishaji wa taarifa za hesabu ili kuweza kuakisi miongozo ya kitaifa na kimataifa.

**WAKALA WA KARAKANA KUU YA MAGARI PEMBA**

#### 6.1.8.4 Ukosefu wa mafundi wenye taaluma ya kutosha

Miongoni mwa majukumu ya Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Pemba ni kutoa huduma bora ya matengenezo ya magari ya Serikali na wananchi kwa ujumla.

Ukaguzi uliofanyika umebaini kwamba Wakala inatoa huduma ya matengenezo ya magari bila ya kuwepo mafundi wenye taaluma ya kutosha wa maswala ya mashine za magari na badala yake inatumia mafundi ambao hutumia uzoefu pekee hivyo kukosa uweledi katika kutekeleza majukumu yao.

Kukosekana kwa mafundi wenye taalumu ya kutosha kumepelekea Taasisi za Serikali, Taasisi binafsi pamoja na wananchi kwa ujumla kushindwa kupeleka gari zao katika Wakala wa Karakana Kuu ya Magari kwa ajili ya kufanyiwa matengenezo jambo ambalo linapelekea kuikosesha mapato Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Karakana kufanya jitihada za kuwasomesha mafundi waliopo pia kuajiri mafundi wenye taaluma ya kutosha. Hali halisi ya mafundi waliopo Karakana Kuu ya Magari Pemba pamoja na taaluma zao ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 102: Mafundi wa Karakana pamoja na taaluma zao**

| Namba | Jina la Fundi | Kiwango cha Elimu | Fani Aliyosomea |
|---|---|---|---|
| 1. | Amir Juma Hassan | Cheti | Machenics |
| 2. | Saleh Moh'd Ali | | |
| 3. | Omar Hamad Hamad | | |
| 4. | Abdulhamid Ahmed | | Machenics/ umeme |
| 5. | Hafidh Faki Kombo | Uzoefu | - |
| 6. | Sharif Ali Othman | | |
| 7. | Khamis Hamad Salim | | |
| 8. | Chande Kombo Chande | | |

### 6.1.8.5 Uwepo wa Upungufu wa Watumishi

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Pemba ina upungufu wa watumishi muhimu ambao wangaliwezesha Wakala kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Upungufu huu unaathiri utendaji wa jumla wa Wakala ikiwa ni pamoja na utoaji duni wa huduma, mrundikano wa majukumu, na kupunguza hamasa ya utendaji kazi kwa watumishi waliopo. Hali inayoweza kupelekea ucheleweshwaji wa utoaji huduma kwa taasisi za umma na jamii kwa ujumla na pia ni kuikosesha mapato Serikali.

Kutokufanya uajiri kwa mujibu wa nafasi zilizowazi ni kwenda kinyume na kanuni nambari 6(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kulipa kipaombele suala la uajiri ili kupunguza changamoto za kiutendaji zinazoikabili taasisi husika. Mchanganuo wa upungufu wa watumishi ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 103: Upungufu wa Watumishi**

| Namba | Kada | Waliopo | Wanaohitajika | Upungufu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Afisa Masoko | 0 | 1 | 1 |
| 2. | Engineer | 0 | 1 | 1 |
| 3. | Mwangalizi | 0 | 1 | 1 |
| 4. | Mshika Fedha | 0 | 1 | 1 |
| 5. | Secretary | 0 | 1 | 1 |
| 6. | Walinzi | 0 | 2 | 2 |
| **Jumla** | | **0** | **7** | **7** |

*Chanzo: Mpango wa Rasilimali Watu*

#### 6.1.8.6 Kutokuuzwa au Kufanyiwa Matengenezo kwa Gari Chakavu

Kwa mujibu wa kifungu nambari 66 cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba Kutakuwa na mpango wa matengenezo wa mali utakaoandaliwa na Taasisi ya Umma unaohakikisha kwamba mali zinabaki katika ubora kwa matumizi yaliyokusudiwa. Aidha kifungu cha 69(1)(2) kinaeleza kuwa Kutakuwa na mpango wa uondoaji wa mali wa mwaka utakaoandaliwa na kila taasisi ya umma na kuwasilishwa katika Ofisi ya Msajili wa Hazina. Taasisi ya Umma itaomba ruhusa kutoka katika Ofisi kwa ajili ya kuondoa mali za Umma.

Ukaguzi umebaini kuwa Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Pemba inamiliki gari aina ya Toyota Prado yenye namba za usajili SLS 137A ambayo ipo maeneo ya Afisi Kuu ya Wakala wa Karakana Tibirinzi Wilaya ya Chake Chake Pemba, gari hii haitumiki kwa muda mrefu sasa bila kufanyiwa matengenezo au kuiondoa kama inavyotakiwa na sheria. Hali hii inaweza kupelekea gari hii kushuka thamani hivyo Serikali kushindwa kunufaika nayo wakati ingeweza kunufaika iwapo Wakala ingeamua kuifanyia matengenezo au kuiondoa mapema inavyowezekana.

Kutokuuzwa au kufanyiwa matengenezo kwa mali chakavu ni kwenda kinyume na vifungu vya Sheria nilivyovinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala kuhakikisha wanaweka mpango mzuri wa matumizi wa mali zake ikiwa ni pamoja na mali zilizochakaa au kuharibika kwa muda mrefu kuziombea ruhusa kutoka Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa ajili ya kuuzwa.

#### 6.1.8.7 Kukosekana kwa kitengo cha unyooshaji, upigaji rangi na usafishaji wa magari

Kwa mujibu wa Sheria ya Uanzishwaji wa Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar ya mwaka 2019, miongoni mwa malengo yake makuu ni pamoja na kutoa huduma bora za matengenezo ya vyombo vya moto, huduma nyenginezo zinazoendana na vyombo vya moto pamoja na ushauri elekezi kwa madhumuni ya kuingizia Serikali mapato.

Ukaguzi umebaini kwamba hadi sasa Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Pemba, haijaanzisha Kitengo cha Unyooshaji na Upigaji Rangi wa Magari wala kuanzisha huduma ya kuwosha magari hali inayoweza kuondoa dhana halisi ya kuwa Karakana Kuu ya utengenezaji wa Magari Pemba na pia ni kuikosesha mapato Serikali.

Kutokufanya shughuli zote zinazoendana na utengenezaji wa magari ni kwenda kinyume na Sheria ya Uanzishwaji Wakala wa Karakana ya Magari ya Serikali ya 2019.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Karakana Kuu ya Magari Pemba kufanya jitihada za makusudi zitakozowezesha kuanzisha vitengo vyote muhimu vinavyohusiana na ufundi wa magari.

#### 6.1.8.8 Kutokutayarishwa kwa Mpango wa Matengenezo wa Mali

Kifungu namba 66 cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaeleza kwamba kutakuwa na mpango wa matengenezo wa mali utakaoandaliwa na Taasisi ya Umma unaohakikisha kwamba mali zinabaki katika ubora kwa matumizi yaliyokusudiwa. Kitengo cha usimamizi wa mali kitatoa taarifa kwa maandishi kwa Afisa Masuuli kuhusiana na hali ya utekelezaji wa mpango wa matengenezo wa Mwaka. Taasisi ya umma itatenga fedha katika bajeti yake kwa ajili ya utekelezaji bora wa mpango wa matengenezo wa mwaka.

Ukaguzi umebaini kwamba Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Pemba haina utaratibu wa kutayarisha mpango rasmi wa matengenezo wa mali zilizo chini ya umiliki wake hali iliyosababisha baadhi ya mali inazozimiliki ikiwemo jengo linalotumika kwa kutengenezea magari kuwa katika hali isiyoridhisha kwa utoaji wa huduma kutokana na uchakavu wake. Hali hii imesababishwa na Wakala kutolipa kipao mbele suala la utengenezaji wa jengo hilo katika bajeti yake ya mwaka.

Kutokutayarishwa kwa mpango wa matengenezo wa mali ni kwenda kinyume na kifungu nambari 66 cha Sheria nambari 6 ya Afisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Karakana Kuu kuandaa mpango wa matengenezo ya mali na kutenga fedha za kutosha katika bajeti ya mwaka ili kuboresha mazingira ya Karakana utakaoendana na wakati.

### 6.1.8.9 Uwepo wa muitiko mdogo wa Taasisi za Umma wa kufanya matengenezo ya magari yake Karakana Kuu

Kwa mujibu wa Sheria ya Uanzishwaji wa Wakala wa Karakana Kuu ya Magari Zanzibar ya 2019 inaagiza magari yote ya Serikali kufanyiwa matengenezo ya aina yoyote na Wakala wa Karakana Kuu ya Magari pia kanuni ya 124(3) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inawataka wakuu wa Taasisi kuhakikisha vyombo vyote vilivyomo katika taasisi yake vinafanyiwa matengenezo katika Karakana Kuu ya Serikali.

Ukaguzi uliofanywa umebaini kwamba muitikio wa Taasisi za Serikali kupeleka gari wanazozimiliki Karakana Kuu kwa ajili ya matengenezo ni mdogo hali iliyosababishwa na kukosekana kwa nguvu ya kisheria katika kuhakikisha taasisi zote za umma zinafanya matengenezo ya magari yake Karakana Kuu.

Kutokuwepo kwa kifungu cha sheria kinachoelezea adhabu au hatua za kinidhamu zitakazochukuliwa kwa Taasisi za Serikali ambazo hazitopeleka gari zake karakana kwa ajili ya matengenezo kumepelekea kujitokeza kwa muamko mdogo kwa Wakuu wa Taasisi kuwasilisha vyombo vya Serikali kufanyiwa matengenezo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Karakana Kuu kufanya maboresho ya sheria yake katika baadhi ya vifungu au kuingiza vifungu vipya na pia kufanya uhamasishaji kwa kutoa uelewa katika Taasisi za umma.

## 6.1.9 WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA MALI ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar (BPRA) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

### 6.1.9.1 Dosari katika uandaaji wa taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka shilingi 15,495,019.86

Kwa mujibu wa IPSAS Cash Basis 1.7 inaelezea juu ya uandaaji wa taarifa za ulinganishi wa Bajeti na utekelezaji ambapo taarifa hizo zitalazimika kuwa ni taarifa sahihi na zisizo na makosa.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya taarifa za ulinganishi wa Bajeti na utekelezaji halisi na kubaini jumla ya shilingi 2,391,798,241.71 hazikuwa na uwiano na taarifa za Mapato na Matumizi ambazo ziliripotiwa kuwa ni shilingi 2,376,303,221.85 na kupelekea uwepo wa tofauti ya shilingi 15,495,019.86 katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka zilizowasilishwa kwa ukaguzi.

Pamoja na uwepo wa taarifa za maboresho ya hesabu iliyowasilishwa kwa mara ya pili kwa ajili ya ukaguzi bado ilibainika uwepo wa tofauti ya shilingi 15,495,019.86 baina ya matumizi halisi yaliyoainishwa katika taarifa za bajeti na utekelezaji halisi dhidi ya matumizi yaliyoainishwa katika taarifa za mapato na matumizi jambo ambalo limepelekea ukiukwaji mkubwa wa miongozo ya Ufungaji wa Hesabu za Taasisi za Umma (IPSAS Cash Basis) na hatimae taarifa hizo kutokuonesha sura sahihi na halisi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar kuhakikisha taarifa za fedha zinawasilishwa kwa Kamati ya Ukaguzi ya Wizara pamoja na Kitengo cha Ukaguzi wa ndani kwa kuweza kupitiwa na kufanyiwa maboresho kabla ya kuwasilishwa kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi.

### 6.1.9.2 Mapato yaliyokusanywa nje ya mfumo wa ZanMalipo shilingi 726,954,846

Kifungu nambari 55(a) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaelezea kwamba "Fedha zote za Umma zitakusanywa kupitia mfumo wa malipo wa kielektroniki uliowekwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali". Katika kutekeleza agizo hilo la Serikali ilianzisha rasmi mfumo wa 'ZanMalipo' ili kuweza kukusanya fedha zote za Serikali kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usimamizi wa mapato ya Serikali.

Ukaguzi ulipitia taarifa za mapato za Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar na kubaini uwepo wa makusanyo yenye jumla ya shilingi 726,954,846 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 yaliyokusanywa nje ya mfumo wa malipo (ZanMalipo).

Kufanya makusanyo nje ya mfumo kunaweza kupelekea viashiria vya upotevu wa mapato ya Serikali pamoja na kwenda kinyume na Kifungu cha 55 (a) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar kuhakikisha fedha zote zinakusanywa kupitia mfumo wa malipo wa kielektroniki kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usimamizi wa mapato ya Serikali.

### 6.1.9.3 Kukosekana kwa taarifa za mapato shilingi 2,693,743,638 katika mfumo wa ZanMalipo

Kwa mujibu wa kanuni ya 25(1) ya Kanuni ya Usimamizi wa fedha za Umma ya 2021 inamtaka Afisa Masuuli kuhakikisha anasimamia vyema taarifa za fedha za taasisi.

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ukaguzi ulifanya mapitio ya taarifa za fedha za mwisho wa mwaka za Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar na kubaini jumla ya shilingi 2,693,743,638 zilikusanywa kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali vya mapato.

Aidha, ukaguzi haukuweza kuthibitisha usahihi wa taarifa hizo za mapato kutokana na kukosekana kwa taarifa muhimu za mapato yaliyokusanywa kupitia mfumo wa ZanMalipo kwa kipindi cha mwezi wa Julai 2022 hadi Disemba, 2022.

Kukosekana kwa taarifa za mfumo wa ZanMalipo kwa ukaguzi juu ya makusanyo ya shilingi 2,693,743,638 yaliyokusanywa na BPRA , ukaguzi haukuweza kuthibitisha usahihi wa taarifa za fedha za mwisho wa mwaka zilizowasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar kuhakikisha unafanya usuluhishi wa taarifa za fedha kabla ya ufungaji wa hesabu na ni vyema taarifa hizo kupitiwa na vitengo vya ndani vya ukaguzi wa hesabu ili kuweza kutolewa maoni na mapendezo kuhusiana na usahihi wa hesabu hizo kabla ya kuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

#### 6.1.9.4 Usimamizi usioridhisha wa fedha za TIRKA

Tirka ni Mali au haki ya kimali aliyoiwacha mtu baada ya kufariki dunia. Ukaguzi ulifanya mapitio ya taarifa mbalimbali za fedha ili kuweza kutathmini endapo usimamizi wa fedha zinazotokana na Tirka zinasimamiwa ipasavyo na kubaini kwamba kwa mwaka wa fedha 2022/2023 usimamizi wa fedha hizo haukua wa kuridhisha.

Kutokana na taarifa za fedha zilizoandaliwa na kuwasilishwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar zilibainisha jumla ya shilingi 632,875,323.59 zilipokelewa kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) kwa ajili ya kulipa Tirka. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 jumla shilingi 299,939,887.99 zilitumika kulipa Tirka na kupelekea uwepo wa bakaa ya shilingi 332,935,435.60 jambo ambalo linatofautiana na taarifa za fedha za shilingi 317,440,415.74 zilizoripotiwa kama bakaa ya fedha ya Tirka kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na kupelekea uwepo wa tofauti ya shilingi 15,495,019.86. Mchanganuo wa taarifa hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 104: Mchanganuo wa fedha za Tirka**

| Bakaa ya Fedha za Tirka 2022/2023 (Tsh.) | Bakaa ya Fedha za Tirka kabla ya kujumuishwa kwa bakaa ya fedha la 2021/2022 (Tsh.) | Tofauti (Tshs) |
|---|---|---|
| **332,935,435.60** | **317,440,415.74** | **15,495,019.86** |

Pamoja na uwepo wa tofauti hiyo ukaguzi ulifanya ufuatiliaji wa majibu ya hoja na kubainika kupitia taarifa za fedha zilizofanyiwa maboresho na kuwasilishwa kwa mara ya pili ilibainika kujitokeza kwa tofauti ya shilingi 31,210,168.93 baina ya bakaa la fedha iliyoainishwa katika taarifa za hesabu za mwisho wa mwaka ukilinganisha na bakaa la fedha lililoainishwa mara ya pili katika hesabu za Wakala jambo ambalo limepelekea kushindwa kujiridhisha juu ya usahihi wa taarifa zilizowasilishwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar kuhakikisha hauchanganyi fedha za Tirka na fedha za matumizi mengineyo ili kuepusha uwezekano wa uwepo wa matumizi mabaya ya fedha ambayo yatapelekea kushindwa kuwalipa warithi kwa wakati. Mchanganuo wa taarifa hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 105: Tofauti ya fedha za Tirka baina ya hesabu za benki na Taarifa ya Ufungaji wa Hesabu**

| Bakaa la Fedha 2022/2023 Kwa Mujibu wa Hesabu za Wakala (Bank Statements) (A) | | Bakaa la Fedha 2022/2023 Kwa mujibu wa Taarifa za Fedha za mwisho wa mwaka (Financial Statement) (B) | Tofauti (A-B) |
|---|---|---|---|
| Nambari ya Hesabu | Kiasi (Tsh) | Kiasi (Tsh) | Kiasi (Tsh) |
| 0404422000 | 100,000 | **383,756,402** | **31,210,168.93** |
| 0404063000 | 414,866,570.93 | | |
| **Jumla** | **414,966,570.93** | | |

## WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA MALI PEMBA

### 6.1.9.5 Uwepo wa Upungufu wa Watumishi

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Pemba ina upungufu wa watumishi muhimu ambao wangaliwezesha Wakala kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Upungufu huu unaathiri utendaji wa jumla wa Wakala ikiwa ni pamoja na utoaji duni wa huduma, mrundikano wa majukumu, na kupunguza hamasa ya utendaji kazi kwa watumishi waliopo. Hali inayoweza kupelekea ucheleweshwaji wa utoaji huduma kwa taasisi za umma na jamii kwa ujumla na pia ni kuikosesha mapato Serikali.

Kutokufanya uajiri kwa mujibu wa nafasi zilizowazi ni kwenda kinyume na kanuni nambari 6(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kulipa kipaombele suala la uajiri ili kupunguza changamoto za kiutendaji zinazoikabili taasisi husika. Mchanganuo wa upungufu wa watumishi ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 106: Upungufu wa Watumishi**

| Namba | Kada | Waliopo | Wanaohitajika | Upungufu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Afisa Mipango | 0 | 1 | 1 |
| 2. | Afisa IT | 1 | 2 | 1 |
| 3. | Afisa Masjala | 0 | 1 | 1 |
| | Walinzi | 1 | 2 | 1 |
| **Jumla** | | **2** | **6** | **4** |

*Chanzo: Mpango wa Rasilimali Watu wa Wakala*

### 6.1.9.6 Kukosekana kwa gari kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za Wakala

Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali inajukumu la kusajili na kushajihisha wananchi kusajili biashara na mali zao kwa lengo la kuongeza pato la Taasisi na Serikali kwa ujumla.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Pemba haina vyombo vya usafiri (Gari) hali iliyopelekea kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu ya kushajihisha wananchi wa maeneo mbali mbali katika kisiwa cha Pemba juu ya umuhimu wa kuwa na nyaraka za biashara na mali wanazozimiliki.

Kukosekana kwa vyombo vya usafiri kunaweza kupelekea Wakala kushindwa kufikia malengo yake iliyojiwekea.

Ukaguzi unaishauri Serikali kuandaa mpango wa dharura wa kuipatia Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Pemba vyombo vya usafiri ili viweze kusaidia katika kufikia lengo la uhamasishaji wananchi juu ya umuhimu wa utafutaji, umiliki na utunzaji wa nyaraka.

### 6.1.10 WAKALA WA SERIKALI MTANDAO ZANZIBAR (eGAZ)

Ukaguzi wa hesabu za Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 6.1.10.1 Mapato yaliyokusanywa nje ya mfumo wa ZanMalipo shilingi 115,129,840

Kifungu nambari 55(a) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaelezea kwamba "Fedha zote za Umma zitakusanywa kupitia mfumo wa malipo wa kielektroniki uliowekwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali". Katika kutekeleza agizo hilo Serikali ilianzisha rasmi mfumo wa 'ZanMalipo' ili kuweza kukusanya fedha zote za Serikali kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usimamizi wa mapato ya Serikali.

Ukaguzi ulipitia taarifa za mapato ya Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar na kubaini uwepo wa makusanyo yenye jumla ya shilingi 152,825,420 kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kutoka kwa wadau mbalimbali, kati ya fedha hizo shilingi 115,129,840 sawa na asilimia 75 zilikusanywa bila ya kutumia Mfumo wa Malipo wa Serikali wa ZanMalipo kupitia hesabu Nambari 792146001 na 792146002 zinazomilikiwa na Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar.

Kufanya makusanyo nje ya mfumo kunaweza kupelekea viashiria vya upotevu wa mapato ya Serikali na pia ni kwenda kinyume na kifungu nambari 55 (a) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya mwaka 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao Zanzibar kuhakikisha fedha zote zinakusanywa kupitia mfumo wa malipo wa kielektroniki kwa lengo la kuongeza ufanisi katika usimamizi wa mapato ya Serikali.

#### 6.1.10.2 Kutokuwepo kwa Mkataba wa ununuzi wa mafuta shilingi 67,555,339.34

Kwa mujibu wa kifungu nambari 42(2) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma ya mwaka 2016 kinaeleza kwamba "Taasisi ya ununuzi na uondoshaji wa mali za umma itapanga mpango wake wa ununuzi na uondoshaji kwa kutumia vigezo vinavyokubalika na hususan utazingatia kutumia mfumo wa mikataba maalumu kwa namna inavyohitajika kutoa huduma bora, zenye gharama nafuu na kwa njia inayoweza kubadilika kwa bidhaa zinazohitajika kila mara au zinazojirudia kila baada ya muda".

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 67,555,339.34 zimelipwa na Wakala wa Serikali Mtandao kwa Kampuni ya Zanzibar Petrol Station kwa ajili ya ununuzi wa mafuta bila ya kuwepo kwa mkataba.

Kufanya hivyo kunaweza kupelekea kutokupata huduma iliyo bora na ya uhakika pamoja na uwezekano wa kutokea kwa ununuzi katika vituo ambavyo havijasajiliwa kwa ajili ya utoaji wa huduma hiyo. Aidha, ni kwenda kinyume na kifungu nambari 42(2)(b) cha Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala kuhakikisha wanafunga mikataba kwa ununuzi wa bidhaa zote wanazotumia kila mara au zinazojirudia kila baada ya muda kama sheria inavyoolekeza. Mchanganuo wa mafuta yaliyonunuliwa bila uwepo wa mkataba na mtoa huduma ni kama unavyoonekana katika jadweli lifuatalo hapo chini:-

### Jadweli Nambari 107: Mafuta yaliyonunuliwa bila ya Mkataba

| Namba | Namba ya Hati | Namba ya Hundi | Maelezo | Kiasi cha Fedha (Tshs) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 29/8 ya 29/08/22 | TISS | Ununuzi wa mafuta ya petrol lita 1,258 | 3,748,840 |
| 2. | 17/9 ya 12/9/2022 | | Ununuzi wa mafuta ya Petrol Lita 2,398 | 7,146,040 |
| 3. | 22/9 ya 20/9/2022 | | Ununuzi wa mafuta ya petrol lita 100 | 298,000 |
| 4. | 16/9 ya 13/10/2022 | | Ununuzi wa mafuta Petrol lita 250 | 745,000 |
| 5. | 15/11 ya 02/11/2022 | | Ununuzi wa mafuta ya petrol lia 100 | 298,000 |
| 6. | 28/11 ya16/11/2022 | | Ununuzi wa mafuta ya Petrol Lita 813 | 2,422,740 |
| 7. | 29/11 ya16/11/2022 | | Ununuzi wa mafuta ya Petrol lita 700 | 2,086,000 |
| 8. | 30/11 ya 16/11/2022 | | Ununuzi wa mafuta ya Petrol lita 700 | 2,086,000 |
| 9. | 2/11 ya 28/11/2022 | | Ununuzi wa mafuta lita 100 | 298,000 |
| 10. | 9/12 ya 07/12/2012 | | Ununuzi wa Petrol Lita 200 | 596,000 |
| 11. | 14/12 ya 12/12/2022 | | Ununuzi wa mafuta lita 1,000 | 2,980,000 |
| 12. | 36/12 ya 20/12/2022 | | Ununuzi wa Petrol Lita 250 | 745,000 |
| 13. | 8/1 ya 02/01/2023 | | Ununuzi wa Petrol lita 100. | 298,000 |
| 14. | 3/1 ya 30/01/2023 | | Ununuzi wa Petrol lita 100 | 298,000 |
| 15. | 4/1 ya 30/01/2023 | | Ununuzi wa Petrol lita 900 | 2,682,000 |
| 16. | 10/2 ya 04/02/2023 | | Ununuzi wa Petrol lita 1,400 | 4,172,000 |
| 17. | 27/2 ya 06/02/2023 | | Ununuzi wa Petrol lita100 | 298,000 |
| 18. | 90/2 ya 27/02/2023 | | Ununuzi wa Petrol lita100 | 288,000 |
| 19. | 19/3 ya 13/03/2023 | | Ununuzi wa Petrol lita100 | 299,000 |
| 20. | 20/3 ya 13/03/2023 | | Ununuzi wa Petrol lita100 | 288,000 |
| 21. | 36/3 ya 22/03/2023 | | Ununuzi wa Petrol lita1256 | 3,744,000 |
| 22. | 42/3 ya 23/03/2023 | | Ununuzi wa mafuta ya Petrol lita 200 | 576,000 |
| 23. | 22/4 ya 10/04/2023 | | Ununuzi wa petrol lita 700 | 2,016,000 |
| 24. | 10/5 ya 05/05/2023 | | Ununuzi wa Petrol lita 1000 | 2,780,000 |
| 25. | 26/5 ya 16/05/2023 | | Ununuzi wa petrol lita 200 | 556,000 |
| 26. | 32/5 ya 16/05/2023 | | Ununuzi wa petrol lita 200 | 556,000 |
| 27. | 37/5 ya 24/05/2023 | | Ununuzi wa Petrol lita 1000 | 2,780,000 |
| 28. | 38/5 ya 24/05/2023 | | Ununuzi wa diesel lita 100 | 290,000 |
| 29. | 39/5 ya 24/05/2023 | | Ununuzi wa mafuta ya Petrol lita 200 | 556,000 |
| 30. | 58/5 ya 29/05/2023 | | Ununuzi wa Petrol lita 300 | 834,000 |
| 31. | 31/6 ya 20/06/2023 | | Ununuzi wa mafuta ya Petrol lita 300 | 834,000 |
| 32. | 32/6 ya 21/06/2023 | | Ununuzi wa petrol lita 1466 | 4,368,680 |
| 33. | 78/6 ya 30/06/2023 | | Ununuzi wa mafuta ya Petrol lita 2700 | 7,803,000 |
| 34. | 79/6 ya 30/06/2023 | | Ununuzi wa mafuta 2614 | 7,789,039.34 |
| **Jumla** | | | | **67,555,339.34** |

**WAKALA WA SERIKALI MTANDAO PEMBA**

### 6.1.10.3 Kutokutekelezeka kwa bajeti ya matumizi

Wakala wa Serikali Mtandao Pemba ilikadiriwa kutumia jumla ya shilingi 227,855,800 kwa kazi za kawaida. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023 jumla ya shilingi 47,040,000 zimetumika kwa kazi za kawaida ambazo ni sawa na asilimia 20.64.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wakala imepatiwa kiwango kidogo cha fedha za bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida. Hali hii imepelekea Wakala kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao Pemba kuhakikisha wanafuatilia upatikanaji wa fedha za bajeti kikamilifu ili waweze kutekeleza majukumu ya Wakala kwa ufanisi zaidi. Aidha, ukaguzi unaishauri Afisi ya Hazina kuingiza fedha za bajeti kwa mujibu wa bajeti iliyoidhinishwa.

### 6.1.10.4 Uwepo wa Upungufu wa Watumishi

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wakala wa Serikali Mtandao Pemba ina upungufu wa watumishi muhimu ambao wangaliwezesha Wakala kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Upungufu huu unaathiri utendaji wa jumla wa Wakala ikiwa ni pamoja na utoaji duni wa huduma, mrundikano wa majukumu, na kupunguza hamasa ya utendaji kazi kwa watumishi waliopo. Hali inayoweza kupelekea ucheleweshwaji wa utoaji huduma kwa taasisi za umma na jamii kwa ujumla na pia ni kuikosesha mapato Serikali.

Kutokufanya uajiri kwa mujibu wa nafasi zilizowazi ni kwenda kinyume na kanuni nambari 6(1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kulipa kipaombele suala la uajiri ili kupunguza changamoto za kiutendaji zinazoikabili taasisi husika. Mchanganuo wa upungufu wa watumishi ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 108: Upungufu wa Watumishi**

| Namba | Kada | Waliopo | Wanaohitajika | Upungufu |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Afisa Tehama | 3 | 8 | 5 |
| 2. | Afisa mipango | 0 | 1 | 1 |
| 3. | Mtunza nyaraka | 0 | 1 | 1 |
| 4. | Mwanasheria | 0 | 1 | 1 |
| 5. | Afisa habari | 0 | 1 | 1 |
| **Jumla** | | **3** | **12** | **9** |

*Chanzo: Mpango wa rasilimali watu*

### 6.1.10.5 Uwepo wa Ufinyu wa Nafasi za Kufanyia Kazi

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Ofisi ya Wakala wa Serikali Mtandao Pemba haina nafasi ya kutosha kwa ajili ya watumishi wake hali iliyopelekea chumba kimoja kutumika na watumishi wa kada tofauti jambo ambalo linaweza kupunguza hamasa na ari ya utendaji kazi kwa watumishi hao, hivyo Wakala kutokufanya kazi kwa ufanisi unaotarajiwa na pia uwepo wa uwezekano wa kuvuja kwa taarifa za siri za Wakala.

Kukosekana kwa nafasi ya kutosha ya kufanyia kazi katika Ofisi ya Wakala ni kwenda kinyume na Sheria nambari 11 ya Ajira ya 2005 pamoja na Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Serikali Mtandao Pemba kuhakikisha wanachukuwa jitihada za makusudi katika kuwatafutia watendaji wake sehemu nyengine iliyo sahihi, salama na inayoweza kuwatosha kwa ajili ya kufanya kazi zao za kila siku ili kuleta ufanisi mzuri.

### 6.1.11 WAKALA WA ULINZI – JKU

Ukaguzi wa hesabu za Wakala wa Ulinzi (JKU) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 6.1.11.1 Kutofuatwa kwa taratibu za manunuzi shilingi 356,935,000

Kwa mujibu wa kanuni nambari 57(1) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma mwaka 2020 imeweka katazo kwa Taasisi ya Ununuzi ya Umma kugawa manunuzi kwa lengo la kukwepa kutoa zabuni za ndani au za nje ya nchi.

Ukaguzi umebaini Wakala wa Ulinzi Zanzibar umefanya manunuzi yenye thamani ya shilingi 356,935,000 kwa ajili ya ununuzi wa chakula kwa mtoa huduma YESS BOSS. Dosari zifuatazo zimebainika katika ukaguzi:-

- Kutokutangazwa kwa zabuni ya wazi ili kumpata mtoa huduma mwenye uwezo na kwa bei nafuu.
- Uwepo wa dosari katika mkataba ambapo haikubainishwa mchanganuo wa malipo utakayotumika kumlipa mtoa huduma.
- Kutokuwasilishwa kwa mkataba huo Afisi ya Mwanasheria Mkuu kwa lengo la kuandaliwa vizuri ili kuepusha kujitokeza kwa mikataba isiyokuwa na tija kwa Serikali.
- Kufanya matumizi kwa njia ya kugawa manunuzi (splitting Tender) jambo ambalo ni kinyume na kanuni nambari 57(1) ya Kanuni ya Manunuzi ya Umma ya 2020.

Kutokana na dosari zilizobainishwa hapo juu zinapelekea kufanya matumizi kusikozingatia nidhamu ya matumizi jambo ambalo huwenda ikapelekea kukosekana kwa ufanisi wa matumizi ya fedha yaliyofanyika na hatimae kuisababishia hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Ulinzi Zanzibar kuhakikisha unazingatia matakwa ya Sheria nambari 11 ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya 2016.

#### 6.1.11.2 Malipo yaliyofanywa nje ya mfumo wa manunuzi shilingi 471,979,845

Kwa mujibu wa barua yenye kumbukumbu namba MUUMU.BA.156/370/001/27 ya tarehe 12/08/2022 kutoka Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma ya Zanzibar kwenda kwa wakuu wa taasisi inaeleza kwamba kuanzia tarehe 15/08/2022 manunuzi yote ya Serikali yanatakiwa yafanywe kwa kutumia mfumo wa ununuzi wa kielektroniki (e-PROZ).

Ukaguzi umebaini kwamba Wakala wa Ulinzi Zanzibar imetumia jumla ya shilingi 471,979,845 kwa ajili ya manunuzi mbali mbali pasipo kutumia mfumo wa kielektroniki wa manunuzi bila ya kuwepo sababu maalum ya kufanya hivyo. Kufanya manunuzi bila kutumia mfumo ni kwenda kinyume na maelekezo ya barua niliyoitaja hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Ulinzi Zanzibar kuhakikisha manunuzi yote yanayofanyika yanapitia katika mfumo wa manunuzi. Mchanganuo wa manunuzi yaliyofanywa nje ya mfumo wa manunuzi ni kama ufuatao:-

**Jadweli Nambari 109: Manunuzi yaliyofanywa Nje ya Mfumo wa Manunuzi (e-Proz)**

| Namba | Huduma | Kiasi (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Ununuzi wa Chakula | 356,935,126 |
| 2. | Ununuzi wa Military Uniform | 75,549,220 |
| 3. | Ununuzi wa Spare Part | 39,495,515 |
| **Jumla** | | **471,979,845** |

### 6.1.11.3 Malimbikizo ya Madeni ya muda mrefu shilingi 507,323,647

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba Wakala wa Ulinzi (JKU) Zanzibar inazidai Taasisi mbali mbali za Serikali kutokana na huduma iliyozitoa zenye thamani ya shilingi 507,323,647.

Uwepo wa madeni ya muda mrefu katika Taasisi za Umma yanayodaiwa kutokana na huduma iliyotolewa yanatoa kiashiria cha kwamba Afisa Mhasibu wa Taasisi za Umma ameshindwa kusimamia ulipwaji wa madeni hayo kwa wakati kutokana na kukosekana kwa sera au muongozo wa ulipwaji wa madeni kwa taasisi za umma.

Kutokulipa madeni kwa wakati kunawakatisha tamaa watoa huduma na wasambazaji wa bidhaa na kunaweza kusababisha washindwe kutoa huduma kwa ufanisi jambo ambalo linaweza kupelekea kudumaza mahusiano mema ya kiutendaji baina ya taasisi za Serikali.

Kutokulipwa madeni kwa wakati ni kwenda kinyume na kifungu nambari 29(1)(b) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016.

Ukaguzi unawashauri Maafisa Masuuli wa Taasisi za Umma kuchukuwa juhudi za makusudi kuhakikisha kwamba kunakuwa na sera ya usimamizi wa madeni ili kuepukana na uwepo wa madeni makubwa ambayo hayatoweza kulipika. Mchanganuo wa malimbikizo ya madeni ya muda mrefu ni kama yanavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 126: Malimbikizo ya Madeni ya Muda Mrefu**

| Namba | Mpewa huduma | Kipindi kinachodaiwa | Jumla ya Miezi | Kiasi kinachodaiwa (Tsh.) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Shirika la Magazeti ya Serikali | Sept 22- Mei 2023 | 20 | 21,600,000 |
| 2. | ZAECA | - | 6 | 15,000,000 |
| 3. | Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya | Julai-Disemba 2020 | 6 | 24,000,000 |
| 4. | Mamlaka ya Maji Zawa | Machi 2021- Mei 2023 | 27 | 97,000,000 |
| 5. | TRA- Pemba | Julai –Mei 2023 | 11 | 23,000,000 |
| 6. | Taasisi ya Utafiti wa Mifugo – Kizimbani | Juni 2021-Mei 2023 | 12 | 24,000,000 |
| 7. | Wakala wa Barabara | Novemba 2021-Mei 2023 | 19 | 22,000,000 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 8. | OR- Fedha na Mipango | Aprili 21–Julai 22 | 16 | 99,360,000 |
| 9. | DPP | Julai 2022-May 2023 | 11 | 52,800,000 |
| 10. | Manispaa Magharib-A | Jan 2022 –May 2023 | 5 | 16,800,000 |
| 11. | Manispaa Magharibi- B | Machi2023- Mei 2023 | 3 | 13,440,000 |
| 12. | Wizara ya Ardhi Maendeleo ya Makaazi | - | 24 | 85,000,000 |
| 13. | ZIPA | Machi 2023- Mei 2023 | 5 | 12,000,000 |
| **Jumla ya Deni** | | | | **507,323,647** |

### 6.1.12 WAKALA WA BARABARA ZANZIBAR

Ukaguzi wa hesabu za Wakala wa Barabara Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 6.1.12.1 Usimamizi na uhifadhi usioridhisha wa Mafuta yanayonunuliwa na Wakala

Kanuni ya 26 ya Kanuni za Usambazaji wa Mafuta ya 2017 (The Petroleum Supply Regulations, 2017) inaeleza kwamba haitaruhusiwa kuhifadhi zaidi ya lita 200 za mafuta bila ya kuwa na kibali maalumu kinachotolewa na Mamlaka. Aidha, Kanuni ya 42 ya Vituo vya Mafuta ya 2016 (The Petroleum Filling Station Regulation, 2016) inaeleza kwamba vituo vyote vya mafuta vitalazimika kuhakikisha uwepo wa njia sahihi za uokozi na vilevile msimamizi wa Mafuta atalazimika kupatiwa mafunzo ya kutosha kuhusiana na masuala ya Usimamizi wa Mafuta.

Kwa mwaka wa fedha 2022/23 Wakala wa Barabara iliainisha matumizi ya jumla ya shilingi 17,690,000 kwa ajili ya ununuzi wa mafuta ya petroli, shilingi 198,500,000 kwa ajili ya Ununuzi wa mafuta ya Diesel na shilingi 290,545,000 kwa ajili ya ununuzi wa Mafuta ya Taa.

Ukaguzi ulitembelea maeneo yanapohifadhiwa mafuta hayo na kubaini kwamba Wakala wa Barabara kutokuwa na sehemu salama ya kuhifadhia mafuta yaliyonunuliwa jambo ambalo linaweza likapelekea viashiria vya upotevu na matumizi mabaya ya mafuta yanayonunuliwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Wakala wa Barabara Zanzibar kuandaa maeneo salama ya kuhifadhi mafuta kwa mujibu wa miongozo iliyoekwa ili kuepusha uwezekano wa kujitokeza upotevu wa mafuta pamoja na kuingiza hasara Serikali.

#### 6.1.12.2 Watumishi kukaimu nafasi kinyume na utaratibu

Kwa mujibu wa kanuni nambari 20(6) ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya 2014 inaeleza kwamba "Kwa kuzingatia masharti ya kifungu hiki hakuna nafasi ya kukaimu zaidi ya muda wa miezi kumi na mbili (12) mfululizo kutoka tarehe ya uteuzi wa kukaimu isipokuwa muhusika atathibitishwa katika wadhifa huo au mwenye dhamana atakaporejea."

Ukaguzi umebaini kwamba Wakala wa Barabara Zanzibar imewakaimisha watumishi wawili nafasi za Utumishi kwa kipindi cha zaidi ya mwaka mmoja jambo ambalo ni kinyume na kanuni ya Utumishi wa Umma niliyoinakili hapo juu.

Kuendelea kuwakaimisha watumishi hao kwa zaidi ya kipindi kilichoelezwa kwa mujibu wa sheria kunapelekea kuwapunguzia hamasa na kuwavunja moyo watendaji hao katika utekelekezaji wao wa majukumu, na hivyo inaweza kusababisha kukosekana kwa ufanisi na tija iliyokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Barabara Zanzibar kuchukua jitihada za makusudi kuhakikisha watumishi hao wanathibitishwa au unaandaliwa utaratibu wa kuwateuwa watumishi wengine wenye sifa toshelevu za kushika nafasi hizo. Mchanganuo wa watumishi waliokaimu kwa zaidi ya kipindi kilichoainishwa kwa mujibu wa sheria ni kama inavyonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 111: Watumishi waliokaimu nafasi kinyume na utaratibu**

| Namba | Kumbukumbu Namba | Nafasi Inayokaimiwa | Tarehe ya Uteuzi | Muda wa Kutokuthibitishwa (Miaka) |
|---|---|---|---|---|
| 1. | CAA/CCA/M.07503/54 | Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Mipango | 07/05/2021 | 3 |
| 2. | OPF-K/281 | Mkurugenzi wa Zana na Mitambo | 15/11/2021 | 3 |

### 6.1.12.3 Kutokufikiwa kwa lengo la Utekelezaji wa Mradi shilingi 27,917,789,000

Kwa mujibu wa kifungu nambari 6(a) cha Sheria nambari 11 ya Kuanzisha Wakala wa Barabara Zanzibar ya 2019 kinaeleza kwamba Wakala ina jukumu la "kujenga barabara mpya na kuzifanyia matengenezo barabara zilizopo kwenye mtandao wa barabara".

Aidha, kifungu nambari 6(e) cha Sheria hiyo kinaeleza kwamba "Wakala ina jukumu la kupanga, kusanifu na kuendeleza barabara zote za Zanzibar ili kuhakikisha kwamba barabara zinakuwa katika hali nzuri na zenye ubora wakati wote".

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Wakala wa Barabara Zanzibar ilisaini hati ya makubaliano na Taasisi mbali mbali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mitatu yenye thamani ya shilingi 27,917,789,000 ambapo Wakala alikuwa na jukumu la kufanya usimamizi na maboresho ya Miundombinu ya Barabara ili kuhakikisha kwamba barabara zinakuwa katika hali nzuri na zenye ubora wakati wote.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya mikataba kwa kulinganisha na hali halisi ya ukarabati wa barabara hizo na kubaini kwamba Wakala wa Barabara haikuweza kufikia lengo lililoainishwa katika mkataba kutokana na kushindwa kukamilisha utekelezaji wa miradi kulingana na muda ulioanishwa katika mkataba ambapo kumesababisha kuongezeka kwa uchakavu wa Barabara zilizokusudiwa kufanyiwa maboresho na kupelekea kuongezeka kwa gharama za matengenezo na kushindwa kufikia lengo lililokusudiwa na kukosekana kwa tija kwa wananchi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Barabara Zanzibar kuhakikisha unasimamia utekelezaji wa vipengele vilivyoainishwa katika mkataba kwa lengo la kujiepusha kuingia katika gharama zisizokuwa za lazima sambamba na kuharakisha upatikanaji wa tija iliyokusudiwa. Mchanganuo wa miradi hiyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 112: Miradi ilioshindwa kukamilika kwa muda uliopangwa**

| Namba | Jina la Mfadhili wa Mradi | Kiasi cha makubaliano (Tsh) | Muda wa kuanza kazi | Muda wa kukamilika kazi | Utekelezaji kwa mujibu wa makubaliano |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mfuko wa Barabara | 20,033,644,000 | 01/06/2022 | 30 Juni, 2023 | Haukukamilika |
| 2. | ZIPA | 6,984,145,000 | 15/08/2022 | 30 Disemba, 2022 | Haukukamilika |
| 3. | The Residence | 900,000,000 | 14/10/2022 | 28 Novemba, 2022 | Haukukamilika |
| | **Jumla** | **27,917,789,000** | | | |

### 6.1.13 WAKALA WA MAENDELEO YA VIWANDA VIDOGO VIDOGO, VIDOGO NA VYA KATI (SMIDA)

Ukaguzi wa hesabu za SMIDA kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 6.1.13.1 Kutokurejeshwa kwa mikopo ya Wajasiriamali shilingi 147,055,000

Kwa mujibu wa kifungu nambari 7(d) cha Sheria nambari 2 ya Uanzishwaji wa Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na Vya Kati ya 2018 inaeleza kwamba "Wakala itakuwa na jukumu la kuanzisha, kuendesha au kuwezesha upatikanaji wa huduma za mikopo zenye masharti nafuu na huduma nyengine za kifedha na zisizo za kifedha kwa ajili ya miradi ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na vya Kati".

Aidha, kwa mujibu wa kanuni nambari 23 (a-d) ya Kanuni za Mfuko wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo Vidogo, Vidogo na Vya Kati imeeleza ya kwamba Mkopo uliopatikana chini ya Kanuni hizi utalipwa ndani ya kipindi kilichoainishwa katika makubalioano ya Mkopo.

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika uwepo wa deni la muda mrefu la shilingi 147,055,000 linalodaiwa kwa Wajasiriamali ambao walipatiwa mikopo nafuu kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kwa lengo la kuimarisha hali zao za kiuchumi.

Pamoja na uwepo wa masharti ya kurudhisha mikopo hiyo kwa mujibu wa mikataba yao hadi ukaguzi unakamilika hakukuwa na juhudi za urejeshwaji wa mikopo hiyo licha ya muda wa makubaliano kumalizika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala (SMIDA) kuhakikisha unafanya ufuatiliaji wa mara kwa mara kwa Wajasiriamali waliopewa mikopo kwa lengo la kuwasaidia utatuzi wa changamoto wanazozipata wakati wa utekelezaji wa miradi yao pamoja na kuwahamasisha mbinu bora za urejeshwaji wa mikopo yao. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 113: Orodha ya Wajasiriamali walioshindwa kurudisha fedha walizokopeshwa kwa muda uliopangwa**

| Jina la Mjasiriamali | Mkopo Halisi (Tshs) | Mkopo na Riba (Tshs) | Muda wa kurudisha mkopo (Miezi) | Kiasi kilichorudishwa (Tshs) | Kiasi kinachodaiwa (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|
| Anfal | 5,000,000 | 5,500,000 | 12 | 200,000 | 5,300,000 |
| Abham | 20,000,000 | 22,000,000 | 12 | 3,500,000 | 18,500,000 |
| Bin Pandu Enterprises | 16,000,000 | 17,600,000 | 18 | 4,250,000 | 13,350,000 |
| Kusudio Sio Hilo | 4,000,000 | 4,400,000 | 12 | 1,400,000 | 3,000,000 |
| Mohd's Tin Works | 2,000,000 | 2,200,000 | 6 | - | 2,200,000 |
| Huasa Zan Trading | 19,000,000 | 20,900,000 | 24 | 15,000,000 | 5,900,000 |
| Shina Association | 6,650,000 | 7,315,000 | 12 | 1,100,000 | 6,215,000 |
| Jam's Tin Works | 2,000,000 | 2,200,000 | 6 | - | 2,200,000 |
| Wema Corperative | 5,000,000 | 5,500,000 | 12 | 800,000 | 4,700,000 |
| Lipi Corperative | 35,000,000 | 38,500,000 | 30 | 23,800,000 | 14,700,000 |
| Salah & Sons | 20,000,000 | 22,000,000 | 24 | 16,500,000 | 5,500,000 |
| Mshimba Food | 16,000,000 | 17,600,000 | 6 | 200,000 | 17,400,000 |
| Kangaroo | 30,000,000 | 33,000,000 | 18 | 6,500,000 | 26,500,000 |
| ZSH | 15,000,000 | 16,500,000 | 18 | 2,860,000 | 13,640,000 |

| Jina la Mjasiriamali | Mkopo Halisi (Tshs) | Mkopo na Riba (Tshs) | Muda wa kurudisha mkopo (Miezi) | Kiasi kilichorudishwa (Tshs) | Kiasi kinachodaiwa (Tshs) |
|---|---|---|---|---|---|
| Wasila Masoud | 500,000 | 500,000 | 1 | 170,000 | 330,000 |
| Masika Said | 500,000 | 500,000 | 1 | 280,000 | 220,000 |
| Rajab Haji Muombwa | 10,000,000 | 11,000,000 | 18 | 8,550,000 | 2,450,000 |
| Faki Rice | 5,000,000 | 5,500,000 | 3 | 3,000,000 | 2,500,000 |
| Amani Salt | 5,000,000 | 5,500,000 | 12 | 3,050,000 | 2,450,000 |
| **Jumla Kuu** | **216,650,000** | **238,215,000** | | **91,160,000** | **147,055,000** |

### 6.1.14 WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

Ukaguzi wa hesabu za Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 6.1.14.1 Kutokufikiwa kwa malengo ya uwasilishaji wa mapato ya asilimia 10 kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenda kwa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi shilingi 955,381,869.98

Kwa mujibu wa Ibara ya 202(h) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2020-2025 inazitaka Mamlaka zote za Serikali za Mitaa Zanzibar kuchangia mapato yao kwa asilimia 10 na kuyapeleka katika Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ili kuwafikia walengwa ambao ni wanawake asilimia 4, vijana asilimia 4 na watu wenye ulemavu asilimia 2 kwa lengo la kupanua wigo wa uwezeshaji hususan katika makundi hayo, kwa kutoa fedha katika makusanyo ya Serikali za mitaa.

Jumla ya shilingi 14,153,548,741.82 zimekusanywa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kutoka katika vianzio mbalimbali vya mapato kwa Unguja na Pemba kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa, aidha ukaguzi umebaini makusanyo halisi yaliyotakiwa kupelekwa Wakala wa Uwezeshaji ni shilingi 1,415,354,874.02.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuwasilishwa kwa mapato pungufu ya shilingi 1,137,177,259 ambapo mapato hayo hayaendani na uhalisia wa kima halisi cha fedha kinachopaswa kuwasilishwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Pamoja na uwepo wa mapungufu hayo ukaguzi umefanya tathmini kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022 hadi 2022/2023 na kubainika Mamlaka za Serikali za Mitaa hazikuwasilishwa jumla ya shilingi 955,381,869.98 jambo ambalo limepelekea Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kushindwa kutekeleza malengo waliyojipangia kwa mujibu wa Ibara ya 202(h) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi (2020-2025).

Ukaguzi unaishauri Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuhakikisha zinawasilisha michango itokanayo na makusanyo ya mapato halisi kwa mujibu wa kiwango kilichowekwa ili kuondosha usumbufu unaoweza kujitokeza kwa kushindwa kuwawezesha wananchi kiuchumi na hatimae kupelekea kutofikiwa kwa malengo yaliyopangwa na Serikali ya kuwapunguzia makali ya maisha Wajasiriamali.

Aidha, ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kuhakikisha unachukuwa jitihada za ufuatiliaji wa madeni yanayodaiwa ili kuweza kukidhi viwango vya utoaji wa mikopo kwa wananchi kwa lengo la kunyanyua vipato vyao. Mchanganuo wa tofauti ya makusanyo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 114: Tofauti ya Makusanyo ya mapato kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa kwenda Wakala wa Uwezeshaji**

| Jina la Taasisi | Makusanyo Halisi kwa mwaka 2022/2023 (Tsh.) | Kilichotakiwa Kuwasilishwa kwa mwaka 2022/2023 (Tsh.) | Kilichowasilishwa kwa mwaka 2022/2023 (Tsh.) | Deni kwa Mwaka 2022/2023 (Tsh.) | Deni kwa Mwaka 2021/2022 (Tsh.) | Jumla ya Deni Hadi 30 Juni 2023 (Tsh.) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **MABARAZA YA MANISPAA** | | | | | | |
| Mjini | 3,738,771,962.00 | 373,877,196.2 | 284,000,000 | 89,877,196.2 | 238,462,873.92 | 328,340,070.12 |
| Chake Chake | 596,419,420 | 59,641,942 | 52,585,010 | 7,056,932 | 0 | 7,056,932 |
| Magharibi A | 1,477,405,381.62 | 147,740,538 | 60,034,869 | 87,705,669 | 120,667,915.05 | 208,373,584.05 |
| Magharibi B | 1,954,953,000 | 195,495,300 | 176,800,474 | 18,694,826 | 145,405,036.33 | 164,099,862.33 |
| **Jumla Ndogo (A)** | **7,767,549,763.62** | **776,754,976.2** | **573,420,353** | **203,334,623.2** | **504,535,825.3** | **707,870,448.5** |
| **MABARAZA YA MJI** | | | | | | |
| Kati | 1,137,246,362 | 113,724,636.2 | 125,190,947.54 | (11,466,311.34) | 20,071,898.6 | 8,605,587.30 |
| Kaskazini A | 1,561,390,454.20 | 156,139,045.42 | 145,173,361.73 | 10,965,683.69 | 100,180,831.2 | 111,146,514.89 |
| Kaskazini B | 1,278,947,752.00 | 127,894,775.2 | 121,302,136.60 | 6,592,638.6 | 18,956,893.19 | 25,549,531.79 |
| Mkoani | 371,474,665 | 37,147,466.5 | 33,402,850.50 | 3,744,616 | 0 | 3,744,616 |
| Wete | 362,914,156 | 36,291,415.6 | 41,395,735 | (5,104,319.4) | 8,000,000 | 2,895,680.6 |
| **Jumla Ndogo (B)** | **4,711,973,389.2** | **471,197,338.92** | **466,465,031.37** | **4,732,307.55** | **147,209,622.99** | **151,941,930.58** |
| **HALMASHAURI** | | | | | | |
| Kusini | 1,408,859,259 | 140,885,925.9 | 71,880,798.30 | 69,005,127.6 | 25,458,807.1 | 94,463,934.7 |
| Micheweni | 265,166,330 | 26,516,633 | 25,411,076.80 | 1,105,556.2 | 0 | 1,105,556.2 |
| **Jumla Ndogo (C)** | **1,674,025,589** | **167,402,558.9** | **97,291,875.1** | **70,126,683.8** | **25,458,807.1** | **95,569,490.9** |
| **Jumla Kuu (A+B+C)** | **14,153,548,741.82** | **1,415,354,874.02** | **1,137,177,259** | **278,177,614.55** | **677,204,255.39** | **955,381,869.98** |

## WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI PEMBA

### 6.1.14.2 Kutokutumika kwa fedha za uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa wakati shilingi 152,794,672

Ibara ya 202(h) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2020-2025 kinataka Mamlaka za Serikali za Mitaa kuchangia asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwenye Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa madhumuni ya kutanua wigo wa uwezeshaji wa wananchi kiuchumi hususani makundi maalumu ya wajasiriamali ikiwemo wanawake asilimia 4, vijana asilimia 4, na asilimia 2 kwa watu wenye ulemavu.

Ukaguzi umebaini kwamba kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi umepokea jumla ya shilingi 152,794,672 kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa Pemba na kuingizwa fedha hizo katika Hesabu ya Mfuko wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi iliyopo katika Afisi ya Rais, Kazi Uchumi na Uwekezaji kwa ajili ya kuwawezesha vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kwa mujibu wa maelekezo ya Ibara ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kuendelea kubakishwa fedha hizo katika hesabu husika bila ya kutumika kwa kuwapatia wajasiriamali ili ziweze kuwasaidia kujikwamua kimaisha kama ilani inavyotaka hali ambayo inapelekea kutokufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa, aidha ni kwenda kinyume na Ibara ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi niliyonakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Afisi kuhakikisha kwamba fedha za Uwezeshaji wajasiriamali zinatumika kwa wakati uliokusudiwa.

# SURA YA SABA






9:41
Contributions
Lorem ipsum dolor sit amet consectetur adipisicing elit. Maxime mollitia,molestiae quas vel sint
Statement
Contribution
SMS & Email
2022

# 7.0 UKAGUZI WA TAASISI ZINAZOJITEGEMEA ZA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umebainisha taarifa ya michango ya vyanzo vya mapato vya Taasisi zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, utendaji wa mwaka kwa kila chanzo cha mapato pamoja na kubainisha dosari za kiutendaji zilizojitokeza wakati wa ukaguzi na kubainisha njia za utatuzi wa dosari hizo.

Yafuatayo ni matokeo ya ukaguzi kwenye ukaguzi wa Taasisi zinazojitegemea za Serikali kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

## 7.1 TAARIFA ZA HESABU ZA TAASISI MBALIMBALI ZINAZOJITEGEMEA ZA SERIKALI KWA MWAKA 2022/2023

Ukaguzi huu umefanywa kwa kuzingatia misingi ya ukaguzi ya kitaifa na kimataifa ambapo mambo mbalimbali yamebainishwa ambayo yanahitaji kushughulikiwa na Serikali, Baraza la Wawakilishi pamoja na Uongozi wa taasisi husika ili kuhakikisha ufanisi katika utendaji wa shughuli za taasisi hizo unaimarika. Matokeo na mapendekezo ya ukaguzi yameainishwa kupitia ripoti hii kwa Taasisi zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kama ifuatavyo:-

### 7.1.1 BENKI YA WATU WA ZANZIBAR (PBZ)

Ukaguzi wa hesabu za Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Disemba, 2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo**

#### 7.1.1.1 Kutokuripotiwa kwa orodha kamili ya mikopo iliyofanyiwa maboresho

Ukaguzi ulifanya mapitio ya mikopo na malipo ya awali kwa wateja waliokopa benki ya PBZ na kubaini kwamba kulikuwa na mkopo kwa mteja aliyefariki dunia, ambao ulifanyiwa marekebisho mwezi wa Machi, 2023 na kubainika uwepo wa bakaa la deni linalodaiwa la shilingi 909,814,450. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokuripotiwa kwa orodha kamili ya mikopo iliyofanyiwa maboresho awali jambo ambalo lilipelekea kutokuonekana kwa deni linalodaiwa.

Kushindwa kuonyesha kwa deni hilo kwenye orodha kamili ya mikopo iliyorekebishwa inaweza kusababisha kukosekana kwa faida au kupatikana kwa hasara kwenye mikopo iliyorekebishwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kuhakikisha kuwa unaandaa na kusimamia orodha iliyokamilika ya mikopo iliyofanyiwa marekebisho katika mwaka wa fedha na kuijumuisha wakati wa kufanya ukokotoaji wa faida/ hasara kwenye mikopo iliyorekebishwa.

#### 7.1.1.2 Dosari zilizobainika katika majalada ya Mikopo (PBZ Conventional)

Ukaguzi ulifanya mapitio ya majalada ya mikopo na kubaini uwepo wa dosari zifuatazo:-

a) Kulingana na sera ya Benki ya Utoaji wa Mikopo imebainisha ukomo wa Ripoti za Tathmni kwa miaka mitatu, ukaguzi ulibaini uwepo wa ripoti za tathmini zilizopitwa na wakati kwa zaidi ya miaka mitano nyuma jambo ambalo ni kwenda kinyume na sera ya Benki ya Utoaji wa Mikopo. Mchanganuo wa ripoti za tathmini zilizopitwa na wakati ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 115: Ripoti za tathmini zilizopitwa na wakati kwa mujibu wa Sera ya Benki**

| Customer Name | Currency | Product Name | Total Exposure in TZS | Valuation report issued from | Valuation report issued date |
|---|---|---|---|---|---|
| THE HERITAGE ZANZIBAR COMPANY LIMIT | USD | TL | 144,694,572.25 | Stan Property | 30/06/2018 |
| SABAH STORE LIMITED SABAH STORE LIMI | TZS | TL | 113,128,860.97 | Stan Property | 02/03/2017 |
| URBAN AND RURAL ENGINEERING SE RVIC | TZS | OD | 2,690,369,686.25 | Stan Properties | 30/06/2016 |

**b) Dhamana zilizothaminiwa na wakadiriaji ambao hawajaidhinishwa na benki**

Ukaguzi ulifanya mapitio ya majalada ya Mikopo na kubaini uwepo wa vifaa (dhamana) ambavyo vimefanyiwa tathmini na wakadiriaji (wathamini) waliokuwa hawakuidhinishwa na Benki, ambapo kwa mujibu wa kumbukumbu na sera za benki zilizotolewa Juni, 2022 imebainika kuwa PBZ iliidhinisha wathamini wawili kutekeleza uthamini wa dhamana ambao ni M/S Nasia Consults na M/S Lipaz Mthamini ambaye hakuidhinishwa na bnki ni Consultants kama anavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 116: Mthamini ambae hakuidhinishwa na benki**

| Customer Name | Currency | Product Name | Total exposure in USD | Valuation report issued from | Valuation report issued date |
|---|---|---|---|---|---|
| Kendwa Limited | USD | Overdraft | 167,314.17 | LP Consultants | 01/12/2022 |

#### 7.1.1.3 Dosari zilizobainishwa katika Uzingatiaji wa sharia (PBZ Islamic)

Wakati wa mapitio ya mafaili ya Mikopo, ukaguzi umebaini dosari zifuatazo:-

**a) Dhamana zilizothaminiwa na wakadiriaji ambao hawajaidhinishwa na benki**

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na benki ya Juni, 2022 iliwaidhinisha M/S Nasia Consults na M/S Lipaz Consultants kuwa wathamini wa dhamana za benki. Katika ukaguzi uliofanyika ulipitia majalada mbali mbali na kubaini uwepo wa tathmini za dhamana zilizowasilishwa ambazo hazikutathminiwa na wathamini walioorodheshwa kwa mujibu wa toleo la Juni 2022, miongoni mwa wathamini hao ni kama inavyoonekana katika jadweli japo chini:-

**Jadweli Nambari 117: Mthamini ambae hajaidhinishwa na benki**

| Customer Name | Currency | Product | Eq Out Balance | Valuation report issued from | Valuation report issued date |
|---|---|---|---|---|---|
| Mwinyi Building Contractors Company Limited | TZS | Murabaha | 363,442,572.70 | Simba Salum | 01/03/2023 |

**b) Uwepo wa orodha kubwa ya mikopo ya awali iliyomaliza muda kwa wateja (matured)**

Ukaguzi ulifanya mapitio ya taarifa za fedha za benki ya Kiislamu ya PBZ kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Disemba, 2023 na kubaini kuwepo kwa jumla ya taarifa 51 za mikopo iliyopitwa na muda hadi kufikia muda wa ukaguzi ambapo bado mikopo hiyo ipo katika orodha ya mikopo iliyobainishwa kwenye vitabu vya benki yenye jumla ya shilingi 175,909,398.54 kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 5.**

Kutokana na uwepo wa dosari hiyo ukaguzi unaushauri uongozi wa Benki ya Kiislamu kuhakikisha unaweka kumbukumbu sahihi za mikopo katika taarifa za awali na pindipo itakapotokezea kufanyika kwa maboresho ya aina yoyote ni vyema kubainishwa tarehe halisi ya kuanza kwa mikopo na tarehe ya kumalizika kwa mikopo hiyo. Aidha, uwepo wa taarifa sahihi za tarehe za kuanza kwa mikopo kutaisaidia benki kufuatilia na kusimamia taratibu za urejeshwaji wa mikopo kwa wakati na hatimae kurahisisha ufuatiliaji wa mwenendo wa ulipwaji wa mikopo pamoja na utambuzi wa bakaa ya deni linalodaiwa kwa wateja.

### 7.1.1.4 Kutokuzingatiwa kwa matakwa ya kisheria katika utoaji wa mikopo

Kwa mujibu wa kanuni ya 9 ya Kanuni za Usimamizi wa Mali hatarishi za Benki na Taasisi za Fedha za 2014. Benki au taasisi ya fedha italazimika, katika kila uhakiki wa robo mwaka, kulipia gharama zote za malipo ya mikopo na mali nyingine hatarishi ambazo zimebakia katika kitengo cha hasara kwa robo mwaka mfululizo.

Ukaguzi ulibaini kuwa kuna mikopo ambayo imekuwa katika makundi ya hasara kwa zaidi ya robo mwaka mfululizo na mikopo hii haijatozwa kulingana na mahitaji ya BoT. Hadi kufikia tarehe 31 Disemba 2022, jumla ya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 2.725 ilikuwa ni mikopo ya muda mrefu iliyochelewa kulipwa. Kati ya mikopo hiyo ukaguzi umebaini kwamba jumla ya bakaa ya shilingi bilioni 2.636 ilikuwa ni mikopo kwa benki ya PBZ Conventional na shilingi milioni 89 kwa benki ya Kiislamu ya PBZ.

Kutokana na kutokufuatwa kwa misingi ya kanuni niliyoinakili hapo juu kunaweza kupelekea kujitokeza kwa vikwazo vinavyoweza kutolewa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kutokana na dosari ya kutokukidhi matakwa ya kanuni hizo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kuhakikisha unafuata na kutekeleza vigezo na masharti yaliyowekwa na Benki Kuu ya Tanzania ili kuepuka kujiingiza katika migongano ya kisheria ambayo inaweza ikashusha hadhi ya benki ya PBZ katika taratibu za utoaji wa mikopo ikiwa ni pamoja na kulipa fidia.

#### 7.1.1.5 Kutokufanyika kwa marekebisho ya thamani ya Mikopo iliyorekebishwa

Kwa mujibu wa aya ya 5.4.3 ya Vigezo vya Kimataifa vya Ufungaji wa Hesabu (IFRS 9) "Marekebisho ya mtiririko wa pesa za kimkataba" inaeleza kwamba Wakati wa kufanya majadiliano kuhusu mtiririko wa kifedha au kufanya marekebisho ya mali kwa mujibu wa vigezo haitopelekea kutokutambuliwa kwa mali iliyojadiliwa pamoja na kiwango cha mali hiyo. Taasisi itatakiwa kuhesabu upya na kufanya utambuzi wa mali pamoja na kubaini uwepo wa faida au hasara unaoendana na thamani halisi ya wakati uliopo au italazimika kufanyika upya kwa majadiliano pamoja na marekebisho ya mtiririko wa fedha utakaozingatia hali halisi ya wakati uliopo pale itakapohitajika.

Faida au hasara itakayopatikana itazingatia hali halisi ya wakati uliopo na itathaminishwa kwa kuangalia bakaa ya muda wa matumizi wa mali ya benki.

Kiasi cha jumla cha kubeba cha mali ya kifedha kitahesabiwa upya kama thamani ya sasa ya mtiririko wa fedha wa mkataba uliojadiliwa upya au uliorekebishwa ambao umepunguzwa kwa kiwango cha awali cha riba cha mali ya kifedha (au kiwango cha riba kinachofaa kilichorekebishwa kwa mkopo kwa kununuliwa au asili ya kifedha iliyoharibika. mali) au, inapotumika, kiwango cha faida kilichorekebishwa kinachokokotolewa na aya ya 6.5.10. Gharama au ada zozote zinazotozwa hurekebisha kiasi cha kubeba cha mali iliyorekebishwa na hupunguzwa kwa muda uliosalia wa mali iliyorekebishwa.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya taarifa za benki na kubaini kuwa kulikuwa na mikopo mitatu iliyopewa jina la Freedom Logistics, Tropical Air na Wakala wa Serikali wa Uchapaji ambayo ilifanyiwa marekebisho kwa kubadilishiwa utaratibu kutoka overdraft hadi muda wa mkopo wa kawaida pamoja na kufanyiwa marekebisho muda wa ulipwaji wa mikopo hiyo jambo ambalo lilipelekea kufanyiwa marekebisho ya mtiririko wa fedha na baadae ulijadiliwa upya bila ya kuzingatia matakwa ya viwango vya kimataifa vya ufungaji wa hesabu (IFRS-9) inayotambua kigezo cha faida na hasara ya utoaji wa mikopo.

Kutokana na mapitio ya taarifa za kibenki pamoja na ukokotoaji uliofanywa imebainika kwamba benki ilitakiwa kupata hasara ya shilingi 327,842,419.35 kutokana na kutofuatwa kwa vigezo na viwango vya Kimataifa vya Ufungaji wa Hesabu (IFRS 9).

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kuhakikisha inabaini faida au hasara ya marekebisho kwenye mikopo iliyorekebishwa na kutambua faida au hasara ipasavyo kulingana na kiwango.

#### 7.1.1.6 Uwepo wa Akaunti za dharura katika matawi ya Benki

Ukaguzi ulifanya mapitio ya vitabu vya kumbukumbu za benki na kubaini uwepo wa akaunti za dharura zinazotumika kuwekea kumbukumbu za miamala isiyohusiana na matawi ya benki ambapo ukaguzi umeshindwa kupata ufafanuzi juu ya uwepo wa akaunti hizo.

Uwepo wa akaunti za dharura inapelekea uwezekano wa kurikodi miamala ya uwongo ambayo inaweza kusababisha kuongezeka kwa mtaji wa benki au kupungua pamoja na kutokuzingatiwa kwa madeni ya benki.

Ukaguzi ulibaini kwamba PBZ ina akaunti mbalimbali za dharura ambazo zinapelekea uwepo wa mali na madeni kutokupitiwa kwa wakati, na bakaa ya fedha kuhaulishwa katika daftari kuu la benki jambo ambalo linaweza kupelekea benki kua katika hali ya hatari ya kuzidisha thamani ya mali ambayo itaenda kuathiri taarifa ya bakaa itakayoainishwa katika hesabu za mwisho wa mwaka.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kufanya mapitio ya sera ya upatanisho ili kuweza kuendana na wakati kwa kufanya upatanisho wa taarifa za fedha pamoja na taarifa za benki kwa lengo la kuonesha usahihi wa taarifa hizo kwa wakati. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 118: Taarifa za akaunti za dharura

| GL code | Amount | Amount (Tsh.) |
|---|---|---|
| 1921 | INTERBRANCH CLRG A/C FOR CENTRAL BR SUSP | 213,957,725.96 |
| 415 | INTERBRANCH SUSPENSE ACCOUNT | 3,157,127.66 |
| 1913 | SUSPENSE INTERBRANCH- OTHER BANKS POS | (304,183.35) |
| 1911 | SUSPENSE INTERBRANCH- OTHER BANKS ATMS | 557,719.80 |
| 1921 | INTERBRANCH CLRG A/C FOR CENTRAL BR SUSP | 9,875.22 |

### 7.1.1.7 Kutokutambulika kwa ada ya Upangaji wa Mikopo na Mapato

Kutokana na utaratibu wa upangaji wa mikopo imebainika ya kwamba Mikopo yote itatozwa asilimia 1 ikiwa ni ada za upangaji na uchakataji ambapo kwa upande wa "letter of Credit" na "Letter of Guarantee" itatozwa asilimia 1 na kwa upande wa mikopo ya nyumba "mortgages" itatozwa asilimia 0.75 kwa thamani halisi ya bima.

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Disemba, 2023 ilibainika uwepo wa gharama za uchakataji wa mikopo zilizofikia shilingi bilioni 5.9 ambazo zilitambulika kikamilifu katika kipindi cha mwaka wa utoaji wa mikopo, ambapo kwa mujibu wa viwango vya ufungaji wa hesabu vinahitaji gharama za uchakataji wa mikopo ziweze kutambuliwa kulingana na muda wa mkopo husika.

Aidha, malipo ya ujira yatokanayo na "letter of Credit" na "Letter of Guarantee" yalibainika kufikia shilingi milioni 479 ambayo yalitambulika kikamilifu kwa mwaka 2023 na kuhitajika kugawanywa katika kipindi chote cha huduma ya mkopo.

Kutokufanyika kwa tathmini vizuri kunaweza kupelekea kujitokeza kwa ongezeko la mikopo pamoja na kushindwa kusimamia vizuri taratibu za utoaji wa mikopo kwa wateja.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kuhakikisha unazingatia tathmini ya gharama za uchakataji wa mikopo katika kipindi chote cha muda wa utolewaji wa mkopo, vile vile si vyema kufanya utambuzi wa ukataji wa mikopo kwa muda wa mwaka mmoja. Hata hivyo, uongozi wa benki ni vyema kuhakikisha unazingatia Viwango vya Kimataifa vya Ufungaji wa Hesabu (IFRS) pamoja na viwango kubalifu vya kiuhasibu (GAAP).

### 7.1.1.8 Kutokuzingatiwa kwa utaratibu wa kushughulikia Malalamiko ya Wateja

Kwa mujibu wa kanuni za Benki ya Tanzania (BoT) zinazohusu ulinzi wa taarifa za fedha kwa watumiaji zimebainisha mambo mbalimbali yanayopaswa kuzingatiwa kama ifuatavyo:-

- Kila mtoa huduma za kifedha atapaswa kumfahamisha mtumiaji utaratibu unaotumika wa kushughulikia malalamiko ya wateja.
- Taarifa inayorejelewa chini ya kanuni ndogo (b) utaratibu wa utatuzi wa malalamiko ya wateja kwa benki.

Ukaguzi umebaini kutokuandaliwa kwa utaratibu wa ukusanyaji wa malalamiko kwa wateja na hatua zinazochukuliwa kushughulikia malalamiko ya wateja. Kutokana na hali hiyo benki inapaswa kuwa na utaratibu wa pamoja wa upokeaji wa malalamiko na ushughulikiaji wa malalamiko ya wateja ili iweze kuboresha utoaji wa huduma kwa wateja wake na hatimae kuweza kuboresha ufanisi wa huduma zinazotolewa.

Aidha, ukaguzi uliomba kupatiwa kumbukumbu za taarifa za malalamiko ya wateja kuhusiana na utoaji wa huduma na kubaini uwepo wa mkanganyiko wa taarifa zilizopokelewa ambazo bado hazijafanyiwa kazi, ingawa mtendaji mwenye dhamana ya kushughulikia malalamiko ya wateja alibainisha kwamba malalamiko yote yamefanyiwa kazi. Mchanganuo wa taarifa hizo ni kama unavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 6.**

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kuzingatia upokeaji wa malalamiko kwa wakati na kuyafanyia kazi kwa lengo la kuboresha huduma za benki zinazotolewa ili kuweza kupatikanwa kwa ufanisi wa huduma hizo ikiwa ni pamoja na kuharakisha upatikanaji wa mrejesho kwa wateja kuhusiana na malalamiko yote yaliyowasilishwa na kufanyiwa kazi.

### 7.1.1.9 Malipo ya posho la usumbufu yaliyolipwa bila ya kuzingatia taratibu za Kiutumishi shilingi 30,000,000

Kwa mujibu wa kanuni nambari 89(1) ya Kanuni ya Utumishi wa Umma ya 2014 inaeleza kwamba mtumishi atakaepewa uhamisho kutoka Unguja kwenda Pemba, Tanzania Bara au kinyume chake atapaswa kulipwa posho la usumbufu litakalokuwa sawa na posho la siku saba (7) pamoja na usafiri wa ndani kwa kufidia usumbufu atakaoupata katika kutekeleza amri hiyo ya uhamisho.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika Benki ya Watu wa Zanzibar imefanya malipo yenye thamani ya shilingi 30,000,000 kwa ajili ya kuwalipa watumishi walioajiriwa kwa ajira ya mkataba kwa vipindi vya rejewa rejewa kwa muda wa miaka mitatu (3) jambo ambalo haliendani na Kanuni ya Utumishi wa Umma kwa mazingatio ya kwamba watumishi hao ni waajiriwa wapya na sio waliohamishwa kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine ambao ndio wanaopaswa kulipwa posho la usumbufu.

Kufanya malipo ya fedha za umma bila ya kuzingatia Kanuni za Utumishi kunaweza kupelekea uwepo wa matumizi mabaya ya fedha ambayo yataisababishia hasara Serikali.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Bodi ya Benki ya Watu wa Zanzibar kuhakikisha unasimamia taratibu za urejeshwaji wa fedha za umma kwa kutoa miongozo kwa uongozi wa benki hiyo ili kuhakikisha wanakatwa wanufaika wote waliolipwa kinyume na utaratibu na kuweka nidhamu ya utekelezaji wa kanuni za utumishi wa Umma. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 119: Malipo ya posho la usumbufu yaliyolipwa bila ya kuzingatia taratibu za kiutumishi

| Namba | Jina la Mtumishi | Kiwango cha fedha alicholipwa (Tsh.) |
|---|---|---|
| 1. | Abdul Bilal Kandoro | 5,000,000 |
| 2. | Eddie Edward Muhina | 5,000,000 |
| 3. | Kassim Salim Said | 5,000,000 |
| 4. | Hilal Said Amour | 5,000,000 |
| 5. | Harith Habib Fentu | 5,000,000 |
| 6. | Dkt. Issa Salim Mohamed | 5,000,000 |
| **Jumla** | | **30,000,000** |

### Kutokufuatwa kwa taratibu za utoaji wa mikopo kwa watumishi waliopo katika muda wa majaribio (probation period) shilingi 1,036,785,631

Kwa mujibu wa Muongozo wa Mtumishi aliye katika kipindi cha majaribio wenye kumbukumbu namba CAB.78/388/01/6 wa tarehe 21/02/2022 umeeleza kwamba Mtumishi wa Umma ambae yupo katika kipindi cha majaribio pamoja na mambo mengineyo hastahiki kupatiwa au kunufaika na kudhaminiwa mkopo.

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar umetoa mikopo yenye thamani ya shilingi 1,036,785,631 kwa wafanyakazi wake bila ya kufuata Miongozo ya Utumishi ambapo wakati wa utoaji wa mikopo hiyo wafanyakazi hao walikuwa hawajathibitishwa kazini jambo ambalo ni kwenda kinyume na toleo nililolinakili hapo juu. Aidha, ukaguzi umebaini mikopo hiyo ilitolewa kinyume na utaratibu wa Sera ya Mikopo ya PBZ na bila ya kuidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya PBZ.

Kutoa mikopo kwa wafanyakazi waliokuwepo katika muda wa majaribio kunaweza kupelekea kuisababishia Serikali hasara pindipo mtumishi huyo atakaposhindwa kutekeleza majukumu yake au kutokuwa na ufanisi wa utekelezaji wa kazi zake na Serikali kuamua kusitisha ajira yake.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa PBZ kuhakikisha unaongeza umakini katika kufuata na kusimamia miongozo ya Utumishi wa Umma kikamilifu ili kuweka nidhamu ya matumizi ya fedha za Serikali. Mchanganuo wa watumishi hao na thamani ya mikopo waliyochukuwa ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 120: Mikopo iliyotolewa kwa watumishi walio katika kipindi cha majaribio

| Namba | Jina la Mtumishi | Kiwango cha Mkopo (Tsh.) | Benki (PBZ) |
|---|---|---|---|
| 1. | Abdul Bilal Kandoro | 206,205,000 | Conventional Bank |
| 2. | Eddie Edward Muhina | 102,881,631 | Conventional Bank |
| 3. | | 149,000,000 | Islamic Bank |
| 4. | Kassim Salim Said | 150,000,000 | Conventional Bank |
| 5. | Hilal Said Amour | 150,000,000 | Conventional Bank |
| 6. | Harith Habib Fentu | 83,000,000 | Conventional Bank |
| 7. | Mohamed Yussuf Nuh | 70,500,000 | H/O Mkopo wa Gari |
| | | 125,199,000 | Islamic Bank |
| **Jumla** | | **1,036,785,631** | |

### 7.1.1.11 Mikopo iliyolotewa bila ya kuzingatia kizingiti cha ukomo wa Utumishi shilingi 1,036,785,631

Kwa mujibu wa mazingatio ya ajira za watumishi walioajiriwa kwa kipindi cha mkataba na kwa mazingatio ya mkataba wa kuingizwa kazini mtumishi wa kujaribiwa anaweza kutolewa kazini kwa kupewa taarifa ya mwezi mmoja au anaweza kutoka kazini kwa kutoa taarifa ya mwezi mmoja au kwa kulipa mshahara wa mwezi mmoja pindipo atakapokosa kutoa taarifa hiyo.

Vile vile, ikiwa muda wa kujaribiwa na kabla ya kuthibitishwa kwake kazini imeonekana kuwa hana uwezo wa kazi au amefanya kosa au amepinga amri ya kazi basi anaweza kuachishwa kazi hapo hapo (bila ya kupewa taarifa).

Ukaguzi umebaini uwepo wa mikopo yenye thamani ya shilingi 1,036,785,631 iliyotolewa kwa watumishi sita (6) wa PBZ ambayo haiendani na muda wa mkataba wa ajira ambapo ajira zilizotolewa zilikuwa na ukomo wa mkataba wa miaka mitatu (3) lakini mikopo iliyotolewa ilikuwa na kikomo baina ya miaka mitano (5) hadi saba (7) jambo ambalo ni kinyume na sera ya mikopo ya benki.

Kutoa mikopo bila ya kuzingatia kizingiti cha ajira ya mtumishi kunaweza kupelekea kusababisha hasara kwa Serikali pindipo mtumishi huyo atakaposhindwa kurejesha mikopo kwa kusimamishwa au kuondoshwa kazini kabla ya ukomo wa kizingiti cha utumishi wake.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Benki ya Watu wa Zanzibar kuongeza umakini katika kusimamia misingi ya haki na taratibu za utumishi ili kujiepusha kujitokeza kwa vitendo vya uvunjwaji wa sheria na hatimae kuibebesha Serikali mzigo wa deni usio wa lazima.

Aidha, uongozi wa Bodi ya Wakurugenzi ya PBZ kuhakikisha unatoa miongozo kwa uongozi wa PBZ ili wanufaika wote wa mikopo iliyotolewa kinyume na kuzingatia kizingiti cha utumishi wao wanawasilisha dhamana ya mikopo yao ili kuwe na kidhibiti cha kushika pindipo watakaposhindwa kulipa mikopo yao au watakaposhindwa kupewa mikataba ya nyongeza inayoendana na ukomo wa muda waliopewa kurejesha mikopo yao.

Mchanganuo wa mikopo iliyotolewa bila ya kuzingatia kizingiti cha ukomo wa utumishi ni kama unavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 121: Mikopo iliyotolewa kwa watumishi walio katika kipindi cha majaribio**

| Namba | Jina la Mtumishi | Kiwango cha Mkopo (Tsh.) | Benki (PBZ) | Ukomo wa ajira | Muda wa kurejesha Mkopo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Abdul Bilal Kandoro | 206,205,000 | Conventional Bank | Miaka 3 | Miaka 7 |
| 2. | Eddie Edward Muhina | 102,881,631 | Conventional Bank | Miaka 3 | Miaka 7 |
| 3. | | 149,000,000 | Islamic Bank | | |
| 4. | Kassim Salim Said | 150,000,000 | Conventional Bank | Miaka 3 | Miaka 5 |
| 5. | Hilal Said Amour | 150,000,000 | Conventional Bank | Miaka 3 | Miaka 5 |
| 6. | Harith Habib Fentu | 94,012,739.92 | Conventional Bank | Miaka 3 | Miaka 7 |
| 7. | Mohamed Yussuf Nuh | 70,500,000 | H/O Mkopo wa Gari | Miaka 3 | Miaka 7 |
| | | 125,199,000 | Islamic Bank | | |
| **Jumla** | | **1,036,785,631** | | | |

### 7.1.1.12 Mikopo iliyoidhinishwa kinyume na Sera ya Mikopo ya Benki shilingi 458,086,631

Kwa mujibu wa utaratibu wa watumishi wanaoajiriwa kutoka sekta nyengine ya benki ambao wanakuja na mikopo yao uongozi wa PBZ unatakiwa uwataarifu Bodi ya Wakurugenzi ya PBZ ili kutoa maamuzi sahihi ya ajira za watumishi hao pamoja na kufanya maamuzi ya kina juu ya uhitaji wa mtumishi huyo kwa lengo la kuinunua mikopo hiyo kutoka benki wanazotoka.

Aidha, kwa mujibu wa sera ya mikopo ya 2023 iliyotolewa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ lending Policy, 2023) iliweka ukomo wa kiwango cha uidhinishwaji wa mkopo kwa watumishi kwa kiwango cha ukomo wa mkopo wenye thamani ya shilingi 200,000,000 ambao utaidhinishwa na Mkurugenzi mtendaji wa Benki ya PBZ, na pindipo kiwango hicho kitakapozidi kwa mtumishi wa PBZ italazimika kuombwa ridhaa kwa Bodi ya Wakurugenzi ya PBZ.

Ukaguzi umebaini uwepo wa watumishi wawili waliochukuwa mkopo binafsi (personal loan) ima kwa kuajiriwa nao au kwa kuomba Benki ya Watu wa Zanzibar uliozidi ukomo wa kiwango kubalifu kwa mujibu wa Sera za Mikopo ya PBZ, 2023 ambao umeidhinishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa PBZ bila ya kutolewa taarifa na kuidhinishwa kwenye Bodi ya Wakurugenzi ya PBZ jambo ambalo ni kwenda kinyume na Sera hiyo pamoja na kukengeuka maamuzi ya Bodi ya Wakurugenzi ya PBZ.

Kufanya maamuzi ya uajiri wa watumishi wenye mikopo mikubwa au kuruhusiwa kuchukuwa mikopo mikubwa yenye ukomo wa idhini ya uongozi wa PBZ bila ya kushirikishwa maamuzi ya Bodi ya PBZ kunaweza kupelekea kujitokeza kwa viashiria vya matumizi mabaya ya Ofisi kutokana na kufanyika maamuzi kwa maslahi binafsi na yenye kuzingatia utashi wa mtu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa PBZ kuhakikisha maamuzi yoyote wanayoyatoa ambayo yapo nje ya mamlaka ya uongozi wa PBZ ni vyema kushirikishwa Bodi ya Wakurugenzi wa PBZ ili kuweza kupata ridhaa ya maamuzi ya pamoja.

Miongoni mwa wanufaika wa mikopo hiyo iliyoidhinishwa kinyume na sera ya PBZ ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 122: Mikopo iliyoidhinishwa kinyume na sera ya mikopo ya Benki**

| Namba | Jina la Mtumishi | Kiwango cha Mkopo (Tsh.) | Benki (PBZ) | Ukomo wa ajira | Muda wa kurejesha Mkopo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Abdul Bilal Kandoro | 206,205,000 | Conventional Bank | Miaka 3 | Miaka 7 |
| 2. | Eddie Edward Muhina | 102,881,631 | Conventional Bank | Miaka 3 | Miaka 7 |
| | | 149,000,000 | Islamic Bank | | |
| **Jumla** | | **458,086,631** | | | |

### TAARIFA ZA UKAGUZI WA BENKI YA MuCoBa – PLC KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 31 DISEMBA, 2022

Katika mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Disemba, 2022 ukaguzi ulifanya mapitio ya taarifa za ufungaji wa hesabu wa Benki ya MuCoBa ambayo ni sehemu ya Benki ya PBZ kutokana na benki hiyo kuuza hisa nyingi kwa PBZ. Katika mapitio hayo imebainika uwepo wa dosari mbalimbali ambazo zimepelekea benki ya MuCoBa kupata **Hati Yenye Shaka** kutokana na uwasilishaji wa taarifa za ufungaji wa hesabu ambazo zilitolewa maoni ya ukaguzi na kubainika uwepo wa dosari mbalimbali ambazo zimepelekea kutokuonesha sura sahihi na halisi ya taarifa za hesabu zilizoandaliwa. Miongoni mwa dosari zilizobainika na kupelekea kutolewa kwa hati hiyo ni kama zifuatazo:-

- **Mikopo ya wateja na malipo ya awali yenye thamani ya shilingi bilioni 4.35 kutokuendana na hali halisi ya orodha ya wateja wanaodaiwa na benki**

Kutokana na dosari hiyo ukaguzi umebaini mikopo ya wateja na malipo ya awali kwa bakaa ya fedha iliyoripotiwa katika taarifa ya fedha ni kubwa kuliko jumla ya kiasi cha mikopo na malipo ya awali kwa wateja katika vitabu vya hesabu (General Ledgers) ambayo inakubaliana na kiasi kilichobainishwa katika vitabu vya mikopo.

Kutokana na hali hiyo jumla ya shilingi bilioni 4.35 za mikopo na malipo ya awali kwa bakaa iliyowasilishwa katika hesabu ya mezania si katika deni ya bakaa ya wadaiwa iliyoripotiwa na uongozi wa benki jambo ambalo hakukuwa na hatua zilizochukuliwa kwa kulifuta au kuliondoa katika taarifa za hesabu.

- **Kutokuendana kwa orodha ya mali nyenginezo zilizobainishwa katika hesabu ya mezania zenye thamani ya shilingi bilioni 1.27**

Ukaguzi umebaini uwepo wa taarifa za mali nyenginezo (other assets) zilizobainishwa katika hesabu za mezania ambazo haziendani na uhalisia wa taarifa hizo katika orodha ya taarifa nyenginezo ambapo kiasi hicho kitapatikana na wala hakuna ushahidi wa kwamba faida za kiuchumi za baadae zitaingia Benki kuhusiana na mali hii. Licha ya hayo, wasimamizi na wakurugenzi wa Benki hawakuchukuwa hatua za kulifuta au kuondoa taarifa za mali nyenginezo katika vitabu vya benki.

Kutokana na uwepo wa dosari zilizobainishwa hapo juu imebainika mali zinazowiana zimezidishwa (overstated) kwa kiasi kilichoonyeshwa vile vile hasara ya ujumla iliyobainishwa ilipunguzwa na kufikia shilingi bilioni 5.62. Iwapo makosa yalisahihishwa, kiwango cha kodi kilipaswa kulipwa zaidi kwa shilingi bilioni 1.7 na uwiano wa msingi na jumla wa utoshelevu wa mtaji unapaswa kuwa hasi asilimia 21.61 na asilimia 16.50 badala ya chanya asilimia 11.88 na asilimia 15.58.

- Kiasi cha Amana kinachodaiwa chenye thamani ya shilingi bilioni 1.22 kilichobainishwa katika rejista ya amana hakikubainishwa katika hesabu za mezania.
- Kiasi linganishi cha mtaji wa hisa na masalio ya mali nyingine yaliyoripotiwa katika taarifa za fedha za mwaka wa ukaguzi zinatofautiana na kiasi husika kilichoripotiwa katika taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita kwa thamani ya shilingi bilioni 1.13. Aidha, taarifa za fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita zilionyesha kuwa mtaji wa hisa na mali nyinginezo ni shilingi bilioni 7.04 na shilingi bilioni 3.31. Kinyume chake, taarifa linganishi za fedha katika taarifa za fedha za mwaka huu zinaonyesha shilingi bilioni 8.17 na shilingi bilioni 4.44 mtawalia.
- Ukaguzi ulifanya mapitio ya taarifa za fedha za benki na kubaini uwepo wa shilingi milioni 598 ambazo zimetambuliwa kwa mwaka uliopita kama marekebisho ya mwaka katika taarifa ya mabadiliko ya mtaji (statement of changes in equity), hata hivyo msingi wa marekebisho hayo na maingizo ya taarifa za fedha zinazokubaliana (contra entry) hazijalingana. Aidha, mahitaji ya uwasilishaji na ubainishaji yanayohusiana na marekebisho ya mwaka uliopita kama ilivyobainishwa katika IAS 1 Uwasilishaji wa taarifa za fedha na Sera za Uhasibu na IAS 8 Mabadiliko katika Makadirio ya Uhasibu na Hitilafu hazijazingatiwa katika taarifa za fedha.
- Ukokotoaji wa mahesabu ya upotevu wa mikopo unaotarajiwa yalionyesha mikopo na malipo ya awali kwa wateja yenye jumla ya shilingi bilioni 11.19 ambayo ilikuwa chini ya kiasi kilichotambulika katika Kielelezo nambari 17 (Note 17) cha taarifa za ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka kwa shilingi bilioni 15.69.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa benki kuzingatia vigezo vya mtazamo wa mbele vya uchumi mkuu (macro-economic variable) katika kukokotoa upotevu wa mikopo unaotarajiwa pamoja na kufanya mazingatio ya viwango vya kimataifa vya ufungaji wa hesabu (IFRS 9).

### 7.1.2 MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR (ZRA)

Ukaguzi wa Hesabu za Mamlaka ya Mapato Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya Kitaifa na Kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 7.1.2.1 Makosa yaliyobainishwa katika Mchakato wa Ununuzi wa Magari

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ukaguzi umefanya mapitio ya daftari la Mali za Kudumu za Mamlaka ya Mapato Zanzibar na kubaini uwepo wa ununuzi wa magari 7 kwa thamani ya shilingi 666,525,000 pamoja na kuangalia mchakato mzima wa manunuzi ukaguzi ulibaini uwepo wa dosari zifuatazo:-

**a) Ucheleweshaji wa uwasilishaji wa Magari uliosababishwa na Wakala wa Serikali anayewajibika na Ununuzi wa Magari (Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango)**

Ilibainika kuwa ZRA ilitoa mahitaji yake ya manunuzi kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha na Mipango tangu tarehe 15/08/2022, hata hivyo, magari 7 yaliwasilishwa na kukabidhiwa kwa ZRA kati ya Januari 2023, hadi Juni, 2023. Hivyo, mchakato wa ununuzi ulichukua takriban miezi 11 kukamilika.

**b) Ugavi wa Magari Kinyume na Masharti ya Mtumiaji**

Mapitio ya nyaraka za uagizaji na uwasilishaji wa magari 7 ulibaini kwamba magari yaliyowasilishwa na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango yalikuwa kinyume na mahitaji ya mtumiaji (SPECS) yalipelekwa kwa wakala wa ununuzi (Ofisi ya Rais Fedha na Mipango) tarehe 15/8/2022. Ilibainika kwamba ZRA ilihitaji idadi ifuatayo ya magari pamoja na sifa zake kama ifuatavyo:-

(i) Magari 6 ya TOYOTA LAND CRUISER STATION WAGON kwa ajili ya shughuli za kukusanya mapato na shughuli nyingine za kila siku za ofisi.

(ii) Basi 1 dogo (TOYOTA HIACE yenye viti 15) kwa ajili ya matangazo na shughuli za kampeni ya uhamasishaji umma ili kuimarisha utii wa ulipaji wa kodi wa hiari kwa walipa kodi.

Kwa mujibu wa mahojiano yaliyofanywa na maofisa wanaohusika na uendeshaji wa magari kila siku yalibaini kuwa maelezo ya kiufundi (Technical Requirements/ SPECS) yaliyopelekwa kwa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango yalilenga kupunguza gharama za uendeshaji wa mafuta wakati wa kuwatembelea walipakodi na shughuli nyingine za kila siku za ofisi kwa kuwa watumishi wengi zaidi wangechukuliwa kwa mara moja kwenye gari moja kwa safari moja badala ya kutumia magari mengi kwa safari moja yenye madhumuni sawa.

Hata hivyo, ilibainika kuwa magari hayo 7 yaliletwa kinyume na matakwa ya mtumiaji ambapo gari tano (5) aina ya Toyota Hilux Double Cabin na gari mbili (2) aina ya hard top double cabins badala ya 6 aina ya TOYOTA LAND CRUISER STATION WAGON na basi moja (1) dogo aina ya TOYOTA HIECE yenye viti kumi na tano (15) kama ilivyohitajika.

Ucheleweshaji usiostahili katika uwasilishaji wa magari kulingana na matakwa ya mtumiaji unaofanywa na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango husababisha uhaba wa magari na usumbufu wa vyombo vya usafiri kwa ZRA katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

Uwasilishaji wa magari kinyume na mahitaji ya mtumiaji huongeza gharama za uendeshaji wa shughuli za ZRA za kila siku katika suala la mafuta na ukarabati na matengenezo kwa kutumia idadi kubwa ya magari kwa safari moja badala ya moja kulingana na mahitaji ya mtumiaji.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar kufanya mambo yafuatayo:-

- Kukaa na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango na kujadiliana juu ya suala la upatikanaji wa magari kwa wakati na kukidhi matakwa ya watumiaji kuhusu mchakato wa ununuzi wa magari ya Mamlaka kwani inachangia uzembe katika ukusanyaji wa mapato kulingana na lengo lililowekwa.
- Pale ambapo inaonekana haiwezekani kununua magari kulingana na mahitaji ya mtumiaji na kwa wakati muafaka, maazimio yanapaswa kufikiwa ili kuruhusu mtumiaji aidhinishiwe kununua magari yake, na Taasisi ya Serikali inayohusika na ununuzi wa magari ibaki na kazi ya usimamizi wa michakato ya ununuzi.

### 7.1.2.2 Utekelezaji duni wa Mpango wa Manunuzi wa Mwaka wa fedha 2022/2023

Mapitio ya utekelezaji wa jumla wa shughuli za manunuzi zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umebaini kuwa kati ya shughuli 95 zilizopangwa, shughuli 50 hazikutekelezwa sawa na asilimia 53 na 45 zilitekelezwa sawa na asilimia 47. Kwa ujumla, hali ya utekelezaji wa mpango wa manunuzi wa mwaka wa fedha 2022/2023 ilionekana hafifu.

Uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa mpango wa mwaka wa manunuzi umebaini mambo makuu yafuatayo yaliyochangia kutokutekelezwa ipasavyo kwa mpango wa mwaka wa manunuzi katika mwaka unaokaguliwa:-

- Uratibu hafifu kati ya Kitengo cha Manunuzi na Ugavi (PDMU) na idara ya watumiaji kuhusiana na utoaji wa mahitaji ya mtumiaji (TOR/Specifications) ili kuwezesha utekelezaji kwa wakati wa shughuli zilizopangwa

Mapitio ya muhtasari wa bodi ya zabuni na taarifa ya utekelezaji kuhusu hali ya mpango wa manunuzi wa mwaka kwa mwaka wa ukaguzi umebaini baadhi ya shughuli zilizopangwa ambazo hazikuweza kufanyika au kucheleweshwa utekelezaji wake kutokana na kutoeleweka kwa mahitaji ya watumiaji hali iliyosababisha matatizo kwa wazabuni kwani haikuweza kueleweka vyema na kusababisha bei kubwa kinyume na kiasi kilichopangwa. Kesi zilizobainishwa ni kama inavyoonyeshwa kwenye jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 123: Cases Noted to Illustrate delay in execution of Annual Procurement Plan caused by user department in furnishing of user requirements/ TOR/Specifications**

| Procurement activity planned | Remarks on the user requirement | Tender Board Decision | Tender Board Minutes Reference |
|---|---|---|---|
| Supply of oracle | There was a big price difference between the Highest and lowest bidder to the tune of TZS 758,772,175 whereas the highest bidder (M/s Dynatec Solutions Ltd) quoted TZS 998,772,175 and the lowest bidder (M/s Rana Technologies) quoted TZS 240,000,000. This casted doubts to the clarity of specification for the tender floated. | The tender was awarded to the second bidder M/s SCI Tanzania LTD at contract sum of TZS 884,773,000 (VAT exclusive). However, the same could not be executed due to price quoted being above the budgeted amount. | 21 dated 27.3.2023 and 23 dated 24.4.2023. |
| Supply of desktop and laptop computers | There was a big price difference between the Highest and lowest bidder to the tune of TZS 541,800,000 whereas the highest bidder quoted TZS 766,275,000 and the lowest bidder quoted TZS 224,475,000. This casted doubts to the clarity of specifications for the tender floated. | The second lowest M/s Visiwani General Supplier was awarded the tender at a contract sum of TZS 723,500,000. However, the ICT department was required to review the specifications and readvertise the tender. | 18 dated 15.02.2023 and 21 dated 27.3.2023 |

Tatizo la ukwasi wa fedha pia lilichangia zaidi katika utendaji duni wa shughuli zilizopangwa za manunuzi kulikosababishwa na zabuni zilizoelezwa kuwa juu ya kiasi kilichopangwa kilichochochewa na bajeti zisizo halisi zilizowekwa na mtumiaji wakati wa kupanga mahitaji na ufinyu wa bajeti toka Serikalini kulichangia kuzorotesha utekelezaji wa mpango wa manunuzi kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini:-

### Jadweli Nambari 124: Procurement Performance Vs Budget Performance

| Procurement Performance 2022/23 | | | | | | Budget Performance 2022/23 (TZS in Billion) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Procurement category** | **Planned** | **Completed** | **Not completed** | **% completion** | **% not completed** | **Budget** | **Actual** | **Percentage (%)** |
| Goods | 50 | 27 | 23 | 28 | 24 | 7.951 | 1.842 | 13.25 |
| Works | 8 | 1 | 7 | 1 | 7 | 2.192 | 0.076 | 0.55 |
| Non-Consultancy | 25 | 15 | 10 | 16 | 11 | 2.972 | 1.368 | 9.84 |
| Consultancy | 12 | 2 | 10 | 2 | 11 | 0.785 | 0.079 | 0.56 |
| **Total** | **95** | **45** | **50** | **47** | **53** | **13.9** | **3.365** | **24.2** |

Mahitaji yasiyo sahihi ya mtumiaji yanasababisha bajeti isiyo halisi iliyowekwa wakati wa hatua ya kupanga manunuzi, kwa hivyo, kufanya Mpango wa manunuzi wa Mwaka kuwa vigumu kutekeleza.

Ukwasi wa kifedha huzuia utekelezaji wa shughuli nyingi zilizopangwa, hivyo huvuruga shughuli za kila siku za Mamlaka na hivyo kushindwa kutekeleza shughuli zake zilizotarajiwa ambazo zilitegemeana na manunuzi yasiyofanyika.

Kuna uwezekano mkubwa kwamba idara za watumiaji hazifahamu kikamilifu jukumu lao muhimu kuhusu utayarishaji na utekelezaji wa mpango wa ununuzi wa kila mwaka, hivyo kukwamisha utekelezaji wa Mpango wa Manunuzi wa Mwaka.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar kufanya yafuatayo:-

- Maandalizi ya mpango wa ununuzi wa mwaka yawe ni shirikishi (mfumo wa kuunganisha). Idara za watumiaji, Kitengo cha Manunuzi na Ugavi (PDMU) na sehemu ya fedha zinapaswa kutekeleza shughuli zilizoratibiwa kwa karibu.
- Kila idara ya watumiaji inapaswa kubainisha wazi mahitaji yake, kufanya uchunguzi au utafiti wa kina wa bei na uwezo wa kufanya shughuli zilizopangwa kabla ya kupeleka mipango hiyo kwa Kitengo cha Manunuzi na Ugavi (PDMU) kwa ajili ya utekelezaji.
- Mahitaji yaliyotambuliwa ya mtumiaji (SPECS/TOR) yanapaswa kutumwa kwa wakati kwa Kitengo cha Manunuzi na Ugavi (PDMU). Pia, Kitengo cha Manunuzi na Ugavi kinapaswa kuwa na utaratibu wa udhibiti wa kuzikumbusha idara za watumiaji kutekeleza jukumu lao muhimu ili kuhakikisha utekelezaji mzuri wa zabuni kama ilivyopangwa katika mpango.
- Kutoa uelewa (mafunzo) kwa idara za watumiaji kuhusu jukumu wanalotekeleza katika mipango ya ununuzi na utekelezaji ili kuepuka utayarishaji wa mipango ya manunuzi isiyo ya kweli kwa kuzingatia bei zisizo halisi.

### 7.1.2.3 Kutokubainishwa kwa Tathmini ya Kodi kwa muda mrefu

Ukaguzi ulifanya mapitio ya orodha ya madeni yanayotokana na kodi ambayo yamebainika kuwa na migogoro kuanzia mwaka 2014 - 2022 na kubaini kwamba mashauri yanayotokana na kodi ya muda mrefu hayakuweza kubainishwa. Vile vile ushahidi unaotokana na ufuatiliaji uliofanywa na uongozi haukuweza kubainika jambo ambalo limepelekea kushindwa kufanya utambuzi unaotokana na usahihi wa madeni yaliyobainishwa. Mchanganuo wa madeni hayo ni kama inavyoonekana katika **Kiambatisho Nambari 7.** Kuendelea kuwepo kwa kodi za muda mrefu ambazo zimeshindwa kufanyiwa tathmini kunapelekea mambo yafuatayo:-

- Kutokuwepo kwa usahihi wa urejeshwaji wa kodi zenye mgogoro kwa muda mrefu ambazo hazijashughulikiwa.
- Upotevu wa mapato ya Serikali kwa kodi iliyopingwa ambayo haijakusanywa na kuthibitishwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka kuimarisha juhudi za ufuatiliaji ili kujua uwepo na usahihi wa tathmini za kodi zenye mgogoro za muda mrefu na kutekeleza hatua za ukusanyaji kulingana na Sheria ya Kodi (TAPA Na.7 ya 2009).

### 7.1.2.4 Kutokuwepo kwa Muongozo wa Taratibu za Kawaida uliohifadhiwa na Uelewa Mdogo kwa Walipakodi Kuhusu Mchakato wa Utatuzi wa Migogoro ya Kodi

Kwa mujibu wa Mpango kazi wa Usimamizi wa Kodi na Tathmini ya Chombo cha Uchunguzi wa Tathmini (TADAT) 2020/2021- 2024/25 umebaini kuwa moja ya maeneo ambayo yanahitaji kuimarishwa ndani ya Mamlaka ili kuongeza ufanisi wa mapato ni kuwa na utatuzi wa migogoro ya kodi na hili linaweza kufikiwa kupitia kuandaa muongozo wa taratibu za kawaida ambao utatoa kwa kina taratibu zote za migogoro ya kodi kuanzia hatua ya awali hadi mwisho na mrejesho wa mchakato unapaswa kutolewa hadharani ili walipakodi waweze kufahamu mchakato na haki zao za kukata rufaa baada ya ukaguzi.

Mchakato wa uhamasishaji unaweza kuundwa kupitia utayarishaji na uchapishaji wa nakala ngumu au laini za vipeperushi inayoweza kufikiwa yenye taarifa muhimu kuhusu mchakato wa utatuzi wa migogoro na haki za walipa kodi za kukata rufaa baada ya ukaguzi (muhtasari wa muongozo wa utaratibu wa Ukaguzi na Rufaa).

Hata hivyo, mapitio yetu ya mawasiliano kati ya Mamlaka na walipakodi mbalimbali kupitia uhakiki wa mafaili ya walipakodi yenye pingamizi zilizotolewa yalidhihirisha uelewa mdogo wa walipakodi kuhusu mchakato wa utatuzi wa mgogoro huo kwani wengi wao walionekana kusita kulipa kiasi kinachohitajika kwa mujibu wa Sheria ya kodi (TAPA namba 7 ya mwaka 2009) ili migogoro hiyo iweze kupokelewa bila sababu za msingi kufanya hivyo, baadhi walirukia ngazi ya Bodi ya Rufaa bila kusikilizwa na Mamlaka na baadhi waliwasilisha pingamizi ambazo zimepitwa na wakati (time bared).

Ukaguzi ulibaini kwamba Mamlaka ya Mapato ilitayarisha muongozo wa utatuzi wa migogoro kama nyenzo ya kufanyia kazi ndani na kwa washikadau wengine ili mchakato wa utatuzi wa migogoro upatikane vizuri na ueleweke ndani na hadharani ili kupunguza machafuko katika kushughulikia migogoro ya kodi na kuimarisha ukusanyaji wa mapato.

Mchakato wa utatuzi wa migogoro ya kodi usio na tija unaweza kusababisha uzembe katika ukusanyaji wa mapato kwa kushindwa kufikia tamati/hatma ya mzozo wa kodi iliyotathminiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar kuanzisha muongozo na kanuni za kawaida kuhusu usuluhisho wa migogoro ya kodi na ufahamu wake unapaswa kupatikana kwa urahisi kwa walipakodi na umma kwa ujumla ili kuwezesha mchakato wa migogoro ya kodi unaolenga kuboresha ukusanyaji wa mapato.

#### 7.1.2.5 Ukosefu wa Sera kuhusu Utambuzi wa Walipakodi Wasiofanya kazi/ Waliolala, Wasiowasilisha ritani na Wasiolipa

Ili Mamlaka iwe na uadilifu wa msingi wa walipakodi waliosajiliwa kama ilivyoainishwa katika mpango kazi wa TADAT (2020/2021 - 2024/2025) Mamlaka inatakiwa kuandaa na kutekeleza taratibu za kuwatambua walipakodi wasiofanya kazi au waliolala ili kuwezesha uainishaji wa walipakodi wote kama hai au asiyefanya kazi, kulingana na tabia yao ya uwasilishaji ritani.

Mapitio ya orodha ya walipakodi kulingana na aina za kodi ambayo yalitolewa kwa madhumuni ya ukaguzi yalionyesha kuwa walipakodi wote waliopatikana waliitwa walipakodi hai kama ilivyobainishwa baada ya mahojiano na wakuu wa idara wanaowajibika. Ilibainika kuwa kupitia orodha kama hiyo walipakodi wasiowasilisha na wasiolipa walipatikana kulingana na tabia zao za uwekaji kumbukumbu na malipo.

Mahojiano zaidi na wakuu wa idara yamebaini kuwa, kwa sasa Mamlaka iko katika awamu ya mpito ya kuhamisha takwimu za walipakodi wakubwa kutoka ZITAS (Mfumo wa mapato unaokaribia kufutwa) kwenda kwenye mfumo mpya unaojulikana kama ZIDRAS kuchukua nafasi ya mfumo wa zamani kwani mfumo wa zamani ulikuwa na takataka nyingi kuhusu kanzidata ya walipakodi ikijumuisha uwepo wa idadi kubwa ya walipa kodi wasiofanya kazi/waliolala. Hata hivyo, haikuwa dhahiri kwetu kama Mamlaka imetayarisha/kuandaa taratibu za utambuzi (vigezo) vya walipakodi wasiofanya kazi au waliolala kulingana na tabia zao za uwasilishaji ritani, ili tatizo la kanzidata isiyo sahihi ya walipakodi isijirudie katika mfumo mpya.

Bila kuweka vigezo vya ufafanuzi na utambuzi wa mlipakodi aliyelala/asiyefanya kazi inaweza kuwa vigumu kuwafuatilia walipa kodi waliokiuka kwa usahihi na kuanzisha hatua za utekelezaji kulingana na kipengele cha ukiukwaji (asiye faili au asiye mlipaji).

Idadi sahihi ya walipakodi waliosajiliwa na waadilifu inaweza isipatikane na hivyo basi kuna uwezekano mkubwa wa hitilafu hii kushindwa kutambua usahihi wa namba ya walipa kodi kujirudia katika mfumo mpya wa ZIDRAS kwa kushindwa kuunda vigezo vya kutambua mlipakodi asiyefanya kazi/aliyelala.

Wasimamizi wanapaswa kuunda sera ya maandishi na kutekeleza taratibu za utambuzi wa walipa kodi wasiofanya kazi au waliolala ili kuwezesha kufichua ripoti sahihi ya walipa kodi wasiotii sheria kwa hatua zaidi za utekelezaji na kuwa na uadilifu wa kanzidata ya walipa kodi.

#### 7.1.2.6 Idadi Kubwa ya Tathmini ya Kodi isiyo sahihi iliyopelekea kuongezeka kwa Tathmini za Kodi zilizowekewa pingamizi

Ilibainika kuwa Mamlaka ilipokea na kushughulikia mapingamizi 34 ya kodi. Mapitio yetu ya mawasiliano yaliyofanywa kati ya ZRA na walipakodi mbalimbali waliowasilisha pingamizi la ukaguzi wa kodi au uhakiki uliofanywa katika mwaka wa ukaguzi ulidhihirisha pingamizi nyingi za kodi zilizotolewa zilitokana na tathmini zisizo sahihi ambazo mwishowe zinaweza kupunguzwa kwa kiasi kikubwa baada ya kutathminiwa upya. Kushindwa kwa wakaguzi wa kodi kuelewa shughuli za walipakodi au kutokuwa na uwezo katika eneo wanalolikagua kulionekana kama sababu kuu za kutolewa kwa tathmini za kodi zisizo sahihi. Kesi hii imebainishwa zaidi katika taasisi zinazohusiana na shughuli za kipekee. Kesi chache kwa madhumuni ya kielelezo zimeonyeshwa kwenye **Kiambatisho Nambari 8.**

Tathmini zisizo sahihi husababisha migogoro mingi ya kodi na mashauri ya kwenda mahakamani (Tax Appeals Board and Tribunal) na hivyo kuinyima Serikali kupata mapato yake yanayohitajika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar kufanya tathmini ya eneo hili kuhusu sababu za tathmini za kodi zisizo sahihi na kuchukua hatua muhimu za kukabiliana na hali hiyo ikiwa ni pamoja na kuwajengea uwezo wakaguzi wa kodi ili kuboresha ukusanyaji wa mapato kwa njia ya ukaguzi wa kodi kwa kuwa ina mchango mkubwa katika ukusanyaji wa mapato ili kufichua kodi iliyopunguzwa katika mwaka husika wa mapato.

### 7.1.2.7 Hatima Isiyojulikana ya Tathmini Zinazobishaniwa

Mapitio ya rekodi za tathmini zilizobishaniwa yalidhihirisha matukio ya idadi ya pingamizi zilizokuwa chini ya utatuzi wa migogoro, hata hivyo hatima yao haikuweza kujulikana kutokana na kukosekana kwa muendelezo/mawasiliano zaidi katika mafaili ya walipa kodi yaliyopitiwa. Pia ilibainika kuwa wakati tathmini za awali za kodi zilizoibuliwa ambazo zilikuwa na mgogoro hazijakamilika tena mlipakodi aliarifiwa kuhusu ukaguzi mpya wa kodi utakaofanywa. Hali iliyobainika inakatisha tamaa walipakodi kufuata sheria ya ulipaji kodi kwa hiari kutokana na usumbufu na mkusanyiko wa tathmini za kodi ambazo haziwezi kulipika kutoka kwa walipakodi hao kutokana na mianya ya sheria za kodi (TAPA Sheria namba 7 ya 2009 RE) ambazo walipa kodi wengi wanazitumia ili kuepuka mzigo wa kodi zilizotolewa kwa njia ya adhabu na riba. Mifano ya kuelezea hali iliyobainika imeonyeshwa chini ya **Kiambatisho Nambari 9.**

Upotevu wa mapato ya serikali kwa kuongeza tathmini ya kodi ambayo haiwezi kukusanywa haikuweza kudhibitishwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar kuhakikisha kuwa usuluhisho wa mizozo ya kodi unatekelezwa na kumalizwa kwa wakati unaofaa inapobidi. Matokeo ya hitimisho lililofikiwa yanapaswa kuandikwa na kuwasilishwa ipasavyo kwa madhumuni ya marejeo ya baadaye na yeyote anayetaka rekodi hiyo kwa madhumuni mbalimbali ya kufanya maamuzi ikiwa ni pamoja na kuanzisha ukaguzi mpya wa kodi.

### 7.1.2.8 Dosari katika Ukusanyaji wa Chanzo cha Mapato ya Bandari-Seaport (Kutobadilisha sarafu ya USD inayolipwa na wageni (foreigners) kuwa Sarafu ya Ndani)

Ukaguzi umebaini kwamba Sheria ya Tozo ya Huduma ya Bandari Na.2 ya mwaka 1998 (R.E 2013) kifungu cha 3 (Jedwali II) inamtaka kila abiria anayetoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara au Zanzibar kwenda Zanzibar alipe fedha za ndani kwa njia ya shilingi za Tanzania. Hata hivyo, kifungu kilichotajwa kilionekana kikiwa na hitilafu ambapo hakikuweza kueleza kwa uwazi ni kiasi gani cha dola kinaweza kulinganishwa na shilingi ya Tanzania kwa mujibu wa kiwango kulingana na tarehe ya muamala wakati mtu asiye mkaazi analipia tiketi kwa sarafu ya Dola kama uthibitishaji wetu wa marejesho ya kodi ya kila mwezi. Kampuni za Meli za baharini zilieleza kuwa abiria wasio wakazi walikuwa wakilipia tiketi hizo kwa sarafu ya Dola, lakini marejesho yaliyowasilishwa yalisema abiria wote ni wa ndani kwani walikuwa wakilipa shilingi 2,000 au 1,000 kulingana na safari kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 125: Tozo zinazotozwa Bandarini kwa wasafiri wa Kigeni na Wazawa**

| Port Revenue Source | Zanzibar to TZ Mainland (Price in TZS payable per PAX Local) | Zanzibar to Zanzibar (Price in TZS Payable per PAX Local) |
|---|---|---|
| Port service charge (paid by passengers) | 2,000 | 1,000 |
| Infrastructure (paid by passengers) | 2,000 | 1,000 |
| Sea transport tax (paid by vessel owners). | **8% of net value of the ticket** | |

Aidha, msingi wa kukokotoa asilimia 8 ya thamani halisi ya tiketi haukuweza kubainishwa na jinsi ilivyopatikana. Mifano ya mapato ya kila mwezi zenye hitilafu zilizobainishwa ni kama inavyoonyeshwa katika **Kiambatisho Nambari 10.**

Hivyo, Mamlaka ya Mapato Zanzibar inapoteza kiasi kikubwa cha Mapato ya Serikali yanayotakiwa kupatikana kutoka chanzo cha bandari kwani Sheria ya Tozo ya Huduma ya Bandari Na.2 ya 1998 (R.E 2013) kifungu cha 3 (Jedwali la Pili) kinatoa mwanya kwa kampuni za bandari kulipa kile wanachotaka bila msingi kwa kushindwa kubadilisha kiasi cha Dola (USD) katika Shilingi ya Tanzania (Tshs) kulingana na tarehe ya manunuzi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar na Mamlaka ya Usafiri Baharini Zanzibar kukaa na kujadili juu ya mianya iliyoainishwa kwenye Sheria (kukwepa kodi) ambayo inaruhusu/kutoa nafasi kwa Kampuni za Meli kutoza abiria wa kigeni kwa TZS badala ya fedha za USD zilizopokelewa na hivyo kupunguza mapato ya Serikali yanayotakiwa kupatikana/kupokelewa.

### 7.1.3 MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (ZSSF)

Ukaguzi wa hesabu za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 7.1.3.1 Kushuka kwa Thamani ya Vifaa vya Makumbusho Katika Mnara wa Mapinduzi na Mgahawa wa Kuzunguka

Mapitio ya ripoti ya tathmini ya uwekezaji wa ZSSF uliofanywa na Mtaalam wa tathmini (ZIBCO) katika mwaka uliomalizika, yalibaini ukweli kwamba vifaa vya Makumbusho na vile vya mgahawa wa kuzunguka katika Mnara wa Mapinduzi vilishuka thamani kwa kiasi kikubwa kama ilivyoorodheshwa hapa chini:-

**Jadweli Nambari 126: Upungufu wa thamani ya vifaa vya Makumbusho katika Mnara wa Mapinduzi**

| Maelezo | Kiasi cha Thamani 30 Juni, 2023 (Tsh) | Kiasi cha Thamani 30 Juni, 2022 (Tsh) | Upungufu wa Thamani (Tsh) | Asilimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| Vifaa vya kumbukumbu ya Mapinduzi | 136,610,000 | 501,558,801 | (364,948,801) | 73 |
| Vifaa vya Mgawaha wa kuzunguka | 126,872,000 | 517,566,096 | (406,694,096) | 79 |

Kutokana na Jadweli lililo hapo juu, tathmini iliyofanywa ilibaini kuwa kupungua kwa kiasi kikubwa kunamaanisha kuwa baadhi ya vitu vinaweza kushindwa kurekebishwa kwa vile vinaharibika au kuchakaa bila kutumiwa na vinakosa matunzo yanayohitajika kwa wakati. Vifaa vya Mnara wa Mapinduzi kwa ajili ya matumizi ya Mgahawa havijatumika kwa muda mrefu kwani mgahawa huo umeshindwa kufanya kazi kwa zaidi ya miaka miwili.

Iwapo juhudi za makusudi hazitachukuliwa kuhakikisha Mnara wa Mapinduzi unaleta tija iliyokusudiwa wakati wa kuanzishwa kwake, mali zilizomo ndani yake zinaweza kuendelea kuharibika bila ya kuzalisha chochote na hivyo kupelekea upotevu wa fedha za wanachama wa Mfuko kutokana na kufanyika kwa uwekezaji usio na tija.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZSSF kuhakikisha unaandaa mikakati bora ya utafutaji wa masoko ili kuhakikisha mnara wa Mapinduzi unatangazwa kama ni kivutio cha Utalii kwa lengo la kuongeza mapato na hatimae kupatikana tija iliyokusudiwa.

Aidha, uongozi wa ZSSF unashauriwa kuandaa mpango wa uuzwaji wa vifaa vya Resta ili kuzuia hasara inayoendelea kujitokeza kutokana na kutotumika kwa vifaa hivyo.

### 7.1.3.2 Kukosekana kwa usahihi katika upunguaji wa thamani ya Vifaa vya Hoteli kwenye Hoteli ya Jengo la Hifadhi (Hifadhi Bulding and Apartment) Pemba

Mapitio ya ripoti ya tathmini ya samani na vifaa vya Hoteli kwenye Jengo la Hifadhi Pemba yalibaini kupungua kwa thamani ya samani na vifaa kwa shilingi 84,535,377 sawa na asilimia 59.37 ambapo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 thamani ya Samani na vifaa vya hoteli iliripotiwa kuwa na jumla ya shilingi 142,390,377 ukilinganisha na thamani halisi ya Samani na Vifaa ya shilingi 57,855,000 kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Ukaguzi haukuweza kutambua sababu zilizopelekea kushuka kwa thamani ya vifaa na samani hizo hasa ukizingatia ya kwamba baadhi ya vifaa vilinunuliwa katika kipindi cha miaka ya karibuni.

Kutokana na kushindwa kutambua sababu zilizopelekea kushuka kwa thamani iliyoripotiwa ya samani na vifaa vya hoteli katika jengo la Hifadhi ukaguzi umetia shaka juu ya usahihi wa taarifa iliyowasilishwa.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZSSF kuhakiksha unakuwa makini na kutoa msaada kwa mthamini wakati wa zoezi la uthaminishaji wa mali ili kuhakikisha kwamba mali zote zinatathminiwa kwa kuzingatia uhalisia ili kufikia thamani inayolingana na mali hizo.

Aidha, sababu zote za kupunguzwa au kuongezeka kwa thamani ya kila mali zinapaswa kujumuishwa katika ripoti ya tathmini ili kuwasaidia wasomaji/watumiaji wa ripoti ya uthamini kwa madhumuni sahihi ya kufanya maamuzi.

### 7.1.3.3 Kukosekana kwa Makubaliano ya Ubia Kati ya ZSSF, UMAWA na Baraza la Manispaa Mjini kwa ajili ya Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Mabasi Kijangwani

Ukaguzi umebaini kwamba ZSSF, Baraza la Manispaa Mjini na Umoja wa Maaskari Wastaafu (UMAWA) walitia saini makubaliano tarehe 26 Mei, 2022 kwa ajili ya Mradi wa ujenzi wa kituo cha mabasi ya Daladala Kijangwani.

Kwa mujibu wa makubaliano hayo ni kwamba uwekezaji wa mradi utamilikiwa kwa pamoja katika ubia kwa uwiano wa mtaji wa uwekezaji wa kila mbia. Kwa upande wa ZSSF mchango wake ni gharama za ujenzi wa miradi yote ambapo UMAWA na Baraza la Manispaa Mjini mchango wao ni Ardhi kwa ajili ya mradi.

Kwa mujibu wa kifungu cha 8.4 cha Makubaliano (MOU), pande hizo tatu zilipaswa kuingia katika Makubaliano ya Ubia (Joint Venture Agreement) baadae kueleza, miongoni mwa mengine, jinsi ya kugawana faida kulingana na thamani ya mtaji wa uwekezaji iliyochangiwa na kila mmoja.

Hata hivyo, hadi ukaguzi unakamilika Makubaliano hayo ya Ubia kati ya pande hizo tatu hayakupatikana kwa ukaguzi ili kuthibitisha vigezo na masharti waliyokubaliana kwa mujibu wa Mkataba uliosainiwa tarehe 26 Mei, 2022.

Ukaguzi unaushuri uongozi wa ZSSF kuhakikisha makubaliano ya Ubia kati yake na washirika wenzake yanaandaliwa ili kuthibitisha vigezo na masharti watakayokubaliana na kuweza kunusuru kujitokeza kwa mgongano wa kimaslahi baina yao.

### 7.1.3.4 Tathmini ya Ufanisi wa Miradi ya Uwekezaji ya Mfuko katika Majengo na Hoteli (Mapinduzi Tower, Mwanakwerekwe Shopping Centre, Mbweni Old, Tibirinzi Amusement Park na Mkoani Hotel)

Ukaguzi ulifanya tathmini ya maeneo ya Vitega uchumi vya Mfuko ili kupima ufanisi unaopatikana kutokana na vitega uchumi hivyo. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ukaguzi umebaini baadhi ya vitega uchumi bado havijafanya vizuri kwa vile havikuweza kuleta mchango wa ziada angalau asilimia 50 na baadhi ya vyengine vilikuwa na mwenendo usioridhisha wa uendeshaji kama ilivyobainishwa katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 127: Tathmini ya Ufanisi wa Miradi ya Uwekezaji ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii**

| Namba | Eneo la Uwekezaji | Mapato Yaliyopatikana kwa mwaka 2023 (Tsh) | Gharama za uendeshaji (Tsh) | Faida/ (Hasara) (Tsh) | Asilimia ya Faida/ (Hasara) (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Mapinduzi Tower and Square | 48,461,963 | 93,457,419 | (44,995,456) | (92.8) |
| 2. | Mwanakwerekwe Shopping Centre | 98,021,172 | 59,755,244 | 38,265,928 | 39.04 |
| 3. | Mbweni old Houses | 72,532,230 | 47,936,245 | 24,595,985 | 33.9 |
| 4. | Tibirinzi Amusement Park | 231,077,000 | 199,992,358 | 31,084,642 | 13.4 |

### 7.1.3.5 Mwenendo usioridhisha wa Utendaji wa Hoteli ya Mkoani

Ukaguzi ulifanya uchambuzi wa mwenendo wa utendaji kazi wa Hoteli ya Mkoani kwa miaka mitatu iliyopita, kuanzia mwaka 2020/2021 hadi kufikia 2022/2023 na kubaini uwepo wa mwenendo usioridhisha katika uendeshaji wa Hoteli hiyo na kupelekea kujiendesha kwa hasara.

Kutokana na hali hiyo ilibainika uwepo wa gharama kubwa za uendeshaji ikilinganishwa na thamani halisi ya mapato yanayopatikana. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 128: Mwenendo wa uendeshaji wa Hoteli Kihasara**

| Maelezo | Mwaka 2023 Kiasi (Tsh) | mwaka 2022 Kiasi (Tsh) | Mwaka 2021 Kiasi (Tsh) |
|---|---|---|---|
| Mtaji uliowekezwa | 53,091,935 | 150,000,000 | 150,000,000 |
| Pesa zilizotolewa | (9,376,692) | 0 | 0 |
| Toa: gharama za uendeshaji | (14,262,319) | (96,908,065) | 0 |
| **Kiasi kilichobakia** | 29,452,924 | 53,091,935 | 150,000,000 |

Jadweli liliopo hapo juu linaonesha kwamba uwekezaji wa Hoteli ulianza na mtaji wa shilingi 150,000,000 kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na kufikia mtaji wa shilingi 53,000,000 kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Ukaguzi umebaini sababu iliyopelekea kushuka kwa thamani ya mtaji ni kutokana na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji ambapo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 gharama za uendeshaji zilikuwa ni shilingi 96,000,000 hadi kufikia shilingi 14,000,000 kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Kuwepo kwa matumizi makubwa ya gharama za uendeshaji kumepelekea kukosekana kwa ufanisi wa uwekezaji uliofanyika jambo ambalo linapelekea upotevu wa fedha za wanachama wa Mfuko.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZSSF kuhakikisha kuwa unaandaa na kutekeleza mikakati ya kimasoko ya kuitangaza na kuikuza Hoteli ya Mkoani ili kuhakikisha mwenendo wa utendaji wa hoteli unaimarika kwa kiwango cha kurudisha gharama za uendeshaji kwa hatua za awali (break even point).

Aidha, kuhakikisha kunakuwa na usimamizi wa karibu wa kila uwekezaji unaofanyika kwenye majengo ili wapangaji wote wazingatie makubaliano ya mikataba yao kwa lengo la kuboresha mwenendo wa ukusanyaji wa mapato (kodi) pamoja na kufanya ukarabati wa mara kwa mara kwa majengo ya zamani ili kupunguza gharama za uendeshaji ambazo zitapunguza mtaji wa uwekezaji.

### 7.1.3.6 Kutorejeshwa kwa Riba za Mikopo inayodaiwa ZSTC

Ukaguzi ulifanya tathmini ya utekelezaji wa hoja za ukaguzi na kubaini uwepo wa dosari za mwenendo wa urejeshaji wa mikopo ya muda mfupi iliyoripotiwa katika hesabu za Mwisho wa Mwaka (financial statement) kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Katika tathmini hiyo ilibainika ya kwamba Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) lilikuwa na kiwango kikubwa cha Riba kinachodaiwa chenye thamani ya shilingi Bilioni 1.6 kwa zaidi ya miaka minne ambapo hatima ya urejeshaji wa riba ya mkopo ambayo haijalipwa kwa muda mrefu haikuweza kujulikana.

Kutokana na ukubwa wa thamani ya deni linalodaiwa ukaguzi umetia shaka ya kwamba kiwango hicho huwenda kisiweze kurejesheka na hatimae kuusababishia hasara Mfuko wa Hifadhi ya Jamii. Hali halisi ya Riba ya Mikopo ambayo haijalipwa kwa muda mrefu ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 129: Riba ya Mikopo ambayo haijalipwa**

| Maelezo ya Mkopo | Tarehe za Mwisho wa Mkopo | Bakaa hadi kufikia Tarehe 30.06.2023 (Tsh) | Bakaa Hadi Kufikia Tarege 30.06.2022 (Tsh) | Maelezo ya Urejeshaji Mikopo |
|---|---|---|---|---|
| ZSTC Mkopo Na. 1 | 15.08.2017 - 15.08.2018 | 797,706,045 | 797,706,045 | Mkopo Mkuu wote ulilipwa na riba ilibaki bila kulipwa tangu mwaka 2018. |
| ZSTC Mkopo Na. 2 | 22.09.2017 - 22.09.2018 | 750,000,000 | 750,000,000 | Mkopo Mkuu wote ulilipwa na riba ilibaki bila kulipwa tangu mwaka 2018. |
| ZSTC Mkopo Na. 3 | 01.10.2017- 01.10.2018 | 150,000,000 | 1,150,000,000 | Mkopo mkuu wa kiasi cha shilingi 1,000,000,000<br>ambao Ulisalia kulipwa tangu mwaka 2018 umelipwa katika mwaka wa ukaguzi. Hata hivyo, kiasi cha riba bado hakijalipwa. |
| **Jumla** | | **1,697,706,045** | **2,650,706,045** | |

Aidha, mapitio ya Kamati ndogo ya Bodi ya Miradi na Uwekezaji (Mkutano wa Kawaida Na.1 uliofanyika tarehe 29 Julai, 2023) yalibaini kuwa ZSTC iliiandikia barua ZSSF kuomba kusamehewa adhabu kwa kushindwa kulipa mikopo hiyo kinyume na kanuni na masharti ya mikopo.

Mikopo hiyo iliongezeka kutokana na adhabu hadi kufikia shilingi 5,272,995,647 na kutaka ibaki na riba ya mkopo ya shilingi 2,937,147,987 ambayo ingerejeshwa kulingana na masharti mapya yatakayokubaliwa mara baada ya ombi hilo kupitishwa. Hata hivyo ukaguzi ulibaini uwepo wa dosari kutokana na mapitio ya muhtasari wa ripoti ya kamati ndogo ya Bodi kama zifuatazo:-

- Kiasi cha adhabu kilichoripotiwa na ZSTC katika barua yao ya maombi hakikuweza kupatikana katika taarifa za fedha za ZSSF.
- Kiasi cha riba cha mikopo kilichoripotiwa katika taarifa za fedha za ZSSF kilitofautiana na kilichothibitishwa na ZSTC katika barua yao ambapo kiasi kilichoripotiwa katika taarifa za fedha kilikuwa shilingi 1,697,706,045 na kilichothibitishwa na ZSTC kilikuwa shilingi 2,937,147,987 na kusababisha tofauti ya shilingi 1,239,441,942.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZSSF kuchukuwa juhudi za ufuatiliaji wa urejeshaji wa bakaa inayodaiwa ZSTC na vile vile kufanya uhakiki wa bakaa ya adhabu na riba ili kuweza kubaini usahihi wa taarifa za fedha zinazohusiana na deni hilo.

### 7.1.3.7 Dosari zilizobainika katika Ripoti zinazohusiana na ukusanyaji wa Mapato ya Upangishaji

Ukaguzi ulifanya mapitio ya ripoti za robo mwaka za M/S Terranova Company Ltd zinazohusiana na hali ya ukusanyaji wa mapato na madeni yanayotokana na upangishaji wa nyumba za ZSSF na kubaini kuwa bili za upangishaji zinatolewa na kutambuliwa katika vitabu vya akaunti vya ZSSF kwa kila mwezi.

Kwa upande mwingine, M/S Terranova Co. Ltd (Msimamizi wa Nyumba) anayehusika kwa ajili hiyo hutayarisha ripoti za robo mwaka za ankara dhidi ya ukusanyaji na mwenendo wa malimbikizo ya madeni ya wapangaji.

Uhakiki wetu wa ripoti za robo mwaka za Msimamizi wa Nyumba za ZSSF ulibaini mapungufu yafuatayo:-

#### a) Uwepo wa tofauti ya Kipindi cha kuripoti Taarifa baina ya ZSSF na Msimamizi wa Nyumba

Ukaguzi ulibaini kuwa Mwaka wa Fedha wa ZSSF (Financial Year) unamalizika Juni wakati muda wa taarifa wa Msimamizi wa Nyumba za ZSSF (TERRANOVA) unamalizika Desemba. Muda wa kuripoti ukusanyaji wa kodi (iliyopatikana na malipo ya awali) na iliyosalia unabaki nyuma kwa miezi sita kati ya vipindi viwili hivyo vya utoaji wa taarifa (reporting period). Licha ya kutolingana kwa muda wa kipindi cha kuripoti, bado hakukuwa na ushahidi wa upatanisho unaofanywa kati ya wahusika (ZSSF na TERRANOVA) ili kuthibitisha usahihi wa kodi iliyokusanywa, iliyolipwa kabla ya muda na iliyobakia kwa kila nyumba.

#### b) Kutokuoneshwa kwa bili za kila mwezi za makusanyo

Ilitarajiwa kwamba ripoti za Msimamizi wa Mali (ya robo mwaka) zingeonyesha bili za kila mwezi dhidi ya makusanyo na ambazo hazijalipwa katika robo husika ili kuwezesha kutambua muda wa madeni na uamuzi wa hatua za urejeshaji kwa haraka zinazofaa kwa wadaiwa sugu. Hata hivyo, ripoti zilizotayarishwa hazikuweza kubainisha taarifa za ukusanyaji wa deni kwa kila mwezi katika robo ya mwaka.

### c) Kutokubainishwa kwa gharama zilizotozwa katika ripoti ya robo mwaka

Ukaguzi umebaini gharama ya jumla ya huduma iliyotozwa, iliyokusanywa na ambayo haijalipwa haikuonyeshwa katika ripoti za robo mwaka. Hata hivyo, ripoti ya makusanyo ya kodi iliyotumika katika kubainisha malipo ya ada za usimamizi kwa mwezi haikuendana na ripoti za ukusanyaji wa kodi katika ripoti za robo mwaka zilizotayarishwa jambo ambalo limepelekea kukosekana kwa usahihi na ukamilifu wa kodi iliyotozwa, iliyokusanywa na ambayo haijalipwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2023.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZSSF kuhakiksha kwamba:-

- Unafanya usuluhishi wa kibenki (Bank reconciliation) kila mwezi au robo mwaka kati ya Msimamizi wa Nyumba za ZSSF na ripoti ya ukodishaji ili kufahamu usahihi wa bili inayotarajiwa kukusanywa, iliyokusanywa na bakaa ya deni lililobakia.
- Ripoti ya Msimamizi wa Nyumba za ZSSF (TERRANOVA) inapaswa kuwa kamili na yenye kujitosheleza ili kuweza kubaini uhalisia wa kodi inayotakiwa kutozwa, iliyokusanywa na ambayo haijalipwa katika mwezi/robo mwaka husika.
- Bakaa ya Kodi kwa mwaka uliopita inapaswa kuonyeshwa ili kuwezesha kubaini ufanisi wa ukusanyaji wa Ankara za mwaka wa sasa na uliopita kwa nia ya kutambua madeni ya zamani na kuchukua hatua zinazofaa.
- Msimamizi wa Majengo (TERRANOVA) anapaswa kuandaa ripoti ya mwaka pia, ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa kiasi cha bili kwa mwaka, iliyokusanywa na salio ambalo halijalipwa.

### 7.1.3.8 Kuongezeka kwa Kasi ya Ukuaji wa Madeni yatokanayo na Ukodishaji wa Nyumba

Ukaguzi umefanya tathmini ya mwenendo wa ulipwaji wa madeni yatokanayo na ukodishwaji wa nyumba kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2020/2021 hadi mwaka 2022/2023 na kubaini ya kwamba uwepo wa mwenendo wa ulipwaji wa madeni usioridhisha au usio na uhakika wa upatikanaji wa malipo ya madeni yatokanayo na ukodishwaji wa nyumba, jambo ambalo linapelekea kuongezeka kwa madeni hayo. Hali halisi ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 130: Mwenendo wa ukuaji wa madeni**

| Maelezo | 30.06.2023 (Tsh) | 30.06.2022 (Tsh) | 30.06.2021 (Tsh) |
|---|---|---|---|
| Madeni ya Ukodishaji (Kiasi cha Jumla) | 2,698,251,628 | 1,958,149,989 | 1,499,716,017 |
| Kiasi Kilichotengwa kwa ajili ya Madeni yenye Shaka kulipika | (169,427,197) | (156,276,341) | (35,226,655) |
| **Jumla ya kiasi kinachodaiwa** | **2,528,824,431** | **1,801,873,646** | **1,464,489,362** |

Kutokana na mwenendo wa hapo juu ukaguzi umebaini dosari zifuatazo:-

- Mwenendo wa madeni yatokanayo na ukodishaji wa nyumba pamoja na kiasi Kilichotengwa kwa ajili ya madeni yenye shaka kulipika umeendelea kuongezeka kwa miaka mitatu mfululizo ikimaanisha kuwa kulikuwa na mfumo dhaifu wa ufuatiliaji wa mapato ya ukodishaji nyumba pamoja na kutofuata sheria na masharti ya mikataba ya upangaji ambayo inalazimu wapangaji kulipa kodi ya pango katika miezi mitatu, miezi sita na kodi ya kila mwaka mapema kabla ya kuanza kwa muda wa kukodisha.

- Pamoja na kuendelea kuongezeka kwa mwenendo wa madeni ambapo baadhi yao ni wadaiwa sugu kwa muda mrefu, juhudi za Uongozi na Msimamizi wa nyumba au majengo ya ZSSF kufuatilia hali ya ulipwaji wa madeni hayo haikufanikiwa.
- Ripoti ya Msimamizi wa Majengo (TERRANOVA) zinazohusiana na Ankara za kodi ya pango na ukusanyaji haikusaidia kuonyesha taarifa ya kodi iliyolipwa katika mwaka wa sasa na ile ya miaka iliyopita ili kusaidia kupima utendaji kazi wa juhudi za urejeshaji wa madeni kwa wapangaji waliokiuka vigezo na masharti ya mkataba na kuchukua hatua za kisheria dhidi yao.
- Kuendelea kuongezeka kwa mwenendo wa kiasi Kilichotengwa kwa ajili ya madeni yenye shaka yasiyoweza kulipika (Provision for doubtful dept) umeonekana kuwa ni wa kiasi kikubwa na umekosa uthibitisho na misingi wa ongezeko hilo.
- Aidha, bakaa la madeni yatokanayo na ukodishaji nyumba lililorekodiwa mwanzo wa mwaka wa ukaguzi (yaani tarehe 01 Julai, 2022) lilinakiliwa kimakosa ambapo salio la mwaka uliopita hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2022 lilikuwa shilingi 1,958,149,989 lakini salio lililorekodiwa tarehe 01 Julai 2022 lilikuwa shilingi 1,835,504,425 na kuleta tofauti ya shilingi 122,745,564, hivyo kupunguza bakaa la madeni ya ukodishaji nyumba yaliyoripotiwa mwisho wa mwaka tarehe 30 Juni 2023 kwa kiasi sawa na hiko.

Kutokana na mapungufu yaliyobainishwa hapo juu, ukaguzi umeshindwa kuthibitisha uwepo wa usahihi katika urejeshaji wa madeni ya muda mrefu ya kukodisha nyumba na Majengo. Zaidi ya hayo, upo uwezekano mkubwa kwamba Msimamizi wa Majengo hufuatilia zaidi wapangaji wanaokidhi masharti ya mikataba ya pango (wapangaji walio na hadhi nzuri ya mkopo) na kupuuza au kutoa umakini mdogo kwa wadaiwa sugu waliokiuka mikataba kwa muda mrefu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZSSF kuhakikisha kuwa unazingatia na kusimamia kikamilifu vigezo na masharti ya mikataba ya ukodishaji. Vile vile kwa wale wote waliokiuka vigezo na masharti ya ukodishaji kwa muda mrefu (wadaiwa sugu), hatua za kisheria zinapaswa kuchukuliwa dhidi yao ili kuhakikisha urejeshwaji kamili wa kiasi cha deni linalodaiwa.

### 7.1.3.9 Mapitio ya Utendaji wa Mfuko wa Uchangiaji wa Hiari - ZVSSS

Ukaguzi ulifanya mapitio kuhusu mwenendo wa utendaji wa Mfuko wa Uchangiaji wa Hiari (ZVSSS) katika makusanyo na malipo kwa michango ya wanachama kwa kipindi cha miaka miwili kuanzia mwaka 2021/2022 hadi mwaka 2022/2023. Katika mapitio hayo ukaguzi ulibaini dosari zifuatazo:-

- Kuongezeka kwa kiwango kidogo cha shilingi 29,332,918 sawa na asilimia 8 kinachotokana na ukusanyaji wa michango ya wanachama ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 michango ya wanachama iliripotiwa kuwa na jumla ya shilingi 371,229,148 ukilinganisha na michango ya wanachama iliyoripotiwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambayo ni shilingi 400,562,066.
- Kuongezeka kwa shilingi 156,466,483 sawa na asilimia 88 ambazo ni kiasi kikubwa cha fedha za marejesho ya michango ya wanachama au mafao ya kujitoa katika Mfuko wa ZVSSS ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya shilingi 176,949,108 zilirejeshwa ukilinganisha na shilingi 333,415,591 kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

Sababu zilizobainishwa kupelekea kujitokeza kwa hali hiyo zilitokana na mambo yafuatayo:-

- Mabadiliko ya taratibu za ukusanyaji ambapo katika mwaka uliopita utaratibu wa ukusanyaji wa mtu kwa mtu ulitumika (ukusanyaji wa fedha kwenye eneo husika kwa kuwatembelea wanachama) na katika mwaka huu wa ukaguzi utaratibu wa ukusanyaji ulitumika kwa njia ya kielektroniki ambapo michango yote inapokelewa moja kwa moja kupitia benki au wakala kwa kutumia nambari za udhibiti. Mabadiliko yaliyofanyika yalikosa ushahidi wa kujulishwa vyema kwa wanachama ili wawe tayari kuyapokea. Inaonekana kuwa wanachama wengi wanaochangia hawako tayari kupokea mabadiliko hali ambayo inasababisha michango mdogo.
- Kutokuwepo kwa kampeni ya kina ya uhamasishaji kwa Umma kuhusu bidhaa za Mfuko wa uchangiaji wa hiari (ZVSSS) ili kuhakikisha wanachama wengi zaidi wanajiunga na Mfuko.

Ukaguzi unashauri uongozi wa ZSSF kufanya mambo yafuatayo:-

- Mashine ya POS kutoka kwa mabenki husika ya ZSSF ya ZVSSS zitumike wakati wa ziara ya wanachama vijijini ili kuhakikisha michango yote ya fedha taslimu kwenye eneo husika inakusanywa ili kudhibiti na kuondoa tatizo la uchangiaji kwa wanachama wasiopenda kutumia njia za kielektroniki za ukusanyaji wa michango na kuimarisha mwenendo wa makusanyo.
- Shughuli za kina za uhamasishaji/mikakati ya kimasoko kuhusu kujenga uelewa wa vifurushi vya Mfuko wa Hiari wa Hifadhi ya Jamii (ZVSSS) na kutafuta wanachama wapya inapaswa kuongezwa na ripoti kuandikwa ili kuboresha makusanyo ya michango.
- Vifurushi vya kuvutia zaidi vya Mfuko wa Hiari (ZVSSS) vinapaswa kuanzishwa ili wanachama waone umuhimu wa kujiunga na Mfuko ili kupunguza kiasi kikubwa cha wanachama kujitoa katika uanachama na kuongeza wanachama wapya.
- Mfuko wa Hiari - ZVSSS unapaswa kufanya kazi kwa kujitegemea yaani, kujiendesha kwa kutumia fedha zake ili kutathmini utendaji kazi wake kwa maamuzi sahihi.

### 7.1.3.10 Vigezo na Masharti ya Kimkataba yasiyoainishwa katika Mkataba wa Usimamizi wa Majengo kati ya ZSSF na M/S TERRANOVA CO. LTD kwa ajili ya Kusimamia Majengo ya Mbweni Mpya

Katika ukaguzi uliofanyika imebainika kuwa ZSSF na M/S TERRANOVA CO.LTD waliingia makubaliano tarehe 10 Agosti, 2022 kwa muda wa miaka miwili kwa ajili ya utoaji wa huduma za usimamizi wa Majengo ya Mbweni Mpya na Kongwe, Kituo cha Biashara cha ZSSF Mwanakwerekwe na Jengo la Treni (Chawl building) yaliopo Zanzibar kwa ada ya usimamizi ya asilimia 4 ya kodi ya jumla inayokusanywa kwa kila mwezi.

Imeelezwa kuwa nyumba za ZSSF za Mbweni Mpya zipo chini ya wanunuzi ambapo ZSSF ndiye mlezi wa wanunuzi anaewawakilisha katika mkataba na TERRANOVA kwa usimamizi wa jengo hilo kutokana na ukweli kwamba wanunuzi wa nyumba hizo za Mbweni hawakuweza kuingia mkataba huo kutokana na kushindwa kutii vigezo na masharti vilivyoanishwa katika Sheria inayosimamia utolewaji wa huduma na utumiaji wa vifaa katika maeneo ya umiliki wa pamoja (Condominium Act of Zanzibar). Katika suala hili, ada za usimamizi za asilimia 4 zinazolipwa kwa Msimamizi wa jengo hili ni kutoka kwa wanunuzi na sio fedha za ZSSF.

Hata hivyo, jinsi mkataba kati ya ZSSF na M/S TERRANOVA Co. Ltd ulivyoandaliwa haukuweza kuweka wazi kipengele hiki cha ZSSF kama wakala anayewakilisha wanunuzi wa nyumba na kwamba ada za usimamizi zitatoka kwao. Mkataba haukuweza kufafanua kama majengo yote yaliyotajwa kwenye mkataba yanasimamiwa na TERRANOVA kwa ajili ya ZSSF na hivyo ZSSF itakuwa na jukumu la kumlipa msimamizi wa majengo ada ya usimamizi ya asilimia 4 kutoka kwenye vyanzo vya pesa vya ZSSF. Vigezo na masharti maalum ya kusimamia nyumba za Mbweni mpya hayakuelezwa katika mkataba huu.

Kwa muktadha huo, Mkataba ulikuwa hauonyeshi uhalisia kwa watumiaji na hivyo inaweza kutafsiriwa vibaya na kusababisha migogoro wakati wa utekelezaji wa mkataba huo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZSSF kuhakikisha unaingia mkataba tofauti na msimamizi wa kusimamia nyumba za ZSSF za Mbweni mpya wenye vigezo na masharti maalum ambayo yatatoa picha ya wazi ya majukumu ya kimkataba ya ZSSF kwa niaba ya wanunuzi wa nyumba ili kuwafanya watumiaji wa mkataba kuelewa yaliyomo kwenye mkataba kwa kusudi la kufanya maamuzi yaliyosahihi.

#### 7.1.3.11 Hatari zinazoukabili Mfuko Hazijatambuliwa Kikamilifu na Hatua za Kupunguza/Kudhibiti

Ukaguzi ulifanya tathmini ya vihatarishi vilivyoainishwa na hatua au udhibiti uliopo kama inavyoonyeshwa kwenye rejista ya vihatarishi na matokeo ya ripoti yalibaini kuwa hatari zinazoukabili Mfuko hazikutambuliwa kikamilifu na udhibiti husika badala yake uchambuzi wa vihatarishi na utoaji taarifa ulikuwa wa ukaguzi zaidi (kuripoti juu ya uchunguzi na mapendekezo juu ya matokeo ya vihatarishi).

Kutokana na ZSSF kushindwa kutambua vihatarishi vya Mfuko ni wazi kwamba nafasi ya Mfuko kuendelea kuingiza fedha kwa miradi na uwekezaji wenye hatari kubwa sana katika siku za usoni ni kubwa sana ambayo inaweza kusababisha hasara kubwa ya fedha za wanachama.

Vile vile Kitengo cha Usimamizi wa Vihatarishi kinaweza kuwa kinafanya shughuli zake kinyume na upeo wa mipaka yake inayohitajika hali inayofanya kitengo hicho kutokuwa na ufanisi katika majukumu yake ya kila siku.

**Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZSSF kuhakikisha unafanya mambo yafuatayo:-**

- Kitengo cha usimamizi wa viashiria hatarishi kufanya jitihada za kuzingatia utambuzi wa hatari na hatua za kupunguza badala ya uchunguzi wa ukaguzi na mapendekezo ambayo yanapaswa kufanywa na kitengo cha ukaguzi wa ndani.
- Kitengo kinachohusika na uchambuzi wa vihatarishi na utaratibu wa udhibiti wa kukabiliana na vihatarishi pamoja na mabingwa wa vihatarishi kipewe mafunzo kuhusiana na kuainisha na kutambua njia za kudhibiti viashiria hatarishi ili kuzuia ZSSF kupata hasara katika miradi yake, uwekezaji na masuala ya hifadhi ya jamii kwa ujumla.

### 7.1.4 MFUKO WA BARABARA (ZRF)

Ukaguzi wa hesabu za Mfuko wa Barabara Zanzibar (ZRF) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

### 7.1.4.1 Muingiliano wa Majukumu ya Ukarabati wa Barabara kati ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi

Tarehe 04 Oktoba 2023, Baraza la Wawakilishi la Zanzibar liliifuta shughuli za Bodi ya Mfuko wa Barabara wa Zanzibar (ZRF) kwa kuidhinisha Sheria nambari 6 ya Mabadiliko mbalimbali ya 2023. Katika Kifungu nambari 37 cha Sheria nambari 6, majukumu yote ya Bodi ya Mfuko wa Barabara yaliyokuwa yanatekelezwa kama ilivyoelezwa katika Kifungu cha 8 cha Sheria ya Uanzishaji wa Mfuko wa Barabara ya Zanzibar, 2001 yalihamia kwa Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa ukarabati wa barabara unapewa kipaumbele; kuhakikisha kuwa mifumo ya usimamizi wa ufanisi wa mtandao wa barabara wa Zanzibar inafanya kazi ipasavyo, ambayo itajumuisha kuhakikisha kuwa mtandao wa barabara unakaguliwa kila mwaka ili kuboresha mfumo wa RMMS; kutoa ushauri kwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuhusu sera za usimamizi na ufadhili wa barabara n.k.

Kulingana na Agizo la Rais, majukumu makuu ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ni kuangalia ukusanyaji wa mapato ya Serikali, kusimamia matumizi ya fedha za umma, kusimamia deni la taifa, na kutoa huduma za uhasibu kwa Serikali. Wakati Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi ina majukumu ya kupanga, kukuza, na kudumisha miundombinu ya Uchukuzi na mawasiliano, kukuza utafiti katika sekta ya uchukuzi, kuimarisha ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi katika utoaji wa huduma mbalimbali za uchukuzi na mawasiliano.

Ukaguzi umebaini kwamba kitendo cha kufanya uhamisho wa majukumu yaliyokuwa yakitekelezwa awali na Mfuko wa Barabara Zanzibar kwenda kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha na Mipango imepelekea uwepo wa muingiliano wa majukumu kati ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango na Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi.

Muingiliano wa Majukumu baina ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango na Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi, inaweza kusababisha mzozo kati ya Wizara hizo mbili katika usimamizi wa matengenezo ya barabara hapo baadae.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi kukaa pamoja na Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ili la kutafuta ufumbuzi juu ya changamoto iliyojitokeza kwa lengo la kuhakikisha kila taasisi inasimamia ipasavyo majukumu yaliyoainishwa katika sheria anayoisimamia katika utekelezaji wa shughuli za kila siku.

### 7.1.4.2 Uingizaji mdogo wa Fedha kwa Wakala wa Barabara baada ya kufutwa kwa Bodi ya Mfuko wa Barabara Zanzibar

Kwa mujibu wa kifungu cha 3.1 cha Mkataba wa Utendaji (Performance Agreement) ambao ulisainiwa tarehe 28 Septemba, 2022 kati ya Mfuko wa Barabara Zanzibar (ZRFB) na Wakala wa Barabara Zanzibar (ZANROADS), ambapo ilikubaliwa kwamba kwa mwaka wa fedha 2022/2023, ZRFB itahaulisha jumla ya shilingi 20,033,644,000 kwa Wakala wa Barabara ZANROADS kwa madhumuni ya matengenezo ya barabara na shughuli zinazohusiana na ukarabati wa barabara. Na kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Bodi ya Mfuko wa Barabara ZRFB ilitarajiwa kuhaulisha jumla ya shilingi 13,718,700,000 kwa mujibu wa Mkataba wa Utendeji baina ya ZRFB na ZANROADS.

Ukaguzi umebaini kwamba kuanzia tarehe 1 Julai, 2022 hadi 30 Juni 2023, Bodi ya Mfuko wa Barabara Zanzibar (ZRFB) ilihaulisha jumla ya shilingi 5,577,466,000 kati ya shilingi 20,033,644,000. Pia kwa mwaka wa fedha 2023/2024, kuanzia Julai, 2023 hadi Agosti, 2023, ZRFB ilihaulisha jumla ya shilingi 245,927,550 kati ya shilingi 13,718,700,000 zilizosainiwa.

Vile vile ukaguzi umebaini kwamba, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ambae ndie aliyepewa majukumu ya kuhaulisha fedha kwenda kwa Wakala wa Barabara hadi ukaguzi unakamilika Disemba, 2023 Ofisi ya Rais Fedha na Mipango haikuweza kuhaulisha fedha hizo jambo ambalo limeplekea kukwamisha utekelezaji wa shughuli zilizopangwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha inahaulisha fedha zote zilizopangwa kupelekwa kwa Wakala wa Barabara kwa wakati ili iweze kutekeleza majukumu yake ya kazi kwa mujibu wa Sheria.

### 7.1.4.3 Kukosekana kwa taarifa za makabidhiano ya mali za Mfuko wa Barabara Zanzibar

Kwa mujibu wa kifungu nambari 68 cha Sheria nambari 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021, kinazitaka taasisi za umma kutohamisha mali za umma bila ya kuwepo kibali kutoka kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina. Vile vile kifungu nambari 69(3) cha Sheria hiyo, kinaitaka Ofisi ya Msajili wa Hazina kabla ya kutoa kibali hicho kufanya uhakiki wa mali kwa kuangalia idadi, thamani, na uwepo wa mali hizo pamoja na uhalisia wake.

Ukaguzi haukuweza kupata taarifa za makabidhiano ya mali za mfuko wa barabara baina ya Mfuko huo na Ofisi ya Msajili wa Hazina ikiwemo kibali cha uhakiki wa mali za Mfuko wa barabara. Badala yake ukaguzi ulipatiwa barua kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango ya tarehe 03/10/2023 yenye kumbukumbu namba BA.26/454/01/36/131 iliyomtaka Mkurugenzi wa Mfuko wa Barabara kukabidhi mali zote za mfuko.

Kukosekana kwa taarifa za makabidhiano ya mali kunaweza kupelekea mali hizo kupotea kwa namna moja au nyengine.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina kufuata taratibu sahihi za uhamishaji wa mali za Umma kutoka Ofisi moja kwenda Ofisi nyengine.

### 7.1.4.4 Kuchelewa kufanyika kwa malipo ya awali ya shilingi 52,297,774.54

Wakala wa Barabara Zanzibar ilisaini hati ya makubaliano yenye kumbukumbu namba ZANROADS/COUNTRY/GOODS/DP/2022-2023/03 ya tarehe 22 Mei, 2023 na mzabuni M/s Panafrican Equipment (T) kwa ajili ya usambazaji wa vipuri vya "Komatsu" kwa gharama ya shilingi 87,162,957.57 ambazo zilitakiwa kulipwa na Mfuko wa Barabara Zanzibar.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 3 cha mkataba huo, msambazaji alitakiwa kuwasilisha vipuri hivyo baada ya kusainiwa kwa mkataba, pamoja na Wakala wa Barabara kumlipa msambazaji malipo ya awali ya shilingi 52,297,774.54 mara tu baada ya kuwasilisha dhamana ya malipo hayo ya awali.

Mnamo tarehe 10 Agosti, 2023 msambazaji Panafrican Equipment (T) Limited aliwasilisha dhamana ya malipo ya awali yenye kumbukumbu nambari P11/2023/100/7001/70/00000513 kutoka Kampuni ya Alliance Insurance Corporation Limited yenye thamani ya shilingi 52,297,774.54 kwa muda wa miezi mitatu.

Pamoja na uwasilishwaji wa hati ya dhamana ya malipo ya awali uliofanywa na msambazaji ukaguzi umebaini uwepo wa kitendo cha ucheleweshwaji wa malipo ya awali uliofanywa na ZRFB na kupelekea kuathiri utekelezaji wa kazi zilizopangwa za ukarabati wa barabara kwa upande wa Unguja na Pemba. Hadi ukaguzi unakamilika mnamo mwezi Disemba, 2023 ZRFB imeshindwa kufanya malipo ya awali na hatimae mzabuni kushindwa kuwasilisha vifaa vilivyotakiwa kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba wao.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa ZRFB kuhakikisha unakuwa makini katika utekelezaji wa makubaliano ya mkataba ili kuepusha kujitokeza kwa viashiria vya upotevu wa fedha za umma utakaotokana na mzabuni kuamua kufungua kesi ya madai dhidi ya ZRFB inayotokana na ukiukwaji wa mkataba.

### 7.1.4.5 Kutowasilishwa kwa Pampu za lami zenye thamani ya Dola za kimarekani 145,161 sawa na wastani wa shilingi 370,160,550

Wakala wa Barabara Zanzibar ilisaini hati ya makubaliano yenye kumbukumbu namba ZANROADS/COUNTRY/GOODS/DP/2022-2023/23 ya tarehe 25 Aprili, 2023 na mzabuni M/s Panafrican Equipment (T) kwa ajili ya usambazaji wa lami tani 2,700 (2,700 metric tonnes of Bitumen Penetration Grade 60/70), tani 30 za Cola binde CRS (30 metric tonnes for Cola binder CRS) na tani 120 za Cola binde CSS-1H (120 metric tonnes for Cola binder CSS-1H) pamoja na Pampu mbili za kusambazia lami na mtambo wa kuchomea lami kwa thamani ya dola za kimarekani 145,161 sawa na wastani wa shilingi 370,160,550.

Kwa mujibu wa kifungu nambari 5 cha mkataba, msambazaji alitakiwa kuwasilisha bidhaa zote ndani ya miezi mitatu baada ya kusainiwa kwa mkataba ambapo ni sawa na tarehe 30 Julai, 2023. Ukaguzi umebaini Wakala wa Barabara amefanya malipo ya dola za kimarekani 145,161 sawa na wastani wa shilingi 370,160,550 kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba. Dosari iliyobainika katika ukaguzi ni kutokuwasilishwa kwa pampu mbili za kusambazia lami pamoja na mtambo wa kuchomea lami.

Kutokana na dosari iliyobainishwa hapo juu imepelekea Wakala wa Barabara kutokuwa na ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za uwekaji wa lami katika barabara mbalimbali za Unguja na Pemba jambo ambalo limepelekea uwepo wa uharibifu mkubwa wa miundombinu ya barabara hususan katika kipindi cha mvua kutokana na changamoto ya kiwango cha lami kinachowekwa ambacho hakiendani na kiwango kinachohitajika.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wakala wa Barabara kuhakikisha unafanya ufuatiliaji wa haraka kwa msambazaji ili aweze kuwasilisha pampu za uwekaji wa lami hata hivyo Wakala alipaswa kuwa makini wakati wa ufanyaji wa malipo ili kuepusha kujitokeza kwa migogoro na changamoto za kufanya malipo kamili bila ya kupokea vifaa walivyokubaliana.

### 7.1.4.6 Mipango na usimamizi duni ya ukarabati wa barabara uliosababisha hasara ya shilingi 3,906,790,769.79

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano, na Uchukuzi ilisaini hati ya makubaliano yenye kumbukumbu nambari SMZ/P01/W/DP/2020-21/27 ya tarehe 20 Aprili, 2023 na mzabuni China Civil Engineering Construction Limited (CCECC) kwa ajili ya kuweka mifuniko ya saruji kwenye mitaro ya maji pembezoni mwa barabara na ujenzi wa njia ya waenda kwa miguu kutoka barabara ya uwanja wa ndege hadi Mazizini kwa thamani ya shilingi 3,906,790,769.79 ambapo Mkataba huu ulikamilika tarehe 23 Novemba, 2021 na kukabidhiwa kwa Wakala wa Barabara.

Hata hivyo baada ya kukamilika kwa mradi huo, Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano, na Uchukuzi iliingia mkataba mwengine wenye kumbukumbu nambari SMZ/PO1/W/DP/2021-2022/49 wa tarehe 06 Agosti, 2023 na mzabuni China Civil Engineering Construction Limited (CCECC) kwa ajili ya ukarabati na uboreshaji wa barabara za mjini ikiwemo kuboresha, kutanua, kufunga vifaa vya mitaro ya maji machafu, njia za watembea kwa miguu, baiskeli, taa za barabarani pamoja na barabara mbili za juu kwa thamani ya Dola za kimarekani 116,131,442.96 sawa na wastani wa shilingi 296,135,179,548.

Pamoja na uwepo wa ukarabati wa njia za waenda kwa miguu, uwekaji wa mifuniko katika mitaro uliotekelezwa kwa mkataba wa awali ukaguzi umebaini uwepo wa upotevu wa fedha zenye thamani ya shilingi 3,906,790,769.79 zinazotokana na kukosekana kwa upembuzi yakinifu uliopaswa kufanywa na Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi ambapo kumepelekea kuvunjwa kwa njia za waenda kwa miguu kwa ajili ya utanuzi na uboreshaji wa barabara ambapo njia hizo zilizojengwa ndani ya kipindi kisichozidi miezi sita ya utekelezaji wa mkataba wa awali.

Ubomoaji wa barabara ya waenda kwa miguu unaonyesha viashiria vya uwepo wa hasara kubwa kwa Serikali kulikosababishwa na kukosekana kwa mipango endelevu ya ujenzi na ukarabati wa barabara, kukosenaka kwa upembuzi yakinifu ambao ulipaswa kufanywa kabla ya utekelezaji wa mkataba wa awali ambao umesababisha uwepo wa hasara ya shilingi 3,906,790,769.79 zilizowekezwa katika miundombinu hiyo.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuhakikisha unaongeza umakini katika kupanga na kuratibu utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwemo kufanya ukarabati wa miundombinu ya barabara kulingana na matokeo ya upembuzi yakinifu uliofanyika. Aidha, Wizara inapaswa kuimarisha upangaji na uratibu wa miradi ya barabara ili kuepuka haja ya kubomoa miundombinu iliyopo wakati wa kutekeleza miradi mipya.

### 7.1.5 KAMPUNI YA UJENZI

Ukaguzi wa hesabu za Kampuni ya Ujenzi Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 7.1.5.1 Dosari ya kutotumia mfumo katika utayarishaji wa taarifa za kifedha

Kifungu nambari 27(2)(a) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kwamba Afisa Mhasibu atahakikisha kuwa Taasisi ya Umma inakuwa na kuendeleza utendaji, ufanisi, mfumo wa fedha uliowazi na usimamizi wa vihatarishi, na udhibiti wa ndani.

Ukaguzi umebaini kuwa Kampuni ya Ujenzi ilinunua mfumo wenye thamani ya shilingi 46,000,000 kutoka kwa Kampuni ya Adotech Coy. Ltd kwa ajili ya utayarishaji na utunzaji wa taarifa za hesabu za Kampuni. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni Kampuni kutokutumia mfumo kwa utayarishaji na utunzaji wa taarifa za hesabu kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Kutokutumia mfumo katika utayarishaji na uandaaji wa hesabu za Kampuni kunapelekea kujitokeza kwa makosa ya kibinadam, na ukosefu wa uwazi katika utoaji wa taarifa za miamala ya kifedha. Aidha, ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria kilichonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kampuni ya Ujenzi kuhakikisha unazingatia matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ikiwa ni pamoja na kufanya utekelezaji wa haraka katika matumizi ya mfumo ulionunuliwa ili kuweza kupatikana kwa ufanisi katika uwekaji wa kumbukumbu za hesabu na hatimae kufikiwa kwa lengo lililokusudiwa.

### 7.1.5.2 Kutowasilishwa kwa kodi ya zuio kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania shilingi 4,067,225

Kifungu nambari 83A cha Sheria ya kodi ya mapato Sura ya 332 (R.E 2014) kinaelekeza kukatwa kwa kodi ya zuio kwa asilimia 5 kuhusiana na utoaji wa huduma na asilimia 2 kuhusiana na usambazaji wa bidhaa. Wakati wa ukaguzi wetu hatukuweza kuthibitisha kuwasilishwa kwa kodi iliyozuiliwa na Kampuni ya Ujenzi kwa mamlaka husika (TRA) kutokana na ukweli kwamba kulikosekana ushahidi wa nyaraka zozote za uwasilishaji wa kodi ya kiasi kilicholipwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kama ilivyokubaliwa kwenye mkataba.

Kutokuwasilishwa kwa kodi ya zuio ni kuikosesha Serikali mapato yatokanayo na kodi ya zuio. Kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria ya Kodi ya Mapato nilichokinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kampuni ya ujenzi kutii matakwa ya Sheria ya kodi kwa Kampuni kwa kutekeleza kikamilifu matakwa ya sheria hio ikiwa ni pamoja na jukumu la uzuiaji wa kodi na kuiwasilisha katika mamlaka husika kwa wakati. Mchanganuo wa mapato ambayo hayakuwasilishwa ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 131: Kodi ya zuio ambayo haijawasilishwa TRA**

| Namba | Aliyelipwa. | Kiasi cha fedha kilicholipwa (Tshs) | Kodi ambayo haikuwailishwa Mamlaka (Tshs) |
|---|---|---|---|
| 1. | Yussuf Ismail Nassor | 34,800,000 | 1,740,000 |
| 2. | Yussuf Zuheri Makame | 23,200,000 | 1,160,000 |
| 3. | Simai Feruz Hussein | 1,844,500 | 92,225 |
| 4. | Machano Hassan Chum | 15,000,000 | 750,000 |
| 5. | Adotech Coy. Ltd | 6,500,000 | 325,000 |
| **Jumla** | | | **4,067,225** |

### 7.1.6 KAMPUNI YA UVUVI ZANZIBAR (ZAFICO)

Ukaguzi wa hesabu za Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

### 7.1.6.1 Kuwepo kwa Hasara ya Shilingi 63,530,617.08

Kifungu nambari 3(h) cha Mkataba na Memoranda ya Kampuni ya Uvuvi Zanzibar, 2017 kinaeleza kuwa lengo la kuanzishwa kwa kampuni hiyo mama ya uvuvi Zanzibar ni pamoja na kuingia katika ubia au mpangilio mwingine wowote wa hisa, faida, muungano wa faida, ushirikiano, makubaliano au vinginevyo mtu au watu, kampuni au kushiriki katika kuendelea au kushiriki katika biashara au shughuli ambayo inaweza kuonekana kwa kampuni ya ushirika yenye uwezo.

Ukaguzi umebaini kwamba Kampuni ya Uvuvi Zanzibar imelipa kiasi cha shilingi 63,530,617.08 ambazo ni hasara zilizotokana na kuingia mkataba wa makubaliano na benki ya Amana kwa lengo la kuwachukulia dhamana Chama cha Wavuvi katika ununuzi wa mashine 16 za boti kwa makubaliano ya kwamba Chama cha Wavuvi kitalazimika kuuza samaki wote wanaopatikana kwa Kampuni ya Uvuvi Zanzibar.

Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kutokutekelezwa kwa makubaliano yalioingiwa baina ya Chama cha Wavuvi (Manahoza corporative) na Kampuni ya Uvuvi jambo ambalo limepelekea Kampuni ya Uvuvi kubeba jukumu la kulipa kiasi cha shilingi 63,530,617.08 katika benki ya Amana zilizotokana na mkopo wa mashine 16 za boti.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kampuni ya Uvuvi kuhakikisha unachukua hatua stahiki dhidi ya Chama cha Wavuvi zitakazopelekea kutelekelezeka kwa makubaliano walioingia ili kuepusha Kampuni ya Uvuvi kuendelea kubeba mzigo wa kulipa deni ambalo lilipaswa kulipwa na Chama cha Wavuvi.

#### 7.1.6.2 Kutokutumia programu ya utayarishaji na utunzaji wa hesabu (Accounting Packages)

Kifungu nambari 27(2)(a) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinaeleza kwamba Afisa Mhasibu atahakikisha kuwa Taasisi ya Umma inakuwa na kuendeleza utendaji, ufanisi, mfumo wa fedha uliowazi na usimamizi wa vihatarishi, na udhibiti wa ndani.

Ukaguzi umebaini kuwa Kampuni ya Uvuvi ilinunua programu yenye thamani ya shilingi 4,766,520 mnamo tarehe 29/09/2022 kwa ajili ya utayarishaji na utunzaji wa taarifa za hesabu za Kampuni. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni Kampuni kutokutumia programu ya utayarishaji na utunzaji wa taarifa za hesabu kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Kutokutumia mfumo katika utayarishaji na uandaaji wa hesabu za Kampuni kunapelekea kujitokeza kwa makosa ya kibinadam, na ukosefu wa uwazi katika utoaji wa taarifa za miamala ya kifedha. Aidha, ni kwenda kinyume na kifungu cha Sheria kilichonakiliwa hapo juu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Kampuni ya Uvuvi kuhakikisha unazingatia matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ikiwa ni pamoja na kufanya utekelezaji wa haraka katika matumizi ya programu iliyonunuliwa ili kuweza kupatikana kwa ufanisi katika uwekaji wa kumbukumbu za hesabu na hatimae kufikiwa kwa lengo lililokusudiwa.

#### 7.1.6.3 Kushindwa kuthibitisha thamani ya bidhaa za ghalani shilingi 42,377,900

Kwa mujibu wa viwango vya kimataifa vya ukaguzi kuhusiana na upatikanaji wa ushahidi wa ukaguzi ISAs 501 (Audit evidence), lengo la mkaguzi kushiriki katika zoezi la kuhesabu mali za ghalani ni kumuwezesha mkaguzi kupata ushahidi wa kutosha wa ukaguzi kuhusu uwepo wa mali au vifaa vya ghalani katika hali halisi ya vifaa hivyo, usahihi na ukamilifu wa taarifa za vifaa hivyo.

Aidha, kifungu cha 71(1) cha Sheria namba 6 ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na Usimamizi wa Mali za Umma ya 2021 kinaitaka kila Taasisi angalau mara moja kwa mwaka kufanya zoezi la utambuzi wa mali za umma.

Wakati wa uhakiki wa mali na bidhaa zilizomo ghalani kipindi cha mwisho wa mwaka wa fedha 2022/2023, ukaguzi umeshindwa kuthibitisha uwepo wa samaki waliohifadhiwa katika mafriji wenye thamani ya shilingi 42,377,900.

Kushindwa kuthibisha thamani ya samaki ya shilingi 42,377,900 kunatia shaka juu ya usahihi wa taarifa za mali za ghalani zilizotolewa katika taarifa ya hesabu ya mwisho wa mwaka.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kampuni kuhakikisha kuwa unaimarisha uwekaji wa kumbukumbu za mali za kampuni wakati wa zoezi la kuhesabu mali ili kutoa taarifa sahihi na za kuaminika juu ya wingi na hali halisi ya mali hizo ikiwemo samaki waliomo ghalani.

#### 7.1.6.4 Dosari katika Usimamizi wa utoaji wa Boti Ghalani shilingi 6,298,735,513

Kupitia fedha za Ahueni ya UVICO-19, Kampuni ya Uvuvi Zanzibar imeingia mkataba na Benki ya CRDB kwa ajili ya utoaji wa mkopo ili kuwasaidia wananchi. Miongoni mwa vipengele vya Mpango huo ni kununua boti na kupewa wananchi. Katika utoaji wa mkopo huo, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi hufanya kazi kama wakala wa kuhifadhi na kusambaza boti hizo kwa wananchi.

Ukaguzi ulifanya mapitio ya bidhaa zilizomo ghalani na kubaini kwamba boti zenye thamani ya shilingi 6,298,735,513 zilitolewa kutoka ghalani na kukabidhiwa wananchi pasipo uwepo wa kumbukumbu za makabidhiano pamoja na orodha ya wanufaika wa boti hizo kwa Kampuni ya Uvuvi Zanzibar.

Kukosekana kwa kumbukumbu ya idadi ya boti zilizogharimu shilingi 6,298,735,513 ambazo zilisambazwa kwa wananchi, kunatia shaka juu ya mfumo wa udhibiti wa ndani wa kampuni pamoja na usahihi wa taarifa ya mali za ghalani ambayo imeripotiwa katika hesabu za mwisho wa mwaka wa fedha 2022/2023.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa kampuni ya Uvuvi Zanzibar kufanya uchunguzi wa kina juu ya zoezi la utoaji wa Boti kwa wananchi waliokabidhiwa pamoja na kuandaa taarifa za usuluhishi kwa kushirikiana na Wizara ya Uchumi wa Bluu na Benki ya CRDB.

### 7.1.7 KAMPUNI YA UUNGANISHAJI WA MAUDHUI (ZMUX)

Ukaguzi wa hesabu za Kampuni ya Uunganishaji wa Maudhui (ZMUX) kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 7.1.7.1 Kukosekana kwa mikataba ya walinzi wa vituo

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika kuwa Kampuni ya Uunganishaji wa Maudhui (ZMUX) ina jumla ya wafanyakazi watano (5) wa mkataba ambao wanafanyakazi ya ulinzi katika minara ya kurushia maudhui Unguja na Pemba. Dosari iliyobainika na ukaguzi ni kukosekana kwa mikataba kulikosababishwa na kumalizika kwa muda wa mikataba ya utendaji kazi ilioingiwa baina ya Kampuni na wafanyakazi hao jambo ambalo linaweza kupelekea kuwakosesha haki zao za msingi na vilevile kunaweza kupunguza hamasa na ari ya utendaji kazi itokanayo na kukosekana kwa uhakika wa kuendelea kubaki katika ajira.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Kampuni ya Uunganishaji wa Maudhui (ZMUX) kufanya mapitio ya mikataba ya awali ili kuangalia uwezekano wa kuwaombea kibali cha ajira ya kudumu kwa lengo la kuepusha kujitokeza kwa vitendo vya uvunjaji wa Sheria ya Utumishi. Orodha ya walinzi wasiokuwa na mikataba ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 132: Walinzi wasiokuwa na mikataba ya ajira**

<table>
<tr><th>Namba</th><th>Jina la Mlinzi</th><th>Tarehe ya Kuanza Mkataba</th><th>Tarehe ya Kumaliza Mkataba</th><th>Mahali pa Kazi</th></tr>
<tr><td>1.</td><td>Mohammed ali khamis</td><td rowspan="5">1/1/2022</td><td rowspan="5">31/12/2022</td><td>Pemba</td></tr>
<tr><td>2.</td><td>Shaaban Ramadhan sadiq</td><td rowspan="2">Muyuni</td></tr>
<tr><td>3.</td><td>Ali Kombo Khamis</td></tr>
<tr><td>4.</td><td>Ame Haji Tubi</td><td rowspan="2">Nungwi</td></tr>
<tr><td>5.</td><td>Abdallah Mussa Koke</td></tr>
</table>

### 7.1.8 CHUO CHA UTAWALA WA UMMA

Ukaguzi wa Hesabu za Chuo cha Utawala wa Umma kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa mujibu wa Sheria, kanuni, taratibu pamoja na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya Kitaifa na Kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 7.1.8.1 Kukosekana kwa vielelezo vya Ununuzi wa gari ya Chuo shilingi 90,540,000

Kifungu nambari 34(1) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016 kinamtaka Afisa Mhasibu kuweka kumbukumbu zinazohusiana na masuala ya fedha za Idara, taasisi za biashara au taasisi za kikatiba kulingana na masharti na viwango na kanuni ya 55(1) pamoja na kanuni ya 57(2) ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inataka malipo yote yanayofanywa na taasisi ya Serikali kuhakikisha yanaambatanishwa na marejesho yaliokamilika.

Ukaguzi umebaini kuwa jumla ya shilingi 90,540,000 zimetumika kwa ununuzi wa gari moja (1) aina ya Toyota Pickup Hilux Rovo yenye namba ya usajili SMZ 638 B kwa ajili ya matumizi ya Chuo kupitia hati namba 69/6 ya tarehe 26/6/2023 ambazo amelipwa Mfuko Mkuu wa Hazina lakini vielelezo vya malipo hayo havikuambatanishwa na hati za malipo ili kuweza kuthibitisha uhalali wa malipo hayo.

Kutokuambatanisha vielelezo vinavyohusiana na matumizi husika ni kwenda kinyume na vifungu vya Sheria nilivyovinakili hapo juu.

Ukaguzi unashauri uongozi wa Chuo cha Utawala wa Umma kuhakikisha inaweka udhibiti mzuri wa uwekaji wa vielelezo ambavyo vilivyotumika kwa ajili ya kupata uhalali wa matumizi yaliyofanyika.

**CHUO CHA UTAWALA WA UMMA PEMBA**

#### 7.1.8.2 Mafuta ambayo hayakurikodiwa katika daftari la kurikodia bidhaa za ghalani shilingi 4,498,000

Kanuni nambari 113 ya Kanuni ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2021 inaelezea kwamba "Bidhaa zote zinazonunuliwa zipokelewe katika daftari la kurikodia bidhaa za ghalani na zitolewe kwa mujibu wa matumzi ya bidhaa hizo".

Ukaguzi umebaini kwamba jumla ya shilingi 4,498,000 zimelipwa kwa ajili ya ununuzi wa mafuta lakini mafuta hayo hayakurikodiwa kwenye daftari la kurikodia bidhaa za ghalani ili kuweza kuthibitisha uhalali wa mapokezi pamoja na matumizi yake, jambo ambalo ni kwenda kinyume na Kanuni niliyoinakili hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Chuo cha Utawala wa Umma Pemba kufuata sheria, kanuni na miongozo iliyopo ikiwemo kuyarikodi mafuta yanayonunuliwa kwa mujibu wa utaratibu wa kisheria uliopo. Mchanganuo wa mafuta hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini: -

**Jadweli Nambari 133: Mafuta ambayo hayakurikodiwa katika daftari la kurikodia bidhaa za ghalani**

| Hati nambari | Hundi nambari | Kiasi cha Fedha Kilicholipwa (Tshs) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| 16/7 ya 18/7/2022 | TT | 596,000 | Chake Chake Petroleum | Ununuzi wa Petrol lita 200 kwa ajili ya matumizi ya Afisi. |
| 65/12 ya 28/12/2022 | | 596,000 | | Ununuzi wa Petrol lita 200 kwa ajili ya matumizi ya Afisi. |
| 57/1 24/1/2023 | | 596,000 | | Ununuzi wa Petrol lita 200 kwa ajili ya matumizi ya Afisi. |
| 82/3 16/3/2023 | | 2,154,000 | | Ununuzi wa Petrol lita 748 kwa ajili ya matumizi ya Afisi. |
| 40/5 11/5/2023 | | 556,000 | | Ununuzi wa Petrol lita 200 kwa ajili ya matumizi ya Afisi. |
| **Jumla** | | **4,498,000** | | |

*Chanzo: Uchambuzi wa Hati za malipo*

### 7.1.9 CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (SUZA)

Ukaguzi wa hesabu za Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umefanywa kwa kuzingatia Sheria, kanuni, taratibu na vigezo vya ukaguzi vilivyokubalika kulingana na viwango vya kitaifa na kimataifa.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

#### 7.1.9.1 Manunuzi ya Vifaa vya Kuandikia kinyume na Sheria ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar shilingi 34,579,297

Kifungu nambari 35(1) cha Sheria nambari 12 ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji ya 2018 kinahitaji kila Taasisi ya Serikali kupeleka kazi zake zote za uchapaji na mahitaji ya vifaa vya ofisi na vya kuandikia kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji.

Ukaguzi umebaini kuwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kimefanya manunuzi ya vifaa vya ofisi na vya kuandikia nje ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji pasi na kupata idhini ya maandishi kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wakala kuruhusu kuchapisha au kununua vifaa vya kundikia na vifaa vya ofisi nje ya Wakala kama ilivyonakiliwa katika kifungu cha sheria hapo juu.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Chuo cha Taifa cha Zanzibar kuhakikisha unafuata miongozo ya Sheria nambari 12 ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji ya 2018 katika ununuzi wa huduma za uchapaji na ununuzi wa vifaa vya ofisi na vya kuandikia. Mchanganuo wa vifaa vya ofisi na vya kuandikia vilivyonunuliwa nje wa Wakala ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 134: Vifaa vya kuandikia vilivyonunuliwa nje ya Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar**

| Hati Namba | Kiasi (Tshs.) | Aliyelipwa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| PY004441 ya 3/01/2023 | 19,898,899 | Multi-Color Printers ltd | Ununuzi wa vifaa vya kuandikia |
| PY004885 ya 5/11/2023 | 7,340,199 | | |
| PY004885 ya 5/11/2023 | 7,340,199 | | |
| **Jumla** | **34,579,297** | | |

### 7.1.9.2 Matumizi madogo ya Fedha za Skuli ya Biashara

Kwa mujibu wa taratibu za kifedha za Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Skuli ya Biashara (Chwaka) inaandaa na kupeleka Makao Makuu ya Chuo, mtiririko wa fedha unaoonyesha mahitaji na matumizi ya fedha kwa kila robo mwaka pamoja na shughuli zote zilizopangwa kutekelezwa, kwa ajili ya kupata idhini na kuingiziwa fedha.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 ukaguzi umebaini kuwa Skuli ya Biashara ilikuwa na bakaa ya fedha ambayo haikutumika yenye jumla ya shilingi 532,048,298.32 jambo linalomaanisha kuwa kuna shughuli nyingi zilizopanga kutekelezwa ama hazikutekelezwa au zimetekelezwa kwa kiasi kidogo.

Ukaguzi umebaini kuwa sababu kubwa iliyopelekea kutokutumika kwa fedha hizo ni kuchelewa kukamilika kwa michakato ya manunuzi pamoja na taratibu za uidhinishaji kutoka Makao Makuu ya Chuo.

Kuwepo kwa matumizi madogo ya fedha za Skuli ya Biashara kunapelekea kuchelewa kukamilika kwa malengo yaliyowekwa na Skuli kwa wakati uliotarajiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kuweka mfumo madhubuti utakaosaidia kuharakisha michakato ya manunuzi na taratibu za uidhinishaji kutoka Makao Makuu ya Chuo ili kuziwezesha Skuli kutekeleza shughuli zao kwa ufanisi.

### 7.1.9.3 Malipo ya fedha taslim kwa wafanyakazi wa kigeni 163,944,000

Kwa mujibu wa Kanuni namba 58(1) ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za 2021, "Malipo yote ya matumizi ya Taasisi ya Kibajeti na Serikali za Mitaa yatafanyika kwa mfumo wa uhaulishaji fedha".

Katika mwaka 2022/2023 ukaguzi umebaini kuwa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kimefanya malipo ya fedha taslim yenye jumla ya shilingi 163,944,000 kwa ajili ya mishahara ya wafanyakazi wa kigeni kutoka nchini Cuba wanaofanya kazi katika Chuo hicho.

Kufanya malipo kwa fedha taslim ni kwenda kinyume na Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma za 2021 na kunaweza kupelekea upotevu wa fedha za umma kunakotokana na kurundikana kwa fedha taslim.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kufuata miongozo ya Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na Kanuni zake katika kufanya malipo ikiwemo kufanya malipo kwa njia za kibenki. Mchanganuo wa malipo hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 135: Malipo yaliyofanywa kwa njia ya fedha Taslimu**

| Namba | Mwezi | Kiasi cha Mshahara (Shs.) |
|---|---|---|
| 1. | Julai, 2022 | 14,904,000 |
| 2. | Agosti, 2022 | 14,904,000 |
| 3. | Septemba, 2022 | 14,904,000 |
| 4. | Oktoba, 2022 | 14,904,000 |
| 5. | Novemba, 2022 | 14,904,000 |
| 6. | Disemba, 2022 | 14,904,000 |
| 7. | Januari, 2023 | 13,041,000 |
| 8. | Febuari, 2023 | 14,904,000 |
| 9. | Machi, 2023 | 14,904,000 |
| 10. | Aprili, 2023 | 5,589,000 |
| 11. | Mei, 2023 | 13,041,000 |
| 12. | Juni, 2023 | 13,041,000 |
| **Jumla** | | **163,944,000** |

### 7.1.9.4 Changamoto zinazolikabili eneo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lilioko Wilaya ya Bagamoyo

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, inamiliki eneo la shamba la Ranchi ya Zanzibar Bagamoyo (RAZABA) lenye ukubwa wa zaidi ya hekari 6,000 liliopo Makurunge katika Wilaya ya Bagamoyo Tanzania Bara lililopatikana mwaka 1976 baada ya kupata kibali kutoka kwa Kamishna wa Ardhi chenye kumbumbukumbu nambari LD/70254/12/TBR cha tarehe 24 Septemba,1971.

Kupitia mazungumzo na watendaji mbalimbali wa Chuo, ukaguzi umebaini kuwa shamba hilo linakabiliwa na changamoto ya kuvamiwa na watu wanaoishi karibu nalo kunakotokana na kukosekana kwa mipango madhubuti ya kuliendeleza pamoja na kukosekana kwa hatua za kulilinda eneo hilo dhidi ya uvamizi.

Aidha ukaguzi umebaini kuwa Chuo hakina Hati ya umiliki inayothibitisha umiliki halali na haki ya matumizi ya shamba hilo.

Kukosekana kwa hati ya umiliki wa shamba hilo kunaweza kukapelekea Serikali kupoteza sehemu ya shamba au shamba lote kutokana na vitendo vinavyoendelea vya uvamizi na uharibifu unaofanywa na wananchi.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kwa kushirikiana na viongozi wa Serikali kuchukuwa jitihada za haraka za kuhakikisha kunakuwa na umiliki halali wa eneo hilo ili kuweza kulidhibiti na kulizuia dhidi ya uharibifu unaoendelea kufanywa na wananchi.

#### 7.1.9.5 Kutokutumika kwa mashine na vifaa vya jikoni kwa muda mrefu

Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar moja katika jukumu lake ni kutoa taaluma kwa wanafunzi wanaojifunza fani ya mapishi, vyakula na vinywaji ambapo wanafunzi hao husoma kwa nadharia na vitendo pamoja na kujifunza mbinu za kuhudumia vikao na mikutano mikubwa kwa kutoa huduma za chakula, vinywaji, usafi na mambo mengineyo.

Katika ukaguzi uliofanyika kwa mwaka wa fedha 2022/2023 wakaguzi pamoja na mambo mengineyo walitembelea eneo la Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar kwa lengo la kutathmini shughuli za utunzaji na uimarishaji wa mali za Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar katika tawi la Chuo cha Maendeleo ya Utalii Zanzibar.

Ukaguzi umebaini uwepo wa vifaa mbalimbali vya jikoni pamoja na mashine ambazo kwa muonekano ni vifaa vipya vilivyopatikana kwa muda mrefu ambavyo hadi ukaguzi unakamilika vifaa hivyo bado havijaanza kutumika jambo ambalo linaweza kusababisha vifaa hivyo kupotea au kuharibika uimara wake kutokana na kutokufanya kazi kama vilivyokusudiwa na hatimae kupelekea uwepo wa hasara kwa Chuo na kukosekana tija iliyokusudiwa.

Ukaguzi unaushauri uongozi wa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar kuhakikisha unachukuwa jitihada za makusudi kuvitumia vifaa na mashine zilizopo kwa ajili ya mafunzo ya wanafunzi, ikiwemo kuanzisha utoaji wa huduma za ufuaji wa nguo (laundry) ili mashine hizo ziweze kutumika kwa lengo la kumudu gharama ndogo ndogo za upatikanaji wa malighafi za kuwafundishia wanafunzi wanaochukuwa taaluma mbali mbali katika chuo hicho.

# SURA YA NANE



# 8.0 UKAGUZI WA AWALI WA MAFAO YA WASTAAFU NA MALIPO YA FIDIA KWA WATUMISHI WA UMMA

Kwa mujibu wa kifungu nambari 34 cha Sheria Nambari 7 ya Ukaguzi wa Umma ya 2023 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar ana jukumu la kufanya ukaguzi wa awali kwa Mafao ya Pencheni, Kiinua Mgongo na Malipo ya Fidia kwa watumishi wanaopata ajali kazini kutoka katika Taasisi mbali mbali za Serikali na Sekta binafsi.

Katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2022/2023, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilipokea fomu za mafao kupitia Majalada ya wastaafu kutoka katika Mawizara, Mamlaka, Mashirika pamoja na Majalada yaliyopokelewa kutoka Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar ikiwemo fomu za mafao ya fidia kwa watumishi wa Umma. Hali halisi ya mafao hayo ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 136: Mafao ya Kiinua Mgongo

| **Fomu ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamiii Zanzibar (ZSSF)** | | |
|---|---|---|
| **Maelezo** | **Idadi ya Majalada (Fomu)** | **Kiasi cha Fedha kilichothibitishwa kwa malipo (Tsh.)** |
| Salio la Nyuma 2021/2022 | 23 | |
| Majalada yaliyopokelewa mwaka 2022/2023 | 1,369 | |
| **Jumla ya Majalada** | **1,392** | |
| Majalada yaliyokaguliwa na kuthibitishwa fomu za Malipo | 1,392 | 27,675,517,259.73 |
| **Salio hadi tarehe 30 Juni, 2023** | **Hakuna** | |
| **Majalada ya Mawizara, Mamlaka na Mashirika** | | |
| Salio la nyuma 1 Julai, 2022 | 103 | |
| Majalada yaliyopokelewa mwaka 2022/2023 | 1,436 | |
| **Jumla ya majalada** | **1,539** | |
| Majalada yaliyokaguliwa na kuithibitishwa fomu za malipo | 1,187 | 23,018,107,983 |
| **Salio la 30 Juni, 2023** | **352** | |

Aidha, kupitia ukaguzi wa awali imebainika katika mwaka wa fedha 2022/2023 wapo wastaafu wanaopata Pencheni kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii na Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 137: Mafao ya Pencheni

| **Mfuko** | **Idadi ya Pencheni 2022/2023** | **Kiasi cha Fedha kwa mwezi (Tsh.)** |
|---|---|---|
| Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar | 1,223 | 371,944,433.3 |
| Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali | 648 | 168,424,472.3 |

Vile vile, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilipokea jumla ya fomu za fidia 29 kwa wafanyakazi wanaoumia kazini ambapo baada ya kufanyiwa uhakiki ilibainika jumla ya shilingi 37,025,347 ziliweza kuthibitishwa kwa ajili ya kufanyiwa malipo.

**Matokeo na Mapendekezo ya Ukaguzi**

**8.1.9.1 Majalada 14 yaliyorejeshwa kwa ajili ya kufanyiwa masahihisho kwa Maafisa Masuuli wa Taasisi mbali mbali za Serikali**

Katika ukaguzi wa Majalada ya Wastaafu kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imebainika uwepo wa jumla ya Majalada 14 ambayo yalikuwa na mapungufu mbali mbali na kupelekea kurejeshwa kwa Maafisa Masuuli kwa ajili ya kufanyiwa masahihisho. Hali halisi ni kama inavyoonekana hapo chini:-

**Jadweli Nambari 138: Majalada yaliyorejeshwa kwa ajili ya kufanyiwa masahihisho**

| Namba | Taasisi | Jumla ya Majalada | Kum. ya Barua ya Marejesho | Dosari iliyobainika | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Bodi ya Huduma za Maktaba Zanzibar. | 1 | AUD/G.18/2/WF/ VOL.III/6 ya tarehe 15/7/2022 | Mapungufu katika ukokotoaji wa hesabu za mafao. | Masahihisho yalifanyika. |
| 2. | KMKM | 1 | AUD/G.18/2/WF/ VOL.III/5 ya tarehe 14/7/2022 | Marejesho ya Jalada la marehemu Choum Ame Nyasa mwenye Nam. ya mshahara 544315 ambaye alibainika, kuwa na jina la Mshenga Mosi Khamis baada ya kufariki. | Jalada halijawasilishwa |
| 3. | Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. | 1 | AUD/G.18/2/WF/ VOL.IV/12 ya tarehe 10/10/2022 | Jalada la Ndugu Salma Rashid Abdul-Wahab, baada ya kubainika kwamba jalada hilo tayari limeshawasilishwa katika Afisi ya Mdhibiti na kufanyiwa kazi. | Kuhifadhiwa kwa Jalada katika Taasisi husika |
| 4. | Wizara ya Afya | 1 | AUD/G.18/2WF/ VOL.V/36 ya tarehe 15/2/2023 | Jalada la mstaafu Raya Ali Khamis lilofanyiwa marejesho baada ya kukosekana taarifa za awali za uajiri. | Taarifa ziliwasilishwa na muhusika aliweza kupata mafao yake. |
| 5. | Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani | 1 | AUD/G.18/2/WF/ VOL.V/35 ya tarehe 15/2/2023 | Marejesho ya Jalada la Ndugu Nasra Nassor Ali, baada ya kukosekana taarifa za awali za uajiri | Taarifa ziliwasilishwa na muhusika aliweza kupata mafao yake |
| 6. | Afisi ya Mkuu wa Mkoa, Kaskazini Unguja | 4 | AUD/G.18/2/WF/ VOL.V/59 ya tarehe 20.3.2023 | Marejesho ya majalada ya masheha wanne kwa ajili ya kupatiwa ufafanuzi wa mikataba yao. | |

| Namba | Taasisi | Jumla ya Majalada | Kum. ya Barua ya Marejesho | Dosari iliyobainika | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| 7. | Wizra ya Elimu | 1 | AUD/G.18/2/WF/ VOL.V/22 ya trehe 23.1.2023 | Kuerejeshwa kwa jalada la Ndg: Masoud Abdalla Masoud, kwa ajili ya kupatiwa ufafanuzi wa kuwepo tarehe mbili za kustaafu baina ya ZSSF na Wizara rya Fedha | Ufafanuzi ulipatikana na kufanyiwa ukaguzi. |
| 8. | Wizara ya Afya | 1 | AUD/G.18/2/WF/ VOL.V/21 ya tarehe 23.1.2023 | Marejesho ya Jalada la Ndugu Mchanga Nassor Khalfan, baada ya kuwepo na mapungufu katika taarifa za ustaafishwaji wake. | Masawazisho yalifanyika na ukaguzi uliendelea |
| 9. | Shirika la Utangazaji Zanzibar | 1 | AUD/G.18/2/WF/ VOL.V/15 ya tarehe 11.1.2023 | Kuerejeshwa kwa jalada la Ndg: Salma Ali Omar, kwa ajili ya kupatiwa ufafanuzi wa kuwepo tarehe mbili za kustaafu baina ya ZSSF kwa mwezi waJune 2022 na Wizara rya Fedha kwa mwezi wa Novemba, 2022 | Hatua za kurejesha mishahara zilichukuliwa na Taasisi ili kumuwezesha muhusika kuwa na tarehe moja tu kuannza kupokea Pencheni. Pia mstaafu kurejeshewa michango ya miezi minne ya ZSSF. |
| 10. | Wizara ya Afya | 1 | AUD/G.18/2/WF/ VOL.IV/51 | Marejesho ya jalada la Ndugu: Mussa Said Mussa Kutokana na kubainika kurejeshwa kazini baada ya kufukuzwa kwa barua na kurejeshwa kazini bila ya kuwepo na barua. | Hakuna mrejesho juu ya kilichobainika. |
| 11. | Wizara ya Afya | 1 | AUD/G.18/2/WF/ VOL.IV/51 ya tarehe 12.12.2022 | Kurejeshwa kwa jalada la Ndugu: Haji Mwita Haji, ambaye aliacha kazi akiwa na miaka 50 ya kuzaliwa . | Muhusika alipoteza haki zake kwa mujibu wa Sheria. |

## Dosari za Ukokotoaji wa Mafao ya Wastaafu

Athari ya ukokotoaji wa ziada au upungufu wa mafao ya wastaafu wanaolipwa kupitia Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, ambayo imebainika kupitia fomu zilizoambatanishwa na Majalada ya wastaafu yaliyowasilishwa katika Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kutoka kwa Maafisa Masuuli wa Taasisi mbali mbali, kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi wa awali na kugundulika kuwepo kwa makosa katika ukokotoaji wa mafao ya baadhi ya wastaafu.

Aidha kama ilivyobainika katika ripoti hii, dosari zinazojitokeza katika ukaguzi wa awali zingepelekea kufanyika kwa malipo ya Kiinua Mgongo kwa ziada ya shilingi 675,426,977 na malipo ya Pencheni ya mwezi kwa ziada ya shilingi 5,758,504 **Kiambatisho Nambari 11 kinahusika.**

Pia kufanyika malipo ya Kiinua Mgongo kwa upungufu wa shilingi 206,007,921 na malipo ya Pencheni ya mwezi kwa upungufu wa shilingi 2,010,919. Kiambatisho **Nambari 12 Kinahusika.**

Mchanganuo wa fomu zilizofanyiwa ukaguzi na kubainika na ziada au upungufu wa hesabu za mafao ni kama inavyoonekana katika jadweli lifuatalo:-

### Jadweli Nambari 139: Dosari za Ukokotoaji wa Mafao ya Wastaafu

| Mafao | Idadi ya Fomu zilizokaguliwa | Idadi ya fomu zilizobainika kuwa na ziada ya Mafao | Ziada ya Fedha iliyobainika (Tsh.) | Idadi ya fomu zilizobainika kuwa na upungufu wa Mafao | Upungufu wa Fedha iliyobainika (Tsh.) |
|---|---|---|---|---|---|
| K/Mgongo | 1,187 | 78 | 675,426,977 | 51 | 206,007,921 |
| Pencheni | 1,187 | | 5,758,504 | | 2,010,919 |

Kutokana na jadweli hapo juu, ukaguzi umebaini kuongezeka kwa dosari ya ukokotoaji ambao unapelekea upungufu au ziada ya hesabu za mafao kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na mwaka wa fedha uliopita 2021/2022 kama inavyoonekana katika jedweli hapo chini:-

### Jadweli Nambari 140: Mlinganisho wa dosari za ukokotoaji wa mafao ya wastaafu

| Mwaka wa fedha | Mafao | Idadi ya Fomu zilizokaguliwa | Idadi ya fomu zilizobainika kuwa na ziada ya Mafao | Ziada ya Fedha iliyobainika (Tsh.) | Idadi ya fomu zilizobainika kuwa na upungufu wa Mafao | Upungufu wa Fedha iliyobainika (Tsh.) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2021/2022 | K/Mgongo | 1,138 | 13 | 24,659,987 | 18 | 55,326,477 |
| 2022/2023 | K/Mgongo | 1,187 | 78 | 675,426,977 | 78 | 206,007,921 |
| **Tofauti** | | **49** | **65** | **650,766,990** | **60** | **150,681,444** |
| 2021/2022 | Pencheni | 1,138 | 13 | 205,501 | 18 | 432,980 |
| 2022/2023 | Pencheni | 1,187 | 51 | 5,758,504 | 51 | 2,010,919 |
| **Tofauti** | | **49** | **38** | **5,553,003** | **33** | **1,577,939** |

Kutokana na taarifa zinazoonekana katika Jadweli la hapo juu ukaguzi umegundua kwamba, mapungufu na ziada ya hesabu za mafao ambayo yameongezeka katika ukokotoaji wa mafao, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ukilinganisha na mwaka uliopita 2021/2022 yamesababishwa na Maafisa Utumishi kutozingatia kanuni ya ukokotoaji wa kutafuta mshahara wa mwisho kwa njia ya wastani, hii kwa wastaafu ambao mishahara yao ya mwisho hawakuitumia na kuipokea kwa muda wa miezi kumi na mbili mfululizo, kutozingatiwa kutolewa muda wa likizo bila malipo miongoni mwa miezi ambayo imefanyiwa kazi na mstaafu pia Maafisa Utumishi wa baadhi ya Taasisi kutumia kanuni ya zamani ya ukokotoaji wa mshahara wa mwisho kwa kutumia wastani wa miezi 24 badala ya 12 ambayo ndio inayotumika kwa sasa.

## UKAGUZI WA MAFAO YA WASTAAFU (OR) FEDHA NA MIPANGO

### 8.1.9.2 Kukosekana kwa ufafanuzi wa ziada ya wastaafu 145 ambao hawakuhakikiwa kupitia uhakiki wa Januari, 2023

Kutokana na taarifa zilizobainika katika Ripoti ya uhakiki wa wastaafu ambao ulifanyika kuanzia tarehe 9.1.2023 hadi 11.2.2023, imebainika kuwepo na ziada ya wastaafu 145 ambao wamejumuishwa katika idadi ya wastaafu 1,565 ambao wameripotiwa kuwa hawakufanyiwa uhakiki kama inavyoonekana hapo chini:-

**Jadweli Nambari 141: Ziada ya wastaafu ambao hawakuhakikiwa**

| Wastaafu waliohakikiwa (A) | Wastaafu wasiohakikiwa (B) | Jumla ya wastaafu C= (A+B) | Wastaafu waliokadiriwa kufanyiwa uhakiki (D) | Ziada kwa wastaafu (C-D) |
|---|---|---|---|---|
| **12,264** | **1,565** | **13,829** | **13,684** | **145** |

Mchanganuo wa wastaafu 1,565 ambao hawakufanyiwa uhakiki ambao walipelekea kulipwa fedha zenye thamani ya shilingi 249,120,079 ni kama inavyoonekana katika jadwali hapo chini:

Aidha, kupitia ripoti ya uhakiki wa wastaafu, ukaguzi umebaini kuwepo na mchanganuo wa idadi ya wastaafu ambao hawakufanyiwa uhakiki kupitia Benki mbali mbali wanazopokelea kama ifuatavyo:

**Jadweli Nambari 142: Malipo ya Wastaafu ambao hawakufanyiwa Uhakiki**

| Benki | Idadi ya Wastaafu | Fedha zilizolipwa (Tsh.) |
|---|---|---|
| PBZ | 1245 | 189,020,425.00 |
| TPB | 215 | 29,299,828.00 |
| NMB | 29 | 3,930,951.00 |
| NBC | 48 | 17,422,208.00 |
| CRDB | 11 | 4,472,710.00 |
| ABSA | 3 | 2,194,320.00 |
| AMANA | 2 | 208,194.00 |
| DTB | 3 | 270,000.00 |
| EXIM | 7 | 2,089,486.00 |
| EQUITY | 1 | 91,250.00 |
| KCB | 1 | 120,707.00 |
| **Jumla** | **1565** | **249,120,079** |

Aidha, ukaguzi ulipitia kwa kina, taarifa za malipo ya Pencheni yaliyofanyika kupitia Benki mbali mbali, kwa mwezi wa Januari na Februari 2022/2023, kwa lengo la kuthibitisha idadi ya wastaafu waliotajwa hapo juu, hivyo ukaguzi uliangalia idadi ya wastaafu waliolipwa Januari na idadi ya wastaafu waliolipwa pencheni kwa mwezi wa Februari. Mchanganuo idadi ya wastaafu waliolipwa kwa mwezi wa Januari na Februari ni kama inavyoonekana katika jadwari hapo chini:-

### Jadweli Nambari 143: Tofauti ya Idadi ya wastaafu kati ya mwezi wa Januari na Februari 2022/2023

| Idadi ya Wastaafu kwa mwezi wa Januari | Idadi ya Wastaafu kwa mwezi wa Februari | Tofauti ya Wastaafu |
|---:|---:|---:|
| 11,170 | 10,041 | 1,129 |
| 1,864 | 1,663 | 201 |
| 212 | 189 | 23 |
| 275 | 232 | 43 |
| 63 | 52 | 11 |
| 33 | 31 | 2 |
| 14 | 12 | 2 |
| 15 | 12 | 3 |
| 19 | 12 | 7 |
| 11 | 10 | 1 |
| 10 | 9 | 1 |
| **13,686** | **12,263** | **1,423** |

Tofauti ya Idadi ya wastaafu iliyobainika kupitia ripoti ya uhakiki na idadi ya wastaafu iliyojitokeza katika malipo ya pencheni za wastaafu kwa mwezi wa Januari na Februari 2022/2023 ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:

### Jadweli Nambari 144: Tofauti baina ya Ripoti ya Uhakiki na Idadi halisi ya Wastaafu kwa mwezi wa Januari na Februari

| Jina la Benki | Taarifa za Ripoti ya Uhakiki | Idadi ya wastaafu kwa Mwezi Januari na Februari | Ongezeko la Wastaafu |
|---|---:|---:|---:|
| PBZ | 1,245 | 1,129 | 116 |
| TPB | 215 | 201 | 14 |
| NMB | 29 | 23 | 6 |
| NBC | 48 | 43 | 5 |
| CRDB | 11 | 11 | 0 |
| ABSA | 3 | 2 | 1 |
| AMANA | 2 | 2 | 0 |
| DTB | 3 | 3 | 0 |
| EXIM | 7 | 7 | 0 |
| EQUITY | 1 | 1 | 0 |
| KCB | 1 | 1 | 0 |
| **Jumla** | **1,565** | **1,423** | **142** |

Kutokuhakikiwa kwa wastaafu kunapelekea kukosekana kwa uhakika wa makisio ya fedha kwa ajili ya malipo ya wastaafu wa Serikali ambao wanaendelea kupokea Pencheni kupitia Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali na vile vile kunaweza kupelekea kujitokeza kwa upotevu wa fedha za umma

Ukaguzi unashauri Kitengo cha Malipo ya Mafao, kuwa makini katika utoaji wa taarifa za wastaaafu na kupitia taarifa za uhakiki wa mwaka wa fedha uliopita, kabla ya kuanza uhakiki ili kuweza kujua idadi halisi ya wastaafu ambao hawajashiriki katika zoezi la uhakiki kwa muda mrefu.

#### 8.1.9.3 Kukosekana kwa ufafanuzi wa idadi ya Penchenia (wastaafu) 28 waliofariki

Katika ukaguzi uliofanyika ambao ulipitia ripoti ya uhakiki ya wastaafu wanaoendelea kupokea Pencheni kwa kila mwezi, imebainika kuwepo kwa idadi ya wastaafu 28 waliofariki ambao walibainika katika zoezi la uhakiki, lakini idadi ya wastaafu hao hawakujumuishwa katika idadi ya wastaafu 12,264 ambao walifanyiwa uhakiki.

Kukosekana kwa ufafanuzi wa idadi ya Penchenia kunaweza kupelekea kutokuwepo kwa uhakika wa makisio ya fedha kwa ajili ya malipo ya wastaafu wa Serikali ambao wanaendelea kupokea Pencheni kupitia Huduma za Mfuko Mkuu wa Serikali jambo ambalo linaweza kusababisha uwepo wa taarifa zisizo sahihi za malipo ya fedha za pencheni kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali, kufanya hivyo ni kinyume na kifungu nambari 17(5) cha Sheria nambari 12 ya Usimamizi wa Fedha za Umma ya 2016. Mchanganuo wa idadi ya wastaafu hao ni kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini:-

**Jadweli Nambari 145: Kukosekana kwa ufafanuzi wa Malipo ya Wastaafu waliofariki**

| Wastaafu Wanaoendelea | | Wastaafu Wapya | | Wastaafu Wenye Malimbikizo | | Wastaafu Waliofariki | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| IDADI | TZS | IDADI | TZS | IDADI | TZS | IDADI | TZS |
| 12,080 | 2,242,245,804 | 107 | 188,004,951 | 77 | 176,566,984 | 28 | 5,969,571 |

## 8.1 MAPENDEKEZO YA UJUMLA

Ukaguzi unatoa mapendekezo ya jumla juu ya dosari zilizoainishwa katika ripoti ya Uhakiki wa Mafao ya Pencheni na Viinua Mgongo kwa Wastaafu waliomaliza kama ifuatavyo:-

- Taasisi zote za Serikali kuhakikisha zinafuata matakwa ya kanuni ya 52(4) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014 inayosisitiza kwamba Majalada yote ya Watumishi wa Umma yatalazimika kuhifadhiwa katika Masjala ya siri na hayatoruhusika kupewa mtumishi yeyote isipokuwa kwa ruhusa ya Katibu Mkuu au Mkuu wa Taasisi.
- Vitengo vyote vya Taasisi za Serikali ambavyo vinahusika na utunzaji wa Majalada binafsi ya watumishi kutochukua fursa ya kubadilisha kumbukumbu zilizomo katika Majalada hayo kwani kufanya hivyo ni kwenda kinyume na kanuni nambari 55 ya Kanuni za Utumishi wa Umma za 2014.
- Maafisa Utumishi kuzingatia siku za likizo bila ya malipo kwa watumishi wanaochukua likizo hizo, katika kipindi cha ukokotoaji wa mafao ya uzeeni bila ya kwenda kinyume na kanuni nambari 63(3) ya Kanuni za Utumishi wa Umma ya mwaka 2014.
- Taasisi za Umma kufanya mapitio ya Majalada ya watumishi kabla ya kustaafu, ili kuweza kubaini mapungufu ya nyaraka muhimu ambazo zinatumika kama ni vielelezo katika utayarishaji wa mafao.
- Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kutoa miongozo rasmi inayohusiana na watumishi waliofukuzwa kazi kimakosa, na baadae kurudishwa kazini wakiwa wameshafikia umri wa kustaafu na kutolewa maelekezo ya kufanyiwa stahiki za mafao ya viinua mgongo kwa kutumia vigezo na mabadiliko ya mshahara na watumishi waliokuwa wanaendelea katika utumishi wao.

